JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO




## PROGRAMU JUMUISHI YA TAIFA YA MALEZI, MAKUZI NA MAENDELEO YA AWALI YA MTOTO (PJT-MMMAM) 2021/22 – 2025/26

DISEMBA 2021

# UTANGULIZI

Ulimwengu mzima una takribani watoto milioni 250 wenye umri chini ya miaka mitano ambao wanapatikana kwenye nchi zenye uchumi wa chini na zile zenye uchumi wa kati ambao wapo kwenye hatari ya kutokufikia hatua zao za ukuaji. Takribani robo tatu sawa na asilimia 66 ya watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano walio kusini mwa jangwa la Sahara wapo kwenye hatari ya kutokufikia hatua timilifu za ukuaji kutokana na kukosa malezi bora, umasikini, utapiamlo pamoja na matatizo mengine ya kijamii na kiuchumi. Hadi sasa maendeleo ya mtoto hayajapewa uzito unaostahili, badala yake msisitizo umewekwa kwenye kupunguza vifo licha ya kwamba kipindi cha miaka 0-8 ni fursa muhimu ya kuboresha maendeleo ya binadamu na hivyo kupata mtaji bora wa rasilimali watu yenye tija.

Pia ifahamike kwamba, kukosekana kwa fursa za ukuaji kwa watoto wenye umri huo kunaweza kusababisha changamoto katika maendeleo yao ambayo yanaweza kuathiri kizazi na kizazi. Kumekua na hatua na jitihada mbalimbali katika kutatua changamoto za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (MMMAM). Mifumo na miongozo mbalimbali imeandaliwa ikiwa imelenga kusaidia utekelezaji wa kina wa shughuli za MMMAM ili kufanikisha malengo ya maendeleo endelevu. Miongoni mwa miongozo iliyoandaliwa ni ule wa malezi jumuishi uliozinduliwa na Shirika la Afya Duniani mwaka 2018 ambao una maono kuwa na "Dunia ambayo mtoto anaweza kufikia hatua zake za ukuaji na hakuna mtoto atakaeachwa nyuma" Mfumo huu wa malezi jumuishi unatoa mwongozo sahihi kwa nchi mbalimbali kuwekeza kwenye hatua zote za ukuaji wa mtoto.

Tanzania ni moja ya nchi zenye uchumi wa kati wa chini ambapo asilimia 43 ya watoto wapo kwenye hatari ya kutokufikia hatua timilifu za ukuaji na maendeleo kutokana na viashiria vya hatari mbalimbali vya maendeleo kama vile utapiamlo, umasikini, kukosekana kwa uhakika wa chakula, msongo wa kifamilia, miundombinu duni na uhaba wa rasilimali pamoja na utelekezaji na unyanyasaji wa watoto. Vilevile wazazi au walezi kutokuwa karibu na watoto wao suala ambalo linachangiwa na kukosekana kwa uelewa wa kina wa MMMAM.

Programu za malezi jumuishi nchini Tanzania zinahitaji kupewa kipaumbele na msisitizo kutokana na kukosekana kwa uratibu mzuri na zinatekelezwa kama sehemu za programu za kisekta au tafiti zinazofanywa na wadau zikilenga baadhi ya umri wa watoto na kutekelezwa kwenye maeneo machache.

Kutokana na umuhimu wa Mfumo wa Malezi Jumuishi, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa MMMAM imeandaa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto itakayo tekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2021/22-2025/26). Mpango huu umelenga kutatua changamoto za ukuaji na maendeleo ya watoto wenye umri wa miaka 0-8. Programu hii itatoa mchango katika kufanikisha Mpango wa tatu wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano 2021/22 - 2025/26 kwa kutambua kwamba watoto ambao wanakosa kufikia kikamilifu hatua za ukuaji ni changamoto kwa maendeleo ya taifa na tishio kwa malengo ya kiuchumi na kijamii ikiwa ni pamoja na kujenga nchi ili kufikia uchumi wa kati. Kutokana na sababu hizo, programu hii imelenga kuwekeza moja kwa moja kwenye maendeleo ya watu ili kuharakisha upatikanaji wa matokeo chanya ya maendeleo ya awali ya mtoto kwa kuhimiza ushiriki wa sekta mbalimbali katika kutoa huduma za malezi jumuishi yenye vipengele vitano: afya bora kwa mtoto na mama/mlezi; lishe ya kutosha kuanzia ujauzito; malezi yenye mwitikio; fursa za ujifunzaji wa awali; ulinzi na usalama kwa watoto. Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM inatakiwa izingatiwe na afua zote za malezi zitekelezwe kwa ujumuishi kwa kuwa inalenga kuleta matokeo chanya katika ukuaji na maendeleo ya awali ya mtoto na kufikia maono: ***"Watoto wote Tanzania wapo kwenye mwelekeo sahihi wa kufikia ukuaji timilifu"***. Juhudi za wadau wote wa MMMAM na rasilimali zielekezwe kutekeleza afua zilizopangwa katika programu hii kwa wakati na ufanisi wa hali ya juu ili kufikia malengo ya programu. Wito unatolewa kwa wadau mbalimbali wa maendeleo kusaidia kufanikisha maono ya programu hii kwa kuhakikisha wanajielekeza kuchangia utekelezaji kwa kufanya kazi kwa karibu na serikali. Aidha, upatikanaji wa rasilimali za kutosha (rasilimali fedha na watu) ni suala la muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa programu hii.

***Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB)***
Waziri Mkuu

# SHUKRANI

Uandaaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM umezingatia ushirikishwaji wa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na serikali, wadau wa maendeleo, na mashirika yasiyo ya kiserikali. Napenda kutambua mchango wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kuona uhitaji wa haraka wa kukuza na kuendeleza huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto hivyo kuamua kuandaa programu jumuishi ya taifa ya MMMAM. Menejimenti ya wizara ikiongozwa na Katibu Mkuu iliwashirikisha wadau mbalimbali katika kuandaa programu hii. Wadau walishiriki kuainisha mahitaji ya watoto wadogo na kuweka vipaumbele vitakavyosaidia kuhakikisha watoto wote Tanzania wapo kwenye mwelekeo sahihi wa kufikia ukuaji timilifu.

Uandaaji wa programu hii umeratibiwa na kikundi kazi ambacho kiliundwa na wataalamu kutoka wizara, idara na wakala mbalimbali wa serikali wanaoshughulikia masuala ya Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali nchini pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo. Wajumbe wa kikundi kazi wamekuwa mstari wa mbele kuhimiza masuala ya MMMAM katika wizara na mashirika yao.

Aidha, naipongeza Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mchango wao mkubwa katika kuongoza kikundi kazi na kuratibu masuala yote ya uandaaji wa programu hii. Kikundi kazi kilihusisha wajumbe kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Raisi-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mamlaka ya Chakula na Lishe Tanzania pamoja na Chuo Kikuu cha Dodoma. Pia napenda kushukuru Mashirika ya Umoja wa Mataifa ikiwa ni pamoja na UNICEF, WHO na UNESCO kwa mchango wao mkubwa wa kitaalamu na rasilimali fedha katika uandaaji wa programu hii.

Napenda kushukuru Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto Nchini Tanzania (TECDEN) kwa kutekeleza wajibu wao kikamilifu kama mwenyekiti mwenza kuratibu Mashirika yasiyo ya Kiserikali katika kuandaa programu hii. Pia nachukua nafasi hii kushukuru Mashirika yasiyo ya Kiserikali ikiwa ni pamoja na Children in Crossfire (CiC), Save the Children, Doctors with Africa (CUAMM), Elizabeth Glaser Paediatrics Foundation (EGPAF), BRAC Maendeleo, Catholic Relief Services (CRS), Aga Khan Foundation, Plan International, International Rescue Committee, Bright Jamii Initiative, Amani Girls Home, ADD Tanzania, Compassion International, World Vision na SOS Children Village Tanzania kwa mchango wao mkubwa wa kitaalamu, kiutawala, na fedha kutoka mwanzo hadi mwisho wa zoezi la uandaaji wa programu hii.

Na mwisho, napenda kuwashukuru Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendelo ya Awali ya Mtoto Afrika – Nairobi (African Early Childhood Network - AfECN) kwa kutoa utaalamu elekezi wakiongozwa na wataalamu wa kitanzania ambao ni Josephine Ferla (kiongozi wa timu) akishirikiana na Elizabeth Macha na Arcard Rutajwaha na wataalamu kutoka Kenya ambao ni Lynette Okengo, Robina Omosa na George Owino katika uandaaji wa programu hii.

Napenda kutambua kwamba mchakato huu unatokana na mkutano wa taifa wa wadau wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto uliofanyika Disemba, 2018 na kusababisha uandaaji wa programu hii ambayo utekelezaji wake utaanza hivi punde. Mkutano huo ni juhudi za wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na serikali, wadau wa maendeleo na mashirika yasiyo ya kiserikali ambao kwa pamoja walitumia rasilimali zao katika kuandaa programu hii. Na sasa ninawaalika wadau wote kuendeleza ari na ushirikiano ulioonheshwa wakati wa uandaaji wa programu hii uendelee hadi wakati wa utekelezaji ili kufikia maono kuwa "Watoto wote wa Tanzania wapo kwenye mwelekeo sahihi wa kufikia ukuaji timilifu".

***Mh. Dkt. Dorothy O. Gwajima (MB)***
Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

# TAMKO LA UTAYARI

Sisi, Makatibu Wakuu kutoka Wizara husika za masuala ya MMMAM ambao tunaunda Kamati Elekezi ya Taifa, chombo cha juu cha utawala kinachosimamia Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM tunatambua kwamba hii ni programu muhimu katika kuhakikisha mahitaji ya watoto wote nchini yanapewa kipaumbele na kuwekewa rasilimali kwa ajili ya utekelezwaji. Hii itawezesha watoto wote Tanzania kuwa kwenye mwelekeo sahihi wa kufikia ukuaji timilifu kwa kuwajengea misingi ya kuwa watu mahiri wenye ujuzi na uwezo wa kuchangia maendeleo ya taifa pindi wanapokua watu wazima;

Tunayo imani kwamba programu hii ya taifa itatafsiri kwa vitendo Sera, Miongozo ya Taifa ya MMMAM na vipengele muhimu vya malezi jumuishi katika Mpango Mkakati unaosadifu malengo ya maendeleo endelevu na mikakati mingine ya kikanda ambayo Tanzania ni sehemu yake;

Tunakubali kwamba upo uwezekano wa kufikia malengo katika kushughulikia masuala jumuishi ya ukuaji na maendeleo ya watoto wenye umri kati ya miaka 0-8 pamoja na watoto walio katika mazingira hatarishi na wenye ulemavu kama hatua muhimu ya kuifikisha nchi kwenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025;

***HIVYO BASI, KWA SAINI ZETU ZILIZOAMBATISHWA HAPA CHINI TUNAO WAJIBU WA KUTEKELEZA YAFUATAYO:***

Tutachukua hatua stahiki kuhakikisha sera zetu za kisekta, mikakati, programu na bajeti zinazingatia mahitaji ya watoto wenye umri wa miaka 0-8;

Tutashiriki kikamilifu katika kuratibu, kutekeleza na kuhakikisha upatikanaji wa taarifa za programu kupitia kamati elekezi ya taifa ya MMMAM; na

Tutasimamia ipasavyo utekelezaji wa shughuli za Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM ambazo sekta zetu zimepewa kutekeleza.

***Dkt. John K. Jingu***
Katibu Mkuu (Maendeleo ya Jamii)
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

***Tixon T. Nzunda***
Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu
(Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)

***Prof. Riziki S. Shemdoe***
Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

***Prof. Abel Makubi***
Katibu Mkuu (Afya)
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

***Dr. Leonard Akwilapo***
Katibu Mkuu
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

***Emmanuel Tutuba***
Katibu Mkuu
Wizara ya Fedha na Mipango

***Christopher D. Kadio***
Katibu Mkuu
Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi

# Yaliyomo


UTANGULIZI ........ i

SHUKRANI ........ ii

TAMKO LA UWAJIBIKAJI ........ iii

VIFUPISHO VYA MANENO ........ vi

TAFSIRI YA MANENO ........ vii

ORODHA YA MICHORO NA MAJEDWALI ........ viii

MUHTASARI ........ ix

SURA YA 1: UTANGULIZI ........ 2

1.1 Maelezo ya utangulizi 2

1.2 Ulinganifu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM na Mfumo wa Kidunia wa Malezi Jumuishi wa Awali 2

1.3 Ushahidi wa kisayansi na sababu za kuwekeza katika Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto 3

1.4 Utashi wa kisiasa na jitihada za kushughulikia MMMAM: 4

1.5 Ulinganifu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM na ajenda ya kitaifa ya maendeleo 5

1.6 Maendeleo ya kiulimwengu katika kusaidia programu jumuishi za MMMAM: 5

1.7 Watekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM 7

1.8 Mchakato wa uandaaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM 7

SURA YA 2: UCHAMBUZI WA HALI NA MUKTADHA WA MKAKATI ........ 9

2.1 Muktadha wa maendeleo Tanzania 9

2.2. Maendeleo ya Rasilimali Watu 10

2.3 Kundi lengwa miaka (0 - 8) na walezi 10

2.4 Hali ya Malezi Jumuishi nchini Tanzania (miaka 0-8) 12

2.4.1 Afya Bora 12

2.4.2 Lishe ya Kutosha 14

2.4.3 Malezi yenye Mwitikio 17

2.4.4 Fursa za Ujifunzaji wa Awali 18

2.4.5 Ulinzi na Usalama 20

2.5 Masuala Mtambuka ya Watoto wa umri wa miaka 0-8 22

2.5.1 Msongo Unaohusiana na Uzazi 22

2.5.2 Mimba za Utotoni 22

2.5.3 Watoto wenye ulemavu 23

2.5.4 Watoto kwenye makazi maalumu (Wakimbizi na Malezi Mbadala) 23

2.5.5 Watoto Yatima 24

2.5.6 Kukabiliana na masuala ya Kijinsia yanayolenga watoto wenye umri wa miaka 0 - 8 24

2.5.7 Namna ya kuyafikia makundi maalumu. 25

2.6 Kwanini kumekua na uwekezaji mdogo wa masuala ya MMMAM katika sekta mbalimbali? 26

2.7 Ukosefu wa usawa katika kuwafikia walengwa 28

2.8 Wadau wa MMMAM nchini Tanzania 29

SURA YA 3: DHANA YA MFUMO WA PROGRAMU JUMUISHI YA TAIFA YA MMMAM........ 32

3.1 Misingi ya dhana ya Mfumo wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM 32

3.2 Nadharia ya mabadiliko 33

**SURA YA 4: MATOKEO TARAJIWA NA MIKAKATI YA KUYAFIKIA....................................... 37**

4.1 Miongozo ya Utekelezaji. 37
4.2 Matokeo tarajiwa, matokeo ya muda mrefu na matokeo ya muda mfupi 37
4.2.1 Kuboresha Mazingira wezeshi 38
4.2.2 Kuimarisha mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora 38
4.2.3 Kuongeza upatikanaji wa huduma bora na zilizoratibiwa vema kwa ajili ya watoto wenye umri wa mika 0-8. 38
4.2.4 Kuwawezesha walezi, wazazi na jamii kutoa huduma ya malezi jumuishi 38
4.3 Matokeo ya muda mrefu, mfupi na wa kati 39

**SURA YA 5: GHARAMA ZA UTEKELEZAJI WA AFUA ZA PROGRAMU JUMUISHI YA TAIFA YA MMMAM KATIKA MAENEO MUHIMU YA MATOKEO....................................... 55**

5.1 Utangulizi 55
5.2 Gharama za utekelezaji ili kuimarisha Programu jumuishi ya taifa ya MMMAM 58
5.2.1 Gharama za utekelezaji za Mazingira wezeshi yameboreshwa kuwezesha uratibu wenye ufanisi na utoaji huduma za malezi jumuishi 58
5.2.2 Gharama za utekelezaji za Mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora imeimarishwa 58
5.2.3 Gharama za utekelezaji wa Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma bora zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa Watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao 58
5.2.4 Gharama za utekelezaji wa kuwajengea uwezo Walezi, familia na jamii wa kutekeleza taratibu sahihi za Malezi jumuishi 58

**SURA YA 6: USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA PROGRAMU JUMUISHI YA TAIFA YA MMMAM....................................... 65**

6.1 Muhtasari 65
6.2 Mfumo wa Uongozi, Usimamaizi na Uratibu 65
6.3: Majukumu na wajibu wa wadau 67
6.4: Mahitaji ya Rasilimali Watu na Uwezo wa Kitaasisi. 67
6.5: Mpango kazi wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM 67

**SURA YA 7: UFUATILIAJI, TATHMINI, UWAJIBIKAJI NA UJIFUNZAJI................................ 70**

7.1 Muhtasari 70
7.2 Malengo ya Mfumo wa ufuatiliaji wa Sekta mbalimbali zinazotekeleza Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM 71
7.3 Mfumo wa pamoja wa matokeo, rasilimali na uwajibikaji (CRRAF) 71
7.4 Ufuatiliaji, Mapitio na Tathmini 72
7.5 Ujifunzaji na Utafiti wa Kiutendaji 72

**SURA YA 8: MPANGO WA UWEKEZAJI KIMKAKATI KWENYE PROGRAMU JUMUISHI YA TAIFA YA MMMAM ....................................... 74**

8.1 Muhtasari 74
8.2 Mahitaji ya kifedha ya Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM 77
8.3 Rasilimali fedha zilizopo na nakisi ya bajeti 79
8.4 Mpango wa kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali 79
8.5 Mkakati wa kuweka vipaumbele kutekeleza shughuli zilizopendekezwa 80

**SURA YA 9: UCHAMBUZI WA VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI NA MBINU ZA KUKABILIANA NAVYO ....................................... 82**

9.1 Uchambuzi wa Vihatarishi vya Utekelezaji 82
9.2 Mbinu za Kukabiliana na vihatarishi vya Utekelezaji 82

***Viambatisho* ....................................... 86**

Kiambatisho 1: Mpango wa Utekelezaji 86
Kiambatisho 2: Maelezo ya kina ya shughuli kwa kila matokeo 110
Kiambatisho 3 Mpango Uliowekewa bajeti Kamilifu 138
Kiambatisho 4: Mfumo wa Matokeo 212
Kiambatisho 5: Uchambuzi wa changamoto za utekelezaji na mbinu za kukabiliana nazo 221

# VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| *AZAKI* | Asasi za Kiraia |
| *MKUKUTA* | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania |
| *MMMAM* | Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto |
| *MTAKUWWA* | Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto |
| *OR TAMISEMI* | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| *OWM* | Ofisi ya Waziri Mkuu |
| *OWM-SUBKVAU* | Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu |
| *TAMISEMI* | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| *TECDEN* | Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto Tanzania |
| *TET* | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| *VVU* | Virusi vya UKIMWI |
| *WAJA* | Watoa Huduma za Afya Kwenye Jamii |
| *WAMJW* | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto |
| *WFM* | Wizara ya Fedha na Mipango |
| *WEST* | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |

# TAFSIRI YA MANENO

| | |
|---|---|
| *Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (MMMAM)* | Kwa muktadha huu ni hatua jumuishi zenye muunganiko wa vipengele vyote vya MMMAM katika ukuaji wa mwili, akili, lugha, kijamii, kitamaduni, kihisia na kimaadili[1]. |
| *Lishe toshelezi* | Inamaanisha ni usalama na uhakika wa chakula bora kinachotosheleza mahitaji ya mwili tangu kutungwa kwa mimba; |
| *Malezi yenye Mwitikio* | Inamaanisha mawasiliano na mwingiliano kati ya mzazi/mlezi wa mtoto na uwezo wa mzazi/mlezi kuitikaia hisia, ishara, mjongeo, sauti na maombi ya matamshi ili kushughulikia mahitaji ya mtoto kama vile ugonjwa, ulinzi, kujifunza, kujenga ukaribu na mshikamano |
| *Fursa za Ujifunzaji wa Awali* | Ni mazingira yanayoandaliwa kumsaidia mtoto kujifunza tangu kutungwa kwa mimba hadi umri wa miaka nane(8) kupitia uchangamani endelevu kati ya mtoto na mlezi ,mazingira ili kumsaidia kupata ujuzi na uwezo |
| *Ulinzi na Usalama* | Ni kuhakikisha Watoto walio katika mazingira hatarishi wanalindwa dhidi ya hatari za kimwili na za kihisia ambazo zinawazunguka. |

1 Sophie Naudeau et al., (2011) Investing in Young Children: An Early Childhood Development Guide for Policy Dialogue and Project Preparation. World Bank.

# ORODHA YA MICHORO NA MAJEDWALI


| | | |
|---|---|---|
| *Mchoro 1* | Mtazamo wa Kihistoria wa MMMAM Tanzania | *4* |
| *Mchoro 2* | Malengo ya Maendeleo Endelevu, yakilenga Maendeleo ya Awali na Viashiria vyake | *6* |
| *Mchoro 3* | Pengo lililopo kati ya huduma za afya na elimu kwa watoto wa miaka 0-8 | *11* |
| *Mchoro 4* | Ramani ya Tanzania ikionesha viwango vya udumavu miongoni mwa watoto wa umri wa 0 hadi miezi 59 | *15* |
| *Mchoro 5* | Kukidhi mahitaji ya familia na watoto | *26* |
| *Mchoro 6* | Wadau wanaotekeleza afua za MMMAM kwa mkoa | *30* |
| *Mchoro 7* | Mfumo wa utekelezaji wa kukuza maendeleo ya watoto kupitia mbinu ya sekta shirikishi | *33* |
| *Mchoro 8* | Nadharia ya Mabadiliko | *35* |
| *Mchoro 9* | Uratibu wa Programu Jumuishi ya taifa ya MMMAM, Ufuatiliaji na tathmini na muundo wa utekelezaji | *41* |
| *Mchoro 10* | Mgawanyo wa asilimia za bajeti ya programu kati ya malengo ya muda mrefu | *56* |
| *Mchoro 11* | Mfumo Jumuishi wa Taifa wa Uratibu wa MMMAM | *66* |
| *Mchoro 12* | Hali halisi ya kifedha | *75* |
| *Mchoro 13* | Matumizi ya fedha kuhusiana na MMMAM | *76* |

| | | |
|---|---|---|
| *Jedwali I* | ***Matokeo ya Muda mrefu 1:*** Mazingira wezeshi yameboreshwa kuwezesha uratibu wenye ufanisi na utoaji wa huduma za malezi jumuishi | *60* |
| *Jedwali II* | ***Matokeo ya Muda mrefu 2:*** Mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora imeimarishwa | *61* |
| *Jedwali III* | ***Matokeo ya Muda mrefu 3:*** Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma bora na zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa Watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao | *62* |
| *Jedwali IV* | ***Matokeo ya Muda mrefu 4:*** Wazazi, walezi, familia na jamii wamejengewa uwezo wa kutekeleza taratibu sahihi za malezi jumuishi | *63* |
| *Jedwali V* | Muhtasari wa Mahitaji ya Fedha kwa Ajili ya Kugharamia Utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM | *78* |
| *Jedwali VI* | Muhtasari wa uchambuzi wa changamoto za utekelezaji | *84* |
| *Jedwali VII* | Mpango wa Kukabiliana na Changamoto Zinazoweza Kujitokeza Wakati wa Utekelezaji | *85* |

# MUHTASARI

## Lengo la Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM

Kwa mujibu wa Takwimu za Taifa za Makisio ya Idadi ya Watu zilizotolewa na Idara ya Takwimu ya Taifa, Tanzania ina takribani watoto 16,524,201 (wavulana 8,328,142 na wasichana 8,196,056) wenye umri wa miaka 0 – 8 (ambao ni 30% ya watu wote). Hii inamaanisha kuwa katika kila watu watatu, kuna mtoto mmoja mwenye umri wa miaka 0 – 8. Kundi hili la watoto wadogo linahitaji kuangaliwa kwa karibu na kufanyiwa uwekezaji ili waweze kuwa rasilimali bora yenye tija kwa familia na taifa. Uwekezaji unaopaswa kufanyika ni pamoja na kukabiliana na tatizo la udumavu, kuwapa huduma bora za malezi ya awali na programu za elimu ambazo zitawawezesha kukua na kufikia ukuaji timilifu na hatimaye kuwa watu wazima wenye uwezo wa kufanya kazi za uzalishaji mali kwa tija na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi wa Tanzania pamoja na kujenga jamii yenye amani na utulivu.

Uwekezaji unaoratibiwa kwenye Maeneo Matano ya Mfumo wa Malezi Jumuishi ambayo ni Afya Bora, Lishe, Malezi yenye Mwitikio, Fursa za ujifunzaji wa Awali na Ulinzi na Usalama, utaongeza kasi ya mafanikio yanayopatikana katika Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (MMMAM) kwa kuimarisha ushirikiano wa wadau wa sekta mbalimbali katika utoaji wa huduma za Malezi Jumuishi kwa watoto. Uwekezaji katika huduma za MMMAM huwasaidia watoto kufikia upeo wa ukuaji timilifu, lakini pia unaleta faida kiuchumi kwani tafiti zimeonesha kuwa kwa kila Dola 1 ya Kimarekani inayowekezwa, kuna uwezekano wa kurudisha faida ya wastani wa hadi Dola 17 hapo baadaye.

***Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto*** itakayotekelezwa kuanzia mwaka 2021/22 hadi mwaka 2025/26 inalenga kuongeza kasi ya mafanikio yanayopatikana katika huduma za MMMAM kwa kuboresha ushirikiano wa kisekta katika utoaji wa huduma za malezi jumuishi kwa watoto. Programu hii itasaidia kuboresha uratibu wa huduma kwa kuimarisha utekelezaji wa sheria na sera zinazohusu masuala ya MMMAM ikiwa ni pamoja na Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, na Sera ya Afya ya mwaka 2007, ili kushughulikia kikamilifu mahitaji yote ya maendeleo ya watoto wenye umri wa miaka 0 – 8.

Programu hii inatoa wito kwa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali wa sekta mbalimbali, Wadau wa Maendeleo, na Asasi za Kiraia waweze kufanya kazi kwa ushirikiano katika kuhakikisha watoto wote (wenye umri wa miaka 0 – 8) nchini Tanzania wanapata huduma za Malezi Jumuishi, wanastawi na kufikia hatua za ukuaji timilifu. Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM inatambua programu zilizopo za kitaifa ambazo utekelezaji wake unajumuisha wadau wa sekta mbalimbali katika kutoa huduma zinazolenga vipengele vyote vya ukuaji na maendeleo ya mtoto. Pia programu hii inalenga kutumia uzoefu wa programu zilizopo. Mfano wa programu hizo ni Program Jumuishi ya Taifa ya Lishe II (2021/22-2025/26) na Mpango kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA, 2017/18 – 2021/22).

Aidha, Programu hii imezingatia Mpango wa tatu wa Taifa wa Maendeleo (2021/22-2025/26) ambao unalenga "Kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu". Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM inaenda sambamba na mpango wa Taifa wa maendeleo kwa sababu unalenga kufanya uwekezaji unaolenga maendeleo ya watu katika miaka ya mwanzo ya maisha yao (kuanzia kipindi cha ujauzito) ili kuwajengea watoto msingi imara wa kuwa nguvukazi yenye afya bora na tija wakati wanapofikia umri wa utu uzima, na hivyo kuweza kuchangia kikamilifu maendeleo ya taifa la Tanzania.

## Programu inalenga kushughulikia mahitaji yaliyoshindwa kutimizwa kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 8

Programu Jumuishi ya MMMAM ina lengo la kushughulikia mahitaji mahsusi yaliyotambuliwa baada ya kufanya uchambuzi wa hali halisi ya huduma za MMMAM kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 8 nchini Tanzania. Changamoto kubwa zilizobainika katika uchambuzi huo ni udhaifu wa mfumo wa uratibu na utoaji huduma sahihi za malezi jumuishi kwa watoto wenye umri wa miaka 0 - 8, zenye ubora na toshelevu, kwenye maeneo yote hapa nchini.

Hakuna usawa katika upatikanaji wa huduma za MMMAM kulingana na hali mbalimbali ikiwemo tofauti baina ya watoto wanaoishi mjini na vijijini; watoto wa kike na wakiume; watoto wanaotoka kwenye kaya masikini na zenye kipato; watoto wenye ulemavu na walio katika mazingira hatarishi. Dhana ya Mfumo wa Uchambuzi Unaozingatia Mtiririko wa Kimantiki ulitumika katika maandalizi ya programu hii kwa kuwashirikisha wadau wa sekta mbalimbali imezingatia afua za MMMAM zilizoonesha kuleta matokeo chanya nchini na duniani kwa ujumla. Dhana hiyo inatambua kuwa maendeleo ya watoto wadogo ni matokeo ya afua mbalimbali zinazohusisha wadau wa sekta mbalimbali. Afua hizo zinapaswa kutolewa kwa kuzingatia hali halisi ya huduma za Malezi Jumuishi za watoto wadogo, zinazolenga maeneo ya afya, lishe, fursa za ujifunzaji wa Awali, Malezi yenye mwitikio, ulinzi na usalama wa mtoto, kwa kutumia mifumo ya usimamizi na utoaji huduma iliyopo nchini.

Maandalizi ya Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM yaliongozwa na muunganiko wa Nadharia ya Mabadiliko na Mfumo wa Uchambuzi Unaozingatia Mtiririko wa Kimantiki. Nadharia hii inaonesha njia ya kufikia mabadiliko yanayotarajiwa.

Kwa ujumla, matokeo tarajiwa ya programu jumuishi ya taifa ya MMMAM ni kwamba mwisho wa miaka mitano ya utekelezaji wa Programu hii "Watoto wote wa Tanzania wapo kwenye mwelekeo sahihi wa kufikia ukuaji timilifu". Mabadiliko hayo yatapimwa kwa kuzingatia viashiria vya matokeo tarajiwa vilivyoainishwa na mipango mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ambavyo vimejengwa kwa kuzingatia viashiria kutoka kwenye mipango ya taifa ya sekta mbalimbali na vile vya Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM ina lengo la kushughulikia maeneo makuu manne ya mabadiliko ambayo yatachangia kuleta matokeo tarajiwa. Maeneo hayo ya matokeo ni:

*i.* Kuboresha Mazingira ya Utoaji Huduma ili kuwawezesha watoa huduma katika sekta mbalimbali zinazotoa huduma kwa watoto wadogo kupitia: Kuimarisha uhamasishaji wa masuala ya MMMAM katika ngazi zote ili kuongeza ushiriki wa wadau na upatikanaji wa huduma katika maeneo yote makuu ya Malezi Jumuishi, Kuimarisha uratibu wa wadau wa sekta mbalimbali, na kuandaa/kuboresha Sera, miongozo, mitaala na miongozo ya mafunzo vijumuishe vipengele vyote vya mfumo wa malezi jumuishi.

*ii.* Kuimarisha utoaji wa huduma na mifumo ya kuhakikisha ubora ili huduma za Malezi Jumuishi zitolewe kwa ubora na ufanisi na kuwafikia watoto wote wenye umri wa miaka 0 – 8 nchini Tanzania. Hii inajumuisha kuwawezesha watumishi kutoa huduma bora za Malezi Jumuishi; kuwepo kwa mfumo imara wa Ufuatiliaji na Tathimini, unaozingatia huduma za rufaa kutoka ngazi ya chini kwenda ngazi ya juu na kutoka ngazi ya juu kwenda ngazi ya chini; na matumizi ya takwimu kwa ufanisi ili kuwezesha utoaji wa huduma bora za malezi jumuishi

*iii.* Kuongeza upatikanaji wa huduma bora za malezi jumuishi zilizoratibiwa ili kuleta mabadiliko yanayotarajiwa. Huduma hizo zinahusisha kuongeza upatikanaji wa huduma bora za malezi yenye mwitikio, fursa za ujifunzaji wa awali, huduma bora za afya, huduma za lishe, na huduma za ulinzi na usalama wa watoto; na

*iv.* Kuwajengea uwezo walezi, familia na jamii ili watekeleze taratibu bora za malezi jumuishi kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 8. Familia na jamii wanahitaji kujengewa uwezo ili waelewe na kuchukua hatua stahiki kutokana na umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wadogo katika kipindi hicho ili kuwajengea msingi imara wa maisha yao ya baadaye.

## Malengo ya Ufuatiliaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM

Ufuatiliaji wa programu jumuishi ya taifa ya MMMAM utafanyika kwa kuhakikisha kuwa malengo yaliyopangwa yamezingatia mfumo wa Malezi jumuishi na viashiria vinavyokubalika duniani. Viashiria hivyo vitajumuishwa kwenye mfumo wa ufuatiliaji wa viashiria vya Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mkakati wa Dunia wa Afya ya Wanawake, Watoto na Vijana Balehe ambao nchi ya Tanzania imeridhia kutoa taarifa zake hadi kufikia mwaka 2030. Mfumo wa kukusanya taarifa za matokeo ya programu jumuishi ya taifa ya MMMAM umejumuisha viashiria vikuu 4 vya Matokeo ya muda mrefu na viashiria 31 vya Matokeo ya muda mfupi ambavyo vitapimwa na kutolewa taarifa katika kipindi cha miaka miwili (2023/24) kufuatia kuanza kwa utekelezaji wa programu na katika mwaka wa mwisho wa utekelezaji (2025/26).

## Ujumuishi wa sekta mbalimbali katika Programu ya Taifa ya MMMAM

MMMAM ni programu jumuishi inayoongozwa na kanuni za Mfumo wa Malezi Jumuishi katika utoaji huduma za Malezi kwa watoto. Kwa ushahidi wa mfumo wa malezi jumuishi ambao umethibitika kutoa matokeo chanya, mfumo huu umezingatia hali halisi nchini katika kushughulikia mahitaji ya malezi jumuishi ili kuleta matokeo chanya yanayotarajiwa.

Mfumo jumuishi unahusisha wadau wa sekta mbalimbali (afya, lishe, elimu, ulinzi na usalama, maji na usafi wa mazingira); kwa kufanya kazi katika ngazi zote (Taifa, Mkoa, Halmashauri, Kata na Kijiji/Mtaa) na kushirikiana na wadau mbalimbali (Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Wadau wa Maendeleo – wakiwemo Mashirika ya Umoja wa mataifa/Mashirika Binafsi ya Misaada/Mashirika ya Misaada ya Serikali za Nchi Mbalimbali, Taasisi zisizo za Kiserikali, Mashirika ya Kijamii, Taasisi za Elimu na Sekta Binafsi).

Utekelezaji wa Programu jumuishi ya taifa ya MMMAM unaongozwa na kanuni za Mfumo wa Malezi Jumuishi ambazo ni: Haki ya mtoto kuishi na kustawi, kwa kuhakikisha kuwa haki za watoto zinatambuliwa na kuetekelezwa; Kutomuacha hata mtoto mmoja nyuma, kwa kuhakikisha kuwa huduma zinapatikana kwa watoto wote wenye umri wa miaka 0 – 8; Huduma kwa familia, zinazolenga kufikia mahitaji ya familia nzima ili ziweze kusaidia upatikanaji wa mahitaji ya watoto; Uwajibikaji wa Serikali, kwa kuwezesha sekta zote zinazotoa huduma za Malezi Jumuishi kufanya kazi katika mfumo unaoratibiwa kwa ushirikiano, hivyo kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma zenye ubora zinazowafikia watoto wote; na Ushiriki wa jamii, hii inahusisha ushiriki kamili wa jamii nzima ikiwa ni pamoja na Serikali, Asasi za Kiraia, Taasisi za Elimu, Sekta Binafsi, Familia na wadau wengine wa MMMAM.

Uchambuzi wa vihatarishi vya utekelezaji ni suala muhimu katika mchakato wa kuandaa mipango. Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM ina muundo wa usimamizi wa vihatarishi uliochambua vihatarishi vinavyoweza kujitokeza na kupendekeza mikakati ya kukabiliana navyo kwa kuzingatia malengo makubwa manne (4). Kila kihatarishi kilichobainishwa kimewekewa mkakati wa kukikabili.

## Uongozi na Menejimenti ya Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM

Ofisi ya Waziri Mkuu (OWM) itaongoza na kuratibu utekelezaji wa Programu kwa kutoa maelekezo kuhakikisha huduma za MMMAM zinapewa kipaumbele, hususani huduma za malezi yenye mwitikio na fursa za ujifunzaji wa awali kwa kujumuishwa kwenye programu mbalimbali. Ujumuishaji wa vipengele vya malezi jumuishi kwenye kamati elekezi inayoratibu masuala ya lishe na kamati tendaji za wataalam itafanyika ili kuepuka masuala hayo kujumuishwa kwenye kamati zaidi ya moja.

Wizara, Idara na wakala wa Serikali watahakikisha kuwa vipengele vyote muhimu vya MMMAM vinajumuishwa kwenye sera, mikakati, programu, kanuni na miongozo inayosimamiwa na sekta zao, pamoja na kutenga rasilimali za kugharamia afua za kisekta katika programu hii. Utekelezaji katika ngazi ya Mkoa, Halmashauri, Kata na jamii, utakuwa chini ya uratibu wa sekta husika. Ufuatiliaji na uratibu utajumuishwa kwenye mifumo iliyopo katika ngazi zote za Serikali za Mitaa. Kwa majumuku iliyonayo Ofisi ya Rais – TAMISEMI, itahakikisha huduma za MMMAM zinaratibiwa, watoa huduma wanasimamiwa, huduma zinafanyiwa ufuatiliaji na tathmini mara kwa mara katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na wadau wengine itaratibu, itahamasisha na kuhakikisha kuwa rasilimali za utekelezaji zinapatikana. Pia itahakikisha kuwa inatoa usimamizi wa kitaalam wa kimkakati kusaidia Serikali, sekta zote na wadau waliotambuliwa kwenye programu hii.

## Ufuatiliaji na Tathmini ya Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM

Mfumo wa matokeo ya programu hii utatumika kutoa mwongozo wa ufuatiliaji (Angalia Kiambatisho 4). Hatua mahsusi za ufuatiliaji na tathmini zitafanyiwa tathmini kupitia mbinu zifuatazo:

*i.* Kanzi data jumuishi ya MMMAM iliyo katika mfumo wa dashibodi kufuatilia viashiria vya malezi jumuishi kutoka katika mifumo mbalimbali ya ukusanyaji taarifa itatengenezwa. Takwimu za huduma zinazotolewa mara kwa mara zitakusanywa kutoka kwenye mifumo iliyopo ikiwemo DHIS2 na BEST ambapo viashiria vipya vya malezi yenye mwitikio na fursa za ujifunzaji wa awali vitaingizwa kwenye kanzi data zilizopo.

*ii.* Kikao cha ngazi ya juu cha wadau wa MMMAM cha mwaka kitapokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa programu kutoka ngazi ya kijiji hadi taifa.

*iii.* Mapitio ya utekelezaji wa programu yatafanyika katikati ya kipindi cha utekelezaji 2023/24. Tathmini mahususi ya utekelezaji wa programu itafanyika.

*iv.* Tathmini ya mwisho ya Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM itafanyika mwaka 2025/26, ikijumuisha taarifa zitakazopatikana kwenye Utafiti wa Hali ya Kidemografia na Afya – Tanzania utakaofanyika mwaka 2025/26.

## Gharama za utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM

Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM imejumuisha Mpango wa Utekelezaji wenye maeneo makuu manne ya matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa. Mpango wa utekelezaji unaonesha kiasi cha rasilimali fedha zinazohitajika kufanikisha utekelezaji kwa kipindi cha miaka mitano, kwa kila eneo kuu la matokeo. Kwa ujumla, utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM utagharimu Shilingi 914,991,351,636 za Tanzania. Bajeti ya ya programu hii imetenga asilimia 76 ya fedha kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa huduma za malezi jumuishi zenye ubora. Kiasi kilichobaki cha asilimia 24 kimetengwa kwa ajili ya huduma zinazosaidia utekelezaji wa programu ikiwemo kujenga mazingira wezeshi, kuimarisha mifumo mbalimbali ya utoaji huduma na utoaji wa elimu kwa jamii wakiwemo wazazi.

## Mpangilio wa andiko la Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM

***Sura ya 1:*** Muhtasari wa programu, ikijumuisha maneno muhimu yaliyotumika, umuhimu wa programu na jinsi inavyohusiana na programu nyingine za kitaifa ikiwa ni pamoja na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

***Sura ya 2:*** Muhtasari wa hali halisi ya huduma kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 8 nchini Tanzania kwa kuzingatia vipengele vikuu vitano (5) vya malezi jumuishi ambavyo ni (afya, lishe, malezi yenye mwitikio, ujifunzaji wa awali, na Ulinzi na usalama wa mtoto). Sura hii imetambua pia upungufu uliopo katika utekelezaji na fursa zinazoweza kutumiwa ili kuboresha utoaji wa huduma.

***Sura ya 3:*** Mpango wa dhana iliyotumika kuandaa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM ikijumuisha umuhimu wa programu na shughuli zinazopendekezwa kutekelezwa kufikia mabadiliko yanayotarajiwa.

***Suya ya 4:*** Matokeo makuu yanayotarajiwa ya Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM, ikiwa ni pamoja na malengo mahsusi na mikakati itakayotumika.

***Sura ya 5:*** Gharama za jumla za Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM na gharama za maeneo makuu manne (4) ya matokeo ya muda mrefu.

***Sura ya 6:*** Usimamizi na uratibu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM pamoja na maelezo ya awali, uongozi na mifumo ya uratibu. Vilevile, inaonesha watendaji muhimu, wajibu na majukumu yao, mahitaji ya rasilimali watu na kujenga uwezo wa kitaasisi.

***Sura ya 7:*** Mfumo wa ufuatiliaji, tathmini, uwajibikaji na mafunzo. Inatambulisha matokeo makuu yanayotarajiwa, rasilimali zinazohitajika na mfumo wa uwajibikaji. Sura hii pia inaelezea mchakato utakaotumika kufanya ufuatiliaji, mapitio na tathmini ya Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM. Tafiti za kiutendaji zitajumuishwa ili kuboresha programu.

***Sura ya 8:*** Mpango wa uwekezaji wa kimkakati kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Programu, uchambuzi wa kina wa gharama, na nakisi ya bajeti. Sura hii pia inaonesha mkakati wa kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali za utekelezaji.

***Sura ya 9:*** Vihatarishi na mbinu za kukabiliana navyo.


Barbie

# *SURA YA 1:* UTANGULIZI

## *1.1 Maelezo ya utangulizi*

Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, ambayo inatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2021/22 hadi 2025/26 (Kiambatisho na 1- Mpango wa utekelezaji) inalenga kuharakisha upatikanaji wa matokeo chanya ya maendeleo ya awali ya mtoto kwa kuboresha mfumo shirikishi wa kisekta katika malezi jumuishi ya watoto. Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM inasaidia utekelezaji wa mifumo ya uratibu kwa kuleta pamoja sheria na sera mbalimbali zinazohusiana na malezi na makuzi ya mtoto, ikiwemo Sheria ya Mtoto Na. 21 ya 2009, Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya (2008) Sera ya Elimu na Mafunzo (2014) na Sera ya Afya (2017) kwa lengo la kushughulikia mahitaji jumuishi ya maendeleo ya mtoto wa umri wa miaka 0-8. Programu hii inawaleta Wadau wote kutoka katika Sekta mbalimbali, wadau wa Maendeleo na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, asasi za kiraia kufanyakazi kwa pamoja ili kuhakikisha Watoto (0-8) nchini Tanzania wanapata Malezi jumuishi, ustawi na kufikia maendeleo timilifu. Programu hii inatambua uwepo wa Programu nyingine za kitaifa ambazo zinatumia mfumo shirikishi wa Kisekta katika maendeleo ya Mtoto ikijumuisha Programu Jumuishi ya Taifa ya Lishe (NMNAP – 2016/2021) na Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA 2017/18-2021/22). Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM itachangia programu za kitaifa zilizopo kwa kuimarisha fursa zilizo ainishwa na kushughulikia mapungufu yaliyopo ili kuboresha utoaji wa huduma jumuishi za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto wote (umri wa miaka 0-8) nchini.

## *1.2 Ulinganifu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM na Mfumo wa Kidunia wa Malezi Jumuishi wa Awali*

Programu Jumuishi ya MMMAM imeandaliwa ili kuendana na mfumo wa kimataifa wa malezi jumuishi ya awali (Nurturing Care Framework – 2018) ambao unapendekeza huduma jumuishi na shirikishi ili kuhakikisha watoto na familia wakiwemo wale wenye mahitaji mbalimbali kama wenye maambukizi ya virusi vya ukimwi, wavulana na wasichana, wenye utapiamlo, wenye ulemavu, familia maskini na watoto wanaishi kwenye taasisi za uangalizi na huduma nyingine za kibinadamu, nao pia wanafikiwa na huduma maalumu na za kutosha. Mwongozo unatambua uwepo wa majukwaa na huduma zilizopo ikiwemo mifumo jumuishi ya kiafya na majukwaa ya ujifunzaji wa awali na huchagiza mifumo na wadau kufanya kazi tofauti tofauti kupitia ushirikiano wa kisekta ili kujumuisha vipengele vyote vya malezi jumuishi ya awali ili kuimarisha maendeleo jumuishi kwa Watoto wote kwa kuzingatia mahitaji yao. Utumiaji wa njia tofauti tofauti ni muhimu katika kupanua wigo wa upatikanaji wa matokeo ya afua za maendeleo ya Watoto. Vipengele vitano vya malezi jumuishi ya awali ni; (1) Afya bora ya mtoto na walezi 2) Lishe Bora tangu kutungwa kwa mimba; 3) Malezi yenye Mwitikio; 4) Fursa za ujifunzaji wa awali; na 5) Ulinzi na Usalama wa mtoto. Ili kufikia lengo lake katika kutoa malezi jumuishi ya awali, mfumo unapendekeza utekelezaji wa maeneo matano ya kimkakati ambayo ni; i) kuongoza na kuwekeza ambayo inahitaji uongozaji wa kiserikali katika sera, fedha, na uratibu katika kusaidia utekelezaji wa huduma jumuishi za MMMAM; ii) kuzingatia familia na jamii zao katika kuandaa mbinu zifaazo kimuktadha kuwawezesha jamii katika nyanja za malezi jumuishi ya awali ambayo pia husaidia kujenga uhitaji; iii) Kuimarisha huduma kwa kutambua majukwaa na nguvu kazi ya kitaifa iliyopo ili, ikiwezeka kutoa huduma kufuatilia maendeleo kwa kuandaa mbinu za kupima maendeleo katika viashirikia vyote vya malezi jumuishi ya awali na kuandaa viashiria pale ambapo havipo; na; v) kutumia takwimu na ubunifu kwa kufanya tafiti za ndani, kuweka kumbukumbu ya utendaji wa kufaa na kubaini njia bunifu kusambaza huduma za malezi jumuishi ya awali na kujenga uwajibikaji [2].

[2] WHO (2018) Nurturing Care Framework for Early Childhood Development: A Framework for helping children survive and thrive to transform health and human potential.

Wakati Malezi Jumuishi ya Awali yanatilia mkazo utendaji unaoendana na muktadha na huduma zitolewazo kuhakikisha watoto wadogo wanastawi na kuhuishwa, neno MMMAM ni pana zaidi, likishughulikia nyanja jumuishi za maendeleo ya mtoto ambazo zinahitaji kushughulikiwa kupitia huduma za malezi jumuishi ya awali. Inatambulika pia kuwa MMMAM ni neno linalojulikana zaidi linalotumika katika muktadha mbalimbali. Kutokana na hayo maneno yote mawili (malezi jumuishi ya awali na MMMAM) yatakuwa yakitumika yakiwa na maana moja katika muktadha huu.

## 1.3 *Ushahidi wa kisayansi na sababu za kuwekeza katika Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto*

Kuna tafiti chache au ushahidi mdogo kuhusiana na masuala ya MMMAM ambazo zimefanyika kwa ngazi ya taifa. Tafiti mbalimbali za kisayansi duniani zinasisitiza kwamba msingi imara unatakiwa ujengwe katika miaka ya awali ya mtoto na kwamba huu ndio wakati muhimu wa kuwekeza kwenye maisha ya mwanadamu. Imedhihirika kuwa, kwa kila dola moja iliyotumika katika afua za MMMAM, kuna matokeo makubwa yanayopatikana yanayokadiriwa kufikia dola za kimarekani 17[3] . Aidha, Ushahidi unaonyesha uwekezaji katika elimu ya awali kwa watoto walio katika mazingira hatarishi ina manufaa yanayokadiriwa kuwa asilimia 7 hadi 16 kwa mwaka[4] chanzo cha rasilimali watu ni kuwekeza katika miaka ya awali ya mtoto. Ukuaji wa ubongo wa mtoto unajengwa kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha miaka 5 ya awali ya ukuaji, ni wakati yakinifu kwani ufanyaji kazi wa ubongo unakuwa katika hatua ya juu ya ukuaji wake[5] . Kimsingi huduma saidizi katika sekta zote ni muhimu katika maendeleo ya mtoto katika kipindi hiki muhimu cha ukuaji wa ubongo wake. Tafiti zinasisitiza kuelekeza usaidizi kwenye huduma jumuishi za MMMAM ni mkakati bora wenye usawa kwa kuwa Watoto walio kwenye mazingira hatarishi, na wale wanaokumbana na vihatarishi mbalimbali wananufaika zaidi na huduma jumuishi za MMMAM. Watoto wanaopata usaidizi katika hatua ya awali ya makuzi, wameandaliwa mazingira chanya ya uwezekano wa kuboresha afya zao, elimu, mahusiano ya kijamii na mafaniko ya kiuchumi katika Maisha yao ya baadaye. Watoto ambao hawapati huduma hizi muhimu za MMMAM, wanashindwa kukuza msingi muhimu wanaouhitaji katika maendeleo na huwa na matumaini madogo ya mafanikio yao ya baadaye[6] . Kumbuka kuwa programu za ziada zitakazotolewa baadae katika maisha, zina gharama kubwa na matokeo yasiyoridhisha. Kiuhalisia sio tu ushawishi kwenye matokeo ya uwekezaji, bali gharama ya kutokufanya maamuzi ni kubwa kwa mtu binafsi na jamii kwa ujumla. Makadirio ya hasara ya wastani wa kipato cha mtu kwa mwaka kwa watoto walio kwenye hatari ya kutofikia utimilifu wa maendeleo yake inaweza kufikia asilimia 26, kupelekea kuporomoka kiuchumi na familia kuwa kwenye umaskini. Katika ngazi ya jamii, gharama za kutochukua hatua ya kuondoa udumavu kufikia kiwango cha asilimia 15 au chini ya hapo na kutoshughulikia ucheleweshaji wa maendeleo katika shule za awali na ziara za majumbani inakadiriwa mara kadhaa kuwa zaidi ya kile ambacho nchi nyingine wanatumia kwenye afya na elimu.[7]

[3] Camaione, D & Muchabaiwa, B (2021) Quantifying Heckman: Are Governments in Eastern and Southern Africa Maximizing Returns on Investments in Early Childhood Development? United Nations Children's Fund (UNICEF), Eastern and Southern Africa Regional Office (ESARO)

[4] WHO (2018) Nurturing Care Framework for Early Childhood Development: A Framework for helping children survive and thrive to transform health and human potential.

[5] WHO (2018) Nurturing Care Framework for Early Childhood Development: A Framework for helping children survive and thrive to transform health and human potential.

[6] Heckman, J. J. (2008) The Case for Investing in Disadvantaged Young Children, CES if DICE Report, ISSN 1613-6373.

[7] Heckman, J. J. (2008) The Case for Investing in Disadvantaged Young Children, CES if DICE Report, ISSN 1613-6373.

## 1.4 Utashi wa kisiasa na jitihada za kushughulikia MMMAM

Uhamasishaji wa huduma jumuishi za MMMAM nchini Tanzania ulianzishwa mwaka 2004 kupitia usaidizi wa Shirika la kuhudimia Watoto Duniani (UNICEF) na majadiliano ya ngazi ya juu ya uhitaji wa mifumo jumuishi, ikizingatiwa masuala ya MMMAM yalikuwa kwa kiwango fulani yamejumuishwa katika sera za kisekta za kijamii[8] . Ushirikishwaji wa ngazi ya juu kati ya serikali na wadau mbalimbali juu ya MMMAM ilipelekea maendeleo muhimu yakijumuisha; uzinduzi wa kikundi kazi kinachojumuisha asasi za kiraia na wadau wengine wa MMMAM; uundwaji wa mtandao wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (TECDEN) na urasimishwaji wake kama mtandao wa MMMAM kitaifa mwaka 2004; kufanyika kwa uchambuzi wa hali ya MMMAM na uchambuzi wa kisera; ujumuishwaji wa Nyanja za MMMAM kwenye mpango mkakati wa Tanzania kwa ukuaji na upunguzaji wa umaskini (MKUKUTA) 2005 – 2010; kufanyika kwa tafiti za majaribio juu ya moduli jumuishi za MMMAM na uanzishwaji wa kamati ya ushauri wa masuala ya MMMAM kitaifa na kamati ya kitaalamu ya MMMAM iliyopo chini ya ofisi ya Waziri mkuu (OWM-TAMISEMI) mwaka 2006. Jitihada za utoaji huduma shirikishi za MMMAM zilizinduliwa 2007 na kutekelezwa na wizara husika kwa wakati huo, ambazo ni, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu, Sayansi na Ufundi, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Miongoni mwa matokeo makuu ni maendeleo ya rasimu jumuishi ya sera ya MMMAM (2011/12) na kuitisha mkutano wa Kitaifa wa pili wa MMMAM mwaka 2012 ambapo Mawaziri wenye dhamana ya MMMAM walijidhatiti kuwekeza zaidi kwenye MMMAM katika sekta husika. Mtazamo huu wa kihistoria umeoneshwa katika jedwali na 1.

***Mchoro namba 1:*** Mtazamo wa Kihistoria wa MMMAM Tanzania[9]




Aidha, pamoja na azimio lililosainiwa mwaka 2012, hapakuwepo na uzatiti kamilifu wa afua za MMMAM zilizolenga watoto wenye umri wa miaka 0 hadi 8, kulingana na sera endelevu, mikakati na hatua zinazo tegemea Ushahidi, zenye ufanisi na zenye matokeo ambazo zinatekelezwa katika viwango, uratibu mzuri, rasilimali na kufuatiliwa. Katika kushughulikia changamoto hii, majadiliano yalianzishwa tena mwaka 2017 na Shirika la Children in Crossfire (CiC) wakishirkiana na TECDEN na wadau wengine katika mifumo ya kuboresha ushirikiano

[8] UNICEF (2007) Joint integrated Early Childhood Development (MMMAM) Service delivery Initiative.

[9] United Nations International Children's Fund (UNICEF) (2009) MMMAM internal briefing notes, 2009-2012.

wa kisekta katika utekelezaji wa shughuli za MMMAM. Kongamano la wadau lilifanyika Dodoma mwaka 2018, ambapo limepelekea uhitaji wa kuandaa -Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM pamoja na bajeti na mfumo wa ufuatiliaji kama azimio la msingi. Katika mchakato huo kikosi kazi cha taifa cha MMMAM kiliundwa mwaka 2018 kikijumuisha serikali, wawakilishi kutoka mawakala mbalimbali, asasi za kiraia na wadau wengine watekelezaji wakiongozwa na WAMJW na TECDEN kama sekretarieti.

## *1.5. Ulinganifu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM na ajenda ya kitaifa ya maendeleo*

Katika kutekeleza sera mbalimbali za kitaifa zinazo husiana na masuala ya MMMAM zilizoelezewa awali, Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM inajibu mpango wa tatu wa kitaifa wa miaka mitano (FYDP-III) ambao lengo lake kuu ni kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025[10].Malengo ya mpango wa tatu wa Taifa ni pamoja na Tanzania kuingia kwenye kundi la nchi zenye uchumi wa kati huku ikiendelea kuimarika kwa kuwa na uchumi wa viwanda wenye maendeleo ya watu au kiwango cha juu cha hali ya maisha. Pale itakapo yafikia malengo yake Tanzania inatarajiwa kuwa na sifa zifuatazo: Amani, utulivu, umoja, utawala bora, jamii iliyoelimika na yenye ari ya kujiendeleza pamoja na uchumi imara unaoweza kuhimili ushindani, wakati huohuo wenye kuwafaidisha walio wengi[11]. Mpango huo natumia viashiria vinavyoendana na MMMAM ikijumuisha kupunguza vifo vya watoto, kupunguza udumavu na kuongeza kiwango cha uandikishaji watoto katika shule za awali. Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM unaendana na Mpango wa taifa wa maendeleo wa miaka mitano (5) wa II kwa kuwekeza katika ukuaji wa binadamu kutoka miaka ya awali (tangu ujauzito) inajenga msingi imara kwa mtoto kuwa mtu mzima mwenye afya, anayewajibika na mwenye tija. Mwanzo mzuri katika maisha huanza kwa kuwekeza katika rasilimali watu kama vile kupunguza vifo vya watoto, kondoa udumavu, na kuwekeza katika programu bora za malezi na elimu. Aidha unapelekea kuwa na jamii yenye afya, lishe toshelezi , na inayowajibika, na kuwa na watu wazima wenye tija katika kukuza uchumi na pia kuwa na jamii yenye amani na utulivu. Vilevile hupelekea kupungua kwa magonjwa, kupungua kwa uhalifu, kupungua kwa idadi ya watoto wanaoacha shule na kuwa idadi ndogo ya watu wazima ambao hawajapata elimu Hivyo, kuongezeka kwa kipato na kupunguza gharama za huduma za kijamii utasaidia kusukuma ukuaji wa uchumi.

## *1.6 Maendeleo ya kiulimwengu katika kusaidia programu jumuishi za MMMAM*

Kumekuwa na ongezeko la jitihada na msukumo ulimwenguni katika kushughulikia maendeleo ya awali ya mtoto kupitia mifumo na miongozo tofauti ikilenga afua jumuishi (mfano, mipango ifuatayo: *The Lancet: Advancing Early Childhood Development 2007, 2011, 2016; Every Woman, Every Child 2010; Sustainable Development Goals 2015; Nurturing Care Framework 2018; Education 2030 Framework for Action 2015; World Bank Human Capital Initiative 2018).* Zaidi ya hapo, nchi 75 zinatumia sera za kisekta za MMMAM; G20 walijumuisha jitihada za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto 2018; na Mkataba wa Kimataifa wa Haki ya Mtoto unaendelea kuwa msingi wa kufikia matamanio hayo[12] . UNICEF ESAR Framework for Action 2019-2021 unatoa mwongozo wa kikanda kwa maamuzi ya kimkakati ya MMMAM kwa kuweka mkazo kwenye mifumo jumuishi ya sekta mbalimbali inayoendana na mfumo wa malezi jumuishi inayozingatia ustawi wa walezi na malezi yenye mwitikio katika kutoa huduma ya za MMMAM[13] . Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM kwa Tanzania inaenda sambamba na kuitikia mikakati hii ya ulimwengu.

Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kwa sasa ni ajenda ya ulimwengu ambapo huduma za MMMAM zinatambulika kuwa muhimu katika kufikia Malengo ya Maendeleo

[10] Ministry of Finance and Planning (2021) The National Five Years Development Planning 2021/22 – 2025/26.

[11] Ministry of Finance and Planning (2021) The National Five Years Development Planning 2021/22 – 2025/26.

[12] Early Childhood Development Action Network (2020) Draft strategic Plan (2020 – 2023).

[13] Early Childhood Development Action Network (2020) Draft strategic Plan (2020 – 2023).

[14] WHO (2018) Nurturing Care Framework for Early Childhood Development: A Framework for helping children survive and thrive to transform health and human potential..

Endelevu ya Dunia (SDGs). Malengo ya Maendeleo Endelevu hutoa fursa muhimu katika kufikia usawa kwa watoto wote ulimwenguni, yanayowezesha kuchangia kwenye Maisha endelevu na salama[14] . Kila nchi inatarajiwa kufanyia kazi kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo 2030, ambapo kuna matumaini na matarajio kwenye uwekezaji katika afua za MMMAM. Zaidi ya hapo, Malengo ya Maendeleo Endelevu yanaweka mkazo kwenye maeneo mbalimbali ya maendeleo ya mtoto kama ilivyo ainishwa kwenye mchoro namba 2. Kati ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ambayo yanahusiana moja kwa moja na MMMAM, ni lengo namba 4 ambalo linahimiza Serikali kuhakikisha elimu bora shirikishi na yenye usawa na kuhamasisha ujifunzaji endelevu maishani. Lengo hili, linaipa kazi Serikali kuhakikisha kuwa hadi kufikia mwaka 2030, wasichana na wavulana wote wanafikiwa huduma bora za maendeleo ya awali, malezi na elimu ya awali ili kuwa tayari kwa elimu ya msingi. Ilisisitizwa pia, kupitia kushughulikia masuala ya MMMAM katika njia jumuishi, kutatoa fursa zaidi za kushughulia Malengo Endelevu 17 yaliyobaki ambayo yamelenga "kutokomeza umaskini na njaa, kutunza utu na usawa, kulinda dunia, kutunza rasilimali za asili, kudumisha maendeleo ya kiuchumi, na kukuza jamii yenye amani, haki na shirikishi. Kwa mfano, katika lengo na 1: kutokomeza umaskini, ambapo kuwekeza kwenye miaka ya awali kunapelekea manufaa makubwa kiuchumi; lengo na 2: kutokomeza njaa na kuboresha lishe; kukiwa na Ushahidi ukionesha matokeo bora ya lishe yanatokana na ujumuishaji wa uchangamshi wa awali na lishe kuliko kuwa afua zinazojitegemea[15]. Tanzania ni moja ya watia saini wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, ikimaanisha kuwa taifa litapimwa kwa mujibu wa viashiria vilivyotajwa. Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM inasaidia mwitiko wa nchi kwenye viashiria hivyo, hususani vile ambavyo kwa sasa havifuatiliwi au kupimwa na serikali kama vile fursa za ujifunzaji wa awali kabla ya elimu ya awali na malezi yenye mwitikio.

***Malengo ya Maendeleo Endelevu, 2030***

***Mchoro namba 2:*** Malengo ya Maendeleo Endelevu, yakilenga Maendeleo ya Awali na Viashiria vyake[16]




[15] WHO (2018) Nurturing Care Framework for Early Childhood Development: A Framework for helping children survive and thrive to transform health and human potential.

[16] Early Childhood Development Action Network (MMMAMAN) (2020) Draft Strategic Plan (2020 – 2023).

## 1.7 Watekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM

Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM inalenga wadau wote wa MMMAM ambao wamegawanyika katika makundi makuu matatu: 1) Watoa Maamuzi katika ngazi zote (ngazi ya taifa hadi ya jamii), ikijumuisha watendaji wa kitaalamu ambao wanahusika kwenye uandaaji wa sera, mipango, ugawanyaji rasilimali, na utetezi; 2) maafisa wote muhimu katika ngazi za utekelezaji na utoaji huduma katika ngazi zote; na 3) Wafadhili, wadau wa maendeleo, Asasi Za Kiraia, Mashirika Binafsi na Taasisi zinginezo zinazojishughulisha na masuala ya MMMAM.

## 1.8 Mchakato wa uandaaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM

Mchakato wa uandaaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM ulianzishwa na serikali ya Tanzania na Kikosi kazi cha MMMAM kama makubaliano tekelezi katika Jukwaa la Taifa la wadau wa MMMAM ulifanyika mwaka 2018. Uandaaji wa Programu hii umekuwa shirikishi ukihusisha wadau mbalimbali kwa kutumia mbinu mbalimbali. Umeongozwa na timu ya wataalamu kwa kushirikiana na idara zote za serikali zinazojihusisha na masuala ya MMMAM na kikosi kazi cha taifa cha MMMAM (ambacho kinajumuisha serikali na AZAKI) kuhakikisha kwamba uandaaji wa programu unamilikiwa na serikali na wadau mbalimbali wa MMMAM, Jamii na kushawishi utekelezaji wenye ufanisi na endelevu. Pia, mchakato ulihusisha upembuzi wa nyaraka muhimu zinazohusiana na MMMAM, kubaini mapungufu na fursa zilizopo kwa ajili ya kusaidia uandaaji wa Programu. Wadau wanaotekeleza masuala ya MMMAM walitambuliwa kwa kuonesha maeneo ya kijiografia wanayotekeleza huduma na huduma wanazotoa zinazohusiana na Mfumo wa Malezi Jumuishi, rasilimali fedha zilizopo na muda wa miradi. Majadiliano na wadau muhimu yalifanyikaPia, Mchakato ulihusisha idadi kadhaa ya mikutano ya majadiliano ya ana kwa ana na washiriki kutoka maeneo mbalimbali ya nchi na uwakilishi kutoka Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Taasisi, wadau wa maendeleo na mashirika yasiyo ya kiserikali ya kitaifa na kimataifa, Asasi za Kiraia, Taasisi za elimu ya juu na wadau wengine wa MMMAM. Hii ilijumuisha mikutano ya majadiliano ya kubuni programu na shughuli zitakazotekelezwa.. Kwenye mchakato mzima, serikali pamoja na kikosi kazi cha taifa cha MMMAM wamekuwa wamiliki wa andiko la programu pamoja na na matokeo yake.



# *SURA YA 2:* UCHAMBUZI WA HALI NA MUKTADHA WA MKAKATI

Sura hii inaelezea muhtasari wa matokeo ya uchambuzi wa hali halisi uliofanywa wakati wa kuandaa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM. Uchambuzi ulipitia huduma, sera, na miongozo iliyopo kuhusiana na afua za utoaji wa huduma za MMMAM kwa watoto walio katika umri wa miaka 0 - 8 kwa kuzingatia mfumo wa Malezi Jumuishi hapa nchini. Mchakato ulichambua sera na afua mahususi zinazofikia makundi maalum kulingana na umri, pamoja na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi; Vilevile mchakato umebaini fursa na changamoto zilizopo katika kuboresha huduma za malezi jumuishi hapa nchini.

## *2.1 Muktadha wa maendeleo Tanzania*

a. ***Maendeleo ya Kiuchumi:*** Tanzania imetambuliwa kuwa nchi ya pato la kati ngazi ya chini ya pato la taifa baada ya ongezeko la kutoka dola 1,020 mwaka 2018 hadi dola 1,080 mwaka 2019 kwa kichwa. Haya ni matokeo ya kasi ya ukuaji wa uchumi wa takribani ya asilimia sita (6%) ya pato la Taifa kwa muongo uliopita. Hata hivyo, kuingia ngazi ya chini ya uchumi wa kati kwa Tanzania kabla ya malengo ya mwaka 2025 ni mafanikio. Ili kujumuisha na kuchangia lengo kuu la ukuaji wa uchumi, nchi bado inahitaji kuwekeza katika maeneo anuwai kama vile miundombinu na rasilimali watu[17] . Uwekezaji katika rasilimali watu utaongeza upatikanaji wa huduma bora za afya, lishe, elimu, usawa wa kijinsia na kukuza ujuzi wa wafanyakazi; uwekezaji katika rasilimali watu unaharakisha kufikia dhamira ya upatikanaji wa ajira zenye tija na kasi ya ukuaji wa uchumi.

b. ***Umasikini:*** Licha ya ongezeko la kasi la ukuaji wa Pato la Taifa, uwekezaji katika rasilimali watu umekuwa changamoto na hivyo kuchangia kuzorotesha kasi ya kupunguza umasikini. Umasikini wa mahitaji ya msingi ulioripotiwa na utafiti wa bajeti ya kaya umepungua kutoka asilimia 28.2 kwa mwaka 2011/2012 mpaka 26.4 katika mwaka 2017/18 kukiwa na tofauti kubwa ya idadi ya watu maskini mijini na vijijini (asilimia 81 ya watu masikini huishi vijijini ikilinganishwa na asilimia 19 katika miji). Ingawa umasikini wa jumla umepungua, ni muhimu kuzingatia kuwa umasikini katika maeneo ya miji umeongezeka kutoka asilimia 15.9 katika mwaka 2011/12 mpaka asilimia 19 katika mwaka 2017/18, kwa mgawanyiko wa watu masikini mkoani Dar es Salaam ikiongezeka mara dufu kutoka asilimia 1.5 hadi asilimia 3.0.

Utafiti huo wa bajeti ya kaya ulionesha kuwa mkoa wa Mwanza una idadi kubwa zaidi ya watu masikini wasio na mahitaji ya msingi, wakati mkoa wa Njombe una idadi ndogo zaidi[18]. Ongezeko la idadi ya watu pia linaripotiwa kuchangia kupunguza kasi ya kutokomeza umaskini[19] , huku Tanzania ikiwa ni kati ya mataifa yanayokua kwa kasi zaidi ulimwenguni na ongezeko la asilimia 3.0 ya idadi ya watu kila mwaka. Sensa ya watu na makazi ya Tanzania ya mwaka 2012 ilionesha kuwa, jumla ya idadi ya watu Tanzania bara ni milioni 44.9 (Asilimia 51.3 ni wanawake na asilimia 48.7 ni wanaume) na inakadiriwa kuwa miongoni mwa nchi tano za Afrika zitakazokua na idadi kubwa zaidi ya watu katika ukanda huo ifikapo 2100[20] .

[17] Battaile, W (2020) What does Tanzania' move to Lower Middle Income status mean? Worldbank Africa

[18] Ministry of Finance and Planning – Poverty Eradication Division (MoFP – PED) Tanzania Mainland and National Bureau of Statistics (NBS) 2019. Tanzania Mainland Household Budget Survey 2017 – 18, Key indicators Report, Dodoma, Tanzania

[19] World Bank Group (2019) Tanzania Economic Update: Human Capital – The Real Wealth of Nations.

[20] UN World Population (2020) By Numbers, Population shift: Countries with the largest number of people

## 2.2 Maendeleo ya Rasilimali Watu

Uwekezaji wa rasilimali watu ni muhimu kwa maendeleo ya taifa na ina uhusiano wa moja kwa moja na vipengele vya MMMAM yenye muunganiko na Malengo ya dunia ya Maendeleo Endelevu . Kuanzishwa kwa mradi wa kuwekeza katika Rasilimali Watu na Benki ya Dunia kunahimiza serikali mbalimbali kuwekeza kwa watu katika viwango anuai ili kufikia kiwango cha juu kabisa cha uzalishaji. Kiashiria cha rasilimali Watu kinapima tija kwa wakati ujao, kikilenga watoto na vijana, rasilimali watu ambapo mtoto aliyezaliwa leo anabashiriwa mafanikio yake ya baadaye. Kipimo hiki kinazingatia hatari zilizopo zinazoweza kuathiri mafanikio ya mtoto ikiwa ni pamoja na afya duni, hali ya lishe, umri wa kuishi na kiwango cha elimu pamoja na ubora wake katika nchi mahususi anayoishi mtoto. Kipimo cha kufikia kiwango cha uzalishaji wa juu ni kati ya 0 - 1; ambapo thamani ya 1 inaashiria nchi kufanya vyema katika eneo la lishe ya watoto, ubora wa elimu inayotolewa, na uwezekano wa kuishi. Tanzania inakadiriwa kuwa na kiashiria cha ubora wa rasilimali watu 0.4 ikimaanisha kuwa kiwango cha uzalishaji ni 0.4 tu. Kiwango cha rasilimali watu cha Tanzania kiko chini ikilinganishwa na nchi zingine za Afrika kama vile Visiwa vya Shelisheli (0.68), Mauritania (0.63), Kenya (0.52), Gabon (0.45) na Zimbabwe (0.44). Inawezekana kufikia kiwango cha juu cha uzalishaji endapo kutakuwa na dhamira ya dhati ya kuwekeza katika MMMAM, kwa mfano katika nchi kama Singapore ambayo ina uwekezaji mkubwa zaidi kwa watu wake kiwango cha 0.88 ambayo ni zaidi ya mara mbili ya kiwango cha uwekezaji wa Tanzania[21]. Viashiria vinavyochangia kufafanua utendaji hafifu wa uwekezaji kwa watu nchini Tanzania ni pamoja na kiwango cha vifo vya watoto chini ya miaka 5 (vifo 67 kati ya vizazi hai 1000 mwaka 2015/16); vifo vya wajawazito (556 kati ya vizazi hai 100,000 mwaka 2015/16); kiwango cha udumavu kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka 5 (asilimia 32 kwa mwaka 2018), na uwepo wa programu chache sana za elimu ya awali zinazolenga watoto wenye miaka 0 - 3.

Gharama za kutokuchukua hatua za kuboresha maendeleo ya watoto kupitia afua za MMMAM hupanda sana katika maeneo yenye huduma chache, na pia katika mazingira ambapo kiwango cha juu cha watoto walio katika hatari ya kutokufikia hatua timilifu za ukuaji. Kutokana na chapisho la lancet, asilimia 43 ya watoto walio kwenye hatari ya kutokufikia ukuaji wao timilifu wapo kwenye hatari ya kushusha wastani wa kipato chao kwa asilimia 26 watakapofikia utu uzima ambacho kitashusha hali ya uchumi na kuweka familia kwenye mtego wa umaskini.

Katika ngazi ya jamii, gharama ya kutokuwekeza katika kupunguza kiwango cha udumavu kwa asilimia 15 au chini ya hapo, na kutoshughulikia ukuaji hafifu wa watoto kupitia utoaji wa elimu ya awali katika vituo vya kulelea watoto wadogo, gharama yake ni kubwa ikilinganishwa na uwekezaji unaofanywa na nchi nyingine kwenye eneo la afya au elimu[22].

## 2.3 Kundi lengwa miaka (0 - 8) na walezi

Ushahidi wa kisayansi unaonesha ni muhimu kuwekeza mapema kwa mtoto, kwa kuwa ukuaji unaanza wakati wa kutungwa kwa mimba hadi miaka nane (miaka 0-8) ambacho ni kipindi cha ukuaji zaidi. Inawezekana kutabiri hali ya baadaye ya mtoto na taifa kwa ujumla kupitia msisitizo uliowekwa kwenye utekelezaji wa programu ya MMMAM yenye ufanisi. Kwa kuzingatia idadi kubwa ya vijana wa Tanzania (asilimia 43.9 chini ya miaka 15; ***na watoto wadogo wa miaka 0 - 9 ambayo ni asilimia 31 ya idadi ya watu wote***[23]***)***, inaleta mashaka kuona kwamba kundi kubwa la watu liko kwenye hatari ya kutofikia uwezo kamili wa maendeleo huku likikabiliwa na uwezekano mkubwa wa kupata udumavu na umasikini wa hali ya juu, hali inayohitaji mipango ya haraka ili kuhakikisha mahitaji yao ya maendeleo yanashughulikiwa vya kutosha. Inaripotiwa kuwa hatari ya kutoshughulikia mapungufu haya mapema itaendeleza athari kwa kundi hilo, kwa mtu binafsi na taifa kwa sasa na hata kwa vizazi vijavyo. Mtu yeyote aliye na mwanzo duni wa maisha anaweza kuendelea kuwa na afya mbaya, lishe duni na kukosa fursa za ujifunzaji ambao unaweza kusababisha kuwa na kipato cha chini wakati wa utu uzima. Ushahidi wa kisayansi unatabiri upo uwezekano wa kundi la watoto wenye mwanzo duni kupoteza takribani robo ya mapato ya baadaye endapo

[21] World Bank Group (2019) Tanzania Economic Update: Human Capital- the real wealth of the nation

[22] Lancet series (2016) Advancing Early Childhood Development: from Science to Scale 1: Early childhood development coming of age: science through the life course

[23] National Bureau of Statistics (2013) Population distribution by age and sex, Dar es salaam Tanzania

hawatakua na mwanzo mzuri kuwezesha kufikia hatua timilifu za ukuaji[24] . Kwa ujumla hali hii inachangia upotevu mkubwa wa pato la taifa. Uchambuzi wa hali hii unaonesha pengo la ufikishaji wa mahitaji muhimu (usambazaji hafifu) wa huduma kati ya makundi ya umri tofauti, ambapo kwa watoto wenye umri wa miaka 0 - 2 msisitizo upo kwenye afya na lishe, hali kadhalika huduma watoto wenye umri wa miaka 5 msisitizo unahamia kwenye huduma za elimu na ulinzi . Tafiti zinaonesha kuwepo kwa programu chache za MMMAM zinazolenga watoto wenye umri wa miaka 3 hadi 4.

***Mchoro namba3:*** Pengo lililopo kati ya huduma za afya na elimu kwa watoto wa miaka 0 - 8[25]




Vilevile, uwekezaji katika programu ya MMMAM ni moja ya uwekezaji bora na wa busara zaidi ambao nchi zinaweza kufanya kwa sababu miaka ya mwanzo ya mtoto hufungua fursa ya kipekee ya kushughulikia changamoto za usawa kati ya mtu na mtu, kuvunja mzunguko wa umaskini, na kuboresha namna mbali mbali za matokeo bora maishani.

Maandalizi ya Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM nchini Tanzania yamekuja wakati muafaka ili kushughulikia mapungufu yaliyopo, ikizingatia ushahidi wa kisayansi, kiuchumi, na kuenda sambamba na harakati zilizopo ulimwenguni ambazo tayari zimeshika kasi. Shughuli jumuishi za MMMAM zimedhihirika kutekelezwa kwa ufanisi kutokana na utumiaji rasilimali zilizopo (watu na fedha) na kutoa fursa kwa wadau kuchangia utekelezwaji wake[26].

[24] WHO & UNICEF (2016) Advancing Early Childhood Development: from Science to Scale: An Executive Summary from The Lancet's Series. The Lancet

[25] Hughes R et al (2019) THRIVE-TZ: Opportunities for DFID Tanzania to invest in human capital in early childhood and adolescence

[26] Lancet series (2016) Advancing Early Childhood Development: from Science to Scale 1: Early childhood development coming of age: science through the life course.adolescence

## 2.4 Hali ya Malezi Jumuishi nchini Tanzania (miaka 0-8)

### 2.4.1 Afya Bora

Serikali ya Tanzania kupitia Sera ya Afya 2007 imewekeza sana katika kuboresha uhai wa mtoto kupitia utoaji wa huduma bure za afya kwa kina mama wajawazito na watoto chini ya miaka 5. Mpango Mkakati wa Taifa wa Kuboresha Afya ya Uzazi, Mzazi, Mtoto, na Vijana nchini Tanzania (2016-2020) umeweka mazingira wezeshi ya kupunguza magonjwa, vifo vya akina mama, watoto wachanga, watoto na vijana kwa kutoa huduma bora, endelevu na jumuishi zinazowafikia watu wote katika ngazi mbali mbali za utoaji huduma katika vituo vya afya na kwenye jamii. Hivyo basi matokeo ya afya za wanawake na watoto yameendelea kuwa bora. Taarifa za tafiti za TDHS-MIS za 2015-16 zinaonesha mafanikio makubwa ya asilimia 98.9 ya mahudhurio ya mama wajawazito waliohudumiwa na wataalamu mwenye ujuzi kutoka asilimia 96 mnamo mwaka 2010. Kuanza kwa wakati mahudhurio ya kliniki kwa wajawazito katika miezi mitatu ya kwanza ni asilimia 24, na 51 ya wanawake wajawazito kuhudhuria mara nne au zaidi kama inavyopendekezwa na WAMJW. Halikadhalika, asilimia 63 ya watoto wanazaliwa katika vituo vya afya na haya ni matokeo bora ikilinganishwa na taarifa za TDHS iliyopita ambapo ni asilimia 50 tu[27]. Mwelekeo wa chanjo za msingi kwa watoto wenye umri wa miezi 12-23 nao unaonesha ongezeko kutoka asilimia 71 mnamo mwaka 2010 hadi asilimia 75 mnamo mwaka 2015/2016.

Uwekezaji wa Serikali katika uhai wa mtoto unaonekana dhahiri kwenye kupungua kwa vifo vya watoto kati ya mwaka 2010 na 2015 ambapo kiwango cha vifo vya watoto wachanga (0-28 days) vimepungua kutoka vifo 40 hadi 25 kwa kila vizazi hai 1,000; kiwango cha vifo vya watoto wachanga (28 days - 11 months) kupungua kutoka vifo 99 hadi 43 kwa kila vizazi hai 1,000; na kiwango cha vifo vya watoto chini ya miaka 5 (12-59 months) vimepungua kutoka vifo 147 hadi 67 kwa kila vizazi hai 1,000. Kinacholeta wasiwasi ni kwamba mafanikio ya awali katika afya ya mama na ustawi yameonekana kuongezeka kwa uwiano wa vifo vya akina mama kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mnamo mwaka 2015/16 ikilinganishwa na vifo 454 kwa kila vizazi hai 100,000 mnamo 2010[28]. Jambo lingine ni ufuatiliaji baada ya kujifungua ambao unamlenga mama na mtoto siku za mwanzo ili kuzuia na kugundua mapema shida yoyote na kushauri juu ya uzazi wa mpango, chanjo, kunyonyesha na huduma za malezi yenye mwitikio, pamoja na huduma zingine. Aidha, inataarifiwa kuwa karibu asilimia 60 ya vifo vya akina mama na karibu robo tatu (asilimia 75) ya vifo vya watoto wachanga hutokea wakati wa wiki ya kwanza baada ya kujifungua. Aidha, takwimu za hivi karibuni zinaonesha kuwa jumla ya asilimia 66 ya akina mama hawapati huduma inayopendekezwa ndani ya siku 2 baada ya kujifungua[29]. Kwa ujumla, licha ya juhudi hizi za uhai wa mama na mtoto, viwango vya vifo bado vipo juu sana. Kwa kuongezea, dhana ya Mfumo wa Malezi Jumuishi ni kuona kuwa watoto wote sio tu wanaishi lakini pia wanastawi na kufikia hatua zao timilifu za ukuaji.

Tanzania ina watoto na watu wazima milioni 1.7 wanaoishi na VVU na mnamo 2019 kulikuwa na maambukizi mapya ya VVU 77,000 nchini (Makadirio ya VVU ya UNAIDS 2020). Ukatili, lishe duni na uyatima huongeza hatari ya udumavu na maambukizi ya VVU. Watoto walioambukizwa VVU na watoto waliopata athari za maambukizi ya VVU wapo kwenye hatari kubwa ya kupata matatizo ya afya ya akili na pia kuwa na lishe duni wakilinganishwa na watoto ambao hawajapata athari hizo[30]. Pia kuna unyanyapaa dhidi ya watoto na watu wazima wanaoishi na VVU ambao unahitaji kushughulikiwa, kupitia programu za MMMAM.

[27] Ministry of Health, Community development, Gender, Elderly and Children (MoHCDGEC) (2019) National guideline for Neonatal Care and Establishment of Neonatal Care Unit. Reproductive and Child Unit.

[28] MoHCDGEC (2016) Tanzania Demographic Health Survey and Malaria Indicator Survey (TDHS-MIS) 2015 – 2016

[29] Ministry of Health, Community development, Gender, Elderly and Children (MoHCDGEC) (2016). The National Road Map strategic plan to improve reproductive, maternal, newborn, child and adolescent health in Tanzania (2016 - 2020): ONE PLAN II

[30] Rollins, N. (2018). Early childhood development among HIV exposed uninfected children. IAS. 6. Knox, J.; Arpadi, S.M., Kauchali, S., et al. (2018). Screening for developmental disabilities in HIV positive and HIV negative children in South Africa: Results from the Asenze Study. PLOS One. 13(7).

Kwa mujibu wa Utafiti wa Kitaifa wa Athari ya VVU wa mwaka 2018, idadi ya wanawake wote waliohudhuria kliniki ya wajawazito sawa na asilimia 98.9, kati yao asilimia 92.4 walishauriwa juu ya hali yao ya maambukizi ya VVU. Aidha, kati ya wale ambao walipima na kuonekana na maambukizi ya VVU, asilimia 97.9 walishauriwa kutumia dawa za kupunguza makali ya VVU (ARVs)[31]. Makadirio yanaonyesha kuwa maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yamepungua hadi asilimia 8 (2015) na kuongezeka hadi kufikia (asilimia11) mnamo mwaka 2020 kulingana na makadirio ya UNAIDS dhidi ya malengo ya ulimwengu ya asilimia 5. Afua zilizotekelezwa kupitia mpango wa Kuzuia Maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT) zimeleta mafanikio makubwa ambapo idadi ya wanawake wajawazito wanaotumia ARV imeongezeka kutoka asilimia 29 (2010) hadi asilimia 93 (2018); na utambuzi wa watoto wachanga wenye maambukizi umeongezeka kutoka asilimia 10 (2010) hadi asilimia 44.8 (2018)[32]. Hata hivyo, taarifa bado zinaonesha kuwa ni asilimia 69 tu ya watoto walio chini ya umri wa miaka 15 ambao wanaishi na VVU wanapokea ARV. Kuna haja ya kuboresha utambuzi na uandikishaji katika huduma na matibabu ya VVU ili kuhakikisha watoto hawa wanapata huduma na matunzo stahiki. Kwa kuwa kuna watoto wengi zaidi waliozaliwa na akina mama wanaoishi na VVU, kuna haja ya kuchukua hatua ya kuhakikisha kuwa watoto hawa pia wanastawi ili kufikia uwezo wao wa ukuaji kama watoto wengine, kwa kuunganisha huduma za VVU na malezi jumuishi. Hivi karibuni Shirika ya Afya Duniani (WHO) na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) walitoa muhtasari wa sera ya malezi na makuzi ili kuhimiza nchi juu ya kujumuisha masuala ya malezi na makuzi sehemu zote muhimu za huduma za VVU[33]. Hii ni kutambua hatari kubwa inayowakabili watoto walio na VVU kushindwa kufikia hatua zao timilifu za ukuaji.

Kulingana na desturi za usafi binafsi na wa mazingira (WASH), taarifa ya TDHS ya 2015/2016 inaonesha kuwa ni asilimia 61 tu ya kaya nchini Tanzania wanapata vyanzo vya maji ya kunywa vilivyoboreshwa huku kukiwa hakuna mgawanyo sawa kijiografia (asilimia 86 ya kaya za mijini ikilinganishwa na asilimia 49 ya kaya za vijijini). Hii inawakilisha ongezeko la upatikanaji wa vyanzo vya maji vilivyoboreshwa kama ilivyoripotiwa, (asilimia 57 mnamo 2010). Kuhusu usafi wa mazingira, bado kuna changamoto kubwa. Ni asilimia 19 tu ya kaya zilizo ripotiwa katika kipindi cha 2015/16, kuwa zinatumia vyoo bora na bila kuchangia na kaya nyingine, na moja kati ya kaya 10 hazina choo kabisa[34]. Vilevile, asilimia 80 ya kaya hazina utaratibu mzuri wa usafi wa mazingira na utupaji salama wa kinyesi[35], na hivyo watoto wanaoishi katika kaya hizo wako kwenye hatari kubwa ya kupata magonjwa ya kuambukiza. Hatari ya maambukizi ya magonjwa miongoni mwa watoto imeongezeka kwa kaya chache sawa na asilimia 2.7 wanaripotiwa kutumia sabuni wakati wa kunawa mikono angalau mara mbili[36]. Desturi hizo duni za usafi binafsi na usafi wa mazingira mara nyingi husababisha magonjwa hatari kama vile kuhara. Kuhara huathiri asilimia 12 ya watoto chini ya miaka mitano. Kwa kuwa kuharisha kunachangia hadi asilimia 50 ya utapiamlo kwa watoto[37], ni wazi kuwa hii ni changamoto kubwa itakayosababisha watoto kutofikia hatua zao timilifu za ukuaji.

Katika kupitia afua za afya zinazolenga watoto wenye umri zaidi ya miaka 3 (yaani miaka 3 - 8) hakuna afua mahsusi zinazotekelezwa kwa kundi hili. Huduma muhimu za kiafya za watoto wadogo kama vile chanjo hukamilika kwa umri wa miaka 2. Ingawa huduma zingine kama vile ufuatiliaji wa ukuaji, nyongeza ya kawaida ya vitamini A, vidonge vya minyoo na usimamizi jumuishi wa magonjwa ya utotoni unaendelea hadi miaka 5, uzoefu unaonyesha kuwa wazazi mara nyingi huacha kuleta watoto wao kwenye kliniki ya mama na mtoto (RCH) mara baada ya kumaliza chanjo mtoto akifikia miaka 2. Machapisho yaliyopo yanaonesha kuwa, programu za huduma ya afya na lishe, maalum kwa watoto wenye umri wa miaka 3-5 hazijapewa msisitizo mkubwa ikilinganishwa na zile zenye kulenga watoto chini ya miaka 2 na hivyo kutozingatia faida kubwa ya ukuaji wa haraka na maendeleo yanayotokea katika umri huo. Vilevile, huduma nyingi za afya zinaishia katika umri wa miaka 5, hili ni pengo linaloendelea na kuwafikia hadi hufaidika na hatua kama vile mgao wa vyandarua vilivyowekewa dawa vya kuzuia malaria, huduma za VVU na maboresho ya sekta

[31] National Bureau of Statistics & TACAIDS (2018) Tanzania HIV Impact Survey

[32] UNAIDS (2019) HIV data

[33] WHO & UNICEF (2020) Nurturing care for children affected by HIV

[34] MoHCDGEC (2016) Tanzania Demographic Health Survey and Malaria Indicator Survey (TDHS-MIS) 2015–2016

[35] MoHCDGEC (2016) Tanzania Demographic Health Survey and Malaria Indicator Survey (TDHS-MIS) 2015–2016

[36] MoHCDGEC (2016) Tanzania Demographic Health Survey and Malaria Indicator Survey (TDHS-MIS) 2015–2016.

[37] Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children (MoHCDGEC) [Tanzania Mainland], Ministry of Health (MoH) [Zanzibar], Tanzania Food and Nutrition Centre (TFNC), National Bureau of Statistics (NBS), Office of the Chief Government Statistician (OCGS) [Zanzibar] and UNICEF, 2018. Tanzania National Nutrition Survey using SMART Methodology (TNNS) 2018. Dar es Salaam, Tanzania: MoHCDGEC, MoH, TFNC, NBS, OCGS, and UNICEF.

ya afya ambayo yanakwenda sambamba na kuwekeza rasilimali katika sekta ya afya ambayo inaongoza fursa kupata matibabu kwenye vituo vya afya vya serikali. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa afua mahsusi kwa kundi hili zitaleta muunganiko mzuri kwenye huduma za vijana balehe kwa kuwa vijana hawa wanatazamwa kama kundi maalumu kuhusiana na vipengele vya maendeleo ya mwanadamu.

### 2.4.2 Lishe ya Kutosha

Jitihada za kushughulikia hali ya lishe ya watoto nchini zimekuwa na mafanikio makubwa kupitia afua maalum za kuboresha lishe (Scaling Up Nutrition - SUN) ambazo ni harakati za kimkakati zinajumuisha wadau mbalimbali.

***a) Udumavu:***

Kwa maboresho yaliyoonekana kwenye taratibu za lishe kwa watoto wachanga na watoto wengine wadogo ni pamoja na unyonyeshaji na lishe ya vyakula vya ziada kuwa ni sababu muhimu zilizochangia katika kupunguza kiwango cha udumavu kitaifa kutoka asilimia 34.7 mnamo mwaka 2015 -16 (TDHS-MIS) hadi asilimia 31.8 mwaka 2018 (TNNS). Licha ya maboresho hayo, ni muhimu kutambua kuwa udumavu mkali bado unaathiri mtoto mmoja kati ya watoto kumi (asilimia 10.0) nchini kote, hii inamaanisha kwenye kila watoto kumi wa umri chini ya miaka 5, 1 anaripotiwa kua na udumavu mkali. Hii inaashirika kwamba watoto milioni tatu walio chini ya miaka mitano nchini Tanzania wamedumaa. Athari ya udumavu inahusishwa na watoto kutokufikia hatua kamilifu za ukuaji na hali hii huongezeka kulingana na umri hadi kufikia asilimia 40 au zaidi kwa watoto wenye umri wa miezi 18- 47. Mtoto mmoja kati ya sita mwenye umri wa miezi 24-35 wana udumavu mkali. Mikoa iliyoathirika kwa udumavu zaidi ya asilimia 40 ni: Njombe (asilimia 53.6), Rukwa (asilimia 47.9), Iringa (asilimia 47.1), Songwe (asilimia 43.3), Kigoma (asilimia 42.3) na Ruvuma (asilimia 41.0) kama ilivyooneshwa kwenye ramani kwenye Mchoro 4 hapa chini. Nchini Tanzania kiwango cha utapiamlo sugu bado kipo juu na suala linalotia mashaka ikizingatiwaa kuwa udumavu ni viashiria mojawapo kinachosababisha watoto kutofikia hatua timilifu za ukuaji.

[37] Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children (MoHCDGEC) [Tanzania Mainland], Ministry of Health (MoH) [Zanzibar], Tanzania Food and Nutrition Centre (TFNC), National Bureau of Statistics (NBS), Office of the Chief Government Statistician (OCGS) [Zanzibar] and UNICEF, 2018. Tanzania National Nutrition Survey using SMART Methodology (TNNS) 2018. Dar es Salaam, Tanzania: MoHCDGEC, MoH, TFNC, NBS, OCGS, and UNICEF.

*Mchoro namba 4:* Ramani ya Tanzania ikionesha viwango vya udumavu miongoni mwa watoto wa umri wa 0 hadi miezi 59




### *b) Lishe kwa watoto wachanga na wadogo:Unyonyeshaji na Ulishaji watoto vyakula vya nyongeza:*

Japokuwa karibu watoto wote (asilimia 96.6) wenye umri wa miezi 0-23 wamewahi kunyonyeshwa, bado ipo haja ya kuboresha kwa kuanza kunyonyesha mtoto saa moja baada ya kuzaliwa ni asilimia 53.5. Vilevile unyonyeshaji pekee wa maziwa ya mama kwa watoto wa miezi 0-6 ni asilimia 58. Pia kuna upungufu mkubwa wa unyonyeshaji katika mwaka wa pili, ambapo asilimia 92.2 ya watoto waliendelea kunyonyeshwa kwa mwaka wa kwanza ikishuka hadi asilimia 43.3 kwa miaka miwili kama inavyopendekezwa. Wakati huo huo, asilimia 92 ya watoto wenye umri wa kati ya miezi 6 hadi 8 walianzishiwa vyakula vya ziada kwa wakati unaofaa[38] .

Ili kufikia vigezo hivyo viwili: Idadi ya chini ya milo inayohitajika kwa siku na makundi ya vyakula mchanganyiko anavyopewa mtoto ni muhimu ili kudhibiti changamoto ya udumavu miongoni mwa watoto wenye umri chini ya miaka miwili. Takwimu za hivi karibuni zinaonesha ongezeko katika utoaji wa makundi mchanganyiko ya vyakula kwa watoto wenye umri wa miezi 6-23 kutoka asilimia 24.5 mnamo mwaka 2015-16 hadi asilimia 35.1 mwaka 2018, ikifuatiwa na kuongezeka kwa idadi ya watoto waliopata idadi ya chini ya milo inayohitajika kwa siku ambayo iliongezeka kutoka asilimia 39 mnamo mwaka 2015- 16 hadi 57.4 mwaka 2018. Vivyo hivyo, idadi ya watoto waliopata kiwango cha chini cha lishe inayokubalika imeongezeka kutoka asilimia 9 mnamo 2015-16 hadi kufikia asilimia 30.3 ilipofika mwaka 2018.

[38] Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children (MoHCDGEC) [Tanzania Mainland], Ministry of Health (MoH) [Zanzibar], Tanzania Food and Nutrition Centre (TFNC), National Bureau of Statistics (NBS), Office of the Chief Government Statistician (OCGS) [Zanzibar] and UNICEF. 2018. Tanzania National Nutrition Survey using SMART Methodology (TNNS) 2018. Dar es Salaam, Tanzania: MoHCDGEC, MoH, TFNC, NBS, OCGS, and UNICEF.

Vilevile watoto wenye umri wa miaka 3 - 4 wanakabiliwa na hatari ya kuwa na uzito wa chini, ambapo tatizo hilo limeathiri  asilimia 14.4-16.6 ya kundi hilo, kiwango ambacho ni juu ya wastani wa kitaifa wa asilimia 14.7%. Mlo wa familia ni kipengele muhimu katika kuhakikisha lishe ya kutosha kwa kundi hili. Hata hivyo, hakuna takwimu za kitaifa juu ya vyakula vinavyotumiwa mahususi kwa watoto wa miaka 2 - 8. Taarifa za mgawanyiko wa watu wanaokabiliwa na umasikini wa chakula zinaweza kutoa vielelezo muhimu, kama ilivyoripotiwa na utafiti wa bajeti ya kaya wa 2018. Aidha, mikoa minne yenye viwango vya juu zaidi vya udumavu (Njombe, Iringa Songwe, na Ruvuma) ni miongoni mwa mikoa ambayo ina umaskini mdogo wa chakula kitaifa.

Kuna uwezekano mkubwa kwa watoto ya vijijini kuwa na lishe duni kuliko wale wa maeneo ya mijini. Virutubisho ni muhimu kwa kuboresha ukuaji na maendeleo ya mtoto, hata hivyo upungufu wa damu ni hali inayosababishwa na uhaba wa madini chuma mwilini ambao unaathiri takribani watoto watatu kati ya watano wenye umri wa miezi 6-59 wakiwemo zaidi ya asilimia 45 ya watoto wenye umri wa miaka 3-4 ambapo walio vijijini ndio waathirika zaidi[39]. Upatikanaji wa nyongeza ya virutubisho haitoshi ambapo ni asilimia 63.7 tu ya watoto wenye umri wa miezi 6-59 waliopata nyongeza ya Vitamini A, ni asilimia 59 tu ya watoto wenye umri wa miezi 12-59 waliopewa vidonge vya minyoo[40].

#### *c) Ukondefu*

Kiwango cha ukondefu kimeshuka sana duniani, ambapo kimepungua kutoka asilimia 3.8 (mwaka 2014) hadi asilimia 3.5 (2018) (TNNS), takwimu hizo zimeainishwa kama kiwango cha chini kulingana na vigezo vinavyo tambulika duniani. Hatahivyo watoto wenye umri miezi 12-23 wameathiriwa zaidi kwa asilimia 5.5. Mkoa wa Singida ambao unaonekana kuwa na kiwango kikubwa cha ukondefu kwa  asilimia 5.2 ikilinganishwa na mikoa mingine, unahitaji  programu za MMMAM ili kusaidia kupunguza tatizo hilo.  Programu Jumuishi a taifa ya MMMAM inatoa fursa ya kuimarisha utoaji wa huduma za malezi yenye muitikio ambazo ni muhimu kwa uhai wa watoto hawa.

Kama ilivyo kwa afua za Afya na Lishe, mapitio ya taarifa yameonesha kuwa miradi mingi imelenga kundi la watoto wa umri wa miaka 0-2, jambo ambalo linaeleweka ikizingatiwa hatari kubwa zinazokabili kundi hili pamoja umuhimu wa siku 1,000 tangu kuzaliwa kwa mtoto. Hivyo basi afua maalum kama vile namna bora ya kulisha watoto wachanga na watoto wengine wadogo (Infant and Young Child Feeding Practices -IYCF), pamoja na unyonyeshaji wa pekee wa maziwa ya mama (miezi 0-6), Lishe ya vyakula mchanganyiko na vya ziada (miezi 6 - 23) vimepewa kipaumbele zaidi. Wakati huo huo, kundi la umri wa miaka 3-5 linaendelea kupata huduma nyingine za lishe kama vile ufuatiliaji wa ukuaji, nyongeza ya vitamini A, vidonge vya minyoo na usimamizi jumuishi wa magonjwa ya watoto. Hata hivyo, kama ilivyooneshwa hapo juu katika muhtasari wa afya, changamoto iliyobaki ni wazazi kuacha kupeleka watoto wao kwenye kliniki za RCH mara kwa mara baada ya kumaliza chanjo wafikapo miaka 2.

#### *d) Utaratibu wa Lishe Shuleni*

Imeonekana kuwa, machapisho mbalimbali ya kitaifa kama vile Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya wa  Tanzania  na Utafiti wa Kitaifa wa Lishe na miongozo mbali mbali ya lishe, hazizungumzii namna bora za lishe kwa watoto wa kati ya umri wa miaka 3-8. Msisitizo upo zaidi kwenye afua za lishe ya mama mjamzito, mtoto mchanga, mtoto mdogo na kijana. Afua za lishe hazishughulikii vya kutosha mahitaji ya watoto walio katika vituo vya kulelea watoto wadogo/ elimu ya awali na madarasa ya chini katika shule za msingi. Hata hivyo maeneo ambayo kumeonekana kuna programu za lishe shuleni ni kutokana na juhudi za wadau zinazotokana na ubunifu wao kama sehemu ya majaribio ya programu hizo shuleni, walimu

[39] MoHCDGEC (2016) Tanzania Demographic Health Survey and Malaria Indicator Survey (TDHS-MIS) 2015 – 2016.

[40] Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children (MoHCDGEC) [Tanzania Mainland], Ministry of Health (MoH) [Zanzibar], Tanzania Food and Nutrition Centre (TFNC), National Bureau of Statistics (NBS), Office of the Chief Government Statistician (OCGS) [Zanzibar] and UNICEF. 2018. Tanzania National Nutrition Survey using SMART Methodology (TNNS) 2018. Dar es Salaam, Tanzania: MoHCDGEC, MoH, TFNC, NBS, OCGS, and UNICEF.

au uongozi wa shule kuchangisha chakula kutoka wazazi/walezi au ni kutokana na michango ya wasamaria wema. Hata hiyo, lishe hiyo haifikii kiwango bora cha vyakula mchanganyiko, ambapo wadau kadhaa waliohojiwa walionesha kuwa uji wa nafaka pekee ndio unaotolewa kwa watoto. Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto (WAMJW) kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania inaandaa toleo la kwanza la Miongozo ya Kitaifa ya Lishe kwa Tanzania ambayo inajumuisha makundi yote ya watu ikiwa ni pamoja na watoto wa umri wa miaka 5-10. Miongozo hii inapaswa pia kuendana na Mwongozo wa Kitaifa wa utoaji wa huduma ya chakula na Lishe kwa wanafunzi wa elimu msingi ulioandaliwa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia. Mwongozo huo utatoa fursa muhimu ya kuweka kipaumbele na kuboresha programu za lishe shuleni, ikiwemo utoaji wa huduma bora kwa shule nyingi Zaidi, ikiwemo matumizi ya vyakula vyenye virutubisho muhimu na kuwekwa ruzuku na Serikali kwenye maziwa ambapo itafaidisha watoto wenye umri wa miaka 3 - 8 pamoja na walengwa wengine.

### 2.4.3 Malezi yenye Mwitikio

Malezi yenye mwitikio yanaangalia mahusiano ya karibu baina ya mzazi / mlezi na mtoto, ikizingatiwa kuwa ushahidi unaonesha umuhimu wa mwitikio wa mahitaji ya watoto kulingana na ishara watakazo onesha katika kuchangia ukuaji wao. Utaratibu wa kujumuisha huduma za malezi jumuishi kwenye huduma zilizopo kama vile afya na lishe bado ni dhana mpya, hivyo inasababisha ufikiaji mdogo kwa walengwa. Mifano michache ya huduma jumuishi ambazo hutekelezwa na wadau katika maeneo mbali mbali nchini hujumuisha uchangamshi wa awali na afya, lishe na ulinzi wa mtoto. Afua zilizopo ni chache na zipo kwenye mfumo wa miradi au utafiti zikitekelezwa kwa kiwango kidogo na kujumuishwa moja kwa moja katika program za Afya na Lishe zinazoendeshwa katika vituo vya Afya na ngazi ya jamii. Kwa hivyo hakuna takwimu za taifa au afua katika kipengele hiki cha MMMAM kinacholenga watoto wenye umri wa miaka 0-3.

#### *a) Malezi kwa Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto:*

Malezi kwa Makuzi na Maendeleo ya Mtoto (CCD) ni mkoba ulioandaliwa wenye mbinu zilizothibitishwa na Shirika ya Afya Duniani (WHO) na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kwa ajili ya watoa huduma za afya ili kutoa unasihi kwenye michezo na mawasiliano kwa wazazi/walezi wenye watoto wa wenye umri wa miaka 0-3 wakati wa utoaji wa huduma za afya. Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kupitia WAMJW kitengo cha Afya ya Mama na Mtoto imeanza kuwekeza kwenye malezi yenye mwitikio kwa kujumuisha mbinu za malezi kwa makuzi na maendeleo ya mtoto pamoja na mafunzo ya ufuatiliaji wa ukuaji na maendeleo ya mtoto. Mpaka sasa rasimu ya Mwongozo wa Malezi kwa Makuzi na Maendeleo ya Mtoto na mkoba wa Malezi kwa Makuzi na Maendeleo ya Mtoto vimeandaliwa. Lengo la Mwongozo wa Kitaifa wa Malezi Kwa Makuzi na Maendeleo ya Mtoto ni kuhakikisha huduma za malezi yenye mwitikio zinafika nchi nzima kupitia mfumo wa afya. Mkoba wa mafunzo ya Malezi Kwa Makuzi na Maendeleo ya Mtoto kinawajengea uwezo wahudumu wa afya wa vituoni na wa kwenye jamii kujumuisha jumbe za uchangamshi wa awali na malezi yenye mwitikio kwenye huduma za afya. Kitengo cha Afya ya Mama na Mtoto kimeonesha jitihada ya kutanua wigo wa matumizi ya mkoba wa Malezi Kwa Makuzi na Maendeleo ya Mtoto kwa kufanya majaribio kwa kuunganisha mkoba wa Malezi Kwa Makuzi na Maendeleo ya Mtoto na Ufuatiliaji wa ukuaji na Maendeleo ya Mtoto katika mafunzo kazini. Pia, Mkoba wa MMMAM unaonekana katika Mwongozo wa Taifa wa huduma kwa watoto wenye umri chini siku 28 na uanzishaji wa kitengo cha matunzo ya watoto wenye umri wa chini ya siku 28. Miongozo hii inatambua umuhimu wa mawasiliano na mtoto kuanzia ujauzito, mtoto mchanga na mtoto mgonjwa. Pia, mwongozo wa huduma kwa watoto wenye umri chini ya siku 28 unatambua ustawi wa mama kwa mahusiano bora na mtoto na ukuaji wake[41] .

Ingawa huduma za malezi yenye mwitikio zinaweza kuonekana kuwa mbinu mpya nchini, ni muhimu kutambua mila na desturi nzuri zilizopo zikiwemo za malezi ya watoto ambazo zinaweza zikaendelezwa na kuboreshwa pale inapowezekana. Aidha, wazazi, walezi na familia washawishiwe kutumia stadi na uwezo wa kutengeneza vifaa vya michezo vinavyopatikana kwenye jamii kwa kutumia malighafi zenye gharama ya chini, mfano chupa

[41] Ministry of Health, Community development, Gender, Elderly and Children (MOHCDGEC) (2019) National guideline for Neonatal Care and Establishment of Neonatal Care Unit. Reproductive and Child Unit

tupu, nguo, vifuu na michanga. Kwa kutumia malighafi hizo familia wanaweza kutengeneza, magari, mwanasesere, chekeche, vitabu na vingenevyo. Huduma za Afya na Lishe zilizopo nchini zinatoa fursa ya kutoa huduma za malezi jumuishi. Hii inajumuisha uwepo wa mkakati wa Huduma za Afya kwenye Jamii ili kusaidia Watoa Huduma za Afya Kwenye Jamii (WAJA) kutembelea kaya na huduma za malezi jumuishi. Hii inajenga mazingira ya watoa huduma jumuishi za malezi yenye mwitikio, uchangamshi wa awali, ulinzi wa mtoto, pamoja na huduma za afya na lishe. Vilevile, kupitia Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe, shughuli za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto zimejumuishwa pamoja na programu ya lishe ambapo inajenga nafasi ya kuenea kwa huduma hizi nchini. Pia, kuna nafasi ya kuunganisha na kusambaza programu na vifurushi vya mawasiliano vilivyopo ambavyo vimejumuisha vipengele vya malezi jumuishi kama vile mradi wa malezi ambao unatekelezwa na Shirika la EGPAF mkoani Tabora; Programu ya kuharakisha kupunguza udumavu inayotekelezwa kupitia Shirika la Kimataifa la kuhudumia Watoto katika mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe; na utafiti wa afua za kuwahusisha kina baba katika Huduma bora za Lishe unaofanyika na Shirika la PCI Mkoani wa Mara.

#### *b) Ajenda ya Kitaifa ya Malezi*

Ajenda ya Kitaifa kwa Malezi na familia Tanzania (Familia Bora, Taifa Imara) kwa watoto kuanzia miaka 0-18 ina nguzo za malezi bora (Lea –Linda – Wasiliana) ambazo zinajitosheleza katika mbinu za malezi yenye mwitikio. Ajenda ya Kitaifa ya Malezi inatoa nafasi ya kushughulikia taratibu za malezi kwa watoto na kuzishughulikia katika programu za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto za kisekta.

### 2.4.4 Fursa za Ujifunzaji wa Awali

Kujifunza huanza tangu ujauzito na sio shule ya awali, na unaendelea katika maisha yote ya binadamu, Ujifunzaji wa awali ni uwezo anaojengewa mtoto kupitia mwitikio wa mlezi ambapo mtoto anapata ujuzi, sifa na uwezo kupitia vitendo rahisi mfano kutabasamu, kutazama machoni, kuzungumza, kuimba, kutoa mifano kwa vitendo, kuigiza, na michezo rahisi ili kuhakikisha mafanikio ya kuzoea mabadiliko kwa haraka yakiwemo ya kujenga mahusiano na watu wengine. Hivyo, ujifunzaji sahihi wa awali ni muhimu kwa makuzi ya mtoto kiakili, kijamii, kijinsia, kimwili na katika maandalizi na utayari wa elimu ya baadae.

#### *a) Elimu katika vituo vya kulelea watoto wadogo Mchana*

Nchini Tanzania watoto wenye umri wa miaka 3-4 hawafikiwi na programu za malezi na makuzi ya mtoto. Mkanganyiko katika sera na Sheria za elimu ya awali unachanganya watekelezaji na wadhibiti katika utoaji wa huduma katika kundi hili. Wakati Sera ya Elimu inasema watoto hawa wanaweza kupata elimu ya awali, Sheria ya Mtoto inatoa mamlaka kwa Kamishina wa Ustawi wa Jamii kusimamia huduma jumuishi za malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto chini ya miaka 5. Hata hivyo mtaala na upimaji wa maendeleo kwa elimu ya awali unalenga watoto wa miaka 5. Aidha, kuwepo kwa changamoto ya mlundikano na mchanganyiko wa umri katika mikondo ya elimu ya awali imepelekea kupunguza uandikishaji wa watoto wa miaka 3-4. Vilevile kama hakuna programu za kitaifa zinazolenga watoto wa umri wa miaka 3-4, wengi wa watoto hawa wanakosa fursa za elimu ya awali. Hii pia ina maana kuwa hakuna programu rasmi ya kitaifa inayoendana na maendeleo ya kundi hili, hivyo kupelekea watoto hawa wanapojiunga na vituo vya kulelea watoto wadogo mchana huishia katika mfumo wa kufundishwa badala ya kujifunza kupitia michezo na kutumia zana kulingana na mazingira yao. Wakati shule binafsi na shule za madhehebu ya dini zikiongeza kutoa elimu ya malezi na elimu ya awali hata hivyo huduma hizi hufikia asilimia 5 tu ya watoto wote wenye umri huo, mathalani wengi wao wakiwa maeneo ya mijini[42].

Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imewekeza katika mipango mbalimbali ya kutatua changamoto hii ikiwa ni pamoja na kuandaa kiongozi cha mlezi cha kuwezeshea watoto chini ya umri wa miaka mitano kujifunza kwa njia ya michezo (draft 2020); Uandaaji

. [42]United Republic of Tanzania. (URT) (2017) situation analysis and baseline study on early childhood education in Tanzania Mainland.

wa muongozo wa Kitaifa wa uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya kijamii vya kulelea watoto wadogo mchana; Mwongozo wa Kitaifa wa uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo chini ya miaka miwili (0-2); Mwongozo wa kitaifa wa uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana (2-4 kabla ya kujiunga na elimu ya awali), ikiongozwa na Kanuni za vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na watoto wachanga ya mwaka 2012. Mchakato pia umehusisha uandaaji wa kiongozi cha utengenezaji wa vifaa vya michezo na kujifunzia watoto chini ya miaka 5.

Vilevile, uelewa juu ya umuhimu wa ujifunzaji kupitia michezo haukupewa kipaumbele katika ngazi zote za maamuzi, udhibiti ubora, watoa huduma, waelimishaji na jamii kwa ujumla ikiwemo wazazi. Ripoti zinaonesha kuwa matarajio makubwa ya wazazi ni watoto wao kuanza kujifunza kusoma na kuandika katika madarasa ya awali hivyo kupelekea watoa huduma kulazimika kuwafundisha watoto badala ya kuacha wajifunze kupitia michezo. Pia mfumo wa elimu ya kuwaandaa walezi na walimu wa awali hauwaandai walimu katika falsafa ya ujifunzaji kupitia michezo katika umri mdogo. Hii inaendelea katika sekta zote zinazotoa afua za huduma za elimu ya awali pamoja na sekta binafsi. Michezo pia inatoa fursa ya kujenga uelewa wa mtoto ambapo itamsaidia mtoto katika elimu ya baadae. Ukosefu wa vifaa vya kuchezea watoto, vitabu, uelewa na ujuzi kuhusu malezi na wazazi kutokuchangamana na watoto mara kwa mara nayo imeripotiwa kama changamoto. Aidha, kumekuwa na upungufu wa ujifunzaji wa watoto kupitia michezo wakiwa nyumbani na hata vituoni. Kwa upande mwingine, kuna upungufu wa walezi wenye mafunzo ya elimu ya awali kukidhi ongezeko la programu za elimu ya awali. Changamoto hii ni kubwa vijijini ambako hakuna programu madhubuti za elimu ya malezi kabla ya watoto kujiunga na elimu ya awali.

### *b) Elimu ya Awali*

Tanzania ni nchi ya kwanza katika ukanda wa Afrika Mashariki katika elimu ya awali kuifanya kuwa ya lazima kwenye  Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ili kujumuisha elimu ya awali katika elimu ya msingi kwa kuzitaka shule zote za msingi kuwa na darasa la elimu ya awali kwa watoto wa chini ya miaka mitano[43].  Vilevile, Mtaala wa Elimu ya Awali unaosaidia ujifunzaji kupitia michezo na mwongozo wa serikali wa mwaka 2016 wa elimu bila malipo hujumuisha elimu ya awali.Aidha, uandikishwaji wa elimu ya awali ni kiashiria muhimu kilichoingizwa katika Mpango wa Kitaifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21.

Kuwepo kwa mazingira rafiki ya kisera kumepelekea ongezeko la uandikishaji wa watoto katika elimu ya awali kufikia 500,000 ndani ya mwaka mmoja kutoka 1,069,823 mwaka 2015 mpaka 1,562,770 mwaka 2016[44]. Ongezeko hilo pia limeonekana katika madarasa ya elimu ya awali  na kufanya uandikishwaji wa darasa la kwanza kuongezeka kwa asilimia 41.1 kutoka watoto 1,404,998 mwaka 2012 mpaka watoto 2,120,667 mwaka 2016 wakati zaidi ya nusu ambayo ni asilimia 54.8  ya watoto walioandikishwa darasa la kwanza wana elimu ya awali[45].

Hata hivyo, ongezeko la uwiano wa idadi ya uandikishaji katika elimu ya awali ambao ni asilimia 102.6 mwaka 2016 inaweza kupotosha ukweli juu ya mchanganyiko wa umri ambapo chini ya nusu ya watoto walionadikishwa ambayo ni asilimia 44.9 walikuwa ni walengwa wa miaka mitano ikiwemo asilimia 37.5 wenye umri zaidi ya miaka 5. Vile vile uwiano wa uandikishwaji wa asilimia 46.7 pia unaonesha nusu ya watoto wa umri wa miaka mitano wanakosa elimu ya awali ambao ni mwendelezo tangu mwaka 2016 ikiripoti kushuka kwa uandikishaji kufikia asilimia 39.9[46].

Katika muktadha huu wa ongezeko la haraka kwa upande mwingine kumeonesha changamoto katika ubora. Aidha, kumekuwa na upungufu wa walimu wa elimu ya awali ambapo wengi wao wanaujuzi wa elimu ya msingi na sio elimu ya awali. Katika mwaka 2018, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia  iliripoti upungufu wa asilimia 31.7 ya walimu wa

[43] Ministry of Education Science and Technology (MoEST) Education and Training Policy 2014.

[44] President's Office Regional Administration and Local Government (PORALG) (2016) Basic Education Statistics Tanzania (BEST) 2012-2016 National Data.

[45] MoEST (2016) Basic Education Statistics in Tanzania (BEST) 2012 – 2016

[46] Ministry of Education, Science and Technology (MoEST) (2018) Education Sector Performance Report 2017/18, Tanzania Mainland, draft for distribution, Sept 15th 2018

elimu ya awali wenye vigezo katika shule za Serikali kutoka walimu 7,861 mwaka 2017 mpaka walimu 5,367 mwaka 2018. Aidha, uwiano wa wanafunzi na walimu katika mkondo wa elimu ya awali ya shule za serikali ililipotiwa kuwa 249:1[47] kinyume na mwongozo wa kisera wa 25:1 ikichangiwa na ongezeko la uandikishwaji na walimu wasio na vigezo. Miundombinu duni huchangia mlundikano wa wanafunzi katika madarasa wenye mchanganyiko wa umri ambapo hupelekea kutofautiana katika maendeleo ya makuzi na ujifunzaji kwa watoto. Ubora wa ujifunzaji unaathiriwa kwa sababu waalimu hawawezi kutoa elimu lengwa kuendana na mahitaji ya watoto.

Mwaka 2019 serikali iliendelea kuwekeza katika kukabiliana na changamoto hizi ili kuongeza ubora, ikiwemo uchapishaji na usambazaji wa mtaala wa elimu ya awali na vitabu vya hadithi katika mikondo yote ya elimu ya awali. Pia juhudi za uandaaji rasimu ya mwongozo wa Kitaifa wa uendeshaji na viwango vya elimu ya awali nchini Tanzania unaendelea kukamilishwa. Kuanzishwa kwa kozi ya diploma ya majaribio ya elimu ya awali mnamo 2020 kutasaidia kupunguza changamoto ya walimu wa darasa la awali waliohitimu darasa la saba. Ili kupunguza uhaba wa walimu wa shule za awali, serikali ilitenga Chuo cha Mafunzo ya Ualimu katika kila kanda kutoa mafunzo ya elimu ya awali kwa wakufunzi. Hata hivyo, kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watoto walioandikishwa katika shule za awali, idadi ya walimu bado haitoshi. Wadau wanaotekeleza programu za MMMAM nchini kama vile kama Children in Crossfire na Shirika la kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF) wameweza kutekeleza programu ya mafunzo kwa walimu wa shule za awali walio kazini ili kutoa elimu bora kwa watoto katika mazingira yenye watoto wengi wenye uhitaji. Mafunzo yao yamezingazia Sera ya Elimu na Mafunzo pamoja na Mitaala ya Elimu ya Awali iliyotolewa na taasisi ya Elimu Tanzania.

### 2.4.5 Ulinzi na Usalama

#### *a) Usajili wa kuzaliwa*

Uelimishaji jamii na juhudi za makusudi za sekta mbalimbali zilizofanywa na serikali katika upatikanaji wa huduma za uandikishaji watoto kupitia afua mbalimbali zimechangia kuongezeka kwa uandikishaji wa watoto kutoka asilimia 26 mwaka 2016 mpaka asilimia 49 mwaka 2020 (Makadirio ya Taasisi ya Usajili wa Vizazi na Vifo (RITA)). Hati ya makubaliano ya pamoja yaliyochukuliwa na Wizara ya Katiba na Sheria, OR-TAMISEMI na WAMJW mwaka 2014 iliongoza utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa uandikishaji wa watoto chini ya miaka 5[48]. Ubunifu wa kutumia vituo vya afya vinavyotoa huduma za wamama wajawazito katika kutoa huduma za usajili wa vizazi umeonesha ufanisi, ukizingatia watoto chini ya miaka 3 na wazazi wao wanashiriki kupata chanjo na huduma zingine za afya. Aidha, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ikishirikiana na Taasisi ya Usajili wa Vizazi na Vifo (RITA), ilizindua kampeni ya uelimishaji juu ya usajili wa watoto chini ya miaka 5 [49]ambao unatumia uandikishaji wa vizazi kupitia simu za mkononi. Hata hivyo, kuna uwiano usiosawa kati ya mijini na vijijini katika usajili wa watoto ambapo vijijini inaripotiwa kuwa ni asilimia 16 ukilinganisha na asilimia 50 mijini. Pia, kaya maskini zimeripotiwa kuwa na asilimia 8 ukilinganisha na kaya zenye kipato cha juu ambazo zimeripotiwa kuwa na usajili kwa asilimia 65[50].

#### *b) Ukatili dhidi ya watoto*

Katika vitendo vya ukatili wa watoto, kuna upungufu wa utoaji taarifa za kesi za unyanyasaji na utelekezaji wa watoto kuanzia miaka 0-8. Kuna utafiti mdogo uliofanywa kwenye jamii kuhusuiana na kesi za ukatili, unyanyasaji na utelekezaji wa watoto wadogo unaofanywa na wazazi na walezi. Mfano, utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia katika mkoa wa Katavi ulionesha asilimia 18 ya wazazi wenye watoto chini ya miaka mitatu kuwapiga vibao watoto wao hali kadhalika asilimia 5 ya wazazi walionekana wakiwapiga watoto wao vibao wakati wa

[47] Ministry of Education, Science and Technology (MoEST) (2018) Education Sector Performance Report 2017/18, Tanzania Mainland, draft for distribution, Sept 15th 2018.Ha

[48] MoHCDGEC (2016) National Plan of Action to End Violence against Women and Children in Tanzania 2017/18 – 2021/22.[43] Ministry of Education Science and Technology (MoEST) Education and Training Policy 2014.

[49] MoHCDGEC (2016) National Plan of Action to End Violence against Women and Children in Tanzania 2017/18 – 2021/22[45] MoEST (2016) Basic Education Statistics in Tanzania (BEST) 2012 – 2016

[50] MoHCDGEC (2016) Tanzania Demographic Health Survey and Malaria Indicator Survey (TDHS-MIS) 2015 – 2016.

utafiti wenyewe[51] . Tafiti za awali za mradi wa malezi uliofanywa na shirika la EGPAF Wilayani Nzega, Tabora manispaa pamoja na Wilaya ya Igunga uliripoti kuwa zaidi ya nusu (53%) ya wazazi wa watoto wenye umri wa miaka 0-2 wanaamini kuwa watoto waadabishwe kwa kuchapwa[52]. Hata hivyo hakuna takwimu zinazoonesha picha halisi ya ukatili, unyanyasaji na utekelezaji wa watoto kitaifa. Adhabu ya viboko imekuwa ni utaratibu wa kawaida wa kuadabisha watoto kwenye shule nyingi hali ambayo hivi karibuni imeongezeka na kufatiliwa kwa ukaribu. Hata hivyo hakuna takwimu rasmi zinazoonesha ukubwa wa adhabu ya viboko. Serikali ilitoa waraka kuhusu adhabu ya viboko mwaka 2012 ambao unadhibiti idadi ya viboko kwa wanafunzi. Waraka unaelezea kuwa mwalimu mkuu pekee ndie anayeruhusuiwa kuchapa viboko visivyozidi 4. Wizara ya Elimu iko kwenye mchakato wa kufanya mapitio ya waraka huo kuhakikisha unalenga zaidi haki za watoto ili kutatua changamoto za utekelezaji wake. Aidha, mapungufu yaliyopo ni kuwa, ingawa kuna miongozo ya kushughulikia adhabu za viboko mashuleni, miongozo hiyo haizingatii mazingira ya kwenye kaya. Kuna uhitaji wa miongozo ya matumizi ya vibiko unaolenga wazazi, walezi, kaya na jamii.

Ripoti ya Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) ya mwaka 2011[53] inayohusiana na ukatili dhidi ya watoto Tanzania ni chanzo muhimu cha takwimu. Ripoti hii inaonesha kuwa msichana 1 kati ya 3 na mvulana 1 kati 3 wanapitia aina mbalimbali za ukatili wa kingono kabla hawajafikia miaka 18. Robo tatu ya watoto wameripotiwa kufanyiwa vitendo tofauti vya ukatili wa kimwili kupitia mtu wa karibu wa familia na walimu; na zaidi robo ya wasichana na wavulana 3 kati ya 10 wameripoti kufanyiwa ukatili wa kihisia. Ripoti pia inaonesha kuwa watoto wamepitia mchanganyiko wa vitendo vya ukatili ikiwemo ukatili wa ngono na kimwili (84%) na ukatili wa kingono na kihisia (43%). Waathirika wachache wa vitendo vya ukatili waliweza kuripoti vitendo hivyo kwa watu wazima wanaowaamini na nusu ya wasichana wote na wavulana wawili kati ya watatu hawakuripoti vitendo hivyo kwa mtu yoyote. Aidha, kati ya hao walioripoti vitendo vya ukatili, ni namba ndogo sana (Msichana 1 kati ya 8 na chini ya mvulana 1 kati ya 20) walipokea huduma zilizohitajika. Hata hivyo, kwa mtazamo wa MMMAM, utafiti huu ulilenga watoto wa miaka 13 au zaidi, kwa hiyo watoto chini ya miaka 8 hawakulengwa.

### *c) Ukatili dhidi ya wanawake na watoto*

Wanawake wajawazito pia wameripoti kupitia aina tofauti za unyanyasaji ambapo kati asilimia 7 mpaka 10 wamepitia ukatili wa kijinsia ukiathiri kushindwa kuhudhuria huduma za afya kama huduma ya mama mjamzito[54].Kiwango kikubwa cha ukatili wa kimwili dhidi ya wanawake wenye umri wa kuzaa kati ya miaka 15-49 wameripotiwa mara kwa mara, ambapo asilimia 40 ya wanawake hao wameripoti kufanyiwa ukatili wa kimwili na asilimia 17 kufanyiwa ukatili wa kingono hali ambayo imekuwepo tangu mwaka 2010. Takwimu zinaonesha kuongezeka kwa kesi za ukatili kwa watoto katika umri wote (kingono, kimwili na kutelekezwa) mwaka 2017 ziliripotiwa kesi 13,457, mwaka 2018 kesi 14,419 (sawa na ongezeko la asilimia 7.2%) ikifuatiwa na kesi 15,980 zilizoandikishwa mwaka 2019 ambayo ni ongezeko la asilimia 10.8 kama ilivyoripotiwa na Rejista ya Polisi ya Uhalifu kwenye kesi za unyanyasaji kati ya mwaka 2017-2019[55].

Kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, Serikali iliandaa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na watoto wa mwaka 2016/17 -2021/22 (MTAKUWWA). Mpango huu jumuishi unalenga kutokomeza ukatili kwa kina ukiwa na afua ambazo zimelenga Elimu ya malezi, usalama shuleni, utekelezaji wa sheria, mazingira salama katika maeneo ya umma na maeneo mengine. Hadi sasa juhudi zilizofanyika kupitia mpango

[51] World Bank (2018) Early Childhood Stimulation in Tanzania: Findings from Pilot Study from Katavi Region.

[52] EGPAF (2020) Report on Baseline Data Collection for the Study: Effectiveness of Early Child Development Multi-Media Communication on Caregiver and Community Health Worker Behaviors: Evaluation of the Malezi II Program.

[53] UNICEF (2011) Violence Against Children in Tanzania Findings from a National Survey 2009.

[54] MoHCDGEC (2016) The National Road Map Strategic Plan to Improve Reproductive, Maternal, Newborn, Child & Adolescent Health in Tanzania (2016 - 2020): One Plan II.

[55] MoHCDGEC (2019) Kitabu cha takwimu ya hati ya uhalifu kilichotolewa na Jeshi la Polisi

huu zimehusisha kuandaa kitini cha taifa cha elimu ya malezi (kwa watoto kuanzia miaka 0-18) na kuandaa rasimu ya miongozo ya vituo vya malezi vya kulelea watoto wadogo (miaka 0-4+). Vilevile kumekuwepo na mfumo imara wa uratibu kutoka kwenye ngazi ya kitaifa hadi kijiji ambapo uratibu unajumuisha uwepo wa kamati za ulinzi kwa watoto wakiwemo Afisa Ustawi wa Jamii na Dawati la Jinsia la Polisi. Dawati la Jinsia limeanzishwa katika vituo vya polisi pamoja na namba ya msaada kwa mtoto[56]. Wadau walioshirikishwa wameongelea umuhimu wa kufanya mapitio ya mbinu zinalomlenga muathirika kupata huduma ya haraka baada ya kufanyiwa vitendo vya ukatili mfano kupunguza muda anaotumia muathirika kupata huduma baada ya kufanyiwa ukatili wa kingono.

## *2.5 Masuala Mtambuka ya Watoto wa umri wa miaka 0-8*

### 2.5.1 Msongo Unaohusiana na Uzazi

Msongo na mashaka yanayohusiana na uzazi unaotokea kipindi cha ujauzito na miaka ya mwanzo ya maisha ya mtoto unajulikana kuwa na athari kwa afya ya mama na kupelekea majonjwa na kushindwa kujitunza na mbaya zaidi inaathari kubwa kwenye ukuaji na maendeleo ya mtoto. Wanawake wenye msongo kipindi cha ujauzito wana uwezekano mkubwa wa kuzaa watoto wenye uzito mdogo au kuzaa watoto njiti. Uhusiano wa mama na mtoto unaathirika wakati mama anapokuwa na msongo wa mawazo ambapo husababisha uchelewaji wa ukuaji wa mtoto ikiwemo kuchelewa kuongea na ukuaji wa kiakili[57]. Ingawa tafiti hazitoi takwimu sahihi zinazoonesha ukubwa wa tatizo la ustawi wa mama wakati wa uzazi nchini, msongo wa mawazo wakati wa uzazi umeonekana kuwa ni tatizo kubwa linaloathiri wanawake ulimwenguni. Hali za kijamii na kimazingira ikiwepo umaskini, kukosekana kwa huduma bora za afya, usalama, ukatili kutoka kwa wenza, vinaonekana kuwa changamoto mojawapo ambazo wanawake wanakutana nazo ambazo zinachangia wanawake kupata msongo wa mawazo.

Tafiti ndogo iliyofanywa na Catholic Relief Services (CRS) kwenye wilaya za Geita, Sengerema na Buchosa kwenye kundi la kina mama wenye watoto wadogo, asilimia 18 ya kina mama wana dalili za kuwa na hofu ambayo inafanana na nchi zingine zinazoendelea. Tafiti hiyo pia ilionesha kwamba tatizo la ustawi wa mama linaweza kutatuliwa kupitia afua jumuishi za kijamii kama vile "care group model" ambayo pia inajihusisha na kutatua maeneo mengine ya matokeo ya ukuaji na maendeleo ya watoto[58].

### 2.5.2 Mimba za Utotoni

Tanzania ina kiwango cha juu cha mimba za utotoni ambapo asilimia 27 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15-19 wameripotiwa kuwa na watoto au wajawazito (TDHS 2015/16). Takwimu zinaonesha kuongezeka kwa idadi ya mimba za utotoni kutoka kwenye tafiti za kitaifa zilizopita ambapo inaonesha asilimia 26 mwaka 2004/5 na asilimia 23 mwaka 2010 - Vijana wa Kike wa vijijini wanaonekana kuwa na watoto mapema ukilinganisha na vijana wa kike wa mjini (asilimia 32 ya vijana wa kike vijijini ukilinganisha na asilimia 19 ya vijana wa kike mijini). Mikoa ya Mara, Tabora, Shinyanga, Morogoro na Dodoma ina kiwango kikubwa cha mimba za utotoni kuanzia asilimia 37 mpaka asilimia 43 ukilinganisha na sehemu zingine nchini. Taarifa pia imeonesha kuwa kiwango cha elimu na kipato cha kaya ni moja ya viashiria muhimu vya mimba za utotoni[59]. Hivyo basi, juhudi zaidi zinahitaji kufanyika kwenye kundi hili ukizingatia athari zinazoweza kuwapata zikiwemo vifo wakati wa ujauzito, kujifungua

[56] MoHCDGEC (2016) National Plan of Action to End Violence Against Women and Children in Tanzania 2017/18 – 2021/22.

[57] FHI 360 (2020) Maternal Depression: The potential role of nutrition in prevention and treatment: Technical brief.

[58] CRS (2018) Endline Evaluation Report: Incorporating Maternal Mental Well-being interventions into an Early Child Developmental Program: Pilot Research Using a Mixed Methods Quasi – Experimental Design in Selected Communities in Geita and Mwanza Regions, in Northern Tanzania.

[59] MoHCDGEC (2016) Tanzania Demographic Health Survey and Malaria Indicator Survey (TDHS-MIS) 2015 – 2016.

watoto wenye uzito mdogo, changamoto zinazompata mama katika kulea watoto katika umri mdogo na pia kushindwa kupata elimu. Wazazi wenye umri mdogo pia wanaripotiwa kutengwa na familia pamoja na jamii. Kutengwa kwao kunaathari kwenye ubora wa malezi ya watoto waliopatikana kwa wazazi wenye umri mdogo[60].

### 2.5.3 Watoto wenye Ulemavu

Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 imekadiria kuwa asilimia 9.3 ya watu wenye ulemavu ni kuanzia miaka 7 na kuendelea, ambapo kila watu 1000, watu 93 wana ulemavu[61]. Hata hivyo, kuna uwezekano kuwa takwimu hizi ni kadirio la chini ukizingatia vijana wadogo na watoto wenye ulemavu wanafichwa na kutojumuishwa kwenye takwimu hizo. Maana ya aina ya ulemavu inatofautiana kati ya mifumo ya tafiti mbalimbali inayopelekea changamoto na kutokuwa na uwiano sawa. Vilevile, kutokuwepo na nyenzo za utambuzi wa mapema wa ulemavu katika vituo vya afya, vituo vya kulelea watoto wadogo mchana, elimu ya awali na elimu ya msingi inaleta changamoto kubwa kwenye kuwatambua na kuwasaidia watoto wadogo. Pia, kuna upungufu wa huduma na wataalamu wa kuwasaidia watoto wenye ulemavu na mkazo uko kwenye watoto wenye umri mkubwa. Ingawa tafiti hulenga watoto wenye umri mkubwa, uzoefu unaonesha kuwa watoto wenye ulemavu ikijumuisha watoto wenye ulemavu wa viungo na wenye ualbino wamekuwa wakitengwa kupata huduma muhimu kwa ukuaji wao. Mfano, tafiti katika kanda ya ziwa zinaonesha kuwa watoto wenye ualbino wanachangamoto kubwa katika kupata elimu na huduma za afya, pia wanakabiliwa na ukatili na kuishi katika hali ya umaskini. Ingawa sensa watu na makazi ya mwaka 2012 inakadiria kuwa asilimia 9.3 ya watu wenye ulemavu, taarifa za Takwimu za Elimu Msingi Tanzania zinaonesha kiwango cha chini cha asilimia 1 ya watoto wenye ulemavu walioandikishwa shule. Changamoto hiyo inaongeza uwezekano wa watoto wenye ulemavu kuathirika katika ukuaji wao kimwili, kiakili, kihisia na kijamii[62].

### 2.5.4 Watoto kwenye makazi maalumu (Wakimbizi na Malezi Mbadala)

Kati ya watoto wanaopitia changamoto, wapo ambao wanapitia changamoto ya vita, kuhamishwa makazi, vifo vya wazazi na majanga mbalimbali, ambao pia wako katika hatari ya kuwa na makuzi duni. Watoto hawa wako kwenye hatari ya kukosa ulinzi na usalama, kutenganishwa na familia zao, lishe duni na kukosa huduma za afya na huduma zingine. Hivyo, ni muhimu Sera na Miongozo ya muhtadha huu zinazingatia mfumo wa malezi jumuishi[63]. Tanzania inapokea wakimbizi kutoka nchi mbalimbali zikiwemo Jamuhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Rwanda na Burundi, kwa sasa inaripotiwa kuwa watu 358,520 wameifadhiwa katika kambi tatu mkoani Kigoma na kuwa na kiashiria ya ongezeko la wakimbizi kutoka Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Burundi kutokana na muendelezo wa migogoro ya kisiasa katika nchi hizo[64]. Sheria zinazoongoza kambi za wakimbizi zinasimamiwa na Sheria ya wakimbizi ya mwaka 1998 na Sera ya Taifa ya Wakimbizi ya mwaka 2003 iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Ndani.

Tafiti ya hivi karibuni zilizofanyika kwenye kambi za wakimbizi mkoani Kigoma zinaonesha changamoto mbalimbali wanazokutana nazo watoto kwenye maeneo hayo. Changamoto hizi zikiwemo usumbufu kwenye elimu ambapo watoto wengi wanachelewa kujiunga na shule au wanaacha shule ikiwa ni asilimia 56.1 ya watoto wote kwenye kambi za wakimbizi wameandikishwa shule za awali hadi sekondari. Watoto wanaotoka kwenye familia maskini, watoto wasio na familia na watoto wenye ulemavu wako kwenye hatari kubwa ya kutoandikishwa shule[65]. Upungufu wa chakula, masuala ya afya ya akili zinazoathiri wazazi,

---

[60] UNICEF (2018) A National Agenda for Responsible Parenting and Family Care in Tanzania

[61] National Bureau of Statistics Ministry of Finance & Office of Chief Government Statistician Ministry of State, President Office, State House and Good Governance (2016) Disability Monograph.

[62] Tanzania Albinism society: 2019 Baseline Survey on Socio-Economic Status of Persons with Albinism and Their Households in The Lake Zone).

[63] WHO (2018) Nurturing Care Framework for Early Childhood Development: A Framework for helping children survive and thrive to transform health and human potential.

[64] Caritas Kigoma Diocese et al (2018) Joint Education Needs Assessment Tanzania: Report of an Assessment of Refugee Education in Three Refugee Camps in The Kigoma Region, Tanzania.

[65] Caritas Kigoma Diocese et al (2018) Joint Education Needs Assessment Tanzania: Report of an Assessment of Refugee Education in Three Refugee Camps in The Kigoma Region, Tanzania.

unyanyasaji na utelekezaji wa watoto pia zinaripotiwa kama changamoto katika familia za wakimbizi. Zaidi ya huduma za afya na lishe, kuna upungufu wa afua za utoaji huduma za watoto chini ya miaka 0-3 zinazolenga malezi yenye mwitikio na uchangamshi wa awali. Bado tafiti zinapendekeza kuwa malezi yenye mwitikio yanawakinga watoto na athari za migogoro na machafuko na kuwasaidia kufikia ukuaji na maendeleo yao kiafya[66]. Hii inamaanisha kuwa, kushughulikia huduma zote za malezi jumuishi za maendeleo ya mtoto na ustawi wa mzazi ni muhimu. Hata hivyo, kuna uwepo wa wadau wa sekta mbalimbali kwenye kambi za wakimbizi wanaotoa huduma za Lishe, Afya na Elimu kushirikiana na Wizara mbalimbali (WAMJW, WyST, OR- TAMISEMI), uchambuzi unaonesha kuwepo kwa uratibu hafifu kati ya taasisi hizo. Katika kambi za wakimbizi kuna vikundi kazi maalumu vya kisekta kama vile Elimu na Afya ambao wanapanga na kufanya kazi pamoja. Vilevile, utegemezi wa fedha za wafadhili pia ni changamoto ambayo inachangia afua zinazowalenga watoto hao kuwa za muda mfupi.

### 2.5.5 Watoto Yatima

Tafiti ya TDHMIS 2015/16, imefafanua kuwa mtoto yatima ni mtoto yoyote chini ya miaka 18 ambaye hana mzazi mmoja au wote. TDHMIS 2015/16 inaripoti kuwa asilimia 8 ya watoto chini ya miaka 18 ni yatima ambayo imeshuka kutoka asilimia 10 iliyoripotiwa mwaka 2010. Asilimia ya yatima inaongezeka kwa umri ambapo watoto chini ya miaka 2 ni asilimia 1 na watoto chini ya miaka 9 ni asilimia 7[67]. Nchini Tanzania, watoto yatima wanalelewa kwa taratibu mbalimbali zikiwemo kupitia familia na ndugu, malezi ya kambo, kuasili, Kaya inayoongozwa na mtoto na makao ya watoto. Imeripotiwa kuwa zaidi ya makao ya watoto 500 kitaifa yanawafikia watoto wenye umri tofauti. Uchambuzi wa tafiti wa hali halisi kuhusu watoto yatima na watoto walio katika mazingira hatarishi zilizopo katika mifumo ya malezi mbadala mkoani Dar es Salaam imeonesha kuwa kuna watoto 11,565 wenye umri tofauti ambao wapo kwenye makao ya watoto wakati watoto 80 wako kwenye jela za watoto, watoto 80 wako katika shule za maadilisho na 453 wako magereza. Hata hivyo kuna tafiti chache zilizofanyika kuonesha hali ya huduma, ubora na viwango kwenye maeneo hayo[68]. Kwa mfano kuna wamama wajawazito au wamama wenye watoto wachanga au watoto wadogo wako katika magereza. Hata hivyo, tafiti hazielezi hali halisi ya huduma kwa wafungwa. Ingawa watoto waliomo kwenye makao wanapata huduma za chakula na malazi bado kuna matukio ya unyanyasaji na malezi duni. Tafiti chache zimeonesha changamoto wanazokumbana nazo watoto hawa ikujumuisha umasikini uliokithiri na uangalizi na malezi duni katika ngazi ya kaya. Hata hivyo, hakuna tafiti zinazoripoti takwimu halisi za hali ya makazi yasio rasmi hasa kwa watoto wenye umri mdogo.

### 2.5.6 Kukabiliana na masuala ya Kijinsia yanayolenga watoto wenye umri wa miaka 0 - 8

Nchini Tanzania idadi ya wanawake ni kubwa kwa asilimia (51.3) ikilinganisha na wanaume asilimia (48.7). Kumekuwa na maendeleo makubwa yaliyopatikana katika kuleta usawa wa kijinsia, kwa mfano kwenye usajili wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari kwa mwaka 2017 usajili wa wanafunzi katika shule za msingi ulikuwa ni asilimia 49.7 kwa wavulana na asilimia 50.3 kwa wasichana. Pia asilimia 49.6 ya wavulana na asilimia 50.4 ya wasichana walisajiliwa katika shule za sekondari[69].

Hata hivyo, tofauti imeanza kuonekana kwenye usajili wa elimu ya juu kwa kidato cha tano na sita, ambapo asilimia 59.1 ya wavulana na asilimia 40.9 ya wasichana walisajiliwa[70]. Tofauti ya usawa wa kijinsia unaongezeka kadiri kiwango cha elimu kinavyoongezeka, ambapo tofauti huonekana zaidi katika taasisi za elimu ya juu, ambapo asilimia 18 ya wavulana wamesajiliwa ikilinganishwa na asilimia 9.6 ya wasichana[71].

[66] Moving Minds (2019) ECD and Early Learning for Children in Crisis and Conflict Brief adapted from a background paper commissioned for the 2019 Global Education Monitoring Report

[67] MoHCDGEC (2016) Tanzania Demographic Health Survey and Malaria Indicator Survey (TDHS-MIS) 2015 – 2016.

[68] Makuu M (2019) Situation Analysis of Orphans and Vulnerable Children in Existing Alternative Care Systems in Dar es Salaam, Tanzania. Social Work and Society International Online Journal

[69] PORALG (2017) Pre-primary, Primary, Secondary, Adult and Non-Formal Education Statistics 2017, Regional Data.[63] WHO (2018) Nurturing Care Framework for Early Childhood Development: A Framework for helping children survive and thrive to transform health and human potential.

[70] PORALG (2017) Pre-primary, Primary, Secondary, Adult and Non-Formal Education Statistics 2017, Regional Data.

[71] National Bureau of Statistics (2015) The 2012 Population and Housing Census Gender Dimension Monograph

Wanaume wameonakana kuwa na nafasi kubwa katika kufanya maamuzi kuhusu masuala ya afya kwa wake zao na watoto. Hata hivyo, ushiriki wa wanaume katika programu za afya ya uzazi, lishe ya wanawake, watoto, na vijana ni mdogo. Kwa mfano ni asilimia 30 tu ya wanawake hufika na wenza wao kupata huduma katika programu ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto[72].

Utamaduni na kazi nyingi vimeonekana kuwa ni vikwazo vinavyozuia wanaume kushiriki katika masuala ya Malezi katika familia[73]. Tatizo hili limeonekana pia Katika malezi ya watoto ambapo kiutamduni ni jukumu la mwanamke kushiriki na ushiriki wa wanaume ni mdogo ingawa ushiriki wao ni muhimu.

Serikali imetekeleza afua mbalimbali za kushughulikia masuala ya kijinsia katika sera za taifa, miongozo na programu mbalimbali.Kuhusu afua zinazolenga watoto wenye umri wa miaka 0 – 8, huduma za afya ya uzazi, inahakikisha kuwa wanaume wanashiriki katika kliniki za wanawake wajawazito, ambapo huduma mbalimbali hutolewa ikiwemo huduma ya unasihi na upimaji wa VVU, kliniki ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano ili kupata chanjo na kufuatilia maendeleo ya ukuaji wa watoto.

Huduma rafiki za familia zinaongezeka kutolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo hivi sasa zinaitwa 'huduma ya mama, baba na mtoto" tofauti na zamani huduma hiyo ilikuwa ikijulikana kama 'huduma ya mama na mtoto'.

### 2.5.7 Namna ya kuyafikia makundi maalumu

Kwa muktadha wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM, kundi la watoto walio katika mazingira hatarishi linajumuisha watoto wote walio katika hatari ya kutofikia ukuaji timilifu kutokana na changamoto za mazingira mbalimbali wanamoishi. Watoto hao ni pamoja na watoto wenye utapiamlo/udumavu; ulemavu wa aina yoyote; wanaochelewa katika hatua za ukuaji; waliozaliwa na maambukizi ya VVU/ au wenye wazazi wenye VVU, yatima; watoto wanaolelewa na wazee, watoto wenzao au walezi ambao ni wagonjwa sana; watoto wanaoishi kwenye maeneo yasiyofikika kwa urahisi na wanaotoka katika familia masikini.

Pia watoto waliofanyiwa ukatili wa aina yoyote, wanaoishi mitaani au kwenye kambi, vituo vya misaada au kwenye mazingira mahususi kama vile watoto wanaoishi na mama zao waliofungwa kwenye magereza, pia wanajumuishwa katika kundi hili. Ili kukabiliana na ukosefu wa usawa na kuhakikisha kuwa hakuna mtoto anayeachwa nyuma, Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM imelenga kushughulikia mahitaji ya watoto wote wakiwemo kundi hili. Watoto wote wanapaswa kupata huduma timilifu, hata hivyo tofauti zinategemea na uhitaji binafsi wa mtoto. Kwa mfano, mtoto mwenye changamoto ya kujifunza anaweza kuhitaji njia tofauti ya kujifunza ukilinganisha na mtoto asiyekuwa na changamoto hiyo.

Hii pia ni sawa kwa mtoto anayelelewa na mlezi ambaye ni mzee au mgonjwa sana, ambapo atahitaji ratiba mahususi ya kumtembelea nyumbani ikilinganishwa na mtoto anayetoka kwenye familia yenye wazazi vijana wenye afya na nguvu. Programu ya MMMAM itatumia neno 'watoto wote' ikimaanisha watoto wote wenye umri kati ya miaka 0 – 8 ikijumuisha watoto walio katika mazingira hatarishi.

[72] MoHCDGEC (2016) The National Road Map Strategic Plan to Improve Reproductive, Maternal, Newborn, Child & Adolescent Health in Tanzania (2016 - 2020): One Plan II.

[73] UNICEF (2018) A National Agenda for Responsible Parenting and Family Care in Tanzania

Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM imezingatia mtazamo wa Mfumo wa Malezi ambao umeweka huduma za msingi za Malezi katika ngazi tatu kama inavyooneshwa katika Mchoro Na 5: Huduma kwa Wote – kuhamasisha na kutoa huduma kwa familia, wazazi/walezi na watoto nchini; Huduma hitaji kwa makundi –Watu binafsi au jamii zilizo katika hatari ya kuathirika kutokana na sababu mbalimbali kama vile umaskini, utapiamlo, mimba za utotoni, maambukizi ya VVU, ukatili, na Waathirika wa majanga mbalimbali. Mfano wa huduma mbalimbali zinazotolewa ni pamoja na kuhaulisha fedha ili kusaidia kaya masikini kupitia mpango wa TASAF; na huduma lengwa – kwa familia au watoto wenye mahitaji ya ziada kama vile watoto wenye ulemavu, changamoto ya ukuaji au utapiamlo mkali. Watoto na familia hizo wanahitaji huduma za ziada na msaada kulingana na mahitaji yao.

***Mchoro namba 5:*** Kukidhi mahitaji ya familia na watoto[74]




## 2.6 Kwanini kumekua na uwekezaji mdogo wa masuala ya MMMAM katika sekta mbalimbali?

Uchambuzi unaonesha kuwa tangu mwaka 2004 Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wameweza kujadili na kuwekeza katika Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya mtoto, lakini kumekuwa na mafanikio hafifu katika maeneo makuu ya maendeleo ya mtoto. Ushahidi unaonesha kuwa maendeleo yamepatikana katika vipengele muhimu vya MMMAM, ikiwemo utungaji wa sheria, sera, miongozo na uwekezaji katika kuboresha afya, lishe na upatikanaji wa elimu ya awali.

Sababu mbalimbali zimechangia kuleta tofauti katika kufanikisha huduma jumuishi za kisekta za MMMAM. Sababu hizo ni pamoja na uelewa mdogo wa umuhimu wa utoaji huduma jumuishi za MMMAM pamoja na faida za ushirikiano na uwekezaji katika utoaji wa huduma zinazolenga vipengele vikuu vya Mfumo wa Malezi ambavyo ni Malezi, Afya Bora, Lishe Bora, Ulinzi na Usalama na Fursa za Ujifunzaji wa Awali.

Wakati ambapo inatambulika kwamba vifo vya watoto, udumavu na upatikanaji wa elimu ya awali ni viashiria muhimu vya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano 2021/22-2025/26, bado kuna changamoto ya uelewa miongoni mwa watunga sera na watoa maamuzi kuhusu umuhimu wa uwekezaji kwa watoto wadogo (miaka 0 – 8), katika ukuaji, maendeleo na faida mbalimbali katika maisha yao ya baadaye. Uelewa duni wa masuala ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto upo pia katika ngazi ya jamii, ambapo jamii bado haijaonesha uhitaji wa huduma jumuishi za MMMAM ikilinganishwa na huduma nyingine zinazotolewa na sekta mbalimbali.

Uratibu duni wa wadau wa MMMAM unaendelea kukwamisha mafanikio, ikichangiwa na uwepo wa sera mbalimbali za kisekta ambazo hazijaratibiwi kikamilifu. Badala yake, kila sekta inayohusika na masuala ya MMMAM ina sera yake na miongozo ya utekelezaji wa afua katika sekta husika. Pia mara nyingi hutokea mgongano wa sera katika sekta mbalimbali.

Jambo la muhimu ni kwamba kuna miundo ya kiutawala na usimamizi katika ngazi ya kitaifa, mikoa na wilaya ambayo inaweza kutumika katika kuratibu masuala ya MMMAM. Pia kuna programu za kitaifa zinazojumuisha sekta mbalimbali ambazo zinatoa fursa ya kujifunza namna ya kutoa huduma za MMMAM. Mfano wa programu hizo ni Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe, na Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto.

Kuwepo kwa sera ya ugatuzi wa madaraka, utaratibu wa kupanga mipango kwa pamoja na kufanya kazi katika ngazi ya mkoa, wilaya na serikali za mitaa chini ya uratibu wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kumesaidia kutoa jukwaa la kujumuisha utoaji wa huduma katika ngazi ya jamii.

Kupitia sera ya ugatuzi wa madaraka, ushirikiano katika kupanga mipango na bajeti ni jambo linalotekelezwa katika ngazi ya halmashauri. Hata hivyo, katika utaratibu wa kiutendaji uliopo sasa, bado kuna changamoto ya mfumo wa uratibu wa wadau wa sekta mbalimbali. Hii ni kwa sababu Wizara, Idara na Taasisi zenye jukumu na mamlaka juu ya masuala mbalimbali ya MMMAM hazina mamlaka au mipango ya kuitisha vikao vya uratibu wa masuala hayo vinavyohusisha viongozi wa ngazi za juu wa sekta mbalimbali kwa ajili ya kufanya maamuzi.

Mamlaka ya kuitisha vikao hivyo yapo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo kwa siku za nyuma haikuwa inajihusisha na masuala ya MMMAM hapa nchini. Hata hivyo katika siku za hivi karibuni Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa ikiandaa na kuratibu vikao na mipango ya sekta mbalimbali inayohusu MMMAM, ambayo ni kwa kuongeza ufanisi katika uratibu.

Kiwango kidogo cha uwekezaji katika masuala ya MMMAM kinachangia utegemezi wa ufadhili kutoka kwa wadau ambapo taarifa zinaonesha kuwa mashirika 25 yameweza kuchangia Dola za Kimarekani takribani milioni 10 -18 kufadhili shughuli za program ya MMMAM. Kiasi halisi cha fedha zilizowekezwa kugharamia shughuli za MMMAM hakijulikani kutokana na kukosekana kwa mfumo wa ufuatiliaji wa fedha za utekelezaji wa shughuli za program.

Katika miaka ya hivi karibuni, wafadhili wa shughuli za MMMAM nchini Tanzania ni pamoja na: UNICEF, WHO, World Bank, UKAID, USAID, Irish Aid, Conrad Hilton Foundation, Better Way Foundation, UK Comic Relief, Dubai Cares, Global Affairs Canada, Firelight Foundation, Johnson & Johnson, Lego Foundation na Sida[75].

Hata hivyo idadi kubwa ya mashirika hayo hayatoi fedha kwa ajili ya shughuli za MMMAM pekee, kwani fedha hizo hujumuishwa kwenye program nyingine ambazo zina afua za MMMAM. Hii ndiyo sababu ya ugumu uliopo katika kutambua kiasi halisi cha rasilimali zilizotengwa na wadau kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za MMMAM hapa nchini.

Katika kuboresha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za MMMAM nchini Tanzania, Serikali inapaswa kuandaa mpango mkakati wenye bajeti, unaojumuisha sekta mbalimbali zinazoshughulikia masuala ya MMMAM. Baada ya kufanya hivyo, wadau watakuwa kwenye nafasi nzuri ya kutafuta rasilimali mahsusi kwa ajili ya shughuli za MMMAM. Asilimia kubwa ya bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano imelenga utekelezaji wa afua ambazo hazina mchango wa moja kwa moja katika kukabiliana na matatizo ya lishe ambapo sekta ya afya imepangiwa asilimia 30, ikifuatiwa na sekta ya Maji safi na usafi wa mazingira asilimia 26, hifadhi ya jamii asilimia 19 ambayo inatolewa kupitia mfuko wa TASAF, sekta ya kilimo asilimia 17, elimu na maendeleo ya awali kwa pamoja zimepangiwa asilimia 8, na sekta ya mazingira imepanyiwa chini ya asilimia 1[76].

Kukosekana kwa viashiria vya ufuatiliaji katika ngazi ya program na kitaifa ni kikwazo kimojawapo katika ufuatiliaji wa masuala jumuishi ya MMMAM. Kwa mfano hivi sasa hakuna mfumo wa ufuatiliaji wa viashiria mbalimbali vikiwemo vya Malezi, ujifunzaji wa awali kwa watoto wenye umri wa miaka 2 – 4; taratibu za ulishaji watoto wenye umri wa miezi 24 – 59; na hali ya afya na lishe kwa watoto wenye umri wa miaka 5 – 8. Hakuna mfumo madhubuti

[74] WHO (2018) Nurturing Care Framework for Early Childhood Development: A Framework for helping children survive and thrive to transform health and human potential

[75] Children in Crossfire (CiC) (2018) Early Childhood Development (ECD) Situational Analysis in Tanzania - May 2018.

[76] National multisectoral nutrition action plan (NMNAP) from evidence to policy to action July 2016 to July 2021.United Republic of Tanzania.

wa ufuatiliaji wa viashiria vya MMMAM katika vipengele vyote vya mfumo wa Malezi. Hii inamaanisha kuwa vipengele muhimu vya MMMAM vipo katika hatari ya kusahaulika na kutotengewa rasilimali za kutosha.

Hivi sasa, viashiria vya kisekta vinafuatiliwa na kutolewa taarifa kwenye Wizara na Idara husika. Pia nchi huendesha tafiti za kitaifa ikiwemo Utafiti wa Hali ya Watu na Afya, ambazo kwa pamoja zinasaidia kupata takwimu zinazohusu masuala ya Malezi kwa kuzingatia viashiria vya kidunia ikiwemo viashiria vya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazopimwa katika kuelekea mwaka 2030, ambapo ufuatiliaji unafanyika ili kupima mafanikio ya utekelezaji wa viashiria vya Malezi. Hii inatoa fursa ya kuhakikisha kuwa viashiria vya MMMAM vinatolewa taarifa.

## *2.7 Ukosefu wa usawa katika kuwafikia walengwa*

Kuna viashiria mbalimbali vinavyoonesha kukosekana kwa usawa katika kufikisha huduma kwa watoto ambavyo ni pamoja na maeneo ya kijiogrofia wanamoishi, jinsia na hali ya kijamii. Katika mikoa 24 kati ya 26 ya Tanzania Bara, mahudhurio ya wanafunzi wasichana shuleni yapo juu ikilinganishwa na wavulana, wakati ambapo ukosefu wa usawa wa kijinsia unaonekana katika elimu ya juu ambapo wavulana wana fursa ya elimu ikilinganishwa na wasichana. Kuna tofauti kubwa ya usajili wa wanafunzi katika elimu ya awali miongoni mwa mikoa na hata ndani ya mikoa, ambapo kiwango cha chini ni katika mkoa wa Dar es salaam ambayo ni asilimia 17.7 na kiwango cha juu ni mkoa wa Mara asilimia 67.8[77]

Watoto wanaotoka kwenye familia zenye hali nzuri ya kiuchumi wana nafasi nzuri ya kupata elimu ya msingi na sekondari ikilinganishwa na watoto wanaotoka kwenye familia masikini. Tofauti hii ya usawa katika upatikanaji wa huduma za elimu unajitokeza pia kwenye upatikanaji wa huduma katika vipengele vingine vya mfumo wa Malezi, ukichangiwa na maeneo ya kijiografia, jinsia na hali ya kijamii. Kwa mfano, idadi ya watoto waliopata vitamin A ya nyongeza inatofautiana kwa kiwango cha asilimia 84.9 katika mkoa wa Iringa na asilimia 30 katika mkoa wa Katavi[78], wakati ambapo watoto waliopata huduma ya chanjo inatofautiana katika mkoa wa Kilimanjaro ni asilimia 93.4 ikilinganishwa na Katavi asilimia 54.1[79].

Aidha, tofauti ya usawa imejitokeza pia kwenye ngazi ya jamii / kaya na sio katika utoaji wa huduma pekee. Kwa mfano, asilimia ya watoto walionyonyesha maziwa ya mama pekee kwa miezi sita baada ya kuzaliwa ni kati ya asilimia 90.8 mkoani Kigoma hadi asilimia 29.7 mkoani Arusha; kiwango cha watoto wenye umri wa miaka 0 – 3 ambao kinyesi chao kinahifadhiwa kwenye sehemu salama ni asilimia 99.7 mkoani Dar es salaam hadi asilimia 68 mkoani Simiyu[80] .

Tofauti ya usawa ni kubwa zaidi miongoni mwa watoto walio katika mazingira hatarishi, ambao ni pamoja na watoto wenye ulemavu kama ilivyoelezewa hapo Mwanzo. Tofauti ya usawa imejitokeza pia katika umri, ambapo watoto walio katika umri 0 – 8 wameonekana kuathirika zaidi.

[77] PORALG (2017) Pre-primary, Primary, Secondary, Adult and Non-Formal Education Statistics 2017, Regional Data.

[78] Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children (MoHCDGEC) [Tanzania Mainland], Ministry of Health (MoH) [Zanzibar], Tanzania Food and Nutrition Centre (TFNC), National Bureau of Statistics (NBS), Office of the Chief Government Statistician (OCGS) [Zanzibar] and UNICEF. 2018. Tanzania National Nutrition Survey using SMART Methodology (TNNS) 2018. Dar es Salaam, Tanzania: MoHCDGEC, MoH, TFNC, NBS, OCGS, and UNICEF.

[79] MoHCDGEC (2016) Tanzania Demographic Health Survey and Malaria Indicator Survey (TDHS-MIS) 2015 – 2016

[80] MoHCDGEC (2016) Tanzania Demographic Health Survey and Malaria Indicator Survey (TDHS-MIS) 2015 – 2016.

Kwa mfano asilimia 36.2 ya watoto wenye ulemavu wenye umri wa miaka 5 – 24 wamehudhuria shule ikilinganishwa na asilimia 49.2 ya watoto wa umri huo ambao hawana ulemavu[81] . Takwimu za elimu zinaonesha kuwa chini ya asilimia 0.1 ya watoto wenye ulemavu wameandikishwa katika elimu ya awali, jambo linaloonesha kuwa idadi kubwa ya watoto wenye ulemavu wanakosa fursa ya elimu ya awali. Umasikini pia umehusishwa kuchangia kukosekana kwa huduma za Malezi kwa watoto, ambapo kiwango cha umasikini ni kikubwa vijijini kwa asilimia 81 ikilinganishwa na mjini asilimia 19.1. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba kasi ya ukuaji wa miji inachangia kuongeza kiwango cha umasikini mijini. Ni muhimu kutambua suala la umasikini na athari zake katika miji na maeneo mengine katika utoaji wa huduma za MMMAM nchini.

## *2.8 Wadau wa MMMAM nchini Tanzania*

Wadau wa MMMAM nchini Tanzania wamechangia kwa kiwango kikubwa kusukuma ajenda ya kuimarisha uratibu wa kisekta. Kikosi Kazi cha Taifa cha MMMAM kinachowaleta pamoja wawakilishi kutoka katika Wizara zote za kisekta, Idara na Taasisi zenye mamlaka katika masuala mbalimbali ya Malezi. Pia jukwaa hilo linawaleta pamoja wawakilishi kutoka taasisi za elimu, wadau, na asasi za kiraia kutoka katika sekta mbalimbali (ikiwa ni pamoja na afya, lishe, elimu, ulinzi na usalama wa mtoto). Kikosi Kazi cha Taifa cha MMMAM kimetokana na kuhuishwa kwa mjadala wa kitaifa wa Malezi. Mchakato wa kuandaa mpango huu ni matokeo ya mjadala wa kitaifa na maazimio ya wadau wa MMMAM uliofanyika Disemba 2018.

Wadau wa MMMAM nchini wanatekeleza afua katika vipengele mbalimbali vya Malezi, kulingana na mamlaka na mipaka ya Taasisi zao. Afua za MMMAM zinazotolewa na wadau zinajumuisha program za afya, lishe, elimu, ulinzi na usalama wa mtoto. Pia kuna program zinazolenga baadhi ya vipengele vya mfumo wa Malezi kwa mfano afya, lishe, elimu, ulinzi na usalama wa mtoto, na ujifunzaji wa awali au uchangamshi wa awali, na Malezi yenye muitikio. Program hizo zinatekelezwa katika mikoa /halmashauri mbalimbali kulingana na mipaka ya taasisi husika. Pia katika kipindi cha utekelezaji wa afua hutofautiana kutoka mwaka mmoja hadi miaka mitano ambapo miradi mingi inaonesha kuwa itafikia ukomo mwaka 2020 – 2023.

Uchambuzi unaonesha kuwa afua za MMMAM zinatekelezwa na wadau mbalimbali waliotawanyika nchini kote, ingawa kuna baadhi ya mikoa yenye wadau wengi zaidi ikiwemo (Morogoro, Dodoma, Singida, Arusha, Mbeya, Mwanza, Iringa na Kigoma), kama inavyoonekana kwenye Mchoro Na 6. Wakati huo huo, baadhi ya mikoa ikiwemo (Katavi, Rukwa, Kagera na Pwani) ina ufadhili mdogo kutoka kwa wadau wanapotekeleza afua za MMMAM, pia baadhi ya mikoa hii haifanyi vizuri katika utekelezaji wa viashiria vya MMMAM kama inavyoonekana kwenye dashbodi ya CiC[82] .

Vilevile, ni muhimu kutambua kwamba ndani ya mikoa kuna halmashauri na maeneo ya kijiografia yanayopokea msaada kwa kiwango kidogo. Kwa upande mwingine, hakuna wadau wanaotekeleza afua za MMMAM katika ngazi ya Taifa na hivyo hakuna taarifa za kutosha kuhusu huduma zinazotolewa kwa ubora ambazo zinaweza kutekelezwa nchini kote, na kujumuishwa kwenye Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM. Uwekezaji mkubwa wa masuala ya MMMAM unatarajiwa kujitokeza katika masuala ya afya, lishe na ujifunzaji wa awali, inatarajiwa kuwa wadau watanufaika kwa kupata miongozo itakayotolewa na Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM. Program hii itasaidia kuweka kwa pamoja afua za MMMAM kwa faida ya Mfumo wa Malezi na hivyo kufikia walengwa wengi zaidi.

[81] National Bureau of Statistics Ministry of Finance & Office of Chief Government Statistician Ministry of State, President Office, State House and Good Governance (2016) Disability Monograph

[82] Children in Crossfire (CiC) (draft 2020) Tanzania ECD Dashboard: Consolidated

*Mchoro namba 6:* Wadau wanaotekeleza afua za MMMAM kwa mkoa





# *SURA YA 3:* DHANA YA MFUMO WA PROGRAMU JUMUISHI YA TAIFA YA MMMAM

## *3.1 Misingi ya dhana ya Mfumo wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM*

Ili kukuza maendeleo ya mtoto katika nyanja zote za ukuaji kunahitajika mbinu shirikishi na rasilimali kutoka sekta zote. Uanzishwaji na utekelezaji wa mpango huu, tumeazima mifumo ya dhana zifuatazo za kukuza maendeleo ya mtoto kwa kutumia mbinu ya sekta shirikishi kutoka kwenye machapisho ya Lancet kuhusu maendeleo ya awali ya watoto wadogo[83]. Mfumo huu unatazama maendeleo ya mtoto kama matokeo ya ushirikiano wa sekta mbalimbali kama vile elimu, afya, usalama na ulinzi. Shughuli hizi zinatekelezwa katika mazingira ya kuwalea watoto na kuakisi vipengele vya malezi ikiwa ni pamoja na afya, lishe, fursa za ujifunzaji wa awali, uwajibikaji wa mzazi/mlezi katika kumlea mtoto pamoja na usalama na ulinzi. Malezi ni umakini wa mzazi/mlezi kwa mahitaji ya mtoto kimwili, kihisia, kumlinda mtoto na madhara, kumpatia mtoto fursa ya kudadisi na kujifunza, kuchangamana na watoto wenzie ambao wanawawezesha kuwajibika, kuchechemua hisia na miili yao[84]" . Maendeleo haya hufanyika katika mazingiza muhimu ya malezi pamoja na nyumbani ambako kuna watoa huduma muhimu kama vile wazazi/walezi, wanafamilia na ndugu ambao huchua jukumu la kumlea mtoto. Pia malezi hufanyika katika vituo vya kulelea watoto vya aina zote.

Ili familia na jamii zitoe malezi bora kwa watoto kama ilivyo kwenye mwongozo wa malezi kwa mtoto, kunahitajika mazingira wezeshi kwa kuwepo na sera jumuishi ya malezi makuzi na maendeleo ya mtoto, uratibishaji mzuri wa kisekta pamoja na rasilimali za kutosha. Jambo la muhimu zaidi katika kufanikisha malezi bora ni kuwawezesha wazazi na walezi kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazohusiana na umasikini, ukosefu wa chakula, afya ya mama mjamzito, msongo wa mawazo, migogoro na kukosekana kwa usalama. Hii inahitaji jamii zima kushiriki kwa kuwepo na mbinu zitakazowalenga wadau wote kutoka kwenye sekta muhimu kwa ukuaji na maendeleo ya mtoto. Sekta hizi ni elimu, afya, haki, ustawi wa jamii, maendeleo ya jamii na ulinzi wa mtoto.

Kwa kuzingatia uzoefu na mafunzo yaliyopatikana katika utekelezaji wa MMMAM nchini Tanzania, Programu hii inawaleta pamoja watendaji kutoka sekta muhimu za serikali na asasi za kiraia. Wigo huu mpana wa wadau umeshiriki katika hatua muhimu za kuandaa programu hii pia wadau watashiriki katika kuutekeleza, kuuboresha na kutathmini maendeleo yake. Mbinu iliyozoeleka kutoa huduma bora za malezi ni mbinu ambayo inazingatia unafuu wa gharama za utekelezaji ikiepuka kutokurudia shughuli ambazo tayari zinafanyika na kusaidia kuleta muunganiko hususani wa malengo yakiongozwa na uratibu jumuishi, uwepo wa rasilimali za utekelezaji, usimamizi, na tathimini tuliyojifunza kutokana na utekelezaji wa programu ya MMMAM.

[83] Richter, Linda M.; Daelmans, Bernadette; Lombardi, Joan; Heymann, Jody; Boo, Florencia Lopez; Behrman, Jere R. et al. (2017): Investing in the foundation of sustainable development: pathways to scale up for early childhood development. In The Lancet 389 (10064), pp. 103–118. DOI: 10.1016/S0140-6736(16)31698-1.

[84] Richter, Linda M.; Daelmans, Bernadette; Lombardi, Joan; Heymann, Jody; Boo, Florencia Lopez; Behrman, Jere R. et al. (2017): Investing in the foundation of sustainable development: pathways to scale up for early childhood development. In The Lancet 389 (10064), pp. 103–118. DOI: 10.1016/S0140-6736(16)31698-1.

***Mchoro namba 7:*** Mfumo wa utekelezaji wa kukuza maendeleo ya watoto kupitia mbinu ya sekta shirikishi[85] .




## 3.2 Nadharia ya Mabadiliko

Uanzishwaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM umeongozwa na mjumuisho wa dhana ya nadharia ya mabadiliko na mfumo wa bao mantiki. Dhana ya nadharia ya mabadiliko ni mchoro unao ainisha njia mbalimbali zinazoweza kutumika kufikia mabadiliko lengwa (mafanikio katika lugha ya bao mantiki). Njia hizi zinaashiria mazingira fulani yanahitaji kubadilishwa (sawia na mabadiliko tarajiwa kwenye bao mantiki) na kwamba yakibadilishwa yataweza kuleta mabadiliko yaliyotarajiwa. Si mara zote m mazingira yote yanaweza kusababisha mabadiliko kwenye uwezo wakati wa utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM. Mazingira haya yanabebwa na mifumo ya kijamii ambayo haitabiriki katika ufanyaji kazi wake kama vile mifumo ya kiutamaduni, kijamii, kisiasa, kidini, kiuchumi, kihistoria kijiografia na mazingira yanayofanana na hayo nchini[86]. Hata hivyo watekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM wanao uwezo wa kukabiliana na mabadiliko (matokeo tarajiwa baada ya utekelezwaji wa shughuli kama ilivyo katika bao mantiki). Mabadiliko haya lengwa ni matokeo ya moja kwa moja ya utekelezwaji wa shughuli mbalimbali zitakazopangwa na kutekelezwa na wadau wa MMMAM. Mabadiliko haya baada ya utekelezwaji wa shughuli mbalimbali yanalenga kuwa chachu ya mabadiliko makubwa hatimaye kupata matokeo yaliyokusudiwa.

[85] Richter, Linda M.; Daelmans, Bernadette; Lombardi, Joan; Heymann, Jody; Boo, Florencia Lopez; Behrman, Jere R. et al. (2017): Investing in the foundation of sustainable development: pathways to scale up for early childhood development. In The Lancet 389 (10064), pp. 103–118. DOI: 10.1016/S0140-6736(16)31698-1.

[86] United Republic of Tanzania (2016): National Multi-sectoral Nutrition Action Plan (NMNAP) for the period July 2016 – June 2021.

Tofauti na nadharia ya bao mantiki, nadharia ya mabadiliko inaruhusu maafisa mipango kuunganisha dhana ambazo zinaweka msisitizo kwenye njia mbalimbali za kufikia malengo yaliyotarajiwa. Dhana hizi huanisha mazingira ambayo ni muhimu katika kufanikisha nadharia ya mabadiliko au sehemu yake lakini huwa ni nje ya uwezo wa mradi[87]. Katika nadharia ya bao mantiki, dhana huwa ni mazingira yanayohitajika kuleta mabadiliko tofauti na nadharia ya mabadiliko ambayo maafisa mipango hutumia kuwaongoza kufikiria au kutabiri njia zitakazoweza kuleta mabadiliko.

Mabadiliko ambayo Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM inatarajia kuyaona baada ya miaka mitano ya utekelezaji ni ***"Watoto wote Tanzania wapo kwenye mueleko sahihi wa kufikia ukuaji timilifu."*** Mabadiliko lengwa yatapimwa kwa kuzingatia viwango vya viashiria vya matokeo ambavyo vimerudubishwa kutoka ngazi ya kitaifa na kimataifa. Viashiria na malengo haya yanatokana na mipango mbalimbali ya kisekta pamoja na malengo ya maendeleo endelevu.

Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM imeweka vipaumbele vinne (4) vya kufikia mabadiliko (mabadiliko tarajiwa) ambavyo ni matokeo ya uchambuzi wa maendeleo ya watoto uliofanyika kusaidia kuelezea hali halisi ya utoaji wa huduma za malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto nchini Tanzania. Uchambuzi huo uliabainisha hali halisi ya huduma ya malezi jumuishi kwa kutambua uwepo wa huduma hizo nchini, fursa zilizopo za kuboresha huduma pamoja na kubainisha mapungufu ambayo yanahitaji utatuzi. Inatarajiwa kwamba mabadiliko haya manne (4) yatachangia kuleta matokeo yanayokusudiwa (matokeo katika lugha ya mfumo wa bao mantiki).

## *Malengo manne ya muda mrefu:*

1. Mazingira wezeshi yameboreshwa kuwezesha uratibu wenye ufanisi na utoaji huduma za malezi jumuishi;

2. Mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora imeimarishwa;

3. Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma bora na zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao;

4. Wazazi, walezi, familia na jamii wamejengewa uwezo wa kutekeleza taratibu sahihi za malezi jumuishi.

***Mchoro wa 8*** ni majumuisho ya njia za mabadiliko kama unavyotazamwa katika mazingira ya Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM. Mchoro huu unaorodhesha ngazi tatu kuu za matokeo pamoja na matokeo ya kati, matokeo ya muda mrefu, dhana za matokeo na mabadiliko yanayotarajiwa

[87] Starr, L. (2019) Theory of Change: Facilitator's Guide. Washington DC: The Technical and Operational Performance Support TOPS) Programme.

*Mchoro namba 8:* Nadharia ya mabadiliko ya Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM





# *SURA YA 4:* MATOKEO TARAJIWA NA MIKAKATI YA KUYAFIKIA

## *4.1 Miongozo ya Utekelezaji.*

Utekelezaji wa Programu jumuishi ya Taifa ya MMMAM utatumia miongozo ya mfumo wa malezi jumuishi ambayo ni:-

*i.* ***Haki ya mtoto ya kuishi na kukua*** inalenga kuhakikisha kuwa haki za mtoto zinatambulika na kutekelezwa tukitambua kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizoridhia na kusaini mkataba wa kimataifa wa haki za mtoto na mapendekezo ya kamati Na. 7 (2005) katika kutekeleza haki za watoto wadogo.

*ii.* ***Hakuna mtoto atakayeachwa nyuma*** inalenga kuhakikisha kuwa huduma za malezi jumuishi ya watoto zinawafikia watoto wote wenye umri wa miaka 0-8 pamoja na kuzingatia masuala ya jinsia. Watoto walio katika mazingira hatarishi kwa mfano watoto wenye VVU, yatima, watoto wanao umwa sana pamoja na wenye utapiamlo, watoto waliopo mahabusu, kambini, na wenye changamoto katika ukuaji na ulemavu.

*iii.* ***Malezi katika Familia*** ni mbinu ya malezi inayohusisha familia kwa ujumla katika kumlea mtoto. Mbinu hii inatambua umuhimu wa kuwahusisha wanafamilia wote katika malezi kama vile mama, baba, babu, bibi na walezi wengine kuhakikisha wanapatiwa elimu ya malezi ili waweze kutoa huduma za malezi jumuishi kwa watoto.

*iv.* ***Ushiriki wa Serikali kwa ujumla*** inalenga kuhakikisha sekta zote za MMMAM zinafanya kazi katika uratibu ili kuhakikisha huduma bora za malezi na makuzi ya watoto zinatolewa.

*v.* ***Ushiriki wa Jamii kwa Ujumla*** inalenga kuhakikisha kuwa jamii yote pamoja na serikali, asasi za kiraia, taasisi za elimu, sekta binafsi, familia na wadau wengine wa MMMAM wanashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa programu, pia inahamasisha umiliki na ushiriki wa jamii katika ngazi mbalimbali huku ikizingatia utofauti wa mila, desturi.

## *4.2 Matokeo tarajiwa, matokeo ya muda mrefu na matokeo ya muda mfupi*

Programu jumuishi ya Taifa ya MMMAM ina lengo la muda mrefu lenye kuhakikisha maendeleo katika ukuaji wa watoto wote wa Tanzania yanapatikana ili waweze kufikia ukuaji timilifu.

Kufanikisha lengo hili programu itafanya kazi katika malengo mahususi ya muda mrefu manne. Malengo hayo yatashughulikia changamoto za kimfumo na kiprogramu zinazoathiri ukuaji na maendeleo ya watoto wadogo wenye umri kati 0-8 nchini Tanzania, kutumia afua za kimkakati zitakazotekelezwa na wadau mbalimbali katika kuboresha matokeo ya ukuaji kwa watoto wadogo. Kwa kila lengo la muda mrefu kutakuwa na mkakati utakaotumika katika utekelezaji wa afua za Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM.

***Programu italeta mabadiliko kwa watoto wadogo kwa kutekeleza mambo yafuatayo:***

### 4.2.1 Kuboresha mazingira wezeshi

Katika kutoa huduma jumuishi kwa watoto wadogo nchini Tanzania ni lazima kuwepo na mazingira wezeshi yatakayosaidia watekelezaji katika kila sekta ili kupata utimilifu wa huduma kwa watoto wadogo. Mazingira yanayohitajika ni pamoja na sheria na mifumo inayotoa kipaumbele katika utoaji wa huduma za MMMAM, kutenga rasilimali za kutosha katika kutekeleza afua za MMMAM katika sekta mbalimbali, kuwepo na mifumo imara ya uratibu katika ngazi zote. Kuwepo na wadau wanaohamasisha utekelezaji wa masuala ya malezi kwa watoto wadogo ili kuleta mabadiliko chanya katika matendo, mtazamo na tabia. Kutokana na mapungufu yaliyoonekana katika maeneo muhimu yatashughulikiwa katika matokeo ya muda mfupi kama yalivyoainishwa katika kipengele Na.1.3. (kuboresha sera/ miongozo/mitaala inayoshughulikia masuala ya MMMAM yatapatikana kupitia matokeo yafuatayo; kufanya mapitio ya sera, miongozo, mitaala na miongozo ya mafunzo), pamoja na kuhakikisha imejumuisha masuala yote ya malezi; kuimarisha uratibu jumuishi na uhamasishaji wa masuala ya MMMAM katika ngazi zote ili kuongeza uwajibikaji kwa kutenga rasilimali kwa ajili ya upatikanaji wa huduma.

### 4.2.2 Kuimarisha mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora

Utekelezaji wa programu ya MMMAM unahitaji nguvu kazi yenye ujuzi na umahiri, uimarishaji wa mifumo ya rufaa, inayohamasisha, tafiti za kutosha na upatikanaji wa taarifa zinazohusu MMMAM na mfumo wa tathmini, ufuatiliaji na kuweka kumbukumbu kwa ajili ya kujifunza, katika kuleta matokeo chanya kwa watoto wenye umri wa miaka 0-8. Matokeo haya yameorodhesha shughuli zitakazosaidia watoa huduma kushiriki katika utekelezaji wa programu hii. Matokeo muhimu ni: upatikanaji wa watoa huduma wenye ujuzi na umahiri katika kutoa huduma za malezi, uimarishaji wa mifumo ya rufaa, upatikanaji wa tafiti za ndani kwa ajili ya kupata taarifa za uandaaji wa programu, kuwepo kwa mfumo mmoja wa tathmini, ufuatiliaji na kuweka kumbukumbu kwa ajili ya kujifunza katika sekta zote.

### 4.2.3 Kuongeza upatikanaji wa huduma bora na zilizoratibiwa vema kwa ajili ya watoto wenye umri wa mika 0-8

Lengo kuu la programu hii ni kuongeza upatikanaji wa huduma jumuishi za MMMAM kwa watoto wadogo ambapo watoto wanapata lishe bora, afya bora, mazingira salama, wanapata mwitikio wa malezi, na fursa ya ujifunzaji wa awali. Huduma hizi zinapaswa kuratibiwa vema na kujumuishwa katika utekelezaji. Watoto wote wadogo wanapata huduma jumuishi za MMMAM zinazochangia ukuaji timilifu wa watoto unaosababisha matokeo chanya kwa watoto wenye umri kati ya miaka 0-8.Upatikanaji wa huduma bora za afya; lishe, kuongezeka upatikanaji wa ulinzi na usalama wa Watoto; kuwepo kwa huduma za malezi yenye mwitikio na fursa ya ujifunzaji wa awali.

### 4.2.4 Kuwawezesha walezi, wazazi na jamii kutoa huduma ya malezi jumuishi

Programu ya MMMAM inalenga kuleta mabadiliko kwa watekelezaji wa masuala ya MMMAM kuanzia ngazi ya taifa hadi ngazi ya jamii ikijumuisha na familia. Hii itafanyika kwa kuhamasisha na kujenga uelewa wa jamii juu ya umuhimu wa uwekezaji kwa watoto wadogo. Jamii na wadau kushiriki katika utoaji wa huduma timilifu za malezi. Programu hii itashirikisha jamii kwa kusikiliza hoja zao, imani, mila na desturi ambapo wazazi na walezi watakua mstari wa mbele katika utoaji wa huduma za MMMAM.

## *4.3 Matokeo ya Muda Mrefu, Mfupi na wa Kati*

Programu jumuishi ya taifa ya MMMAM imetoa maelezo katika matokeo ya muda mrefu, wa kati na mfupi. Uchambuzi wa shughuli zitakazofanyika zimeelezwa katika kiambatisho cha 2.

### Matokeo ya Muda Mrefu 1: Mazingira wezeshi yameboreshwa kuwezesha uratibu wenye ufanisi na utoaji huduma za malezi jumuishi

Matokeo yatahakikisha uwepo wa mazingira wezeshi ya kutoa hudumu jumuishi za malezi zinawafikia watoto wote nchini. Mazingira haya yatahakikisha uwepo na upatikanaji wa msaada wa kifedha, sera, sheria na miongozo, kuendelea kuhamasisha kujumuishwa kwa masuala ya malezi na makuzi katika mitaala na miongozo ya mafunzo kwa watoa huduma katika sekta zote ili waweze kutoa huduma jumuishi kwa Watoto wote.

### Matokeo ya muda mfupi 1.1: Uhamasishaji wa masuala ya MMMAM katika ngazi zote umeimarishwa ili kuongeza uwajibikaji na upatikanaji wa huduma za malezi jumuishi

Matokeo haya ya muda mfupi yatahakikisha kuna ongezeko la uelewa , elimu na ujuzi miongoni mwa wafanya maamuzi katika ngazi zote na kwa wadau wa MMMAM ili kuona umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wadogo wenye umri wa miaka 0-8 kuanzia ngazi ya taifa hadi ngazi ya jamii. Ili kupata matokeo haya mikakati mbalimbali itatumika.

#### Matokeo ya papo kwa papo 1.1.1: Mkakati wa uhamasishaji wa MMMAM umeandaliwa

Mkakati wa kitaifa wa uhamasishaji wa MMMAM utatengenezwa ili kutoa mwongozo katika kutekeleza programu ya kufanya uhamasishaji wa utekelezaji katika ngazi zote ili kuboresha huduma jumuishi za malezi na makuzi zinazotolewa kwa watoto wadogo.

***Shughuli 1.1.1.1:*** Kuandaa Mkakati Jumuishi wa Taifa wa MMMAM unaotafsiri mfumo wa malezi jumuishi

#### Matokeo ya papo kwa papo 1.1.2: Uhamasishaji wa viongozi katika ngazi zote umefanyika

Miongoni mwa shughuli za awali zitakazofanyika katika utekelezaji wa Programu jumuishi ya taifa ya MMMAM ni kutoa elimu na uhamasishaji kwa viongozi kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwa Watoto wadogo. Elimu itatolewa kwa viongozi wote katika ngazi mbalimbali ili waweze kushiriki na kufanya maamuzi kuhusu utekelezaji wa MMMAM.

***Shughuli 1.1.2.1:*** Kufanya mkutano na wadau wa maendeleo ili waweze kuchangia gharama za utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM

***Shughuli 1.1.2.2.:*** Kufanya mkutano wa uhamasishaji kwa kamati mbalimbali za bunge kuwajengea uelewa kuhusu Programu Jumuishi ya MMMAM

***Shughuli 1.1.2.3:*** Kufanya mikutano ya uhamasishaji kwa maafisa kutoka ngazi za juu za wizara za kisekta ili waweze kuingiza viashiria vya masuala ya MMMAM katika mifumo ya utoaji taarifa

***Shughuli 1.1.2.4:*** Kutoa mafunzo ya awali kwa waandishi wa habari ili kuwajengea uelewa kuhusu masuala ya MMMAM waweze kutoa taarifa sahihi juu ya masuala ya watoto wenye umri wa miaka 0-8

***Shughuli 1.1.2.5:*** Kuhamasisha mapitio ya mitaala ya vyuo vikuu (vyuo vya ualimu, vyuo vya uuguzi na taasisi za ustawi wa jamii) ili kuingiza masuala ya elimu ya awali na ya malezi jumuishi

***Shughuli 1.1.2.6:*** Kuhamasisha viongozi wa dini ili kujumuisha masuala ya malezi jumuishi katika mwongozo wa kidini

## Matokeo ya muda Mfupi 1.2: Uratibu wa sekta mbalimbali kwenye ngazi zote umeimarishwa

Famila na jamii inahitaji mfumo jumuishi katika kusaidia kutoa malezi jumuishi. Hii itafanyika kwa kuboresha mifumo ya uratibu wa programu, kufanya mikutano ya mara kwa mara ya kupitia utekelezaji wa aprogramu na kuhamasisha utekelezaji wa MMMAM ili kuongeza uwajibikaji katika ngazi zote.

### Matokeo ya papo kwa papo 1.2.1: Mfumo wa kitaifa wa uratibu wa programu umeimarishwa

Shughuli za MMMAM zitaratibiwa kwa kuzingatia mifumo iliyopo katika ngazi zote (kitaifa na ngazi za chini) ili kuhakikisha ufanisi katika utoaji huduma jumuishi za malezi na makuzi. Hivyo kutakua na mchakato wa kuimarisha mifumo iliyopo ili kujumuishi masuala jumuishi ya malezi na makuzi katika uratibu thabiti.

***Shughuli 1.2.1.1:*** Kufanya mapitio ya mwongozo wa uratibu/hadidu za rejea ili kujumuisha Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM katika ngazi zote (Taifa-Mkoa-Halmashauri-Kata-vijiji/mtaa)

***Shughuli 1.2.1.2:*** kutoa mafunzo ya awali kwa wajumbe wa kamati wa sekta mbalimbali kuhusu masuala ya MMMAM na uratibu katika ngazi ya taifa (kamati elekezi, kamati tendaji, vikundi kazi vya afya, lishe, ulinzi na usalama wa mtoto, ujifunzaji wa awali na malezi yenye mwitikio)

***Shughuli 1.2.1.3:*** Kutoa mafunzo ya awali kwa wajumbe wa vikundi kazi vya Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM kuhusu Programu, majukumu na wajibu wao

***Shughuli 1.2.1.4:*** Kutoa mafunzo ya awali kuhusu Program Jumuishi ya Taifa ya MMMAM kwa wawezeshaji 20 kwa kila Mkoa katika mikoa 26 ya Tanzania bara.

### Matokeo ya papo kwa papo 1.2.2: Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM imefanyiwa mapitio

Programu itajumuisha mikutano ya mwaka, mikutano ya mara kwa mara ya kikosi kazi katika ngazi ya taifa na ngazi ya chini ambayo itasaidia Serikali kufahamu hali ya utekelezaji, mafanikio na changamoto ili kufanya maboresho.

***Shughuli 1.2.2.1:*** Kufanya kongamano la MMMAM kila baada ya miaka 2

***Shughuli 1.2.2.2:*** Kufanya mikutano ya pamoja ya mwaka ya sekta mbalimbali ya mapitio ya programu ya MMMAM

***Shughuli 1.2.2.3:*** Kufanya Mkutano wa mwaka wa viongozi wa ngazi ya juu

***Shughuli 1.2.2.4:*** Kufanya mikutano ya kitaifa ya robo mwaka ya vikundi kazi vya watalaam wa MMMAM

***Shughuli 1.2.2.5:*** Kufanya mikutano ya robo mwaka ya mkoa ya mapitio ya Programu Jumuishi Taifa ya MMMAM

***Shughuli 1.2.2.6:*** Kufanya mikutano ya robo mwaka ya mapitio ya programu ya MMMAM katika ngazi ya Halmashauri kwa ajili ya kushirikisha na kutoa mapendekezo ya taarifa ya utekelezaji wa MMMAM kutoka katika ngazi ya Kata na Vijiji/Mtaa

***Mchoro namba 9:*** Uratibu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM, Ufuatiliaji na tathmini na muundo wa utekelezaji




## Matokeo ya muda mfupi 1.3: Sera, Miongozo, Mitaala na vitini vya kufundishia Vimeandaliwa/ kufanyiwa mapitio ili kuingiza vipengele vyote vya malezi jumuishi

Utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM unaongozwa na mfumo wa malezi jumuishi hivyo unahitaji sera, miongozo, mitaala na miongozo ya ujifunzaji kuhakikiwa na kuboreshwa ili kuleta ufanisi katika utelekelezaji wa programu.

Matokeo ya papo kwa papo 1.3.1: Sera zinazohusiana na MMMAM zimefanyiwa mapitio na kupitishwa

Serikali ina mpango wa kufanya kazi pamoja na wadau katika kupitia na kuboresha sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 ili kuimarisha kipengele cha malezi jumuishi ambacho ni muhimu sana katika maendeleo ya ukuaji wa mtoto. Pia sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 itafanyiwa mapitio na maboresho na kusambazwa ili kuhakikisha masuala jumuishi ya malezi yanazingatiwa. Pia kutengeneza kwa muhtasari ili kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu haki za watoto na jinsi ya kuzilinda.

***Shughuli 1.3.1.1:*** Kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 ili kujumuisha masuala ya malezi jumuishi

***Shughuli 1.3.1.2:*** Kusambaza Sera ya Afya iliyofanyiwa mapitio

***Shughuli 1.3.1.3:*** Kufanya mapitio ya Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ili kuingiza masula ya malezi jumuishi

Matokeo ya papo kwa papo 1.3.2: Mingozo imefanyiwa mapitio imeandaliwa Ili kuhakikisha kuwa huduma jumuishi za malezi na makuzi zinazingatiwa miongozo mbalimbali itafanyiwa maboresho na mingine kutengenezwa.

***Shughuli 1.3.2.1:*** Kufanya mapitio na kuoanisha miongozo iliyopo (kutoka huduma ya baba, mama na mtoto, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Jamii, Elimu na Serikali za Mitaa) kwa ajili ya kufanya usimamizi saidizi wa pamoja ili kuingiza masuala ya malezi jumuishi

***Shughuli 1.3.2.2:*** Kufanya vikao vya mapitio ya Mwongozo wa Walezi wa watoto wadogo ili kuingiza maudhui maalum ya watoto kuanzia miaka 0-2.

***Shughuli 1.3.2.3:*** Kukamilisha rasimu ya Mwongozo wa kitaifa wa utekelezaji wa Malezi kwa Makuzi na Maendeleo ya awali ya Mtoto

Matokeo ya Papo kwa papo 1.3.3: Mitaala/Miongozo imepitiwa

Mitaala na miongozo iliyopo itafanyiwa mapitio ili kuhakikisha vipengele jumuishi vya malezi na makuzi vimeingizwa katika mitaala /miongozo hiyo.

***Shughuli 1.3.3.1:*** Kuandaa Mtaala wa MMMAM wa kitaifa unaozingatia utamaduni na mahitaji ya ukuaji wa watoto kwa Walezi wa Watoto Wadogo (ngazi ya Astashahada na Stashahada kulingana na viwango vya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi ngazi 4-6)

***Shughuli 1.3.3.2:*** Kuandaa mkoba wa mafunzo Jumuishi ya MMMAM ili kuongeza vipengele vya Malezi Jumuishi

## Matokeo ya Muda Mrefu 2: Mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora imeimarishwa

Matokeo ya muda mrefu 2 yataangalia uimarishaji wa mifumo kwa ajili ya utoaji wa huduma ili kuhakikisha ubora na uimara wa huduma jumushi za malezi na makuzi zinawaafikia watoto wote nchini Tanzania. Hii itajumuisha kuwajengea uwezo watoa huduma ili waweze kutoa huduma bora, miongozo inayosimamia ubora, zana, kuwepo na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini mifumo ya kutoa rufaa kutoka ngazi ya chini kwenda ngazi ya juu na ngazi za juu kwenda ngazi za chini, pia kufanya utafiti na kuweka kumbukumbu za ubunifu wa utekelezaji wa masuala ya MMMAM kwa ajili ya kupanga mipango ya baadaye.

## Matokeo ya muda mfupi 2.1: Uwepo wa watoa huduma wenye ujuzi na umahiri kwenye malezi jumuishi

Matokeo tarajiwa ni kuhakikisha kuwa Tanzania ina rasilimali watu ambao wana ujuzi na umahiri wa kutoa huduma za MMMAM katika ngazi zote. Ili kufanikisha hayo mikakati mbalimbali itatumika.

Matokeo ya papo kwa papo 2.1.1 Timu ya wakufunzi wa MMMAM wa kitaifa (Wakufunzi wakuu) imeundwa

Ili kuwa na ufanisi katika utekelezaji wa programu hii kitaindwa kikosi cha taifa cha wawezeshaji wa MMMAM kitakachotoa huduma za malezi na makuzi. Kufanikisha shughuli hii waweeshaji watachaguliwa na kupatiwa mafunzo kwa kutumia mkoba wa mafunzo wa MMMAM yatakayotolewa katika ngazi zote na kikosi hicho kilichopatiwa mafunzo.

***Shughuli 2.1.1.1:*** Kufanya mafunzo ya kitaifa ya mkoba Jumushi wa MMMAM (Malezi Jumuishi) kwa timu ya wakufunzi ya uendeshaji katika ngazi ya taifa (Mafunzo ya Wakufunzi wakuu)

***Shughuli 2.1.1.2:*** Kufanya vikao vya mafunzo kuhusu mkoba jumuishi wa Kitaifa wa MMMAM kwa wakufunzi katika ngazi ya Mkoa (Mafunzo kwa Wakufunzi wakuu ngazi ya Mkoa)

***Shughuli 2.1.1.3:*** Kufanya mafunzo ya ngazi kwa ngazi kuhusu Mkoba Jumuishi wa Kitaifa wa MMMAM kwa wakufunzi katika ngazi ya Halmashauri.

Matokeo ya papo kwa papo 2.1.2: Uwezo wa walimu wa elimu ya Awali na walezi wa watoto wadogo kuhusu MMMAM kuimarishwa

Elimu ya MMMAM kwa walimu wa elimu ya awali ni muhimu sana katika ujifunzaji na uelekeo wa makuzi ya watoto wadogo kwenye madarasa ya elimu ya Awali.

***Shughuli 2.1.2.1:*** Kufanya mapitio ya programu ya mwendelezo wa maendeleo ya taaluma ya walimu wa elimu ya Awali

S***hughuli 2.1.2.2:*** Kufanya mafunzo kazini kwa wakufunzi katika vyuo vya ualimu, Vyuo vya elimu ya Walezi wa watoto wadogo, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na vyuo vikuu kuhusu MMMAM

***Shughuli 2.1.2.3:*** Kuwezesha kuajiri/ kuwapangia vituo maafisa wakujitolea na kuwapa fursa wanaojifunza kazi kwa vitendo kutoka kwenye vyuo vikuu na vyuo vya ualimu kusaidia kutoa elimu ya Awali na madarasa ya mwanzo ya shule ya Msingi (darasa la kwanza mpaka la tatu).

Matokeo ya Papo kwa papo 2.1.3: Uwezo wa watoa huduma za moja kwa moja kwa walengwa kutumia Mkoba Jumuishi wa MMMAM umeimarishwa

Matokeo haya yanalenga kuimarisha uwezo wa watendaji wa masuala ya MMMAM ili waweze kutoa huduma bora kwa watoto wadogo wenye umri kati ya miaka 0-8. Kujifunza kunaanza kabla mtoto hajazaliwa na anapokua amezaliwa, hivyo ni lazima kuwe na mazingira wezeshi ya uchangamshi ambayo yataendelea muda wote kama sehemu ya kujifunza katika miaka ya mwanzo ambapo msingi wa maisha ya baadaye unajengwa. Kwenye njia hii ya kujifunza, wazazi, walezi, wahudumu wa afya, walimu wa elimu ya Awali ni makundi muhimu. Kuwapatia mbinu, ujuzi na vifaa itawasaidia katika kazi yao ya kutoa elimu ya MMMAM. Mfunzo ya ujengaji uwezo yatahusisha mkoba wa mafunzo ya MMMAM, mkoba wa huduma za Afya ya wanawake, Watoto wenye umri wa siku 0-28 na watoto wadogo wenye umri wa miezi 0-59, kitabu kipya cha ufuatiliaji wa ukuaji na maendeleo ya mtoto. Ufuatiliaji na usimamizi wa karibu utakuwa ni sehemu ya ufuatiliaji katika ngazi ya Halmashauri.

***Shughuli 2.1.3.1:*** Kutoa mafunzo kwa kutumia Mkoba Jumuishi wa MMMAM

***Shughuli 2.1.3.2:*** Kutoa mafunzo katika ngazi ya Halmashauri kuhusu unasihi wa afya ya akili na kisaikolojia na kutoa msaada kwa waliofanyiwa ukatili.

***Shughuli 2.1.3.3:*** Kutoa mafunzo katika ngazi ya Kata kuhusu unasihi wa afya ya akili na kisaikolojia na kutoa msaada kwa waliofanyiwa ukatili nchi nzima

***Shughuli 2.1.3.4:*** Kutoa mfunzo kwa watoa huduma wa afya kuhusu kijitabu cha ufuatiliaji na maendeleo ya mtoto kilichounganishwa na mkoba wa malezi kwa makuzi na maendeleo ya mtoto

***Shughuli 2.1.3.5:*** Kuimarisha malezi yenye mwitikio, ujifunzaji wa awali na vipengele vya huduma za maji safi na mazingira kwa kutumia mkoba uliofanyiwa mapitio wa watoa huduma za afya katika ngazi ya jamii

Matokeo ya Papo kwa papo 2.1.4:  Mkoba jumuishi wa mafunzo ya MMMAM kwa wanafunzi waliopo vyuoni umeandaliwa

Wanafunzi walio katika vyuo vya mafunzo ni kundi muhimu katika kuendeleza ukuaji na maendeleo ya watoto wadogo. Ili kufanikisha jambo hili programu hii inalenga kuwajengea uwezo kundi hili kwa kujumuisha mafunzo ya MMMAM katika vyuo vya mafunzo.

***Shughuli 2.1.4.1:*** Kuandaa programu ya mtandao ya Elimu masafa kuhusu MMMAM kwa walezi wa watoto wadogo na vyuo vya ualimu vya elimu ya Awali

***Shughuli 2.1.4.2:*** Kutoa mafunzo ya awali kwa walimu wa elimu ya Awali na shule za msingi (darasa la Kwanza mpaka la Tatu) kuhusu mtaala uliofanyiwa mapitio wa elimu ya Awali ambayo umejumuisha vipengele vya MMMAM

***Shughuli 2.1.4.3:*** Kutoa mafunzo ya awali kwa kamati za usajili wa vizazi katika Mikoa 8

## Matokeo ya muda mfupi 2.2: Mifumo ya rufaa na mahusiano ya utoaji huduma ya malezi jumuishi imeimarishwa

Watoto na familia zao wanahitaji mifumo imara ya rufaa ili kuhakikisha mahitaji yao yanajulikana na kupatiwa huduma jumuisha za malezi. Huduma zinazohitaji rufaa ni kama vile afya, lishe na ulinzi wa mtoto. Pia kunahitajika kuwepo na uhusiano wa wadau ili kuhakikisha huduma hizi zinatolewa katika uratibu imara.

### Matokeo ya papo kwa papo 2.2.1: Mifumo ya kutoa rufaa ya kesi za ukatili dhidi ya watoto imeimarishwa

Mifumo ya rufaa inalenga kutoa huduma rafiki kwa watoto kuhakikisha mfumo mkuu wa utoaji taarifa unaunganishwa na huduma ya simu bila malipo namba 116 ambayo itakusanya taarifa juu ya ukatili kwa watoto. Serikali kwa kushirikiana na wadau itahakikisha upatikanaji wa huduma salama za utoaji taarifa za ukatili kwa Watoto na kuzishughulikia. Pamoja na ukweli kwamba mahakama za mwanzo zote 144 zimepewa majukumu ya kushughulikia kesi zinazohusiana na ukatili halmashauri 86 tayari zimepatiwa mafunzo kuhusiana na masuala ya ukatili kwa Watoto (VAC) pia kuna mifumo ya rufaa na madawati 420 ya polisi ya jinsia na watoto ambayo yameundwa nchi nzima, na juhudi zinandelea kufanyika kuhakikisha huduma hizi zinapatiana nchi nzima.

***Shughuli 2.2.1.1:*** Kufanya mapitio ya mifumo ya ulinzi wa mtoto (Dawati la Jinsia) na kuandaa mwongozo wa kijamii kwa ajili ya kumbukumbu, kutoa taarifa na mfumo wa rufaa wa unyanyasaji wa watoto na utelekezaji ambao wanafanyiwa watoto kuanzia miaka 0-8.

***Shughuli 2.2.1.2:*** Kutoa mafunzo ya awali kwa wataalamu wanaoishi katika jamii kuhusu mwongozo wa kijamii kwa ajili ya kumbukumbu, kutoa taarifa na mfumo wa rufaa wa unyanyasaji wa watoto na utelekezaji ambao unawafikia watoto wadogo kuanzia miaka 0-8

***Shughuli 2.2.1.3:*** Kufanya utambuzi wa wadau wa MMMAM katika ngazi mbalimbali (Mkoa, Halmashauri na Kata) kwa ajili ya kuwezesha ufanisi wa mfumo wa rufaa na mahusiano

***Shughuli 2.2.1.4:*** Kuwatambua na kuwafikishia huduma za malezi jumuishi wanufaika wote wa TASAF wenye watoto wa umri wa miaka 0-8

### Matokeo ya Papo kwa papo 2.2.2: Njia salama/rafiki za utoaji wa taarifa za ukatili dhidi ya watoto zimeongezwa

Taarifa za ukatili dhidi ya watoto zinaendelea kuwa chache ingawa matendo ya ukatili dhidi ya watoto yanaendelea kutokea katika jamii. Kutengeneza njia rafiki na salama za utoaji wa taarifa za watoto itatoa fursa zaidi katika utoaji wa taarifa za ukatili dhidi ya watoto.

***Shughuli 2.2.2.1:*** Kutoa mafunzo ya awali kwa walimu wa elimu ya awali/walezi wa watoto wadogo/watoa huduma za afya wa kijamii kuhusu njia rafiki za utaoji wa taarifa za ukatili dhidi ya watoto na kuwateua kuwa wanasihi

***Shughuli 2.2.2.2:*** Kuwatambua na kuwapa rufaa watoto wasio na vyeti vya kuzaliwa kwenda kwenye vituo vya usajili wa vizazi vilivyo karibu

## Matokeo ya muda mfupi 2.3: Uwepo wa mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji uliokubalika

Ushirikiano katika utoaji wa huduma za MMMAM ni muhimu katika kuleta matokeo chanya kwa watoto wadogo. Hii itawezekana kama kutakuwepo na mfumo wa ufuatiliaji wa pamoja ili kupata taarifa za maendeleo ya utekelezaji wa shughuli za MMMAM. Shughuli muhimu zilizopangwa kufanyika ili kuhakikisha matokeo haya yanafanikiwa ni pamoja na:

### Matokeo ya papo kwa papo 2.3.1: Mfumo wa ukusanyaji taarifa za MMMAM na kuboresha masuala jumuishi ya MMMAM katika ngazi ya wilaya umeimarishwa

Viashiria vya MMMAM ni muhimu katika kila mfumo wa ukusanyaji taarifa unaotumika hapa nchini. Ili kuhakikisha kila mfumo unakusanya taaria za MMMAM kikamilifu programu hii itaitisha kikao cha siku moja cha wataalam ili kutambua viashiria vya taifa vya MMMAM katika mifumo ya kisekta ya utoaji taarifa ambayo ni pamoja na taarifa za kimradi zinazohusiana na masuala ya MMMAM (mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za afya, mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za elimu ya Msingi, mfumo wa takwimu za elimu ya msingi mifumo ya ukusanyaji wa taarifa zinazohusu shule) inaunganishwa na mfumo wa ukusanyaji taarifa za elimu ya Msingi, Childhood Protection Management Information System (CPMIs), mfumo jumuishi wa ukusanyaji taarifa, na kujumuisha viashiria vinavyokosekana.

***Shughuli 2.3.1.1:*** Kufanya uchambuzi wa mifumo iliyopo ya usimamizi wa taarifa zinazohusiana na MMMAM na kutambua viashiria vinavyokosekana

***Shughuli 2.3.1.2:*** Kuingiza viashiria vya MMMAM vilivyokosekana kwenye mifumo ya utoaji taarifa ya kisekta iliyopo kwenye Tafiti za Kitaifa

***Shughuli 2.3.1.3:*** Kutengeneza Kanzidata jumuishi ya MMMAM katika mfumo wa dashibodi kwa ajili ya kufuatilia viasharia vya malezi jumuishi kutoka katika mifumo ya utoaji taarifa ya kisekta iliyopo

***Shughuli 2.3.1.4:*** Kutoa mafunzo ya awali kwa kupitia majukwaa kwa wajumbe wa MMMAM katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri kuhusu matumizi ya dashibodi ya kanzidata jumuishi kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji wa viashiria vya malezi jumuishi

***Shughuli 2.3.1.5*** Kutoa mafunzo ya matumizi ya kanzidata jumuishi ya MMMAM kwa watoa huduma kwa ajili ya kufuatilia viashiria vya malezi jumuishi

***Shughuli 2.3.1.6:*** Kufanya ufuatiliaji wa pamoja wa mwaka wa MMMAM katika ngazi ya Halmashauri (Shule, vituo vya kulelea watoto na Vituo vya Afya)

### Matokeo ya papo kwa papo 2.3.2: Zana za uthibiti ubora zimeimarishwa kwa kuingiza vigezo vya uwezo maalumu wa mtoto

Matokeo ya ujifunzaji bora yanaweza kupatikana ikiwa kuna viwango bora vinavyosimamia utoaji huduma za MMMAM katika ngazi zote kuanzia vituo vya kulelea watoto wadogo mchana, elimu ya malezi na elimu ya Awali. Kwa muktadha huu mahali ambapo pana viwango, changamoto inabaki kwenye utumiaji wa viwango hivyo. Hivyo ni muhimu kuhakikisha kuwa kunakuwepo na mifumo ya kupima ubora kwenye vituo vya kulelea watoto mchana, shule za elimu ya awali, madarasa ya awali na masuala ya uwezo wa mtoto mmoja mmoja.

***Shughuli 2.3.2.1*** Kufanya mapitio ya zana za uthibiti ubora kwa elimu ya awali ili kuingiza vipengele vya uwezo maalumu wa mtoto

***Shughuli 2.3.2.2:*** Kusambaza zana za uthibiti ubora za elimu ya awali, vituo vya kijamii vya kulelea watoto wadogo chini ya miaka 5 ambazo zimejumuisha uwezo maalumu wa mtoto

Matokeo ya papo kwa papo 2.3.3: Zana za uchunguzi kutambua watoto wenye ulemavu kwenye vituo vya kulelea watoto wadogo chini ya miaka 5 zimeandaliwa.

Utambuzi wa mapema wa Watoto wenye changamoto kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ulemavu na uchelewaji wa ukuaji ni muhimu katika maendeleo ya mtoto. Hii imekua ikifanyika katika sehemu tofauti mahali ambapo watoa huduma za afya wanakutana na watoto.

***Shughuli 2.3.3.1*** Kupitia na kuboresha zana zilizopo za uchunguzi na utambuzi wa watoto chini ya umri wa miaka mitano

***Shughuli 2.3.3.2:*** Kutoa mafunzo ya awali kwa maafisa wa Halmashauri ukijumuisha Afisa elimu wa Wilaya, Afisa taaluma wa Wilaya, Mthibiti ubora wa Shule, Maafisa Elimu wa Kata, Walimu wa Taaluma, Afisa Ustawi wa Jamii na walimu Wakuu juu ya zana za uchunguzi na utambuzi wa watoto wenye ulemavu na mahitaji maalumu iliyoboreshwa

***Shughuli 2.3.3.3:*** Kufanya mapitio na kukamilisha rasimu ya orodha ya hatua za maendeleo ya ukuaji wa mtoto ili kuongeza umri wa mpaka miaka 8

## Matokeo ya muda mfupi 2.4: Takwimu za ubora na viwango zinapatikana ili kusaidia utekelezaji wa programu ya MMMAM

Matumizi ya takwimu sahihi ni muhimu katika upangaji Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM. Programu hii inatarajia kuwasaidia watafiti ambao watatoa takwimu ili kuwezesha utekelezaji wa afua stahiki.

Matokeo ya papo kwa papo 2.4.1: Utafiti kuhusu kiwango cha magonjwa na vifo kwa watoto wenye umri kati ya miaka 5-8 umefanyika

Kwa sasa hivi kuna uhaba wa taarifa za hali ya afya na lishe kwa watoto wenye umri kati ya miaka 5-8 ingawa wapo katika kundi hatari katika ukuaji timilifu kutokana na sababu mbalimbali kama vile umaskini, njaa, msongo wa mawazo unaotokana na ukatili. Taarifa zitakazopatikana zitaingizwa kwenye mfumo utafiti wa idadi ya watu na hali ya afya chini ya Taasisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), taarifa za kiwango cha magonjwa na vifo zinazopatikana katika vituo vya afya/ bima ya afya. Utafiti unapaswa kuzingatia mazingira yao ili kutengeneza afua zitakazosaidia ukuaji wao.

S***hughuli 2.4.1.1:*** Kuandaa andiko la utafiti

***Shughuli 2.4.1.2:*** Kukusanya takwimu

***Shughuli 2.4.1.3:*** Kufanya warsha ya uchambuzi, wa takwimu kutafsiri na uandishi wa taarifa

***Shughuli 2.4.1.4:*** Kufanya warsha ili kutoa matokeo ya utafiti

Matokeo ya papo kwa papo 2.4.2: Tafiti kuhusu malezi yenye mwitikio kwa watoto wenye umri kati ya miaka 0-8 umefanyika

Kutokana na uhaba wa taarifa ya malezi yenye mwitikio serikali na wadau wengine watafanya utafiti wa kujua hali halisi na taarifa hiyo itasaidia katika kupanga mipango. Programu za majaribio za malezi yenye mwitikio kwa sasa zinafanywa kwa kiwango kidogo na shirika la kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF) na EGPAF.

***Shughuli 2.4.2.1:*** Kuandaa andiko la utafiti

***Shughuli 2.4.2.2:*** Kukusanya takwimu

***Shughuli 2.4.2.3:*** Kufanya warsha ya uchambuzi wa takwimu, tafsiri na uandishi wa taarifa.

***Shughuli 2.4.2.4:*** Kufanya warsha ili kutoa matokeo ya utafiti

Matokeo ya papo kwa papo 2.4.3: Tafiti za viashiria vya malezi jumuishi zimefanyika

Ili kuimarisha mifumo iliyopo ya ufuatiliaji kwa kuweka viashiria vya malezi jumishi, Wizara za kisekta za MMMAM kwa kushirikiana na wadau watafanya utafiti wa MMMAM na kukusanya matokeo ya viashiria vya malezi jumuishi. Kutokana na ugumu wa kuingiza viashiria vya malezi jumuishi katika tafiti za kitaifa kama vile tafiti za idadi ya watu na hali ya afya kuna uwezekeno wa kufanyika utafiti mwingine mkubwa wa pamoja na taarifa hizo ziingizwe kwenye mfumo wa utafiti wa idadi ya watu na hali ya afya chini ya Taasisi ya Takwimu ya Taifa, mfumo taarifa za elimu ya msingi na utafiti wa kitaifa wa hali ya lishe ambapo baadhi ya viashiria vya malezi jumuishi havitolewi taarifa katika mifumo hii. Hivyo kipaumbele kitatolewa kwenye orodha ya viashiria vya malezi jumuishi na kukusanya taarifa ya hali ya MMMAM kila baada ya miaka miwili kufikia mwaka 2022.

***Shughuli 2.4.3.1:*** Kuandaa andiko la utafiti

***Shughuli 2.4.3.2:*** Kukusanya takwimu

***Shughuli 2.4.3.3:*** Kufanya warsha ya uchambuzi wa takwimu, tafsiri na uandishi wa taarifa

***Shughuli 2.4.3.4:*** Kufanya warsha Ili kutoa matokeo ya utafiti

Matokeo ya papo kwa papo 2.4.4: Mapitio ya programu jumuishi ya Taifa ya MMMAM yamefanyika

Programu itafanyiwa mapitio na kuboreshwa katika ngazi mbalimbali ili kupima maendeleo ya utekelezaji. Tathmini ya programu hii itakayofanyika baada ya muhula wa kwanza wa utekelezaji itapima maendeleo ya utekelezaji wa afua za programu kwa kuangalia malengo ya programu, ubora wa huduma , mapungufu, na kupanga upya kabla ya programu kuisha. Tathmini ya mwisho itaangalia mafanikio ya programu kwa ujumla, changamoto na kupanga programu kwa awamu nyingine.

***Shughuli 2.4.4.1: Kufanya tathmini ya muhula wa kwanza wa utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM***

***Shughuli 2.4.4.1.1:*** Kuandaa andiko la tathmini

***Shughuli 2.4.4.1.2:*** Kukusanya takwimu

***Shughuli 2.4.4.1.3*** Kufanya warsha ya uchambuzi wa takwimu, tafsiri na uandishi wa taarifa

***Shughuli 2.4.4.1.4*** Kufanya warsha ili kutoa matokeo ya tathmini

***Shughuli 2.4.4.2:*** Kufanya tathmini ya mwisho wa Utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM

***Shughuli 2.4.4.2.1:*** Kuandaa andiko la tathmini

***Shughuli 2.4.4.2.2:*** Kukusanya takwimu

***Shughuli 2.4.4.2.3*** Kufanya warsha ya uchambuzi wa takwimu, tafsiri na uandishi wa taarifa

***Shughuli 2.4.4.2.4*** Kufanya warsha ili kutoa matokeo ya tathmini

## Matokeo ya Muda Mrefu 3: Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma bora zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa Watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao

Huduma kwa watoto wenye umri kati ya miaka 0-8 zinatofautiana na zinahitaji kupangwa, kuratibiwa na kuhakikisha zitatolewa kwa utaratibu unaofaa ili kupata matokeo chanya. Upatikanaji wa huduma bora za malezi jumuishi unahitaji upatikanaji wa huduma stahiki katika malezi yenye mwitikio, fursa za ujifunzaji wa awali, upatikanaji wa huduma bora za afya, lishe na ulinzi na usalama wa mtoto.

### Matokeo ya muda mfupi 3.1 Utoaji wa huduma bora za afya umeboreshwa

Matokeo yanajumuisha afua zote ambazo zitaimarisha utoaji huduma bora za MMMAM zinazohusiana na afya na upatikanaji wake kwa watoto wote.

Matokeo ya papo kwa papo 3.1.1: Hali za afya na lishe kwa watoto wenye umri kati ya miaka 0-8 zimetambuliwa

Afya na ustawi wa watoto wadogo katika ukuaji ni muhimu kwa maendeleo yao ya baadaye katika maisha. Ufuatiliaji wa hali zao za afya katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana, elimu ya awali, na darasa la kwanza la pili na la tatu katika shule za msingi ni muhimu katika kuwasaidia katika maendeleo yao.

***Shughuli 3.1.1.1:*** Kutoa huduma za mkoba mara kwa mara ili kuwatambua watoto wenye changamoto za ukuaji kwenye vituo vya kulelea watoto chini ya miaka 5, shule za awali na madarasa ya mwanzo ya shule za msingi (darasa la kwanza hadi la tatu.

Matokeo ya papo kwa papo 3.1.2: Utoaji wa huduma za afya kwa kina, ufuatiliaji na uchunguzi kwa watoto wadogo kwenye vituo vya afya umeongezaka.

Utoaji wa huduma za afya kwa watoto wenye umri chini ya miaka 5 na waliopo kwenye elimu ya awali na madarasa ya awali ya shule za Msingi (1-3) ni muhimu sana katika kuhakikisha kwamba Watoto anabaki salama na kuwa na uwezo wa kujifunza na kucheza. Programu hii itatoa huduma hii kwa kuhakikisha inawafikia Watoto wote nchini.

***Shughuli 3.1.2.1:*** Kupitia na kuboresha huduma za afya kwa wanawake wajawazito, huduma za mama na mtoto baada ya kujifungua, huduma za afya kwa watu wenye maambukizi ya VVU na huduma jumuishi za matibabu ya watoto ili kuingiza vipengele vya malezi jumuishi katika kuwezesha utoaji wa huduma za kina; ufuatiliaji na uchunguzi wa hatua za ukuaji wa watoto

***Shughuli 3.1.2.2:*** Kuandaa Kijitabu cha afya na maendeleo ya mtoto kutumia maandishi ya nukta nundu (braille) ili kuongeza upatikanaji wa huduma kwa watu wenye uoni hafifu

***Shughuli 3.1.2.3:*** Kuanzisha huduma mkoba za kliniki ya mama, baba na mtoto kufikia kwenye vituo vya kulelea watoto wadogo chini ya miaka 5, shule za awali na madarasa ya mwanzo ya shule za msingi (darasa la kwanza hadi la tatu)

***Shughuli 3.1.2.4:*** Manunuzi ya vifaa vya ufuatiliaji wa ukuaji na maendeleo ya mtoto (mizani ya kupimia uzito, ubao wa kupimia urefu/kimo na vifaa vya michezo vinavyoendana na umri wa mtoto) katika vituo vya afya

## Matokeo ya muda mfupi 3.2 Upatikanaji wa huduma toshelezi na sahihi za lishe umeongezeka

Ingawa huduma za lishe zimefikiwa kwenye mpango jumuishi wa taifa wa lishe, bado zinahitaji kuboreshwa kwenye vipengele vya Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM kuongeza upatikanaji wake

Matokeo ya papo kwa papo 3.2.1 Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe umepitiwa kuongeza vipengele vya malezi jumuishi

Kutambua kuwa malezi jumuishi hayajagusiwa sana katika mpango jumuishi wa taifa wa lishe hasa katika ujifunzaji wa awali na malezi yenye mwitikio. Serikali na wadau wanaoshuguikia masuala ya watoto wataufanyia mapitio mpango huu ili kuingiza vipengele hivi.

***Shughuli 3.2.1.1*** Kufanya mkutano wa kupitia Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe wa pili ili kuhakikisha vipengele vya malezi jumuishi vimeingizwa

Matokeo ya Papo kwa Papo 3.2.2: Afua za lishe zinatolewa katika shule za awali na madarasa ya mwanzo ya shule za msingi (darasa la kwanza hadi la tatu)

Ufuatiliaji wa hali ya lishe kwa Watoto waliopo shuleni utaisaidia Serikali kutambua changamoto na hivyo kutengeneza afua zitakazotatua changamoto hizo ili kuboresha matokeo ya watoto wadogo katika vituo.

***Shughuli 3.2.2.1:*** Kuchunguza na kutambua hali ya lishe na hatua za ukuaji kwa watoto wenye umri wa miaka 5 - 8 katika shule za awali na madarasa ya mwanzo ya shule za msingi (darasa la kwanza hadi la tatu) kama sehemu ya programu za afya

Matokeo ya papo kwa papo 3.2.3 Programu ya utoaji chakula shuleni kwa watoto wa darasa la awali na madarasa ya mwanzo ya shule za msingi (darasa la kwanza hadi la tatu) imetekelezwa

Mwongozo huu wa kutoa huduma za chakula shuleni umeandaliwa na umekamilika. Ili kuhakikisha uendelevu wa programu hii, na upatikanaji wa huduma hii kwa usawa kwa Watoto wote serikali kwa kushirikiana na wadau mabalimbali watatoa elimu kwa wadau wanaohusika na programu ya kutoa chakula shuleni na kuhamasisha utekelezaji wa programu hii kwa kuwahusisha wazazi, walezi na wadau mbalimbali katika ngazi zote.

***Shughuli 3.2.3.1:*** Kutoa mafunzo ya awali ya siku 3 kwa wawezeshaji 20 wa kitaifa juu ya namna ya kutumia Mwongozo wa Programu ya Utoaji wa Chakula Shuleni

***Shughuli 3.2.3.2:*** Kutoa mafunzo ya awali ya siku 3 kwa wawezeshaji na wakufunzi kuhusu namna ya kutumia Mwongozo wa Programu ya Utoaji wa Chakula Shuleni katika ngazi ya mkoa na halmashauri

***Shughuli 3.2.3.3:*** Kutoa mafunzo ya awali ya siku 3 kwa walimu na watendaji Kata kuhusu namna ya kutumia Mwongozo wa Programu ya Utoaji wa Chakula Shuleni katika halmashauri zote

***Shughuli 3.2.3.4a:*** Kuanzisha shughuli za ufugaji kuku, wanyama wadogo na kilimo cha bustani katika ngazi ya shule ili kutoa chakula chenye virutubisho muhimu kwa watoto kupitia programu ya utoaji wa chakula shuleni na kubadilisha taratibu za ulishaji wa watoto katika ngazi ya kaya

***Shughuli 3.2.3.4b:*** Kufuatilia utekelezaji wa shughuli za ufugaji kuku, wanyama wadogo na kilimo cha bustani

Matokeo ya papo kwa papo 3.2.4 Maadhimisho ya Siku ya afya na lishe vijijini yamefanyika yakijumuisha utoaji wa huduma mkoba za afya ya mama, baba na mtoto

Matokeo haya yanamaanisha kuongeza upatikanaji wa huduma ya malezi jumuishi kwa Watoto wadogo ikijumuishwa kwa kupitia vituo vya kijamii vya creches, vituo vya kulea watoto wadogo mchana, vituo vya kijamii vya MMMAM na shuleni. Siku ya afya na lishe vijijini imekua jukwaa muhimu ambapo jamii pamoja na wazazi, walezi na watoto wao chini umri wa miaka 5 huhudhuria na kupata taarifa na huduma mbalimbali kuhusu afya, lishe, malezi yenye mwitikio, usafi wa mazingira pamoja na ulinzi wa mtoto unaotolewa kwa kupitia upimaji, unasihi na maonesho.

***Shughuli 3.2.4.1:*** kufanya maadhimisho ya Siku ya Afya na Lishe Vijijini

## Matokeo ya muda mfupi 3.3: Huduma sahihi za malezi yenye mwitikio zimetolewa

Ukuaji wa mtoto na maendeleo yake unategemea ubora wa huduma anayopatiwa kwa kadri anavyokua. Watoto wanahitaji kukua katika mazingira changamshi wanapochangamana na watoto wenzao na walezi. Unasihi kwa wazazi na walezi juu ya majukumu yao katika malezi yenye mwitikio. Upatikanaji wa zana sahihi za kutosha za kucheza na kujifunza nyumbani na vituo vya utoaji huduma inasaidia kutoa fursa na kuboresha ujifunzaji kwa mtoto.

Matokeo ya papo kwa papo 3.3.1: Kona jumuishi za MMMAM zenye vifaa vya kutosha vya michezo na vya kujifunzia zimeanzishwa

Watoto hujifunza kupitia michezo. Programu hii imedhamiria kutoa fursa za ujifunzaji mapema kwenye vituo vyote ambavyo vinatumiwa na watoto na wazazi/walezi wao wanapokwenda kupata huduma, au wanapohudhuria vituo vya mafunzo kwa watoto. Vifaa vya kuchezea, kujifunza na kufundishia watoto ni zana muhimu zinazosaidia kuboresha uwezo wa watoto kujifunza. Vifaa hivyo vinatoa fursa ya kucheza na kuwasiliano baina ya mlezi na mtoto pamoja na kusaidia utambuzi wa watoto wenye ulemavu au changamoto za maendeleo ya ukuaji, hivyo kuwezesha utoaji wa rufaa kwa ajili ya kupata huduma za udhibiti mapema.

***Shughuli 3.3.1.1:*** Kuanzisha kona jumuishi za MMMAM zenye vifaa vya kutosha vya michezo na kujifunzia vinavyoendana na umri wa mtoto kwenye vituo vyote vya afya elfu kumi na mbili miatatu na kumi na tisa (12,319) katika Halmashauri zote 184 nchini ili kutoa nafasi ya michezo na mawasiliano kati ya mlezi na mtoto; pia kusaidia kutambua uwezo na mahitaji ya mtoto na kufanya rufaa sahihi

Matokeo ya papo kwa papo 3.3.2: Huduma za mara kwa mara za unasihi wa malezi jumuishi kwa wazazi na walezi zimetolewa

Familia na jamii ndiyo walezi wa msingi wa watoto wadogo. Huduma ya unasihi zinazotolewa kwa wazazi, walezi na watoto wao wanapohudhuria kwenye vituo vya huduma za afya zina umuhimu mkubwa katika kuwaongezea uelewa kuhusu malezi yenye mwitikio na vipengele vingine vya Malezi jumuishi. Hii husaidia kuboresha ukuaji na maendeleo ya watoto.

***Shughuli 3.3.2.1:*** Kutoa huduma za mara kwa mara za unasihi wa malezi jumuishi kwa wazazi na walezi

## Matokeo ya muda mfupi 3.4: Fursa za ujifunzaji wa awali zimeongezeka

Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM itafanya uwekezaji kuongeza fursa za ujifunzaji wa awali katika ngazi zote. Hili litafanyika kwa kuanzisha vituo vya huduma kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 2, vituo vya Malezi ya watoto wakati wa mchana vinavyomilikiwa na jamii kwa ajili ya watoto wenye umri wa miaka 3 – 4; na vituo vya elimu ya awali, na madarasa ya elimu ya awali kwa watoto wenye umri wa miaka 5 na watoto wa darasa la kwanza mpaka la tatu, ambavyo ni rasmi kwa kuzingatia Sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014. Programu Jumuishi itafanya uhamasishaji kwa wazazi, walezi, familia na jamii kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wadogo kama ilivyoainishwa kwa kina kwenye Eneo la 4 la Matokeo kwenye programu hii.

### Matokeo ya papo kwa papo 3.4.1: Fursa za ujifunzaji wa awali kwa watoto zimeongezeka

Watoto wanajifunza kwa kuchunguza mazingira yanayowazunguka, pamoja na makazi wanamoishi, vituo vya malezi, na mazingira ya shule. Ubora wa mazingira hayo ni sehemu muhimu katika kujenga mwelekeo wa watoto kujifunza. Uanzishaji wa vituo vya malezi ya watoto wenye umri wa miaka 0 – 2, vituo vya kujifunza vya watoto wadogo, vituo vya elimu ya Awali, na madarasa ya elimu ya awali vitawekewa vifaa vya michezo, vifaa vya kujifunzia na kufundishia vinavyozingatia umri wa watoto. Serikali itawekeza katika vituo na kuimarisha mafunzo kwa watoto wadogo.

***Shughuli 3.4.1.1:*** Kusaidia uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya malezi ya watoto wenye umri wa miaka 0 - 2 kwenye maeneo rasmi na yasio rasmi ya kazi ili kuimarisha unyonyeshaji, malezi yenye mwitikio na ujifunzaji wa awali

***Shughuli 3.4.1.2:*** Kusaidia uanzishaji wa vituo vya kulelea watoto vya MMMAM vinavyomilikiwa na jamii

***Shughuli 3.4.1.3:*** Kusaidia uanzishaji wa ujenzi wa madarasa ya awali kwenye maeneo rasmi na yasiyo rasmi

### Matokeo ya papo kwa papo 3.4.2 Msaada unaotolewa kwa familia na jamii kwa kuwapa elimu ya malezi na kutoa huduma za malezi jumuishi umeongezeka

Hizi ni huduma zinazotolewa kwenye vituo vya Malezi kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 2, vituo vya MMMAM katika jamii, vituo vya elimu ya Awali na madarasa ya elimu ya Awali.

***Shughuli 3.4.2.1:*** Kusaidia uanzishwaji wa vikundi vya malezi katika jamii

***Shughuli 3.4.2.2:*** Kusaidia upatikanaji wa mitaji kwa vikundi vya malezi

## Matokeo ya muda mfupi 3.5: Upatikanaji wa huduma za ulinzi na usalama wa mtoto umeongezeka

Ulinzi na usalama wa watoto ni kipengele muhimu cha Mfumo Jumuishi wa Malezi. Hili ni jukumu la wazazi na walezi wa watoto hao. Taarifa ya uchambuzi wa hali halisi imeonesha kuwa kuna taarifa chache za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto wenye umri wa miaka 0 -8. Jambo hili linaonesha umuhimu wa kuanzisha mfumo utakao ongeza upatikanaji wa taarifa na huduma za ulinzi na usalama kwa watoto wote.

### Matokeo ya papo kwa hapo 3.5.1: Vituo vya mkono kwa mkono vinavyotoa huduma za ulinzi na usalama kwa watoto wadogo vimeanzishwa.

Ili kukabiliana na changamoto ya ulinzi na usalama wa watoto kuna umuhimu wa kuanzisha vituo vya mkono kwa mkono katika jamii zote, vyenye wataalamu, vifaa na sehemu salama kwa ajili ya kutoa huduma rafiki kwa kuzingatia umri wa watoto wanaohitaji huduma. Tayari kuna vituo 16 vya mkono kwa mkono ambavyo vimeanzishwa nchini. Kupitia Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM, vituo vingi zaidi vitaanzishwa katika maeneo yote nchini.

***Shughuli 3.5.1.1:*** Kuwezesha uanzishwaji wa vituo 97 vya mkono kwa mkono katika hospitali za wilaya ambazo zitatoa huduma za ulinzi na usalama kwa mama na mtoto wakiwemo watoto wenye umri wa miaka 0-8

***Shughuli 3.5.1.2:*** Kutoa mafunzo ya awali kwa watoa huduma (wanasihi, manesi, madaktari, polisi na Afisa Ustawi wa Jamii) kuhusu huduma rafiki kwa mtoto

***Shughuli 3.5.1.3:*** Kuanzisha / Kujenga vituo vipya 81 vya huduma ya mkono kwa mkono kwenye hospitali za Wilaya na kukarabati vituo 40 vya huduma ya mkono kwa mkono kwa kutumia majengo yaliyopo kwenye hospitali na kuweka samani na vifaa vikiwemo kona rafiki ya michezo yenye vifaa vya michezo

## Matokeo ya Muda Mrefu Na. 4: Wazazi, Walezi, familia na jamii wamejengewa uwezo wa kutekeleza taratibu sahihi za malezi jumuishi

Uimarishaji wa uwezo wa walezi, familia na jamii ni jambo la muhimu linalopaswa kuzingatiwa katika uwekezaji wa miaka ya awali ya maisha ya watoto. Hii ni kwa sababu inatarajiwa kwamba makundi hayo yakiwezeshwa yatapata elimu itakayosaidia kuongeza uhitaji wa huduma na utekelezaji wa taratibu sahihi za malezi jumuishi. Makundi haya ya wadau yanaweza kufikiwa kwa njia mbalimbali za mawasiliano ikiwemo vyombo vya habari na mikutano.

## Matokeo ya muda mfupi 4.1: Uelewa kuhusu umuhimu wa huduma za malezi jumuishi katika jamii umeongezeka

Familia na jamii zinahitaji kujengewa uwezo kwa kupatiwa elimu ili waweze kuelewa umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wadogo kwa ajili ya kuwajengea msingi imara wa maisha yao ya baadaye. Jambo hili linaweza kufanyika kwa kutoa huduma za malezi jumuishi ili kuwezesha ukuaji na maendeleo ya watoto. Familia na jamii ni wadau wakubwa na wa kwanza ambao wanatarajiwa kuwajibika ipasavyo na kusaidia utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM. Programu hii itatumia mbinu mbalimbali ili kutoa elimu kwa familia na jamii.

### Matokeo ya papo kwa papo 4.1.1: Uhamasishaji wa jamii kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wadogo katika miaka ya awali umefanyika

Eneo hili la matokeo litafanikiwa kupitia uhamasishaji utakaofanyika kwa njia ya vyombo vya habari na mikutano katika jamii. Uhamasishaji ni jambo muhimu katika kuleta mabadiliko miongoni mwa familia na jamii kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wakiwa katika umri mdogo. Ili kuhakikisha kuwa taratibu bora za malezi zinaendelezwa katika jamii, lazima jamii iwe na uhitaji na ibadilishe mitazamo, taratibu na tabia kuhusu utoaji wa huduma za malezi jumuishi. Programu hii itatumia mbinu ya kuhamasisha na kushirikisha jamii kwa kuiweka kuwa mojawapo kati ya ajenda za kitaifa inayohusu malezi na matunzo katika familia. Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM itatumia mikakati mbalimbali kuhakikisha kuwa wadau wote wanapata elimu kuhusu umuhimu wa kuwekeza katika MMMAM.

***Shughuli: 4.1.1.1:*** Kuandaa ujumbe wa MMMAM ili kuhamasisha na kuongeza uelewa wa umuhimu wa kuwekeza katika huduma za malezi jumuishi kupitia vyombo vya habari

***Shughuli 4.1.1.2:*** Kujenga uelewa wa wadau muhimu katika jamii kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wadogo kuanzia miaka ya awali kwenye ngazi ya kata

***Shughuli 4.1.1.3:*** Kuandaa mikutano ya kuhamasisha viongozi wa kijamii, dini, sekta binafsi na viongozi mashuhuri kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wadogo kuanzia miaka ya awali

***Shughuli 4.1.1.4:*** Kufanya mikutano ya uhamasishaji kwa madiwani ili kuongeza kiwango cha uwekezaji kwenye huduma za malezi jumuishi

## Matokeo ya muda mfupi 4.2: Wazazi/Walezi na jamii wameshirikishwa kutoa/kuchangia huduma za malezi jumuishi

Kuwahusisha wazazi, walezi, familia na jamii katika masuala ya Malezi ya watoto ni jambo linalosaidia kuongeza wigo wa ubora wa huduma, na hivyo kuhakikisha kuwa watoto wanapata ulinzi na usalama wa kutosha kwenye familia na jamii. Programu hii itashirikiana kwa karibu na wadau mbalimbali ili kuhakikisha kuwa masuala ya MMMAM yanazingatiwa katika ngazi zote.

Matokeo ya papo kwa papo 4.2.1: Mwongozo wa Uanzishaji wa Dawati la Ulinzi wa Mtoto Shuleni umesambazwa.

Suala la kukidhi viwango vya ubora katika utoaji wa huduma kwa watoto wadogo ni jambo umuhimu katika kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata huduma kwa wakati kadiri ya mahitaji yao. Watoa huduma kwa upande mwingine wanahitaji kuwa na uelewa mpana na stadi za kutosha ili waweze kutoa huduma kwa ufanisi

***Shughuli 4.2.1.1:*** Kusambaza mwongozo wa uanzishaji wa dawati la ulinzi wa mtoto shuleni kupitia kuwajengea uwezo wa awali waratibu wa elimu, maafisa ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii kwenye Kata na Halmashauri zote

Matokeo ya papo kwa papo 4.2.2: Vituo vya kulelea watoto wadogo chini ya miaka 5 vimeanzishwa

Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM itawezesha utaratibu mahususi wa utoaji matunzo na kujifunza kwa watoto wadogo hapa nchini kwa kuhamasisha uanzishwaji na uwendeshaji wa vituo vya malezi ya watoto wenye umri wa miaka 0 – 8, vituo vya kulelea watoto mchana, vituo vya huduma za MMMAM vya kijamii, na madarasa ya elimu ya awali nchini kote.

***Shughuli 4.2.2.1:*** Kushirikisha wazazi / walezi na jamii katika kusaidia kuendeleza huduma za malezi jumuishi kwenye vituo vya kulelea watoto wadogo chini ya miaka 5, elimu ya awali na madarasa ya mwanzo ya shule za msingi (darasa la kwanza hadi la tatu)

***Shughuli 4.4.2.2:*** Kuwezesha uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto chini ya miaka 5, (Creches, Day care centre, community based ECD centres) kwenye maeneo rasmi na yasio rasimi ili kuwezesha huduma za malezi jumuishi



# *SURA YA 5:* GHARAMA ZA UTEKELEZAJI WA AFUA ZA PROGRAMU JUMUISHI YA TAIFA YA MMMAM KATIKA MAENEO MUHIMU YA MATOKEO

## *5.1 Utangulizi*

Mpango kazi wa utekelezaji wa programu hii ya miaka mitano, utatoa matokeo manne ya muda mrefu ambayo ni: Mazingira wezeshi yameboreshwa; Mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora imeimarishwa; Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma bora na zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao; na walezi, familia na jamii wamejengewa uwezo wa kutekeleza taratibu sahihi za Malezi jumuishi.

Bajeti ya jumla ya Programu ya Taifa ya MMMAM kwa kipindi cha miaka mitano ni TSH 914,991,351,636 ambazo ni sawa na Dola za Kimarekani 394,392,824. (Rejea kwenye jedwali Na. 5: Muhtasari wa Mahitaji ya Fedha kwa Ajili ya Kugharamia Utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM).

Bajeti imetengwa kusaidia matokeo yote makuu manne ya muda mrefu kama inavyooneshwa katika mchoro Na. 10. Sehemu kubwa ya bajeti ( 76%) inaelekwezwa kwenye utoaji huduma kwa walengwa(watoto na walezi) ambayo ni Matokeo ya Muda Mrefu Na. 3: Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma bora na zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa Watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao. Mapungufu makubwa yaliyobainika ni pamoja na ha maeneo machache yaliyofikiwa na huduma ya malezi jumuishi, hususani maeneo ya vijijini na huduma stahiki zinazolenga watoto wa miaka 2 – 4. Mazingira duni au miundombinu hafifu ya kujifunzia ni amoja na upatikanaji hafifu wa malezi yenye mwitikio na vifaa vya kujifunzia/michezo ni changamoto zilizobainishwa. Hivyo, uwekezaji mkubwa umepewa kipaumbele kushughulikia mapungufu hayo ikiwemo, usaidizi wa kuanzisha vituo 200 vya kulelea watoto wachanga katika maeneo ya kazi na ndani ya jamii ili kuhamasisha unyonyeshaji, malezi yenye mwitikio, uchangamshi wa awali au ujifunzaji kwa watoto walio na miaka 0-2. Pia, uanzishwaji wa vituo vya kijamii vya kuelelea watoto wadogo katika vijiji/mtaa 12,319 vikilenga watoto wa miaka 3-4, ujenzi madarasa bora ya elimu ya awali katika shule zote 16,401 za msingi za serikali wakilenga watoto wa miaka 5-6; Pamoja na uanzishwaji wa sehemu rafiki na salama kwa watoto katika vituo vya mkono kwa mkono vya malezi katika hospitali 97 za halmashauri na ununuzi wa zana za ufuatiliaji maendeleo na ukuaji wa mtoto.

Uchambuzi huo pia ulibaini mapungufu katika suala la uratibu kati ya wadau, idadi ndogo ya watendaji waliopatiwa mafunzo yanaohusiana na MMMAM, viwango duni vya ubora na hitaji la kuwa na sera, miongozo/mitaala itakayoshughulikia huduma za malezi jumuishi.Uelewa mdogo wa masuala ya MMMAM kwa watoa maamuzi na jamii kwa ujumla pia ulionekana kama kikwazo. Kwa kuwa programu hii ni mpya, ni muhimu mifumo na miundo ianzishwe kufanya programu iwe endelevu.  Bajeti iliyobakia imepelekwa kwenye matokeo ya muda mrefu matatu yaliyobakia ambayo ni:

*i.* Tokeo la muda mrefu Na. 1: Mazingira wezeshi yameboreshwa ili kuwezesha uratibu wenye ufanisi na kutoa huduma jumuishi za malezi kupitia utetezi, kuandaa/kupitia sera na miongozo husika na uwezeshaji wa uratibu kati ya wadau ambao umetengewa 14% ya bajeti ya programu.

*ii.* Tokeo la muda mrefu Na. 2: Mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora imeimarishwa. Tokeo hili limetengewa 7% ya bajeti ya programu inayolenga kuwajengea uwezo maafisa ugani, kufanya tafiti za ndani kuboresha programu, kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini, uhakiki ubora na utoaji wa rufaa.

*iii.* Tokeo la muda mrefu Na. 4: Walezi, familia na jamii wamejengewa uwezo wa kutekeleza taratibu sahihi za Malezi jumuishi ambayo imetengewa 3% ya bajeti ya programu. Tokeo hili limelenga kwenye kujenga uelewa na uhitaji kwa wazazi na jamii kupitia mikutano ya uhamasishaji, ujumbe wa redio na makundi zaidi ya mfumo wa malezi jumuishi.

***Mchoro namba 10:*** Mgawanyo wa asilimia za bajeti ya programu kati ya malengo ya muda mrefu




Gharama za Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM zimegawanya kwenye maeneo makuu matatu: 1. Gharama wezeshi (uongozi wa juu katika serikali, muundo, uanzishaji na tathmini); 2. Gharama za moja kwa moja (ujenzi wa miundo mbinu, mikutano, mafunzo, chakula na virutubisho, sare za shule, utoaji ruzuku kwenye kaya maskini, vifaa, usimamizi wa moja kwa moja na ufuatiliaji); na 3. Gharama zilizotengwa (muda wa kujitolea na gharama za fursa za majengo yaliyotumika).

## Vigezo muhimu vinavyoathiri gharama za Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM ambavyo vimejumuishwa katika zana za viwango vya bajeti[88] ni:

*i.* ***Huduma zinazotolewa:*** huduma za malezi jumuishi zitatolea kwa ujumla; (kwa mfano, ujumuishwaji wa ujumbe wa malezi yenye mwitikio katika huduma za afya; kufanya tathmini ya lishe katika shule za awali na vituo vya kulelea watoto wadogo mchana). Kuna faida ya kutumia mifumo iliyopo kujumuisha huduma kwa mfano, afya na malezi yenye mwitikio kwani itapunguza uzito wa kazi haitaongeza kazi kubwa kwa programu zingine na gharama za uendeshaji wa programu za uendeshaji zinaweza kuwa chini. Badala yake kuongeza huduma zinazohitaji nguvu kazi nyingi mfano elimu ya awali zinaweza zisitoe matokeo yenye ufanisi. Aidha kuna uwezekano wa wa ongezeko la gharama za uratibu baina ya wizara.

*ii.* ***Muda wa programu:*** programu jumuishi ya Taifa ya MMMAM hasa katika malezi ya watoto, programu za malezi, elimu ya awali, vituo vya kulelea watoto wadogo, zinatofautiana muda au idadi ya siku za kutoa huduma. Mfano kutoka masaa matano hadi kumi kwa siku na siku tano kwa wiki. Watoto walio katika mazingira hatarishi watahitaji huduma zaidi na zenye gharama kubwa.

[88] The Standardized Early Childhood Development Costing Tool (SECT). A Global Good to Increase and Improve Investments in Young Children. Emily Gustafsson-Wright, Izzy Boggild-Jones and Sophie Gardiner. September, 2017

*iii.* ***Usimamizi wa watumishi na kujiendeleza kitaaluma:*** kiwango cha utekelezaji wa programu za MMMAM hutofautiana kwa kiasi kikubwa katika ubora kitu ambacho kina athari katika programu husika. Idadi ya siku za mafunzo huweza kutofautiana kati ya siku moja hadi siku tano. Mafunzo ni moja ya maeneo yenye gharama kubwa katika programu kutokana na uhitaji wa fedha za kujikimu na usafiri. Mara nyingi matumizi yanayohusiana na mafunzo huwa hayatoshelezi kwa sababu ni vigumu kupima matokeo yake ukilinganisha na ubora wa miundombinu.

*iv.* J***iografia:*** programu za vijijini zinaweza kuwa na gharama kubwa kwasababu mbali mbali kama vile watoa huduma kuhudumia watoto wachache, gharama kubwa ya usafiri na usafirishaji wa vifaa vya ujenzi na vya kujifunzia kwenda maeneo ya mbali.. Kwa upande mwingine, viwango vya mshahara maeneo ya mijini vinaweza kufanya programu kuwa ghali zaidi.

*v.* ***Maeneo ya utoaji huduma:*** huduma za MMMAM zinazotolewa katika nyumba za walengwa badala ya vituo maalum, zinahitaji gharama za chini za miundombinu lakini zinaweza kuhitaji gharama kubwa za usafirishaji, mfano huduma za majumbani zinazofanywa na Wahudumu wa Afya wa Jamii (WAJA).

*vi.* ***Eneo la utekelezaji wa Programu:*** programu zinazoanza kwa upana mkubwa kama Programu jumuishi ya taifa ya MMMAM zinaweza kuwa na gharama kubwa kwa sababu ya uwekezaji unaohitajika kwenye ujenzi wa mifumo na gharama za ziada za kupanua huduma kwenye jamii zenye zinazofikika kwa ugumu. Hata hivyo, programu zinazofanyika katika eneo dogo zinaweza kuwa na gharama kubwa ukilinganisha na zile zinazofanyika katika eneo kubwakubwa kwani gharama za uendeshaji kwa ujumla huwa kubwa kufidia gharama za uanzishaji.

Kwa kuzingatia tofauti hii, ilikuwa ni muhimu kupata taarifa juu ya shughuli za Programu jumuishi ya Taifa ya MMMAM, na kukusanya taarifa za gharama kwa ajili ya kuelewa muktadha na ubora wa huduma zinazotolewa. Pia makisio yalitumika katika kuamua gharama ya shughuli. Taarifa hii imejumuishwa katika kiambatisho 3 (gharama za utekelezaji).

Kuna changamoto kadhaa za ukusanyaji takwimu zinazohusiana na programu za MMMAM zenye gharama ya utekelezaji (a uwepo wa watendaji wengi wanaotoa huduma moja, hivyo ni vigumu kupata picha halisi na kuepuka makosa ya kuhesabu wanufaika mara mbili (b) Mara nyingi huduma za MMMAM kwa ngazi ya jamii hutegemea zaidi wafanyakazi wa kujitolea ukilinganisha na huduma zinazotolewa kwenye taasisi mfano Elimu na Afya. Pamoja na umuhimu wa kazi za kujitolea gharama zinazohusiana na kazi hizo bado zinaondolewa kwenye uchambuzi wa bajeti[89] . (c) Mfumo wa mahesabu mara nyingi unahesabu matumizi kuliko gharama za uendeshaji na kutofautisha gharama za mtaji kutoka gharama za uendeshaji[90]. Matokeo yake matumizi ya uwekezaji mara nyingi hayahesabiwi ipasavyo; kwa mfano, huesabiwa mwanzo wa mwaka tu[91]. (d) Makadirio ya gharama ya kitu kimoja badala ya gharama za jumla za programu, inaleta changamoto ya upimaji idadi ya wanufaika katika programu husika. Programu za MMMAM zinaweza kuwa na manufaa ya ziada kwa watoto wengine katika familia; kwa mfano, kwa watoto watakaozaliwa baada ya kutolewa kwa elimu ya malezi.

[89] Myers, R. (2008b). A note on costs and costing of early childhood care and development programmes. in E. Vargas-Barón & S. Williams (Eds.), Coordinators' Notebook, 30, 29-32.

[90] Myers, R. (2008b). A note on costs and costing of early childhood care and development programmes.In E. Vargas-Barón & S. Williams (Eds.), Coordinators' Notebook, 30, 29-32.

[91] Myers, R. (2008b). A note on costs and costing of early childhood care and development programmes.In E. Vargas-Barón & S. Williams (Eds.), Coordinators' Notebook, 30, 29-32.

## *5.2 Gharama za utekelezaji ili kuimarisha Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM*

Gharama za utekelezaji wa Programu hii zimeelezewa kwa undani kwenye kiambatisho 3 na zimetokana na gharama za utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe 2016-2021 na kusambaza afua za lishe katika maeneo ya matokeo muhimu ya huu. Programu hii itaonesha vipengele vingine ambavyo vimetengewa bajeti tayari hivyo havitawekewa bajeti kwenye kwenye Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM.

### 5.2.1 Gharama za utekelezaji za Mazingira wezeshi yameboreshwa kuwezesha uratibu wenye ufanisi na utoaji huduma za malezi jumuishi

Mpango kazi uliopendekezwa unatarajiwa kufanikisha matokeo ya muda mfupi yafuatayo: (i) Uhamasishaji wa masuala ya MMMAM katika ngazi zote ili kuongeza uwajibikaji na upatikanaji wa huduma za malezi jumuishi umeimarishwa; (ii) Uratibu wa sekta mbalimbali kwenye ngazi zote umeimarishwa; (iii) Sera, Miongozo, Mitaala na vitini vya kufundishia vimeandaliwa/kufanyiwa mapitio ili kuingiza vipengele vyote vya malezi jumuishi kama ilivyo kwenye jedwali 1. Fedha mahsusi za kuboresha mafunzo na uratibu wa MMMAM ndani ya Wizara na baina ya Wizara unaweza kufungua uelewa zaidi wa kisera na kukuza mahusiano ya kitaasisi.

### 5.2.2 Gharama za utekelezaji za Mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora imeimarishwa

Matokeo yafuatayo ya muda mfupi yatafanikisha matokeo ya muda mrefu ya mfumo wa utoaji huduma ulioimarishwa: (i) Uwepo wa watoa huduma wenye ujuzi na umahiri kwenye malezi jumuishi; (ii) Mifumo ya rufaa na mahusiano ya utoaji huduma ya malezi jumuishi imeimarishwa (iii) Uwepo wa mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji uliokubalika, na (iv) Takwimu za ubora na viwango zinapatikana ili kusaidia utekelezaji wa programu ya MMMAM, kama inavyoonyeshwa katika jedwali II.

### 5.2.3 Gharama za utekelezaji wa Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma bora zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa Watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao

Mpango kazi pendekezi kwa kuongeza ufikiwaji, ubora na huduma zinazoratibiwa za MMMAM unatarajiwa kujumuisha matokeo ya muda mfupi yafuatayo: (i) Utoaji wa huduma bora za afya umeboreshwa; (ii) Upatikanaji wa huduma toshelezi na sahihi za lishe umeongezeka; (iii) Huduma sahihi za malezi yenye mwitikio zimetolewa; (iv) Fursa za ujifunzaji wa awali zimeongezeka; (v) Huduma za ulinzi na usalama wa mtoto zimetolewa; kama inavyoonekana kwenye jedwali III.

### 5.2.4 Gharama za utekelezaji wa kuwajengea uwezo Walezi, familia na jamii wa kutekeleza taratibu sahihi za Malezi jumuishi

Malengo ya muda mfupi yafuatayo yatafanikisha tokeo ya muda mrefu la maarifa, hamasa na usaidizi kwa walezi yameongezeka: (i) Uelewa kuhusu umuhimu wa huduma za malezi jumuishi katika jamii umeongezeka; na, (ii) Wazazi/Walezi na jamii wameshirikishwa kutoa/kuchangia huduma za malezi jumuishi, kama ilivyoainishwa kwenye jedwali na IV.



***Jedwali namba 1:*** Matokeo ya Muda Mrefu na 1: Mazingira wezeshi yameboreshwa kuwezesha uratibu wenye ufanisi na utoaji wa huduma za malezi jumuishi

| Bajeti ya PROGRAMU JUMUISHI YA TAIFA YA MMMAM 2021/22-2025 /26 | JUMLA | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Matokeo ya Muda Mrefu na 1: | | | | | | |
| Mazingira wezeshi yameboreshwa kuwezesha uratibu wenye ufanisi | TSHS | TSHS | TSHS | TSHS | TSHS | TSHS |
| Matokeo ya muda mfupi | | | | | | |
| 1.1: Uhamasishaji wa masuala ya MMMAM katika ngazi zote ili kuongeza uwajibikaji na upatikanaji wa huduma za malezi jumuishi umeimarishwa | 719,353,513 | 543,280,000 | 81,433,000 | 28,592,300 | 31,451,530 | 34,596,683 |
| 1.2: Uratibu wa sekta mbalimbali kwenye ngazi zote umeimarishwa | 124,122,243,178 | 19,825,730,000 | 24,012,010,000 | 23,194,223,800 | 29,025,268,580 | 28,065,010,798 |
| 1.3: Sera, Miongozo, Mitaala na vitini vya kufundishia vimeandaliwa/ kufanyiwa mapitio ili kuingiza vipengele vyote vya malezi jumuishi | 3,006,432,000 | 1,188,330,000 | 1,818,102,000 | 0 | 0 | 0 |
| ***JUMLA NAMBA 1*** | ***127,848,028,691*** | ***21,557,340,000*** | ***25,911,545,000*** | ***23,222,816,100*** | ***29,056,720,110*** | ***28,099,607,481*** |

***Jedwali Namba II:*** Matokeo ya Muda Mrefu na 2: Mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora imeimarishwa

| Matokeo tarajiwa | JUMLA | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Tokeo la Muda Mrefu na 2:** | | | | | | |
| Mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora imeimarishwa | JUMLA | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| **Matokeo ya muda mfupi** | | | | | | |
| 2.1: Uwepo wa watoa huduma wenye ujuzi na umahiri kwenye malezi jumuishi | 29,086,421,300 | 2,883,444,000 | 23,870,570,500 | 2,038,522,000 | 293,884,800 | 0 |
| 2.2: Mifumo ya rufaa na mahusiano ya utoaji huduma ya malezi jumuishi imeimarishwa | 22,675,640,800 | 186,660,000 | 22,488,980,800 | 0 | 0 | 0 |
| 2.3: Uwepo wa mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji uliokubalika | 13,127,891,110 | 7,530,850,000 | 1,312,300,000 | 1,312,661,000 | 1,427,214,100 | 1,544,866,010 |
| 2.4: Takwimu za ubora na viwango zinapatikana ili kusaidia utekelezaji wa programu ya MMMAM | 4,595,801,000 | 923,620,000 | 1,215,577,000 | 962,160,000 | 0 | 1,494,444,000 |
| ***JUMLA NAMBA 2*** | ***69,485,754,210*** | ***11,524,574,000*** | ***48,887,428,300*** | ***4,313,343,000*** | ***1,721,098,900*** | ***3,039,310,010*** |

***Jedwali namba III:*** Matokeo ya Muda Mrefu Na 3: Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma bora zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa Watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao

| Matokeo tarajiwa: | JUMLA | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Tokeo la Muda Mrefu na 3 | | | | | | |
| Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma bora zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa Watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao | TSHS | TSHS | TSHS | TSHS | TSHS | TSHS |
| Matokeo ya muda mfupi | | | | | | |
| 3.1: Utoaji wa huduma bora za afya umeboreshwa | 32,942,277,628 | 859,280,000 | 14,182,685,000 | 15,498,539,100 | 1,143,701,680 | 1,258,071,848 |
| 3.2: Upatikanaji wa huduma toshelezi na sahihi za lishe umeongezeka | 39,022,388,457 | 10,986,462,000 | 16,104,453,200 | 3,604,674,700 | 3,965,142,170 | 4,361,656,387 |
| 3.3: Huduma sahihi za malezi yenye mwitikio zimetolewa | 13,456,043,700 | 0 | 4,065,270,000 | 4,471,797,000 | 4,918,976,700 | 0 |
| 3.4: Fursa za ujifunzaji wa awali zimeongeze | 605,205,889,120 | 99,131,200,000 | 109,044,320,000 | 119,948,752,000 | 131,943,627,200 | 145,137,989,920 |
| 3.5: Huduma za ulinzi na usalama wa mtoto zimetolewa | 2,168,089,000 | 432,355,000 | 374,000,000 | 411,400,000 | 452,540,000 | 497,794,000 |
| ***JUMLA NAMBA 3*** | ***692,794,687,905*** | ***111,409,297,000*** | ***143,770,728,200*** | ***143,935,162,800*** | ***142,423,987,750*** | ***151,255,512,155*** |

***Jedwali namba IV:*** Matokeo ya Muda Mrefu na 4: Wazazi, walezi, familia na jamii wamejengewa uwezo wa kutekeleza taratibu sahihi za malezi jumuishi

| Matokeo tarajiwa: | JUMLA | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Tokeo la Muda Mrefu: 4** | | | | | | |
| Wazazi, walezi, familia na jamii wamejengewa uwezo wa kutekeleza taratibu sahihi za malezi jumuishi | TSHS | TSHS | TSHS | TSHS | TSHS | TSHS |
| **Matokeo ya muda mfupi** | | | | | | |
| 4.1: Uelewa kuhusu umuhimu wa huduma za malezi jumuishi katika jamii umeongezeka | 16,900,042,320 | 4,866,800,000 | 6,776,528,000 | 2,620,376,000 | 1,255,399,200 | 1,380,939,120 |
| 4.2: wazazi/walezi na jamii wameshirikishwa/wamehusishwa katika kutoa/kuchangia huduma za malezi jumuishi | 7,962,838,510 | 0 | 2,330,130,000 | 2,563,143,000 | 2,736,189,940 | 333,375,570 |
| ***JUMLA NAMBA 4*** | ***24,862,880,830*** | ***4,866,800,000*** | ***9,106,658,000*** | ***5,183,519,000*** | ***3,991,589,140*** | ***1,714,314,690*** |



# SURA YA 6: USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA PROGRAMU JUMUISHI YA TAIFA YA MMMAM

## 6.1 Muhtasari

Ushirikiano baina ya sekta mbalimbali ni muhimu katika kuboresha ustawi wa watoto ili kukabiliana na changamoto ngumu tunazokutananazo katika juhudi zetu za kuboresha malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto na kupunguza tofauti katika usawa. Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM imeandaliwa kuhakikisha sekta zote zinazohusiana na MMMAM zinaunganisha na kujumuisha shughuli na miundo ili kuongeza juhudi za upatikanaji wa huduma na kufikia watoto wote bila kujali hali zao. Uchambuzi umeonesha kuwa Tanzania ina fursa kubwa za kutekeleza Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM kwa sababu ya kuwepo kwa sera nzuri, miongozo ya kitaifa, miundo ya utekelezaji, utayari wa serikali na washirika wa maendeleo ambao unaweza kutumika katika kuchangia rasilimali ili kuongeza utoaji wa huduma za MMMAM. Mfano, uzoefu unaweza kutumika kutoka kwenye miradi iliyopita na iliyopo kama vile huduma jumuishi za MMMAM uliotekelezwa mwaka 2008-2011, ambao ulikuwa na mfumo wa uratibu unaofanya kazi. Mifano mingine iliyoonekana ni Program Jumuishi ya Taifa ya Lishe (2016-2021) na MTAKUWWA (2016/17-2021/22) ambayo imefanikiwa kutekelezwa kwa ushirikiano wa sekta mbalimbali.

Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM itashughulikia changamoto zilizoonekana miaka ya nyuma kupitia maazimio ya utekelezaji yaliofanywa na Mawaziri wa Wizara za kisekta zinazohusiana na MMMAM mwaka 2012 katika mkutano wa MMMAM ambapo waliazimia yafuatayo: ***Kuimarisha uratibu wa sekta mbalimbali na kuhakikisha uwezo wa kitaasisi wa kuratibu masuala ya MMMAM na kila mamlaka kutimiza wajibu wake; Uandaaji wa programu ya MMMAM uliobajetiwa; Kuimarisha ushirikiano wa kisekta kwenye ngazi ya taifa na mikoa; Kujengea uwezo watoa huduma; Ubunifu na uhamasishaji wa rasilimali za MMMAM.***

## 6.2 Mfumo wa Uongozi, Usimamizi na Uratibu

Mfumo uliopendekezwa umeandaliwa kwa ajili ya uongozi na usimamizi wa Programu Jumuishi ta Taifa ya MMMAM ambapo unaelezea majukumu na wajibu wa wadau muhimu. Ofisi ya Waziri Mkuu itaongoza na kuratibu utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM, itatoa mwongozo kuhakikisha MMMAM inapewa kipaumbele hasa vipengele vya malezi yenye mwitikio na fursa za ujifunzaji wa awali na kujumuisha programu zote zinazowiana. Uwezekano wa kujumuisha vipengele vya malezi jumuishi katika ngazi ya juu ya kamati elekezi ya lishe na vikundi kazi itafikiriwa ili kuepuka mwingiliano. Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zitahakikishi vipengele vya MMMAM vinaonekana katika Sera, Mikakati, Programu, Kanuni na Miongozo; na kutenga rasilimali za kutosha ili kutekeleza maeneo yao maalumu kwenye Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM. Utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM katika ngazi ya mikoa itakuwa chini ya sekta husika lakini ufuatiliaji na uratibu utajumuishwa katika mifumo iliyopo kwenye ngazi zote za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kutokana na wajibu wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, itahakikisha uratibu, usimamizi, ufatiliaji na tathmini vinafanyika katika ngazi ya mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa ushirikiano na wadau husika, WAMJW Idara kuu ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI watafuatilia, watahamasisha na kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali. Pia watatoa uongozi wa jumla wa kiutendaji, kimkakati kwa kushirikiana na Serikali na Sekta zote pamoja na wadau waliomo kwenye Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM.

***Mchoro namba 11:*** Mfumo Jumuishi wa Taifa wa Uratibu wa MMMAM




***Ufunguo:***

***W-EST:*** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
***W-AMJW:*** Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
***OR-TAMISEMI:*** Ofisi ya Raisi – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
***W-FM:*** Wizara ya Fedha na Mipango
***W-MD:*** Wizara ya Mambo ya Ndani
***KM:*** Katibu Mkuu

## 6.3: Majukumu na wajibu wa wadau

Programu Jumuishi ya Taifa inaongozwa na Mfumo wa Malezi jumuishi ambayo ina vipengele vitano (5) ambavyo ni Afya, Lishe. Ujifunzaji wa awali, Malezi yenye mwitikio, Ulinzi na Usalama vinatekelezwa kupitia Wizara na idara za kisekta (Ofisi ya Rais- TAMISEMI, OWM, WEST, WAMJW, Wizara Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Fedha (WF) kwa ajili ya kutenga bajeti. Kwenye Wizara hizi kuna idara na taasisi ambazo zina wajibu wa kutoa huduma za MMMAM zikiwemo Idara ya Maendeleo ya Jamii, Elimu Msingi, Ustawi wa Jamii, Huduma za Afya ya mama na Mtoto, Dawati la Jinsia na taasisi ya Chakula na Lishe nakadhalika. Kila Wizara ina mamlaka maalumu inayohusiana na kusaidia watoto katika mfumo wa malezi jumuishi kutokana na sheria na sera.

## 6.4: Mahitaji ya Rasilimali Watu na Uwezo wa Kitaasisi

Kuna umuhimu wa kuwajengea uwezo rasilimali watu kuhakikisha Program Jumuishi ya Taifa ya MMMAM inasimamiwa kimkakati katika ngazi zote. Programu hii itahakikisha utoaji wa huduma bora za MMMAM kupitia nguvu kazi zenye uwezo na ujuzi kwa kujumuisha vipengele vya malezi jumuishi kwenye vitini vya kufundishia, mitaala na miongozo ili kuimarisha uwezo wa watoa huduma kwenye ngazi zote zikiwemo taasisi za elimu ya awali, vituo vya afya na kwenye jamii. Pia Program Jumuishi ya Taifa ya MMMAM itahamasisha kuongezeka kwa watoa huduma hasa kwa elimu ya awali, walezi wa watoto wadogo vituoni na kuimarisha mfumo wa rufaa kuhakikisha huduma zote za malezi jumuishi zinatolewa kwa usawa na kwa kina.

## 6.5: Mpango kazi wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM

Kulingana na uchambuzi wa hali halisi na upungufu ulioanishwa, Program Jumuishi ya Taifa ya MMMAM imejikita katika matokeo muhimu manne (4) pamoja na matokeo ya papo kwa hapo na namna ya kuyafikia yakiwemo: (i) Kuboresha mazingira wezeshi, (ii) Kuimarisha uwezo wa mifumo ya kutoa huduma za MMMAM katika sekta zote, (iii) Kuongeza upatikanaji wa huduma bora za MMMAM kwa watoto wadogo wa umri wa miaka 0-8 na (iv) Kuwawezesha walezi, familia na Jamii kwa ujumla kuweza kushiriki kikamilifu na kutoa huduma bora za MMMAM. Matokeo tarajiwa yanahusishwa na maeneo makuu manne ambayo ni:

| | |
|---|---|
| Matokeo ya Muda Mrefu 1: | Mazingira wezeshi yameboreshwa kuwezesha uratibu wenye ufanisi na utoaji huduma za malezi jumuishi |
| Matokeo ya muda mfupi 1.1: | Uhamasishaji wa masuala ya MMMAM katika ngazi zote umeimarishwa ili kuongeza uwajibikaji na upatikanaji wa huduma za malezi jumuishi |
| Matokeo ya muda mfupi 1.2: | Uratibu wa sekta mbalimbali kwenye ngazi zote umeimarishwa |
| Matokeo ya muda mfupi 1.3: | Sera, Miongozo, Mitaala na vitini vya kufundishia zimeandaliwa/kufanyiwa mapitio ya ili kuingiza vipengele vyote vya malezi jumuishi |
| Matokeo ya Muda Mrefu 2: | Mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora imeimarishwa |
| Matokeo ya muda mfupi 2.1: | Uwepo wa watoa huduma wenye ujuzi na umahiri kwenye maeneo ya malezi jumuishi |
| Matokeo ya muda mfupi 2.2: | Mfumo wa rufaa na mahusiano ya utoaji huduma ya malezi jumuishi umeimarishwa |
| Matokeo ya muda mfupi 2.3: | Uwepo wa mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji uliokubalika |
| Matokeo ya muda mfupi 2.4: | Takwimu za ubora na viwango zinapatikana ili kusaidia utekelezaji wa programu ya MMMAM |
| Matokeo ya Muda Mrefu: 3: | Kuongezeka kwa huduma bora na zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao |
| Matokeo ya muda mfupi 3.1 | Utoaji wa huduma bora za afya zimeboreshwa |
| Matokeo ya muda mfupi 3.2 | Upatikanaji wa huduma toshelezi na sahihi za lishe umeongezeka |
| Matokeo ya muda mfupi 3.3 | Huduma sahihi za malezi yenye mwitikio zimetolewa |
| Matokeo ya muda mfupi 3.4 | Fursa za ujifunzaji wa awali zimeongezeka |
| Matokeo ya muda mfupi 3.5 | Huduma za ulinzi na usalama wa mtoto zimetolewa |
| Matokeo ya Muda Mrefu 4: | Wazazi, walezi, familia na jamii wamejengewa uwezo wa kutekeleza taratibu sahihi za malezi jumuishi |
| Matokeo ya muda mfupi 4.1 | Uelewa kuhusu umuhimu wa huduma za malezi jumuishi katika jamii umeongezeka |
| Matokeo ya muda mfupi 4.2 | Wazazi/walezi na jamii wameshirikishwa/wamehusishwa katika kutoa/kuchangia huduma za malezi jumuishi |



# *SURA YA 7:* UFUATILIAJI, TATHMINI, UWAJIBIKAJI NA UJIFUNZAJI

## *7.1 Muhtasari*

Mfumo jumuishi wa ufuatiliaji, tathmini, uwajibikaji na ujifunzaji ni muhimu katika kuhakikisha matumizi yenye tija na utekelezaji wa shughuli kwa wakati ili kufikia malengo tarajiwa ya programu. Mfumo wa ufuatiliaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM unalenga kuakisi mfumo wa utoaji taarifa uliounganishwa kwa ajili ya kufuatilia viashiria vya malezi jumuishi vya MMMAM vinavyoendana na utekelezaji wa programu. Taarifa hizo zitatumika kutengeneza ushahidi kupitia mapitio ya Mwaka ya MMMAM na tathmini ya kati na ya mwisho na kupitia tafiti za utekelezaji. Ushahidi utakaopatikana utatumika kutaarifu maendeleo ya utekelezaji, mipango, kutengeneza sera na miradi ijayo. Mfumo wa ufuatiliaji unaleta pamoja sekta mbalimbali na wadau wakiwemo Wizara na Idara za kisekta, Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wadau wa watekelezaji, Wadau wa Maendeleo, Asasi za Kiraia, Sekta binafsi, makampuni na jamii.

Taarifa na takwimu kwenye MMMAM zilizopo Tanzania zipo kisekta na zinatunzwa kupitia mifumo mbalimbali iliyopo ambayo inaendana na programu ya malezi Jumuishi. Mifumo hiyo ni: *"DHIS2, BEMIS, DHS, CPMIS, Integrated Case Management Information System, Health Management Information Systems, Growth Monitoring, Education Information Management System (EIMS), Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) Information System, and the Multi-sectoral Nutrition Information System (MNIS)".*

Pamoja na mifumo hii kujumuisha vipengele vya malezi jumuishi, taarifa zake hazijafanyiwa tathmini kwa jicho la MMMAM. Kwa sababu hiyo, viashiria vichache ambavyo ni muhimu vya malezi jumuishi vinakosekana kwenye mifumo hii. Kupitia mpango huu, uchambuzi utafanyika kwenye mifumo iliyopo kutambua na kuongeza viashiria vinavyokosekana. Vilevile, miaka ya hivi karibuni tafiti mbalimbali zimefanyika kushughulikia masuala ya malezi jumuishi. Tafiti hizi zikiwemo *"Situation Analysis and Baseline Study on Early Childhood Education in Tanzania Mainland, Analysis and Mapping of Parenting and Family Care Practices and Interventions in Tanzania (UNICEF), Early Childhood Development Situation Analysis in Tanzania (2018) by Children in Crossfire (CiC), and Tanzania National Nutrition Surveys"* pamoja na zinginezo. Hata hivyo tafiti hizi hazikufanyika kwa nia ya kuimarisha mifumo hivyo haziwezi kutumika kwenye maeneo mengine ya nchi. Kupitia mpango wa ufuatiliaji, tathmini, uwajibikaji na ujifunzaji, mbinu thabiti zilizoratibiwa zitatumika kukusanya takwimu zitarasimishwa.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto-Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii inawajibu wa kusimamia mfumo jumuishi wa taarifa za MMMAM na kuangalia mpango wa Ufuatiliaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM. Idara kuu wa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na wadau wengine watatoa msaada wa kiufundi na rasilimali ili kujengea uwezo watoa huduma kwenye matumizi ya kanzi data jumuishi ya MMMAM kwa ajili ya kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa viashiria vya malezi jumuishi. Wajibu huo wa Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii utahakikisha ukusanyaji wa takwimu, uchambuzi na matumizi yanayoendana na utekelezaji wa programu.

## 7.2 Malengo ya Mfumo wa ufuatiliaji wa Sekta mbalimbali zinazotekeleza Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM

Lengo la mfumo wa ufuatiliaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM ni kufikia matokeo mawili ambayo ni: Kuhakikisha kwamba mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na kujifunza uko kwenye sekta zote na unakusanya takwimu kwa ajili ya kutaarifu Programu. Ili kufanikisha lengo hilo, Programu inapendekeza mikakati ifuatayo:

*i.* Kuimarisha mfumo wa utoaji taarifa za MMMAM na kujumuishwa kwenye mifumo ya taarifa na tafiti za wilaya (District Information System and Surveys)

*ii.* Kuimarisha zana za uthibiti ubora ili kujumuisha uwezo wa kipekee wa mtoto

*iii.* Kutengeneza zana za uchunguzi kwa ajili ya kutambua watoto wenye mahitaji maalumu kwenye vituo ya kulelea watoto chini ya miaka mitano

*iv.* Kuendeleza utafiti wa magonjwa na vifo vya watoto wa miaka 5-8

*v.* Kufanya tafiti katika matendo ya malezi yenye mwitikio kwa watoto wenye umri wa miaka 0-8 nchini Tanzania; na

*vi.* Kufanya utafiti wa viashiria jumuishi vya MMMAM ili kutambua maendeleo ya viashiria hivi nchini.

## 7.3 Mfumo wa pamoja wa matokeo, rasilimali na uwajibikaji (CRRAF)

Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM imefuata Mfumo wa pamoja wa matokeo, rasilimali na uwajibikaji kutoka Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe uliotengenezwa mwaka 2016.

Mfumo huu (Kiambatisho 4) unatumika kama msingi wa kujumuisha utekelezaji wenye ufuatiliaji na tathmini, rasilimali na uwajibikaji kwa vitendo: Viambata vya mfumo huu ni:

*i.* Matokeo tarajiwa (Matokeo ya muda mfupi, kati, mrefu)

*ii.* Kufafanua idadi ya watu ambao nafasi za maisha yao zinaweza kuboresha kwa kutumia afua zilizopendekezwa;

*iii.* Mpangilio wa afua ambao ukitekelezwa utachangia mabadiliko tarajiwa

*iv.* Ufafanuzi uliowazi wa wajibu wa kila Wizara husika, Idara na Taasisi za Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa afua zilizopangwa

*v.* Wajibu na majukumu ya wadau wasio serikali

*vi.* Mfumo wa pamoja wa ufuatiliaji utendaji na tathmini

*vii.* Jedwali la gharama ambayo inatambua michango kutoka kwa serikali na wadau.

## 7.4 Ufuatiliaji, Mapitio na Tathmini

Utekelezaji wa Programu ya Taifa ya MMMAM utafuatiliwa kupitia mikutano jumuishi ya mapitio ya mwaka katika ngazi ya Taifa, Mikutano ya nusu mwaka katika ngazi ya Mkoa na mikutano ya robo mwaka katika ngazi ya Halmashauri, Kata na Kijiji/Mtaa. Mikutano hii ipo kama njia ya ufuatiliaji wa huduma zinazotolewa ingawa inafanyika kisekta. Hata hivyo, malezi jumuishi hayajajumuishwa kikamilifu kwenye mipango yao. Programu hii imeweka mipango ya kujumuisha viashiria vya malezi jumuishi vilivyokosekana kwenye mipango ya kisekta iliyopo na kuhakikisha ufuatiliaji wa viashiria hivi kupitia mikutano ya mapitio ya programu iliyopo katika ngazi mbalimbali za Serikali.

Vilevile, tathmini ya kati imepangwa kufanyika mwaka wa fedha 2023/24 na tathmini ya mwisho imepangwa kufanyika mwaka wa fedha 2025/26. Taarifa za mwaka zitaandaliwa kutokana na hali ya utekelezaji wa kila mwaka mpaka mwisho wa programu ikiwa kama sehemu ya utaratibu wa kawaida wa utekelezaji. Mikutano ya robo mwaka itatumika kama jukwaa la kupima maendeleo na mafanikio ya matokeo ya muda mfupi baada ya utetekelezaji. Mafanikio ya matokeo ya muda mfupi yatachangia matokeo makubwa yaliyooneshwa kwenye mfumo wa Matokeo na nadharia ya mabadiliko. Mapitio ya matokeo ya kati yatafanyika mwaka 2023/24 yatatumika kama njia ya kufuatilia maendeleo katika kufikia matokeo. Vilevile, katika mwaka wa mwisho, mkutano wa pamoja wa mapitio ya programu utatumika kama fursa ya kutathmini programu yote.

## 7.5 Ujifunzaji na Utafiti wa Kiutendaji

Tafiti zimepangwa ili kusaidia mchakato wa kutengeneza taarifa ya utekelezaji ili kutambua ubunifu, mbinu zilizoleta matokeo chanya, vizuizi na viwezeshi. Tafiti mbili zinapangwa kufanyika ili kuleta takwimu katika maeneo muhimu ya malezi yenye mwitikio kwa watoto kuanzia miaka 0-8 na hali ya magonjwa na vifo kwa watoto wenye umri wa miaka 5-8. Matokeo kutoka kwenye tafiti hizi yatatumika kama takwimu za awali kwenye viashiria ambavyo kwa sasa havipo kwenye mipango ya kisekta. Mikutano ya mwaka ya mapitio ya programu itachangia kutambua maeneo yanayohitaji uchunguzi wa kina na ushahidi ili kuboresha na kutaarifu programu za baadae. Ili kuimarisha upimaji wa viashiria vinavyowalenga watoto wenye mahitaji na uwezo maalum, zana za uchunguzi na uthibiti ubora zitaandaliwa.


8
3

# *SURA YA 8:* MPANGO WA UWEKEZAJI KIMKAKATI KWENYE PROGRAMU JUMUISHI YA TAIFA YA MMMAM

## *8.1 Muhtasari*

Upatikanaji wa huduma za MMMAM umeenea ulimwenguni. Hata hivyo, nchi zenye uchumi wa chini na wa kati kama Tanzania, watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu hukosa huduma na pia utekelezwaji wa Programu hizo huwa wa kiwango cha chini. Licha ya uhitaji mkubwa ya kuwekeza kwa watoto wadogo, kwa sasa kiwango cha fedha kilichowekezwa kwa MMMAM hakitoshelezi na hivyo huathiri utoaji wa huduma bora kwa watoto wote tangu kuzaliwa[92].

Kumekua na tafiti za kina ulimwenguni kuhusu uwekezaji wa kifedha kwa huduma za MMMAM. Wataalamu wanakadiria kwamba uwekezaji wa umma wa japo asilimia moja ya mapato ghafi unahitajika ili kuweza kutoa huduma bora za malezi jumuishi ya awali na elimu[93] . Ukijumuisha uwekezaji wa umma unaohitajika kwa shughuli za elimu, afya na ulinzi zinazohusiana na MMMAM, inakadiriwa kwamba kati ya asilimia 2 na asimilia 2.5 ya mapato ghafi yanahitajika kuwekezwa kwenye MMMAM[94]. Licha ya makadirio haya, serikali zimekua zikiwekeza wastani wa asilimia 0.1 tu ya mapato ghafi kwenye MMMAM. Vyanzo vingine vya fedha kwa ngazi zote za kitaifa na kimataifa imesaidia kutatua uhaba wa fedha. Katika upande wa misaada ya kimataifa, misaada kutoka mashirika ya fedha ya kimataifa wa maendeleo umekua ni chanzo kikubwa cha fedha tangu mwaka 2012 ikilinganishwa na misaada inayotoka kwa nchi moja moja. Misaada ya kimataifa kwa ajili ya MMMAM ni asilimia mbili tu ya misaada yote inayoelekezwa kwenye elimu ya msingi. Mifuko ya misaada pia inachangia kwa kiasi kikubwa kutoa misaada ya kifedha kwenye huduma za MMMAM[95]. Sawia na huduma nyingine za kijamii, michango ya wazazi/walezi ikiwa ni pamoja na ada na kujitolea muda wao ni muhimu katika kutoa huduma za MMMAM.

Ni vigumu sana kuchangisha fedha kwa ajili ya huduma za MMMAM kwa sababu serikali nyingi zinaitazama huduma hizi kama sio rasmi na hivyo hakuna sababu ya kuwekeza kwa ajili hiyo. Kwa kiasi kikubwa fedha za kuendesha sekta hii hutegemea wafadhili ambao fedha zao zimekua sio za uhakika. Kwa sasa serikali na wafadhili wanashindwa kuakisi umuhimu wa elimu ya awali katika kuweka vipaumbele vya bajeti zao. Sawia na ngazi nyingine za elimu, sekta hii ina rasilimali fedha kidogo sana hususani katika nchi zenye uchumi mdogo na wa kati. Hali ya kukosekana kwa fedha kitaifa na kimataifa inazorotesha upatikanaji wa huduma bora za MMMAM ulimwenguni[96] .

[92] Financing Early Childhood Development -An analysis of International and Domestic sources in Low- and Middle-Income countries August 2016. International commission on financing Global Education Opportunity. Results for Development.

[93] Neuman, M.J. & Devercelli, A. E. (2013). What matters most for early childhood development: A framework paper. Systems Approach for Better Education Results (SABER) working paper series; No. 5. Washington, DC: World Bank Group. Retrieved from: https://openknowledge.worldbank. org/handle/10986/20174

[94] Vargas-Baron, E. (2008). Participatory ECD policy planning in francophone West Africa. In M. H. Garcia, J. E. Evans & A. Pence (Eds.), Africa's future, Africa's challenge: Early childhood care and development in Sub-Saharan Africa (pp. 187–198). Washington, DC: The World Bank.

[95] Financing Early Childhood Development -An analysis of International and Domestic sources in Low- and Middle-Income countries August 2016. International commission on financing Global Education Opportunity. Results for Development

[96] A World Ready to Learn: Prioritizing quality early childhood education, UNICEF, April 2019.

*Mchoro namba 12* unaonesha hali ya kifedha kwa sasa kwa nchi nyingi ulimwenguni[97].




Aina ya matumizi ya fedha ambayo kwa ujumla wake yanatoa picha halisi ya kiasi cha fedha kinachopatikana kwa ajili ya huduma ya MMMAM ni pamoja na matumizi ya afya yanayohusiana na huduma ya mama na mtoto, na chanjo. Afua maalum za lishe ni pamoja na lishe kwa wamama wajawazito, watoto mchanga, watoto wenye umri chini ya miaka mitano na vijana balehe, program maalumu za kupambana na utapiamlo mkali, virutubisho mbadala na kuhamasisha unyonyeshaji wa maziwa ya mama. Matumizi kwenye program maalumu za lishe yakijumuisha kilimo na ulinzi wa chakula, Afya na VVU, Maji na Usafi na Mazingira; Elimu na MMMAM; Ulinzi wa jamii, mazingira pamoja na mabadiliko ya tabia nchi. Matumizi kwenye elimu (elimu ya awali na program za malezi) pamoja na program za ulinzi wa jamii (pamoja na kutoa fedha za kujikimu kwa kaya masikini na program za watoto yatima na wale wanaoishi kwenye mazingira hatarishi au watoto wenye ulemavu. Matumizi yalioanishwa hapo juu yamewekwa kwa muhtasari kwenye mchoro namba 12.

Fedha kwa ajili ya huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto hupatikana kutoka kwa serikali na taasisi zisizo za serikali. Hii inahusisha serikali kuu, serikali za mitaa, wadau wa maendeleo, wafadhili, AZAKI, mashirika ya dini, mashirika ya kibiashara, jamii na Kaya Inakadiriwa kwamba wadau wa maendeleo kwa kushirikiana na serikali, mashirika yasiyo ya serikali, shule na jamii watawekeza rasimali zao ambazo zaweza kua ni rasilimali fedha au rasilimali watu ili kutekeleza Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM.

[97] Transforming the Financing of Early Care and Education. Committee on Financing Early Care and Education with a highly qualified workforce La Rue Allen and Emily P. Backes 2018.

***Mchoro namba 13:*** Matumizi ya fedha kuhusiana na MMMAM Chanzo: Denboba na wenzake 2014[98]

<table>
<tr><th colspan="2">Ujauzito</th><th>kuzaliwa</th><th>Miezi 12</th><th>Miezi 24</th><th>Miezi 36</th><th>Miezi 48</th><th>Miezi 60</th></tr>
<tr><td rowspan="5">Lishe</td><td rowspan="2">Unasihi utoaji wa chakula wakati ujauzito</td><td rowspan="3">Unyonyeshaji wa maziwa ya mama pekee</td><td colspan="2">Ulishaji vyakula vya nyongeza</td><td colspan="3">Vyakula vya nyongeza vya ziada</td></tr>
<tr><td colspan="5">Unasihii wa taratibu za ulishaji watoto na lishe</td></tr>
<tr><td rowspan="2">Kutumia vidonge vya madini chuma na foliki asidi wakati wa ujauzito</td><td colspan="5">Kutumia vidonge vyenye madini ya zinki ili kutibu ugonjwa wa kuharisha</td></tr>
<tr><td colspan="6">Kufuatilia ukuaji na maendeleo ya mtoto (kuzuia na kutibu utapiamlo kwa watoto)</td></tr>
<tr><td colspan="7">Kuongeza virutubisho kwenye vyakula</td></tr>
<tr><td rowspan="6">Afya</td><td>Kuhudhuria kliniki</td><td colspan="6">Chanjo</td></tr>
<tr><td colspan="2">Kupaa huduma za ukunga</td><td></td><td colspan="4">Dawa ya kutibu  minyoo</td></tr>
<tr><td colspan="7">Kuzuia magonjwa  (malaria, kuzuia maambukizi ya VVU toka kwa mama kwenda kwa mtoto na magonjwa mengine )</td></tr>
<tr><td colspan="7">Uzazi wa Mpango</td></tr>
<tr><td colspan="7">Upatikanaji wa huduma za Afya  (kuhudhuria kliniki, kupima na kutambua watoto wenye ulemavu na kutibu majeraha na magonjwa )</td></tr>
<tr><td colspan="7">Kuzuia na kutibu sonona kwa wanawake baada ya kujifungua</td></tr>
<tr><td rowspan="3">Maji na usafi wa mazingira</td><td colspan="7">Upatikanaji wa maji safi na salama</td></tr>
<tr><td colspan="7">Usafi wa mwili na kunawa mikono</td></tr>
<tr><td colspan="7">Usafi wa mazingira</td></tr>
<tr><td rowspan="3">Elimu</td><td colspan="7">Kuwasaidia na kuwapa wazazi mafunzo uchangamshi wa awali, ukuaji na maendeleo ya mtoto)</td></tr>
<tr><td></td><td colspan="6">Uchangamshi wa awali</td></tr>
<tr><td colspan="3"></td><td colspan="4">Programu za elimu ya awali zenye ubora</td></tr>
<tr><td rowspan="4">Ulinzi na usalama</td><td></td><td colspan="6">Usajili wa vizazi</td></tr>
<tr><td></td><td colspan="6">Likizo ya uzazi na matunzo bora ya watoto au vituo vya malezi ya watoto wakati wa mchana</td></tr>
<tr><td colspan="7">Programu ya hifadhi ya jamii(mfuko wa msaada kwa watoto, kuhaulisha fedha kwa kaya maskini kwa masharti nafuu au bila masharti</td></tr>
<tr><td colspan="7">Afua za ulinzi na usalama wa watoto (kuzuia na kushughulikia vitendo vya ukatili dhidi ya  watoto na ulinzi wa watoto yatima</td></tr>
<tr><td rowspan="2">Utawala Bora</td><td colspan="7">Kuwa na utawala unaoakisi masuala ya MMMAM</td></tr>
<tr><td colspan="7">Kuwa na sera au kanuni za Lishe, Afya, Elimu na Hifadhi ya Jamii (Kanuni za Ulinzi na Usalama wa mtoto)</td></tr>
</table>

[98]Denboba, A.; Sayre, R.; L, Wodon; Rawlings, Elder, L; Lombardi, J..2014.Investing in young children: key interventions and principles to ensure all young children reach their full potential (English). Education notes; no. 3 Washington, D.C: World Bank Group.

Muundo wa fedha unahitaji mfumo ambao ni wa kimkakati, unaolenga kupata matokeo, kushirikisha wadau muhimu, kuhamasisha umiliki wa kitaifa, uongozi na ushiriki. Hii ina maana kwamba Programu ihakikishe kuwa MMMAM kipaumbele cha serikali na kwamba inaingizwa katika mijadala ya kimkakati na unakua ni sehemu ya ufuatiliaji, ripoti na tathmini ya malengo ya kati na ya muda mrefu kama vile Dira ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Kupunguza na Kuondoa Umasikini (MKUKUTA). Pia ikumbukwe kwamba Tanzania tayari imeshavuka kutoka kwenye uchumi mdogo kwenda kwenye uchumi wa kati hivyo basi Programu hii Jumuishi ya Taifa ya MMMAM imekuja wakati muafaka. Upo uwezekano wa kubadilika kwa muundo na fursa za upatikanaji wa fedha kutoka kwenye muundo wa sasa wa misaada inayolenga maendeleo ya mwanadamu kwenda kwenye mikopo kwa ajili ya miundombinu. Mabadiliko haya yanatakiwa kuwa sehemu ya mijadala ya kimkakati.

Kuongeza fedha kwenye ngazi ya serikali za mitaa ambazo huratibu huduma za MMMAM itasaidia kuhakikisha matumizi mazuri ya rasilimali pesa sambamba na kuongeza umiliki wa serikali kwenye mpango husika, usimamizi na ushiriki wa wadau wote kama serikali jamii, shule, kaya, wadau wa maendeleo, mashirika ya dini na Mashirika binafsi.

## *8.2 Mahitaji ya kifedha ya Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM*

Muhtasari wa kiwango cha fedha kinachohitajika kutekeleza Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM kwa kuzingatia matokeo tarajiwa ya muda mrefu yameanishwa kwenye jedwali hapa chini. Mpango uliowekewa bajeti ya utekelezaji katika kipengele cha 5.2 inatoa picha halisi ya kiasi cha fedha kinachohitajika kwa ajili ya kufikia malengo ya kati na kutekeleza shughuli muambata kulingana na nadharia ya mabadiliko iliyokubaliwa.

Ukiangalia bajeti kwa ajili ya matokeo tarajiwa ya muda mrefu, fungu kubwa limetengwa kwa ajili ya lengo la namba 3 ambalo ni kuongeza uratibu wa upatikanaji huduma bora za MMMAM ambazo zimelenga kutoa huduma (asilimia 75.72), na kufuatiwa na lengo la muda mrefu namba 1 lililolenga kuboresha sera na uratibu kama sehemu ya kuboresha mazingira ya utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM na lengo la muda mrefu namba 2 lililolenga kuimarisha mifumo (asilimia 7.59). Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa lengo la muda mrefu namba 4 ambalo limelenga kutekeleza shughuli kwa upande wa wahitaji hususani kuongeza uelewa, kuwapa motisha na kuwasaidia walezi wa watoto na jamii kwa ujumla ni 2.72 (angalia jedwali hapa chini).

Jedwali Na. V: Muhtasari wa mahitaji ya fedha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM

| Bajeti ya PROGRAMU JUMUISHI YA TAIFA YA MMMAM 2021/22-2025/26 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | Jumla | Jumla* | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ***MATOKEO YA MUDA MREFU*** | TZS | TZS | TZS | TZS | TZS | TZS | USD | |
| ***1: Mazingira wezeshi yameboreshwa kuwezesha uratibu wenye ufanisi na utoaji huduma za malezi jumuishi*** | 21,557,340,000 | 25,911,545,000 | 23,222,816,100 | 29,056,720,110 | 28,099,607,481 | 127,848,028,691 | $ 55,106,909 | 13.97% |
| ***2: Mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora imeimarishwa*** | 11,524,574,000 | 48,887,428,300 | 4,313,343,000 | 1,721,098,900 | 3,039,310,010 | 69,485,754,210 | $ 29,950,756 | 7.59% |
| ***3: Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma bora na zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa Watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao*** | 111,409,297,000 | 143,770,728,200 | 143,935,162,800 | 142,423,987,750 | 151,255,512,155 | 692,794,687,905 | $ 298,618,400 | 75.72% |
| ***4: Wazazi, walezi, familia na jamii wamejengewa uwezo wa kutekeleza taratibu sahihi za malezi jumuishi*** | 4,866,800,000 | 9,106,658,000 | 5,183,519,000 | 3,991,589,140 | 1,714,314,690 | 24,862,880,830 | $ 10,716,759 | 2.72% |
| *Jumla* | *149,358,011,000* | *227,676,359,500* | *176,654,840,900* | *177,193,395,900* | *184,108,744,336* | ***914,991,351,636*** | $ 394,392,824 | *100 %* |

* Kiwango cha ubadilishaji hela kilichotumika kutoka TSHS kwenda USD ni 2,320 sawa na wastani wa kiwango cha ubadilishaji hela cha mwaka 2021 kilichotumika na Benki Kuu ya Tanzania.

## 8.3 Rasilimali fedha zilizopo na nakisi ya bajeti

Mchakato wa kutengeneza mkakati wa kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM utakadiria rasilimali zilizopo kwa upande wa serikali, wadau wa maendeleo, asasi za kiraia, jamii, mashirika ya dini, na mashirika binafsi, na kubainisha nakisi ya bajeti. Mchakato huu utafanyika kwa kushirikisha wadau mbalimbali kwa kuzingatia uwasilishwaji wa matokeo lengwa yaliyoanishwa kwenye mpango huu na kuwaomba wadau kutoa makadirio yao ya fedha walizotenga kwa kwa kipindi cha utekelezaji 2021/22-2025/26.

Serikali inapaswa kujikita kwenye agenda za Malengo ya Maendeleo endelevu, imeakisiwa katika mipango yake ya maendeleo ya miaka mitano ili kuongeza upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza afua za MMMAM. Vyanzo vingine vya fedha ni kutoka kwa mashirika yasiyo ya serikali ya hapa nchini na yale ya kimataifa; mashirika ya dini, mashirika na watu binafsi, fedha za shule zitokanazo na miradi ya kujitegemea. Michango ya jamii kama vile fedha taslimu, nguvu kazi na vifaa; na vyanzo vya mapato kutoka kwenye halmashauri, vijiji na mitaa inatakiwa kujumuishwa. Wadau wote wanahamasishwa kuweka wazi bajeti zao, suala ambalo ni nguzo muhimu kwenye sera ya uwazi kati ya serikali na asasi za kiraia. Hali hii itasaidia kuweka na mipango ya ugawaji wa rasilimali fedha kulingana na mahitaji pamoja na kufuatilia matumizi yake.

## 8.4 Mpango wa kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali

Mkakati wa kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali utaandaliwa ili kuratibu uhamasishaji wa upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM. Sehemu ya rasilimali za utekelezaji zitatokana na michango kutoka serikali za mitaa na baadhi ya fedha nyingine zitatokana na michango wa wadau mbalimbali ikiwemo Taasisi za fedha za kimataifa wafadhili mmoja mmoja na wadau wengine wa MMMAM.

Mkakati utakaotumika katika kukusanya rasilimali ni kuunda kikosi kazi kitakachokua na jukumu la kuandaa mpango mkakati utakaotumika kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali. Kikosi kazi hicho kitaongozwa na kikosi kazi cha kusimamia Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto (Idara ya Watoto) na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) watasaidia uhamasishaji wa rasilimali katika ngazi ya taifa, mikoa na kimataifa kwa kutumia mikakati ifuatayo:

Kuimarisha mifumo ya serikali na kuleta umiliki na usimamizi thabiti

- Kuingiza viashiria vya MMMAM katika mipango na mikakati mbalimbali ya taifa, ili kuongeza hamasa ya kuwekeza kwenye bajeti ya MMMAM. Ili kufanikisha lengo hilo, serikali inatakiwa kuhakikisha Mpango wa tatu wa maendeleo ya taifa unahusisha viashiria vya rasilimali watu pamoja na MMMAM; kufuatana na mikakati ya kisekta ya elimu, lishe, afya, ulinzi na usalama. Mipango hii yote ambayo muda wake wa utekelezaji unaishia 2021 ina viashiria vya muhimu vya MMMAM.

- Kuhusisha idara muhimu za mipango na fedha katika shughuli zinazohusiana na mapango wa kitaifa wa MMMAM ili kufahamu umuhimu wa kuwekeza kwenye MMMAM au rasimali watu katika umri mdogo. Walengwa wawe wakurugenzi wa Wizara ya Fedha pamoja na kamati zinazohusika na mipango na bajeti; Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na wadau wengine ambao wanahusika na kupanga bajeti za serikali pamoja na Ikama ya watumishi ili kuhakikisha nguvu kazi kwa ajili ya MMMAM inaongezeka.

- Kuongeza msaada wa OR-TAMISEMI kuhakikisha vipaumbele ya MMMAM vinakua sehemu ya muongozo wa bajeti ya mwaka. Muongozo huu utagawiwa kwenye halmashauri ili kuhakikisha bajeti ya MMMAM inazingatiwa kama ilivyo kwenye Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM kutoka kwenye ngazi za chini za hatua za utengenezwaji wa bajeti kwenda kwenye ngazi za juu za uandaaji wa bajeti. Maelekezo haya kutoka kwenye ngazi ya juu ya serikali yatahakikisha bajeti zinazotengezwa kutoka ngazi ya chini hadi juu zinazingatia masuala ya MMMAM yanawekewa msisitizo kwenye bajeti ya taifa hususan kwenye kila sekta.

- Uhamasishaji wa jamii: kuhamasisha jamii kuchangia huduma za MMMAM kama ujenzi wa vituo vya MMMAM na madarasa ya elimu ya awali, upatikanaji wa chakula pale inapowezekana, na kuwapa motisha wanaojitolea katika utoaji huduma n.k

### Kuimarisha ushirikiano wa wadau

| 3.1.2.4 | Manunuzi ya vifaa vya ufuatiliaji wa ukuaji na maendeleo ya mtoto (mizani ya kupimia uzito, Ubao wa kupimia urefu/kimo na vifaa vya michezo vinavyoendana na umri wa mtoto) katika vituo vya afya | WAMJW | OR-TAMISEMI, Wadau wa maendeleo, AZAKI | Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe | Idadi ya vituo vya afya vyenye vifaa vya ufuatiliaji wa ukuaji na maendeleo ya mtoto (mizani ya kupimia uzito, Ubao wa kupimia urefu/kimo na vifaa vya michezo vinavyoendana na umri) | Orodha ya usambazaji wa vifaa; Orodha ya vifaa; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Hakuna | | 6160 (lengo limegawanywa kwa miaka 2 ya utekelezaji) | 6159 (lengo limegawanywa kwa miaka 2 ya utekelezaj) | | | Vituo vyote vya afya vimefikiwa (12,319) (mizani 12,319 za kupimia uzito, Vibao 12,319 vya kupimia urefu/kimo na vifaa vya michezo vinavyoendana na umri) | | | | | |
| 3.2 | Matokeo ya muda mfupi 3.2: Upatikanaji wa huduma toshelezi na sahihi za lishe umeongezeka | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.2.1 | *Matokeo ya papo kwa papo 3.2.1 Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe umepitiwa kuongeza vipengele vya malezi jumuishi* | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.2.1.1 | Kufanya mkutano wa kupitia mpango jumuishi wa Taifa wa Lishe wa pili ili kuhakikisha vipengele vya malezi jumuishi vimeingizwa. | WAMJW | WAMJW, OR-TAMISEMI, OWM-SUBKVAU na WEST | Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe | Mpango jumuishi wa lishe uliopitiwa wenye vipengele vya malezi jumuishi | Mpango jumuishi wa taifa wa lishe uliopitiwa; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Mpango jumuishi wa taifa wa lishe uliopo | 1 | | | | | Mpango jumuishi wa taifa wa lishe uliopitiwa | | | | | |
| 3.2.2 | *Matokeo ya papo kwa papo 3.2.2: Afua za lishe zinatolewa katika shule za awali na madarasa ya mwanzo ya shule za msingi* | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.2.2.1 | Kuchunguza na kutambua hali ya lishe na hatua za ukuaji kwa watoto wenye umri wa miaka 5 - 8 katika shule za awali na madarasa ya mwanzo shule za msingi (darasa la kwanza hadi la tatu) kama sehemu ya programu za afya | WAMJW | OR-TAMISEMI, WEST | Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe | Idadi za shule za awali zilizotembelea ili kuchunguza na kutambua watoto wenye matatizo ya ukuaji na lishe | Taarifa za uchunguzi za watoto; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Hakuna Takwimu | 16401 (Kufikiwa kwenye robo 4) | 16401 (Kufikiwa kwenye robo 4) | 16401 (Kufikiwa kwenye robo 4) | 16401 (Kufikiwa kwenye robo 4) | | Jumla ya matembezi 65,604 kwenye shule za awali yamefanyika | | | | | |

| Na | Matokeo ya muda mfupi na Shughuli | Taasisi inayoongoza | Taasisi zinazoshirikiana | Kuunganisha na programu za kitaifa zilizopo | Viashiria vya matokeo ya muda mfupi | Mbinu za uthibitishaji | Taarifa za awali | Lengo la mwaka wa fedha | Lengo la mwaka wa fedha wa 2 | Lengo la mwaka wa fedha wa 3 | Lengo la mwaka wa fedha wa 4 | Lengo la Mwaka mwaka wa fedha wa 5 | Target Malengo ya Jumla | Mwaka wa fedha 1 | | | | Mwaka wa fedha 2 | | | | Mwaka wa fedha 3 | | | | Mwaka wa fedha 4 | | | | Mwaka wa fedha 5 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | | Q1 | Q2 | Q3 | Q4 | Q1 | Q2 | Q3 | Q4 | Q1 | Q2 | Q3 | Q4 | Q1 | Q2 | Q3 | Q4 | Q1 | Q2 | Q3 | Q4 |
| 3.2.3 | Matokeo ya papo kwa papo 3.2.3 Programu ya utoaji chakula shuleni kwa watoto wa shule za awali na madarasa ya mwanzo ya shule za msingi (darasa la kwanza hadi la tatu) imetekelezwa | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.2.3.1 | Kutoa mafunzo ya awali ya siku 3 kwa wawezeshaji 20 wa kitaifa juu ya namna ya kutumia Mwongozo wa programu ya utoaji wa chakula shuleni | WEST | OR-TAMISEMI, WEST, Wadau wa maendeleo, AZAKI | Programu za afya za shule zilizopo na Mpango wa maendeleo ya sekta ya elimu | Idadi na wawezeshaji kitaifa waliopatiwa mafunzo ya awali ili kutumia mwongozo wa programu ya utoaji wa chakula shuleni | Taarifa za mafunzo/mafunzo ya awali; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Hakuna Takwimu | 20 | | | | | Wawezeshaji 20 wa kitaifa waliopatiwa mafunzo ya awali kwenye matumizi ya mwongozo wa programu ya lishe | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.2.3.2 | Kutoa mafunzo ya awali ya siku 3 kwa walimu na watendaji kati kuhusu namna ya kutumia Mwongozo wa programu ya utoaji wa chakula shuleni katika halmashauri zote. | WEST | OR-TAMISEMI, WEST, Wadau wa maendeleo, AZAKI | programu za afya za shule zilizopo na Mpango wa maendeleo ya sekta ya elimu | Idadi ya walimu waliopatiwa mafunzo ya awali ya matumizi ya mwongozo wa programu ya utoaji wa chakula shuleni | Taarifa za mafunzo/mafunzo ya awali; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Hakuna Takwimu | Walimu 16,401 (walimu 2 kwa kila shule* shule 8,201) | Walimu 16401 (walimu 2 kwa shule * shule 8200) | | | | Walimu 32,802 wamepatiwa mafunzo ya awali | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | Idadi ya afisa watendaji wa kata waliopatiwa mafunzo ya awali ya matumzi ya mwongozo wa programu ya utoaji wa chakula shuleni | Taarifa za mafunzo/mafunzo ya awali; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Hakuna Takwimu | Afisa Mtendaji kata 3720 (Afisa elimu kata 2 kwa kata *Kata 1860) | Afisa Mtendaji Kata 3720 (afisa elimu kata 2* kata 1860) | | | | Afisa watendaji kata 7,440 waliopatiwa mafunzo | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.2.3.3 | Conduct 3 days orientation meeting to teachers and ward officers in all LGAs on school feeding program guideline | MoEST | PO-RALG, MoEST, NGOs, INGOs, DPs | Existing School Health Program and ESDP | Number of teachers oriented on school feeding program guideline; | Training/ Orientation reports; ECD Progress Report | No data | 16401 teachers ( 2 teachers per school* 8201 schools) | 16401 teachers ( 2 teachers per school* 8200 schools) | | | | 32,802 teachers oriented | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | Number of Ward Officers oriented on the use of the school feeding program and guidelines | Training/ Orientation reports ;ECD Progress Report | No data | 3720 ward officers (2 ward officers per ward*1860 wards) | 3720 ward officers (2 ward officers per ward*1860 wards) | | | | 7,440 Ward Officers (WEOs) oriented | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.2.3.4 | a) Kuanzisha shughuli za ufugaji kuku, wanyama wadogo na kilimo cha bustani katika ngazi ya shule ili kutoa chakula chenye virutubisho muhimu kwa watoto kupitia programu ya utoaji wa chakula shuleni na kubadilisha taratibu za ulishaji wa watoto katika ngazi ya kaya | OR-TAMISEMI | OR-TAMISEMI, WEST, Wadau wa maendeleo, AZAKI, Kitengo cha chakula na lishe Tanzania | Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe | "Idadi ya shule zenye shughuli zilizoanzishwa za bustani, ufugaji wa wanyama wadogo na kuku " | Taarifa za shughuli za lishe kwenye halmashauri na shule; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Mikoa 9 iliyofikiwa na mashirika ya Equip-T and PCI (yamefikia shule 5,331) | | Shule 11,070 zilizoanzisha shughuli za bustani, ufugaji wa wanyama wadogo na kuku. | | | | Shule 16,401 zilizoanzisha shughuli za bustani, ufugaji wa wanyama wadogo na kuku. | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | OR-TAMISEMI, WEST, Wadau wa maendeleo, AZAKI, Taasisi ya Chakula na lishe | Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe | Idadi ya wajumbe wa kamati za shule waliopatiwa mafunzo ya awali ya kuanzisha shughuli za bustani, ufugani wa wanyama wadogo na kuku | Taarifa za shughuli za lishe kwenye halmashauri na shule; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Wajumbe wa kamati za shule 63, 972 | | Wajumbe wa kamati za shule 132,840 (12 x 11,070) wamepatiwa mafunzo ya mwanzo ya uanzishaji shughuli za bustani, ufugaji wa wanyama wadogo na kuku | | | | Wajumbe wa kamati za shule 196,812 (12 x 16,401) wamepatiwa mafunzo ya mwanzo ya uanzishaji shughuli za bustani, ufugaji wa wanyama wadogo na kuku | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |

| Na | Matokeo ya muda mfupi na Shughuli | Taasisi inayoongoza | Taasisi zinazoshirikiana | Kuunganisha na programu za kitaifa zilizopo | Viashiria vya matokeo ya muda mfupi | Mbinu za uthibitishaji | Taarifa za awali | Lengo la mwaka wa fedha | Lengo la mwaka wa fedha wa 2 | Lengo la mwaka wa fedha wa 3 | Lengo la mwaka wa fedha wa 4 | Lengo la Mwaka mwaka wa fedha wa 5 | Target Malengo ya Jumla | Mwaka wa fedha 1 (Q1 Q2 Q3 Q4) | Mwaka wa fedha 2 (Q1 Q2 Q3 Q4) | Mwaka wa fedha 3 (Q1 Q2 Q3 Q4) | Mwaka wa fedha 4 (Q1 Q2 Q3 Q4) | Mwaka wa fedha 5 (Q1 Q2 Q3 Q4) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | b). Kufuatilia utekelezaji wa shughuli za ufugaji kuku, wanyama wadogo na kilimo cha bustani katika ngazi ya shule | OR-TAMISEMI | MISEMI, WEST, Wadau wa maendeleo, AZAKI, Taasisi ya Chakula na lishe | Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe | Idadi ya ya kamati za shule zilizopatiwa mafunzo ya awali ya namna ya kuanzisha ufugaji kuku, wanyama wadogo na kilimo cha bustani zilizofatiliwa | "Taarifa za ufuatiliaji, Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM " | Hakuna Takwimu | | Kamati za shule 33,210 zimetembelewa | Kamati za shule 33,210 zimetembelewa | Kamati za shule 33,210 zimetembelewa | Kamati za shule 33,210 zimetembelewa | Kamati ya shule 132,840 zimetembelewa | | | | | |
| | | OR-TAMISEMI | MISEMI, WEST, Wadau wa maendeleo, AZAKI, Taasisi ya Chakula na lishe | Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe | Idadi ya wajumbe wa kamati za shule waliopatiwa mafunzo ya awali ya kuanzisha shughuli za bustani, ufugani wa wanyama wadogo na kuku waliotembelewa | "Taarifa za ufuatiliaji, Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM " | Hakuna Takwimu | | Shule 4,100 | Shule 4,100 | Shule 4,100 | Shule 4,100 | Shule 16,401 | | | | | |
| 3.2.4 | *Matokeo ya papo kwa papo 3.2.4: Maadhimisho ya Siku ya afya na lishe vijijini yamefanyika yakijumuisha utoaji wa huduma mkoba za afya ya mama, baba na mtoto* | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.2.4.1 | Kufanya maadhimisho ya siku ya afya na lishe vijijini | OR-TAMISEMI | WAMJW (Idara za mandeleo ya jamii na afya), OWM-SUBKVAU, WEST, Taasisi ya chakula na lishe, AZAKI | Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe | Idadi za vijiji vilivyoadhimisha siku za afya na lishe | Taarifa ya utekelezaji ya wakuu wa mikoa kuhusu shughuli za lishe, Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Jumla ya vijiji 1,597 vimefikiwa kupitia mashirika ya UNICEF (4- Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa imefikia vijiji 1549); na shirika la IMMA World Health (Vijiji 48 vya shinyanga 48 ) | 2,144 (Asilimia ya 20 ya vijiji) | 3,216 (Asilimia 30 ya vijiji) | 3, 217 (Asilimia 30 ya vijiji) | 2,144 (Asilimia 20 ya vijiji) | | Maadhimisho 24,638 yamefanyika katika 12,319 hadi kufikia mwaka 2025 | | | | | |
| 3.3. | Matokeo ya muda mfupi 3.3: Huduma sahihi za malezi yenye mwitikio zimetolewa | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.3.1 | *Matokeo ya papo kwa papo 3.3.1: Kona jumuishi za MMMAM zenye vifaa vya kutosha vya michezo na kujifunzia zimeanzishwa* | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.3.1.1 | Kuanzisha kona jumuishi za MMMAM zenye vifaa vya kutosha vya michezo na kujifunzia vinavyoendana na umri wa mtoto kwenye vituo vyote vya afya (12,319) katika Halmashauri zote 184 ili kutoa nafasi ya michezo na mawasiliano kati ya mlezi na mtoto; pia kusaidia kutambua uwezo na mahitaji ya mtoto na kufanya rufaa sahihi | WAMJW | OR-TAMISEMI, Wadau wa maendeleo, Wadau wa MMMAM | Mkoba wa malezi kwa makuzi (CCD) & mwongozo wa uandaaji wa vifaa vya michezo/ kujifunzia kupitia MMMAM | Idadi ya vituo vya afya vyenye kona jumuishi za MMMAM | Taarifa za ufuatiliaji uliofanyika; Taarifa za halmashauri za utekelezaji; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Hakuna Takwimu | | Vituo vya afya 4,106 vyenye kona jumuishi za MMMAM | Vituo vya afya 4,106 vyenye kona jumuishi za MMMAM | Vituo vya afya 4,106 vyenye kona jumuishi za MMMAM | | Vituo vya afya 24,638 vyenye kona jumuishi za MMMAM kwenye halmashauri 184 LGAs hadi mwaka 2025 | | | | | |

| Na | Matokeo ya muda mfupi na Shughuli | Taasisi inayoongoza | Taasisi zinazoshirikiana | Kuunganisha na programu za kitaifa zilizopo | Viashiria vya matokeo ya muda mfupi | Mbinu za uthibitishaji | Taarifa za awali | Lengo la mwaka wa fedha | Lengo la mwaka wa fedha wa 2 | Lengo la mwaka wa fedha wa 3 | Lengo la mwaka wa fedha wa 4 | Lengo la Mwaka mwaka wa fedha wa 5 | Target Malengo ya Jumla | Mwaka wa fedha 1 | | | | Mwaka wa fedha 2 | | | | Mwaka wa fedha 3 | | | | Mwaka wa fedha 4 | | | | Mwaka wa fedha 5 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | | 01 | 02 | 03 | 04 | 01 | 02 | 03 | 04 | 01 | 02 | 03 | 04 | 01 | 02 | 03 | 04 | 01 | 02 | 03 | 04 |
| 3.3.2 | *Matokeo ya papo kwa papo 3.3.2: Huduma za mara kwa mara za unasihi wa malezi jumuishi kwa wazazi na walezi zimetolewa* | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.3.2.1 | Kutoa huduma za mara kwa mara za unasihi wa malezi jumuishi kwa wazazi na walezi | WAMJW | OR-TAMISEMI, Wadau wa maendeleo, Wadau wa MMMAM | Mkoba wa malezi kwa makuzi (CCD) & mwongozo wa uandaaji wa vifaa vya michezo/ kujifunzia kupitia MMMAM | Idadi ya vituo vya afya vilivyotoa huduma za unasihi kwenye malezi jumuishi | Orodha ya washiriki; Orodha ya vituo vya afya vinavyotoa huduma za unasihi wa malezi jumuishi; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | 0 | | Vituo vya afya 3,077 vilivyotoa huduma za unasihi za malezi jumuishi | Vituo vya afya 3,077 vilivyotoa huduma za unasihi za malezi jumuishi | Vituo vya afya 3,077 vilivyotoa huduma za unasihi za malezi jumuishi | Vituo vya afya 3,077 vilivyotoa huduma za unasihi za malezi jumuishi | Vituo vya afya 12,319 vilivyotoa huduma za unasihi 24,638 (12,319 x 2 ) | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.4 | Matokeo ya muda mfupi 3.4: Fursa za ujifunzaji wa awali zimeongezeka | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.4.1 | *Matokeo ya papo kwa papo 3.4.1 Fursa za ujifunzaji wa awali kwa watoto zimeongezeka* | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.4.1.1 | Kusaidia uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya malezi ya watoto wenye umri wa miaka 0 - 2 kwenye maeneo rasmi na yasio rasmi ya kazi ili kuimarisha unyonyeshaji, malezi yenye mwitikio na ujifunzaji wa awali. | WAMJW | OR-TAMISEMI, AZAKI | Miongozo na viwango kwa ajili ya kuendesha vituo vya malezi vya watoto chini ya miaka 0-2 | Idadi za vituo vya malezi vya watoto chini ya miaka 0-2 zilizoanzishwa kwenye jamii na maeneo ya kazi | Taarifa za mamlaka ya serikali za mitaa, Taarifa kwenye mfumo wa taarifa za afya; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Hakuna Takwimu | 50 | 75 | 75 | | | Vituo vya malezi ya wototo miaka 0-2, 200 vimeanzishwa kwenye halmashauri 184 | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.4.1.2 | Kusaidia uanzishaji kwa vituo vya kulelea watoto vya MMMAM vinavyomilikiwa na jamii | WAMJW | OR-TAMISEMI, AZAKI | Miongozo na viwango kwa ajili ya kuendesha vituo vya malezi vya watoto chini ya miaka 5 | Idadi ya vituo vya kulelea watoto chini ya miaka 5 vilivyoanzishwa kwenye/karibu shule za msingi | Taarifa za mamlaka ya serikali za mitaa, Taarifa kwenye mfumo wa taarifa za afya; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Hakuna Takwimu | 3280 | 4920 | 4920 | 3281 | | Vituo 16,401 vya kulelea watoto chini ya miaka 5 vilivyoanzishwa kwenye halmashauri 184 | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.4.1.3 | Kusaidia uanzishaji wa ujenzi/uanzishaji wa madarasa ya awali kwenye maeneo rasmi na yasio rasmi | OR-TAMISEMI | WEST, AZAKI | Miongozo na viwango vya elimu ya awali | Idadi ya madarasa ya elimu ya awali yaliojengwa/ anzishwa kwenye maeneo rasmi na yasio rasmi | Taarifa za mamlaka ya serikali za mitaa, Taarifa kwenye mfumo wa taarifa za afya; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Hakuna Takwimu | 3280 | 4920 | 4920 | 3281 | | Madarasa ya awali mapya 16,401 yaliyojengwa kwenye halmashauri 184 | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.4.2 | *Matokeo ya papo kwa papo 3.4.2 Msaada unaotolewa kwa familia na jamii wa kuwapa elimu ya malezi na kutoa huduma za malezi jumuishi umeongezeka* | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.4.2.1 | Kusaidia uanzishaji wa vikundi vya malezi katika jamii | WAMJW | OR-TAMISEMI, AZAKI | Muongozo wa uanzishaji wa vikundi malezi | Idadi ya vikundi malezi vilivyoanzishwa kwenye vijiji vyote 12,319 | Taarifa za mamlaka ya serikali za mitaa, Taarifa kwenye mfumo wa taarifa za afya; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Vikundi 3,963 vimeshaanzishwa | 4,135 | 6,203 | 6,202 | 4,135 | | vikundi malezi 24,638 vimeanzishwa (vikundi 2 kwa kila kijiji 12,31) | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |

| Na | Matokeo ya muda mfupi na Shughuli | Taasisi inayoongoza | Taasisi zinazoshirikiana | Kuunganisha na programu za kitaifa zilizopo | Viashiria vya matokeo ya muda mfupi | Mbinu za uthibitishaji | Taarifa za awali | Lengo la mwaka wa fedha | Lengo la mwaka wa fedha wa 2 | Lengo la mwaka wa fedha wa 3 | Lengo la mwaka wa fedha wa 4 | Lengo la Mwaka mwaka wa fedha wa 5 | Target Malengo ya Jumla | Mwaka wa fedha 1 (Q1 Q2 Q3 Q4) | Mwaka wa fedha 2 (Q1 Q2 Q3 Q4) | Mwaka wa fedha 3 (Q1 Q2 Q3 Q4) | Mwaka wa fedha 4 (Q1 Q2 Q3 Q4) | Mwaka wa fedha 5 (Q1 Q2 Q3 Q4) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.4.2.2 | Kusaidia upatikanaji wa mitaji kwa vikundi vya malezi | WAMJW | WEST, OR-TAMISEMI, AZAKI | Muongozo wa uanzishaji wa vikundi malezi | Idadi ya vikundi malezi vilivyopokea fedha ya mtaji | Taarifa za mamlaka ya serikali za mitaa, Taarifa kwenye mfumo wa taarifa za afya; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Hakuna Takwimu | 4,928 | 7,391 | 7,391 | 4,928 | | Vikundi 24,638 vimesaidiwa na fedha ya mtaji | | | | | |
| 3.5 | **Matokeo ya muda mfupi 3.5: Upatikanaji wa huduma za ulinzi na usalama umeongezeka** | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.5.1 | ***Matokeo ya papo kwa hapo 3.5.1 : Vituo vya mkono kwa mkono vinavyotoa huduma za ulinzi na usalama kwa watoto wadogo vimeanzishwa.*** | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3.5.1.1 | Kuwezesha uanzishaji wa vituo 97 vya mkono kwa mkono katika hospitali za wilaya ambazo zitatoa huduma za ulinzi na usalama kwa mama na mtoto wakiwemo watoto wenye umri wa miaka 0-8. | WAMJW | OR-TAMISEMI,Wizara ya Mambo ya ndani ya nchi, Wizara ya Katiba na Sheria (Watoa msaada wa kisheria), OWM-SUBKVAU, Wadau wa Maendeleo, Wadau wa MMMAM, AZAKI | MTAKUWWA (Mwongozo wa kuanzisha vituo vya mkono kwa mkono) | Idadi ya vituo vya mkono kwa mkono vilivyoanzishwa kwenye vituo vya afya | "Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM " | Vituo vya mkono kwa mkono vilivyopo ni 16 | Idadi ya vituo 16 vya mkono kwa mkono vitakavyoanzishwa | Idadi ya vituo 16 vya mkono kwa mkono vitakavyoanzishwa | Idadi ya vituo 16 vya mkono kwa mkono vitakavyoanzishwa | Idadi ya vituo 16 vya mkono kwa mkono vitakavyoanzishwa | Idadi ya vituo 17 vya mkono kwa mkono vitakavyoanzishwa | Jumla ya Vituo 97 vya mkono kwa mkono kuaanzishwa kwenye hospitali za Wilaya | | | | | |
| 3.5.1.1.1 | Kutoa mafunzo ya awali kwa watoa huduma (wanasihi, manesi, madaktari, polisi na afisa ustawi jamii) kuhusu huduma rafiki kwa mtoto | WAMJW | OR-TAMISEMI,Wizara ya Mambo ya ndani ya nchi, Wizara ya Katiba na Sheria (Watoa msaada wa kisheria), Wadau wa MMMAM, AZAKI | MTAKUWWA (Mwongozo wa kuanzisha vituo vya mkono kwa mkono) | Idadi ya watoa huduma walio kwenye vituo vya mkono waliopata mafunzo ya usimamizi wa vituo hivyo | "Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM; Taarifa za mafunzo " | Watoa huduma kwenye vituo 16 vya mkono kwa mkono wameshapatiwa mafunzo ya awali | Watoa huduma 485 | | | | | Watoa huduma 485 kwenye vituo 97 mkono kwa mkono waliopata mafunzo | | | | | |
| 3.5.1.1.2 | Kuanzisha/ Kujenga vituo vipya 81 vya huduma ya mkono kwa mkono kwenye hospitali za Wilaya na kukarabati vituo 40 vya huduma ya mkono kwa mkono kwa kutumia majengo yaliyopo kwenye hospitali na kuweka samani na vifaa vikiwemo kona rafiki ya michezo yenye vifaa vya michezo | WAMJW | OR-TAMISEMI,Wizara ya Mambo ya ndani ya nchi, Wizara ya Katiba na Sheria (Watoa msaada wa kisheria), Wadau wa MMMAM, AZAKI | MTAKUWWA (Mwongozo wa kuanzisha vituo vya mkono kwa mkono) | Idadi ya vituo vya mkono kwa mkono vilivyoanzishwa katika hospitali za Wilaya | Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM; | Vituo 16 kwenye hospitali za Wilaya vimeshanzishwa | 16 | 24 | 25 | 16 | | Vituo 81 vya mkono kwa kwa mkono vilivyoanzishwa | | | | | |
| | | | | | Idadi ya vituo vilivyokarabatiwa | Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM; | Hakuna Takwimu | 8 | 12 | 12 | 8 | | Vituo 40 vya mkono kwa kwa mkono vilivyokarabatiwa | | | | | |

| Na | Matokeo ya muda mfupi na Shughuli | Taasisi inayoongoza | Taasisi zinazoshirikiana | Kuunganisha na programu za kitaifa zilizopo | Viashiria vya matokeo ya muda mfupi | Mbinu za uthibitishaji | Taarifa za awali | Lengo la mwaka wa fedha | Lengo la mwaka wa fedha wa 2 | Lengo la mwaka wa fedha wa 3 | Lengo la mwaka wa fedha wa 4 | Lengo la Mwaka mwaka wa fedha wa 5 | Target Malengo ya Jumla | Mwaka wa fedha 1 (Q1 Q2 Q3 Q4) | Mwaka wa fedha 2 (Q1 Q2 Q3 Q4) | Mwaka wa fedha 3 (Q1 Q2 Q3 Q4) | Mwaka wa fedha 4 (Q1 Q2 Q3 Q4) | Mwaka wa fedha 5 (Q1 Q2 Q3 Q4) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4 | **Matokeo ya Muda Mrefu 4: Wazazi, walezi, familia na jamii wamejengewa uwezo wa kutekeleza taratibu sahihi za malezi jumuishi** | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 4.1 | **Matokeo ya Muda Mfupi 4.1:Uelewa kuhusu umuhimu wa huduma za malezi jumuishi ktk jamii umeongezeka** | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 4.1.1 | ***Matokeo ya papo kwa papo 4.1.1: Uhamasisha wa jamii kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wadogo katika miaka ya awali umefanyika*** | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 4.1.1.1 | Kuandaa ujumbe wa MMMAM ili kuhamasisha na kuongeza uelewa kwenye umuhimu wa kuwekeza katika huduma za malezi jumuishi kupitia vyombo vya habari | WAMJW | Kitengo cha mawasiliano cha Wizara ya Afya, Wizara ya Habari, OR-TAMISEMI, AZAKI | Mkakati wa Kitaifa wa Malezi/ MTAKUWWA | Idadi za ujumbe wa MMMAM zilizoandaliwa | Taarifa zinazotolewa na redio jamii & Ujumbe wenyewe kupitia radio; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Ujumbe 12 za MMMAM zimeshaandaliwa na shirika EGPAF | 10 | 10 | 10 | 10 | 8 | Ujumbe 60 za MMMAM zimeandaliwa | | | | | |
| | | | | | Idadi ya redio za kijamii zilizorusha ujumbe za MMMAM | Community radio report & Actual radio spots monitoring database; ECD Progress Report. Taarifa ya redio za kijamii na redio zilizorusha jumbe ;Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | 3 radio stations under EGPAF Vituo vya redio vitatu (3) chini ya shirika la EGPAF | 31 | 34 | 34 | 34 | 34 | Redio za jamii 34 zimerusha ujumbe wa MMMAM | | | | | |
| 4.1.1.2 | Kujenga uelewa wa wadau muhimu katika jamii kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wadogo kuanzia miaka ya awali kwenye ngazi ya kata. | WAMJW | OR- TAMISEMI, WEST,Wizara ya Mambo ya ndani ya nchi, OWM-SUBKVAU, AZAKI | Mkakati wa Kitaifa wa Malezi/ MTAKUWWA | Idadi ya Kata zilizofanya uhamasishaji kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wadogo kuanzia miaka ya awali. | Taarifa za vikao; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | 0 | 989 | 989 | | | | 1,978 (= Asilimia 50 ya Kata 3,956) | | | | | |
| 4.1.1.3 | Kuandaa mikutano ya kuhamasisha kwa viongozi wa kijamii, viongozi wa dini, sekta binafsi na viongozi mashuhuri kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wadogo kuanzia miaka ya awali | WAMJW | OR- TAMISEMI, WEST,Wizara ya Mambo ya ndani ya nchi, OWM-SUBKVAU, AZAKI | Mkakati wa Kitaifa wa Malezi/ MTAKUWWA | Idadi ya vijiji vilivyofanya uhamasishaji kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wadogo kuanzia miaka ya awali kwa viongozi. | Taarifa za vikao. | 0 | | 4,146 | 4,146 | | | Vijiji/Mitaa 8,292 | | | | | |
| 4.1.1.4 | Kufanya mikutano ya uhamasishaji kwa madiwani ili kuongeza kiwango cha uwekezaji kwenye huduma za malezi jumuishi | WAMJW | OR- TAMISEMI, WEST, Wizara ya Mambo ya ndani ya nchi, OWM-SUBKVAU, AZAKI | MTAKUWWA | Idadi ya madiwani waliohamasishwa kuhusu huduma za jumuishi za malezi kwenye halmashauri zao. | Taarifa za vikao; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | 0 | | 1340 | 500 | | | Madiwani 1,840 kwenye halmashauri (20 Madiwani * 92 halmashauri) | | | | | |

| Na | Matokeo ya muda mfupi na Shughuli | Taasisi inayoongoza | Taasisi zinazoshirikiana | Kuunganisha na programu za kitaifa zilizopo | Viashiria vya matokeo ya muda mfupi | Mbinu za uthibitishaji | Taarifa za awali | Lengo la mwaka wa fedha | Lengo la mwaka wa fedha wa 2 | Lengo la mwaka wa fedha wa 3 | Lengo la mwaka wa fedha wa 4 | Lengo la Mwaka mwaka wa fedha wa 5 | Target Malengo ya Jumla | Mwaka wa fedha 1 (Q1 Q2 Q3 Q4) | Mwaka wa fedha 2 (Q1 Q2 Q3 Q4) | Mwaka wa fedha 3 (Q1 Q2 Q3 Q4) | Mwaka wa fedha 4 (Q1 Q2 Q3 Q4) | Mwaka wa fedha 5 (Q1 Q2 Q3 Q4) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4.2 | Matokeo ya muda mfupi 4.2: Wazazi/Walezi na jamii wameshirikishwa kutoa/kuchangia huduma za malezi jumuishi | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 4.2.1 | *Matokeo ya Papo kwa papo 4.2.1: Mwongozo wa uanzishaji wa dawati la ulinzi wa mtoto shuleni imesambazwa* | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 4.2.1.1 | Kusambaza mwongozo wa uanzishaji wa dawati la ulinzi wa mtoto shuleni kupitia kuwajengea uwezo wa awali waratibu wa elimu, maafisa ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii kwenye kata na halmashauri zote. | WAMJW | OR-TAMISEMI, WEST na AZAKI | MTAKUWWA, muongozo ya uanzishaji wa dawati la ulinzi wa mtoto shuleni | Idadi ya Maafisa ustawi wa jamii, maafisa maendeleo ya jamii na maafisa wa elimu waliopatiwa mafunzo ya awali kwenye mwongozo ya uanzishaji wa dawati la ulinzi wa mtoto shuleni uliyosambazwa kwenye ngazi za kata na halmashauri | Taarifa za vikao; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | 0 | | 4,232 | 4,232 | | | Maafisa wa ustawi wa jamii, Maendeleo ya Jamii, na elimu 8,464 wamepatiwa mafunzo ya awali hadi mwaka 2024 | | | | | |
| 4.2.2 | *Matokeo ya Papo kwa papo 4.2.2: Vituo vya kulelea watoto wadogo chini ya miaka 5 vimeanzishwa* | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 4.2.2.1 | Kushirikisha wazazi / walezi na jamii katika kusaidia kuendeleza huduma za malezi jumuishi kwenye vituo vya kulelea watoto wadogo chini ya miaka 5, elimu ya awali na madarasa ya mwanzo ya shule za msingi (darasa la kwanza hadi la tatu) | WAMJW | WAMJW, OR-TAMISEMI, AZAKI, Wadau wa maendeleo | Mpango wa Jumuishi wa Taifa wa Lishe | "Idadi ya vijji vilivyotoa mafunzo ya awali kwa wadau wake ili kuendeleza huduma za malezi jumuishi. " | Taarifa za shughuli; Taarifa ya utekelezaji ya MMMAM | Hakuna takwimu | | 6160 | 6159 | | | Vijiji 12,319 | | | | | |
| 4.2.2.2 | Kuwezesha uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto chini ya miaka 5, (Creches, Day care centre, community based ECD centres) kwenye maeneo rasmi na yasio rasimi ili kuwezesha huduma za malezi jumuishi. | WAMJW | WEST, OWM-SUBKVAU, OR-TAMISEMI, AZAKI | Miongozo ya viwango vya uanzishaji wa vituo vya watoto wadogo chini ya miaka 5 na creches | Idadi ya afisa maendeleo wa jamii na afisa ustawi wa jamii waliopata mafunzo ya awali kuhusu miongozo ya taifa ya kuanzisha Creches na vituo vya kulelea watoto wadogo mchana chini ya miaka 5. | Taarifa za Mamlaka za serikali za Mtaa na taarifa za mafunzo ya awali; Taarifa ya utekelezaji wa MMMAM | Hakuna takwimu | | 105 | 105 | 105 | 105 | 420 Maafisa wa ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii wamepatiwa mafunzo ya awali | | | | | |

## *Kiambatisho 2: Maelezo ya kina ya shughuli kwa kila matokeo*

### Matokeo ya Muda Mrefu, Mfupi, na ya Papo kwa Papo

### *Matokeo ya muda mrefu 1: Mazingira wezeshi yameboreshwa kuwezesha uratibu wenye ufanisi na utoaji huduma za malezi jumuishi.*

### Matokeo ya muda mfupi 1.1: Uhamasishaji wa masuala ya MMMAM katika ngazi zote umeimarishwa ili kuongeza uwajibikaji na upatikanaji wa huduma za malezi jumuishi

Matokeo ya Papo kwa papo 1.1.1: Mkakati wa uhamasishaji wa MMMAM umeandaliwa

Shughuli 1.1.1.1: Kuandaa mkakati jumuishi wa taifa wa MMMAM unaotafsiri mfumo wamalezi jumuishi

Mchakato wa kutengeneza mfumo huu utasimamiwa na WAMJW kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, wadau wa utekelezaji, wizara, Idara na wakala wa Serikali, na wajumbe 10 waliopatiwa mafunzo na mtandao wa Afrika wa masuala ya malezi Jumuishi (AfECN) kuhusu utengenezaji wa mkakati wa uhamasishaji wa masuala ya MMMAM. Mchakato utahusisha vipindi vitatu vya mikutano na kutambua mikakati ya uhamasishaji iliyopo katika vipengele vingine vya malezi jumuishi kwa ajili ya rejea. Hii ni kuhakikisha kuwa mkakati wa uhamasishaji unakamilika ifikapo Disemba mwaka 2021

Matokeo ya Papo kwa Papo 1.1.2: Uhamasishaji wa viongozi katika ngazi zote umefanyika.

Shughuli 1.1.2.1: Kufanya mkutano na wadau wa maendeleo ili waweze kuchangia gharama za utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM

OWM na WAMJW wataitisha mkutano wa siku moja na wadau wa maendeleo, Asasi za kiraia, ili kuwajengea uelewa kuhusu masuala ya MMMAM na kufanya uhamasishaji wa rasilimali. Mkutano huo utakuwa ni jukwaa la kutoa elimu kuhusu MMMAM, sayansi ya MMMAM na vipengele vingine vya malezi jumuishi. Mkutano huu unategemea kufanyika mwaka 2021.

Shughuli 1.1.2.2: Kufanya mkutano wa uhamasishaji kwa kamati mbalimbali za bunge kuwajengea uelewa kuhusu Programu Jumuishi ya MMMAM.

OWM na WAMJJW watafanya mkutano wa siku moja wabunge kutoka kamati mbalimbali za bunge mwanzoni mwa mwaka 2021 ili kuwajengea uelewa kuhusu programu ya MMMAM, kuwekeza katika miaka ya karibuni, na kusaidia katika utekelezaji wa programu. Mkutano huo utakuwa ni jukwaa la kutoa elimu kuhusu MMMAM, sayansi ya MMMAM na vipengele vingine vya malezi jumuishi pia kuingiza shughuli za MMMAM katika mipango na bajeti ya kisekta.

Shughuli 1.1.2.3: Kufanya mikutano ya uhamasishaji kwa maafisa kutoka ngazi za juu za wizara za kisekta ili waweze kuingiza viashiria vya masuala ya MMMAM katika mifumo ya utoaji taarifa

Ingawa kuna njia mbalimbali za kisekta za ufuatiliaji wa programu, taarifa za MMMAM zimetawanyika na hazijakusanya taarifa za viashiria vingine kama malezi yenye mwitikio na fursa ya ujifunzaji wa awali. Ili Kujumisha viashiria vingine katika mfumo wa kisekta wa ukusanyaji taarifa inahitaji idhini kutoka kwa wafanya maamuzi. WAMJW kwa kushirikiana na wizara, Idara na wakala wa Serikali, wadau, Ofisi ya Waziri Mkuu wataitisha mkutano wa siku 2 kufanya uhamasishaji wa awali kwa wataalamu wa TEHAMA na mkutano wa siku 1 wa uhamasishaji kwa wakuu wa idara wa wizara husika. Lengo la mkutano huo ni kuwajengea

uelewa kuhusu umuhimu wa kutengeneza kanzi data ya MMMAM na kujumuisha viashiria vilivyokosekana katika mfumo uliopo.

Shughuli 1.1.2.4: Kutoa mafunzo ya awali kwa waandishi wa habari ili kuwajengea uelewa kuhusu masuala ya MMMAM waweze kutoa taarifa sahihi juu ya masuala ya watoto wenye umri kati ya miaka 0-8

Kwa kutambua umuhimu wa vyombo vya habari katika kufanya uhamasishaji wa uhitaji wa huduma, OR-TAMISEMI ikishirikiana na WAMJJW, wadau wa maendeleo, wizara ya Habari,Utamaduni,Sanaa na Michezo watatoa mafunzo ya siku mbili kwa waandishi wa habari 10 kwa kila mkoa nchini. Mafunzo haya yatatoa uelewa kuhusu huduma jumuishi za MMMAM. Lengo la mafunzo haya ni kuwawezesha waandishi wa habari waendelee kurusha ujumbe unaohusu masuala jumuishi ya MMMAM katika vyombo vya habari na kuifikia jamii

Shughuli 1.1.2.5: Kuhamasisha mapitio ya mitaala ya vyuo vikuu ( Vyuo vya Ualimu, Vyuo vya uuguzi na Taasisi za Ustawi wa jamii) ili kuingiza masuala ya elimu ya Awali na ya malezi jumuishi

Elimu na ujuzi wa masuala ya MMMAM/ Malezi jumuishi ni muhimu katika sekta zote ikiwemo Taasisi ya Elimu. Kuwepo na programu za MMMAM katika taasisi za elimu ikiwemo vyuo vya mafunzo ya ualimu inaongeza uelewa mkubwa kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwenye malezi ya awali. Kwa sasa ipo mitaala inayotumika katika vyuo vya mafunzo ya ualimu ambayo haijaingiza masuala ya elimu ya awali na vipengele vya Malezi Jumuishi. Hali hii inapelekea kuwepo na walimu wasio na ujuzi wa kufundisha Watoto katika ngazi ya elimu ya awali. WEST pamoja na WAMJW watashirikiana na wadau wa Maendeleo ambao ni UNICEF na UNESCO, wadau watekelezaji, MDAs na Mamlaka za serikali za mitaa watafanya angalau mikutano sita ya mapitio na wadau mbalimbali ili kuingiza masuala ya MMMAM katika mitaala ya kufundishia walimu. Mchakato huu utahusisha utoaji elimu kwa wakuu wa vyuo/taasisi kuhusu umuhimu wa kuingiza masuala ya MMMAM kwenye mitaala yao.

Shughuli 1.1.2.6: Kuhamasisha viongozi wa dini ili kujumuisha masuala ya malezi jumuishi katika mwongozo wa kidini

Kwa sasa kuna miongozo inayoongoza mahubiri ya dini mbalimbali ambayo inatakiwa iboreshwa ili kuingiza vipengele vya malezi jumuishi. WAMJW itatumia jukwaa la Imani kuhakikisha taarifa muhimu kuhusu masuala ya MMMAM zinawafikia jamii kubwa. Wizara kwa kushirikiana na wadau kama MoHA, OR-TAMISEMI, Interreligious Council for Peace in Tanzania (IRCPT) na wadau wengine wa MMMAM wataitisha kikao cha siku 3 kitakachoshirikisha taasisi 60 za dini ili kupitia miongozo yao ya mahubiri na kuhakikisha wanaingiza masuala ya MMMAM katika miongozo yao.Activity 1.1.2.7: Establishment of NM-ECDP secretariat.

## Matokeo ya muda mfupi 1.2: Uratibu wa sekta mbalimbali kwenye ngazi zote umeimarishwa

Matokeo ya papo kwa papo 1.2.1: Mfumo wa kitaifa wa uratibu wa programu umeimarishwa

Shughuli 1.2.1.1: Kufanya mapitio ya mwongozo wa uratibu/hadidu za rejea ili kujumuisha Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM katika ngazi zote (Taifa- Mkoa- Halmashauri-Kata-vijiji/mtaa)

Kuweka kipimo cha miongozo iliyopo ya uratibu wa kitaifa katika programu zilizopo pamoja na MTAKUWWA, Programu ya jumuishi ya taifa ya Lishe, afya na elimu. Lengo la shughuli hii ni kuingiza masuala ya uratibu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM - Malezi Jumuishi yanayolingana na miundo iliyopo, rasilimali na kuongeza uwajibikaji juu ya huduma za malezi jumuishi katika ngazi zote. Ili kuwezesha mchakato huu, WAMJW & OWM watashirikiana na idara za serikali zinazohusika, wadau wa maendeleo, wadau wanaotekeleza maendeleo na mamlaka ya serikali za mitaa kufanya angalau vikao vitatu vya kufanya mapitio ili kuingiza maswala yanayohusiana na utaratibu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM katika miongozo ya uanzishaji wa MTAKUWWA, TASAF III, Programu jumuishi ya taifa ya lishe na Kamati za Elimu. Shughuli imepangwa kukamilika mapema 2022.

Shughuli 1.2.1.2: Kutoa mafunzo ya awali kwa wajumbe wa kamati wa sekta mbalimbali kuhusu masuala ya MMMAM na uratibu katika ngazi ya taifa (Kamati elekezi na kamati tendaji, Vikundi kazi vya Afya, lishe, ulinzi na usalama wa mtoto, ujifunzaji wa awali na malezi yenye mwitikio)

Mkutano wa siku mbili wa utoaji elimu kwa kamati ya taifa na wajumbe wa kikosi kazi juu ya kuingizwa kwa vipengele vya Malezi Jumuishi katika miongozo iliyopo ambayo ni MTAKUWWA, Programu jumuishi ya taifa ya lishe, TASAF III, kamati za afya na elimu. Mchakato wa utoaji elimu utahusisha kuwaelimisha washiriki juu ya masuala husika ya MMMAM kama vile Sayansi ya MMMAM, Mfumo wa Malezi Jumuishi na vifurushi vingine vya mafunzo ya MMMAM, uhusiano wa programu na majukumu. WAMJJW & OWM-SUBKVAU zitafanya kazi na idara za serikali zinazohusika, wadau wa maendeleo, wadau wanaotekeleza maendeleo na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwezesha shughuli hii ambayo imepangwa kufanyika mnamo mwaka 2022.

Shughuli 1.2.1.3: Kutoa mafunzo ya awali kwa wajumbe wa vikundi kazi vya Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM kuhusu Programu, majukumu na wajibu wao

Kutoa mafunzo kwa wajumbe wa kitaifa wa kikosi kazi juu ya maswala ya MMMAM-Malezi Jumuishi na uratibu. Mafunzo yatatolewa kwa ushirikiano wa WAMJW, OR-TAMISEMI na TECDEN. Kikundi hicho kinajumuisha wadau wa MMMAM pamoja na MDAs zinazohusika, wadau wa maendeleo na wadau wa utekelezaji. Mafunzo ya siku mbili yatazingatia kuhakiki njia zinazotumika kufanya uratibu wa Programu Jumuishi ya MMMAM (kwa serikali na asasi za kiraia) pamoja na majukumu yao.

Shughuli 1.2.1.4: Kutoa mafunzo ya awali kuhusu Programu Jumuishi ya Taifa ya MMAM kwa wawezeshaji 20 kwa kwa kila mkoa katika mikoa 26 Tanzania Bara

Kikundi kazi cha Programu Jumuishi ya taifa ya MMMAM kitafanya mkutano wa kutoa mafunzo kwa wawezeshaji 20 kwa kila mkoa katika mikoa 26 kwa siku 3. Wawezeshaji waliopatiwa mafunzo watatoa maarifa kwa wawezeshaji watano katika ngazi ya Halmashauri na kufuatiwa na ngazi ya Kata na Kijiji / Mtaa. Mchakato wa utoaji mafunzo umepangwa kufanyika katika kipindi cha mwaka 2021 - 2022.

## Matokeo ya papo kwa papo 1.2.2: Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM imefanyiwa mapitio

Shughuli 1.2.2.1: Kufanya kongamano la MMMAM kila baada ya miaka 2

Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na WAMJW wataandaa jukwaa la siku 3 la Kitaifa la masuala ya MMMAM kila baada ya miaka miwili. Jukwaa hili litahusisha mawaziri kutoka sekta mbalimbali zinazotekeleza Programu jumuishi ya kitaifa ya MMMAM, makatibu wakuu, wakurugenzi, wadau wa maendeleo, wadau watekelezaji na wadau wengine wa kitaifa na kimataifa ili kubadilishana uzoefu juu ya utekelezaji wa Programu jumuishi ya Kitaifa ya MMMAM la siku moja mara moja kila mwaka. Jukwaa hili litahusisha Makatibu wakuu, Wakurugenzi, wadau wa maendeleo na wadau watekelezaji kutoka sekta mbalimbali zinazotekeleza programu na litaongozwa na Waziri Mkuu

Shughuli 1.2.2.2 Kufanya mikutano ya pamoja ya mwaka ya sekta mbalimbali ya mapitio ya programu ya MMMAM

Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na WAMJW wataandaa mkutano wa siku moja wa mwaka kufanya mapitio ya shughuli za MMMAM nchini. Mkutano huu utashirikisha wizara zote zinazotoa huduma za MMMAM, wadau wa maendeleo, wadau watekelezaji kutoka sekta mbalimbali zinazotekeleza programu, na kikao kitaongozwa na ofisi ya Waziri mkuu.

Shughuli 1.2.2.3 Kufanya Mkutano wa mwaka wa viongozi wa ngazi ya juu

Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na WAMJW wataandaa mkutano wa Taifa wa MMMAM

wa siku moja kila mwaka. Mkutano huu utahusisha makatibu wakuu na wakurugenzi wa wizara zote zinatotoa huduma za MMMAM, wadau wa maendeleo na wadau watekelezaji kutoka sekta mbalimbali zinazotekeleza programu. Kikao kitaongozwa na ofisi ya Waziri Mkuu.

Shughuli 1.2.2.4: Kufanya mikutano ya kitaifa ya robo mwaka ya vikundi kazi vya watalaam wa MMMAM

WAMJW itaandaa kikao cha kikundi kazi cha Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM kila robo mwaka ili kujadili maendeleo yaliyopatikana katika utekelezaji wa afua za MMMAM. Vikao hivi vitaongozwa na WAMJW na TECDEN. Vikao hivyo vitafanyika kwa siku 2 vikihusisha maafisa wa serikali kutoka wizara husika na wadau wa utekelezaji. Pia vikao hivi vitaratibiwa na Sekretarieti ya kitaifa ya MMMAM.

Shughuli 1.2.2.5: Kufanya mikutano ya robo mwaka ya mkoa ya mapitio ya Programu Jumuishi Taifa ya MMMAM

MMMAM katika ngazi ya Mkoa itatekelezwa kupitia sekta mbali mbali inayohitaji uratibu jumuishi. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) itakuwa na jukumu la kuratibu mikutano mbalimbali ya kisekta ya MMMAM.

Mikutano ya mapitio inayofanyika kila robo mwaka katika ngazi ya Mikoa katika sekta mbalimbali haijaingiza vipengele vya malezi yenye mwitikio na fursa ya ujifunzaji wa awali. Masuala ya Malezi jumuishi yatajumuishwa katika mikutano inayofanyika katika ngazi ya Mikoa. Mkutano huo utajadili taarifa za maendeleo ya utekelezaji wa Programu katika ngazi ya Wilaya / Halmashauri na kupendekeza kwa kamati ya juu ya MMMAM juu ya hatua zinazofaa za ufuatiliaji. OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau wa mikoa wa MMMAM watatoa fursa ya ujumuishaji wa masuala ya MMMAM katika vikao vyao na kufanya hadidu rejea ifikapo mwaka 2022 ili kuhakikisha vipengele hivi muhimu vya Malezi Jumuishi vimejumuishwa katika mikutano ya mapitio ya kila mwaka.

Shughuli 1.2.2.6: Kufanya mikutano ya robo mwaka ya mapitio ya programu ya MMMAM katika ngazi ya Halmashauri kwa ajili ya kushirikisha na kutoa mapendekezo ya taarifa ya utekelezaji wa MMMAM kutoka katika ngazi ya Kata na Vijiji/ Mtaa

Mikutano ya upitiaji wa programu ya MMMAM katika ngazi ya Wilaya huzingatia zaidi sekta maalum ambapo masuala ya malezi yenye mwitikio na fursa ya ujifunzaji wa awali hayashughulikiwi. Wakati wa mikutano hii taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa MMMAM kutoka katika ngazi ya Kata na Kijiji/Mtaa zitatolewa katika ngazi Halmashauri na hatua zinazofaa za ufuatiliaji. Uhamasishaji utafanywa ili kuhakikisha ujumuishaji wa masuala ya malezi yenye mwitikio na fursa za ujifunzaji wa awali kwa mfano katika siku ya afya na lishe vijijini (COMPACT). OR-TAMISEMI itahakikisha mikutano ya mikoa na halmashauri Inajumuisha maswala ya MMMAM na kutengeneza Hadidu za Rejea (TOR) ifikapo mwaka 2022 ili kuhakikisha kuwa vipengele hivi muhimu vya MMMAM vimejumuishwa katika mikutano ya robo mwaka katika ngazi ya Wilaya/Halmashauri .

## Matokeo ya muda mfupi 1.3; Sera, Miongozo, Mitaala na vitini vya kufundishia zimeandaliwa/ kufanyiwa mapitio ili kuingiza vipengele vyote vya malezi jumuishi

Matokeo ya papo kwa papo 1.3.1: Sera zinazohusiana na MMMAM zimefanyiwa mapitio na kupitishwa

Shughuli 1.3.1.1: Kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 ili kujumuisha masuala ya malezi jumuishi

WAMJW itafanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wadau wa utekelezaji, Idara za serikali na uongozi wa serikali za mitaa ili kupitia Sera ya sasa ya Maendeleo ya Mtoto ili kuingiza masuala yanayohusu na MMMAM. Hivi sasa WAMJW imeanza kufanya

tathmini ya sera ambayo itasaidia mchakato huo. Mchakato wa upitiaji wa sera utamhusisha mtaalamu elekezi na kufanya mikutano ya wadau. Sera ya Maendeleo ya Mtoto imepangwa kukamilika ifikapo 2025.

Shughuli 1.3.1.2: Kusambaza Sera ya Afya iliyofanyiwa mapitio

WAMJW ipo katika mchakato wa kukamilisha mchakato wa mapitio ya sera ya Afya. Sera iliyoboreshwa inatarajiwa kusambazwa kwa wadau kwa kupitia jukwaa hili.

Shughuli 1.3.1.3: Kufanya mapitio ya Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ili kuingiza masuala ya malezi jumuishi

Mapitio ya sheria ya Mtoto yatakayofanywa na WAMJW yatahusisha wahusika wakuu pamoja na OR-TAMISEMI, WEST, Wizara ya Katiba na Sheria (MoCLA), OWM-SUBKVAU, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (MICAS) na Watendaji. Utaratibu huu utahusisha mtaalamu elekezi ili kutoa msaada wa kitaalam na pia kufanya angalau mikutano miwili ya wadau kwa kupata ushauri, idhini na kuzindua Sheria ya mtoto. Mpango ni kuhakikisha kwamba Sheria ya sasa ya Mtoto ya mwaka 2009 imepitiwa ifikapo mwaka 2024.

Matokeo ya Papo kwa papo 1.3.2: Miongozo imefanyiwa mapitio/imeandaliwa

Shughuli 1.3.2.1: Kufanya mapitio na kuoanisha miongozo iliyopo (kutoka Hudama ya Baba, Mama na Mtoto, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Jamii, Elimu na Serikali za Mitaa) kwa ajili ya kufanya usimamizi zaidi wa pamoja ili kuingiza masuala ya malezi jumuishi

Miongozo iliyopo ya usimamizi wa programu za pamoja haishughulikii vipengele vya malezi jumuishi, WAMJW imepanga kupitia miongozo hiyo na kujumuisha maswala ya MMMAM ili kuongeza rasilimali na kuwezesha uratibu na uwajibikaji katika ngazi zote. WAMJW inafanya kazi pamoja na wizara za kisekta (kutoka RCH, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Jamii, elimu na serikali za mitaa) na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali yanapanga kufanya angalau kikao kazi cha siku sita ili kukagua miongozo iliyopo. Mchakato huo unatarajiwa kukamilika ifikapo 2022.

Shughuli 1.3.2.2: Kufanya vikao vya mapitio ya mwongozo wa walezi wa watoto wadogo ili kuingiza maudhui maalum ya watoto wa kuanzia miaka 0-2.

WAMJW itafanya kazi na wadau wa maendeleo, wadau watekelezaji, MDAs na LGAs kuingiza masuala maalumu yanayohusu watoto wenye umri wa miaka 0 - 2 katika mwongozo wa walezi wa watoto. Mapitio hayo yatajumuisha mambo anayopitia mtoto kutoka nyumbani, hadi kituo cha malezi ya watoto na darasa la awali, mambo ya maji, na usafi wa mazingira (WASH).

Hivi sasa kupitia MTAKUWWA juhudi mapitio ya mwongozo uliopo zimefanyika. Mpango ni kufanya angalau mikutano sita ya upitiaji kwa kushirikiana na wadau waliotajwa, kuchapisha nakala 1000 ya miongozo hiyo na kusambaza. Miongozo imepangwa kupitiwa upya mwaka 2021 na kusambazwa mwaka 2022.

Shughuli 1.3.2.3: Kukamilisha rasimu ya Mwongozo wa Taifa wa utekelezaji wa Malezi kwa Makuzi na Maendeleo ya Mtoto

Mwongozo upo katika rasimu na unajumuisha vipengele vyote vya malezi jumuishi na kujumuisha mahitaji ya watoto wote pamoja na wale walio na utapiamlo, ucheleweshwaji wa ukuaji, watoto wagonjwa, jinsia, walio na maambukizi ya VVU + au, watoto waliofanyiwa ukatili, na watoto wenye shida ya akili utakamilishwa na WAMJW kwa kushirikiana na wadau wengine. Kukamilisha kutahusisha mkutano wa wadau wa kupitia mwongozo huo, mkutano wa kiufundi ili kufanya maboresho na mkutano wa menejimenti (Wakurugenzi).

Matokeo ya Papo kwa papo 1.3.3: Mitaala/Miongozo imepitiwa

Shughuli 1.3.3.1: Kuandaa Mtaala wa MMMAM wa kitaifa unaozingatia utamaduni na mahitaji ya ukuaji wa watoto kwa walezi wa watoto wadogo (Astashahada na Stashahada kulingana na viwango vya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi ngazi 4-6)

Hivi sasa kuna programu za MMMAM katika taasisi za utoaji elimu kwa walezi wa watoto hapa nchini, hata hivyo bila kuwa na mtaala unaofaa na ulioidhinishwa na Baraza la Kitaifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) katika kiwango cha cheti na diploma. Kuna tathmini inayoendelea katika taasisi 21 zinazojihusisha na masuala ya malezi kwa watoto ili kupata taarifa ya mchakato wa uundaji wa programu hii. WAMJW itafanya kazi na wadau wa maendeleo, NACTE, WEST, OR-TAMISEMI, wadau watekelezaji, Halmashauri na Serikali za Mitaa. Watafanya vikao kazi angalau sita ili kukubaliana umri wa kitaifa na kujumuisha watoto wote (utashughulikia mahitaji kibinafsi ya watoto pamoja na wale walio na utapiamlo, watoto wenye ulemavu, uchelewaji wa ukuaji, watoto wagonjwa, jinsia, watoto wenye maambukizi ya VVU, wanaonyanyaswa) wenye umri wa miaka 0-8. Kwa ngazi ya cheti na diploma kufikia kiwango cha NACTE cha NTA level 4-6. Hii itafuatiwa na usambazaji wa nakala za mtaala wa Kitaifa wa MMMAM katika kanda sita. Shughuli hii imepangwa kukamilika ifikapo 2022.

Shughuli 1.3.3.2: Kuandaa mkoba wa mafunzo Jumuishi ya MMMAM ili kuongeza vipengele vya Malezi Jumuishi

Ili kupata mkoba kamili wa mafunzo ya MMMAM, WAMJW kwa kushirikiana na WEST, OR- TAMISEMI, TET, OWM-SUBKVAU, TFNC, NACP, TACAIDS, Wadau wa Maendeleo, wadau watekelezaji watafanya warsha ya ya siku 21 kwa waandishi kukagua, kuboresha, kuthibitisha, kufanya mapitio ya mwisho ya mkoba wa mafunzo wa Malezi Jumuishi ambacho kinajumuisha mwongozo wa mafunzo, mwongozo wa washiriki na chati pindu. Timu ya uandishi itatumia mikoba mafunzo kutoka kwenye programu za kitaifa ikiwa ni pamoja na MTAKUWWA, msaada wa kisaikolojia kwa wahanga wa ukatili, Programu Jumuishi ya taifa ya lishe, Afya ya Familia, mkoba wa Malezi kwa Makuzi, mkoba wa watoa huduma za afya katika jamii (WAJA) na mikoba mingine ya kutoa mafunzo ya ujifunzaji wa awali na malezi yenye mwitikio yanayopatikana nchini ambayo yanatumiwa katika miradi mbalimbali. Mwongozo kamili wa mafunzo utahusisha vipengele vya malezi jumuishi ikiwa ni pamoja na Afya, Lishe, malezi yenye mwitikio, ulinzi na Usalama (pamoja na Usajili wa Kuzaliwa, usafi wa mazingira na maji salam (WASH), hifadhi ya Jamii-TASAF), fursa za ujifunzaji wa awali) na moduli ya afya ya akili kwa ngazi ya kituo na jamii. Watoa huduma watashughulikia (mahitaji ya kibinafsi ya watoto pamoja na wale walio na utapiamlo, ulemavu, uchelewaji wa ukuaji, watoto wagonjwa, jinsia, wenye maambukizi ya VVU, wanaonyanyaswa, afya ya akili kwa wazazi). Mchakato wa kuunganisha mkoba ya utoaji elimu ya malezi jumuishi utafanyika mapema 2022 nchini nzima. Mkoba huu utalenga wafanyakazi wanaolea watoto wenye umri wa miaka 0 - 8 pamoja na walimu wa elimu ya awali, wafanyakazi wa huduma ya watoto, wauguzi, madaktari, maafisa ustawi wa jamii, maafisa maendeleo ya jamii, wataalam wa lishe, ulinzi wa watoto, watoa huduma za afya katika jamii (WAJA) na kamati zilizopo. Mkoba wa mafunzo utakua ukiboreshwa kulingana na mahitaji na sifa ya mtoa huduma husika.

## *MATOKEO YA MUDA MREFU 2: Mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora imeimarishwa*

### Matokeo ya muda mfupi 2.1: Uwepo wa watoa huduma wenye ujuzi na umahiri kwenye malezi jumuishi

Matokeo ya Papo kwa Papo 2.1.1 Timu ya wakufunzi wa MMMAM wa kitaifa (Wakufunzi wa Kuu) imeundwa

Shughuli 2.1.1.1: Kufanya mafunzo ya kitaifa ya mkoba Jumushi wa MMMAM (Malezi Jumuishi) kwa timu ya wakufunzi ya uendeshaji katika ngazi ya taifa (Mfunzo ya Wakufunzi Wakuu)

Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia (Idara ya Elimu ya Msingi), OR - TAMISEMI, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), taasisi ya chakula na lishe, Afya na huduma ya Afya ya Uzazi (WAMJW), wadau wa maendeleo, wadau watekelezaji wa mradi watahusika kutoa mafunzo kwa Wakufunzi wakuu wa masuala ya MMMAM nchini kutoka sekta zote nchini kwa kipindi cha miaka mitano. WAMJW kupitia Idara ya Maendeleo itakaa kuandaa orodha ya wakufunzi wakuu wa MMMAM waliopo kwenye sekta mbalimbali kuhusiana vipengele vya lishe, ulinzi wa mtoto, malezi kwa makuzi kwa maendeleo ya mtoto ili kupata idadi kamili ya wakufunzi wakuu waliopo, kisha kufuatiwa na Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Wizara ya WEST (Idara ya Elimu ya Msingi), OR-TAMISEMI, TET, Taasisi ya chakula na lishe,  Kitengo cha huduma ya Afya ya Uzazi (WAMJW),  wadau wa maendeleo, wadau watekelezaji wa programu ambao watatoa mafunzo kwa wakufunzi wakuu  kwa kutumia mkoba wa mafunzo wa elimu jumuishi  ya MMMAM. Wakufunzi hao baada ya kupatiwa mafunzo watatakiwa kutoa mafunzo kwa wakufunzi katika ngazi ya mikoa na kusimamia mafunzo yatakayotolewa katika ngazi ya Halmashauri. Mafunzo ya wakufunzi wakuu yatafanyika mwishoni mwa mwaka 2022 ili kuweza kusaidia kutoa mafunzo kwenye mikoa yote 26. Wakufunzi hawa kwenye ngazi za mikoa wataendelea kuwajengea uwezo na kusimamia utekelezaji kwenye Halmashauri zao.

Shughuli 2.1.1.2: Kufanya vikao vya mafunzo kuhusu mkoba jumuishi wa Kitaifa wa MMMAM kwa wakufunzi katika ngazi ya Mkoa (Mafunzo kwa Wakufunzi Wakuu)

Ili kuifikia nchi nzima, itatakiwa kuwa na Wakufunzi katika ngazi ya Mikoa kusaidia kutoa mafunzo kwenye ngazi ya Wilaya. Katika kila mkoa kutakua na Wakufunzi 5 hivyo kuwa na jumla ya wakufunzi 130 ambao watapatiwa mafunzo ya elimu jumuishi ya MMMAM na wakufunzi wakuu wa kitaifa kwa siku tano. Wakufunzi hawa kwenye ngazi za Mikoa watatakiwa kutoa mafunzo kwenye ngazi za Halmashauri; na kuwajengea uwezo na kusimamia utekeleza kwenye Halmashauri zao. Mafunzo yanatarajia kufikia mikoa yote 26 ya Tanzania bara hadi kufikia 2025.  WEST Idara ya Elimu ya Msingi, OR-TAMISEMI, TET, taasisi ya taifa ya lishe, Kitengo cha huduma ya Afya ya Uzazi (WAMJW), wadau wa maendeleo, wadau watekelezaji wa mradi watasaidia utekelezaji wa mafunzo hayo katika ngazi ya Mkoa..

Shughuli 2.1.1.3: Kufanya vikao vya mafunzo ya ngazi kwa ngazi kuhusu Mkoba Jumuishi wa Kitaifa wa MMMAM kwa wakufunzi katika ngazi ya Halmashauri

Lengo la kutoa mafunzo ni kupata wakufunzi katika ngazi za Halmashauri ambao wana uwezo wa kutumia mkoba wa mafunzo ya elimu jumuishi ya MMMAM. Kwa misingi hiyo, wakufunzi 5 kutoka katika Hamashauri 184 watachaguliwa na kupatiwa mafunzo kwa siku 5 hivyo kufanya jumla ya wakufunzi 920 kufundishwa kwenye Halmashauri zote Mafunzo haya yatatolewa na wakufunzi katika ngazi ya mkoa kwa msaada kutoka kwa wakufunzi ngazi ya taifa. Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wana wajibu wa kuhakikisha mafunzo yamefanyika katika halmashauri zote 184 mpaka kufikia mwaka 2025.

Matokeo ya papo kwa papo 2.1.2:  Uwezo wa walimu wa elimu ya Awali na walezi wa watoto wadogo kuhusu MMMAM kuimarishwa

Shughuli 2.1.2.1: Kufanya mapitio ya programu ya mwendelezo wa maendeleo ya taaluma ya walimu wa elimu ya Awali

Ili watoto waweze kujifunza kikamilifu wanahitaji idadi ya kutosha ya walimu wa shule ya Awali waliopatiwa mafunzo ya MMMAM katika uwiano ambao unaruhuru walimu kuwashirikisha ipavyo watoto ili kuhamasisha kujifunza. Kwa sasa uwiano wa waalimu na watoto darasani ni 1:129 (WEST 2018) tofauti na uwiano unatakiwa wa 1:25. Uwiano huu mkubwa wa watoto tofauti na idadi ya waalimu unasababisha matokeo hasi ya ujifunzaji kwa sababu wanafunzi hawawezi kucheza na kujifunza kwa urahisi.  Ili kuhakikisha kwamba walimu wenye sifa wanakuwepo, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia na  Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Vyuo vya Ualimu, wadau wa maendeleo wadau watekelezaji wa programu ya MMMAM watafanya kazi na vyuo vikuu kufanya mapitio ya programu ya  mafunzo endelevu ya kitaaluma ambayo tayari iliandaliwa na Taasisi ya Elimu Tanzania. Mapitio hayo

yanahusu kuboresha programu hiyo ya mafunzo na kuhakikisha masuala ya elimu ya Awali yanazingatiwa. Tayari kuna mwongozo wa taifa wa mafunzo endelevu ya kitaaluma ambao unaelekeza namna gani mafunzo kazini yafanyike pamoja na mafunzo endelevu ya kitaaluma. Katika mapitio ya mwongozo huu nyongeza ya mkoba wa elimu ya Awali utaongezwa na kutekelezwa. Zoezi hili litahitajI mtaalamu wa kulipwa atakaye fanya warsha kwa siku 5 na washiriki wapatao 20 ili kufanya mapitio ya rasimu ya mwongozo na kufanya warsha ya siku 3 kufanya mapitio na kuandaa rasimu ya mwisho ya mwongozo huo. Mapitio ya mwongozo wa mafunzo endelevu ya kitaaluma utatoa fursa ya kutambua program nyingine zilizopo pamoja na Programu ya kusaidia walimu (programu ilioandaliwa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi ya Elimu Tanzania). (MoEST & TIE). Mapitio ya mwongozo wa mafunzo endelevu ya kitaaluma yanatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2022.

Shughuli 2.1.2.2: Kufanya mafunzo kazini kwa wakufunzi katika vyuo vya ualimu, vyuo vya elimu ya walezi wa watoto wadogo, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na vyuo vikuu kuhusu MMMAM

Ili kuhakikisha kunakuwepo uelewa na muendelezo wa utekelezaji wa masuala ya MMMAM na huduma za malezi jumuishi, Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto watatoa mafunzo kwa wakufunzi 85 kwa siku 10 (kutoka vyuo vya elimu, vyuo vya mafunzo vya malezi ya watoto, vyuo vya maendeleo ya wananchi na vyuo vikuu). Mafunzo yatatolewa na wakufunzi wakuu kwa kutumia mkoba wa taifa MMMAM. Mafunzo haya yamepangwa kukamilika katika robo ya mwaka 2022.

Shughuli 2.1.2.3: Kuwezesha kuajiri/kuwapangia vituo maafisa wa kujitolea na kuwapa fursa wanaojifunza kazi kwa vitendo kutoka kwenye vyuo vikuu na vyuo vya ualimu kusaidia kutoa elimu ya awali na madarasa ya mwanzo ya shule ya msingi ( darasa la Kwanza mpaka la Tatu)

Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia , Wazee na watoto Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na vyuo vya elimu husika, vyuo vikuu, wadau mbalimbali wa maendeleo, wadau watekelezaji wa program ya MMMAM wataajiri maafisa wa kujitolea ambao majina yao yatabandikwa kwenye halmashauri zao kila mwaka ili kushiriki kwenye program ya kujifunza kwa vitendo kwenye elimu Awali na darasa la II - III, Programu hii itatoa fedha za kujikimu kwa mwezi kwa kila mwalimu anayejitolea ili kumudu maisha katika kipindi cha kujitolea. Mpango wa awali ni kuajiri walimu wa kujitolea na wanaojifunza kazi kwa vitendo 368 kwa mwaka (2 kwa Halmashauri 184 kwa mwaka). Programu hii imepangwa kuanza mwaka wa kwanza wa program (2022).

Matokeo ya Papo kwa papo 2.1.3: Uwezo wa watoa huduma za moja kwa moja kwa walengwa kutumia Mkoba Jumuishi wa MMMAM umeimarishwa.

Shughuli 2.1.3.1: Kutoa mafunzo kwa kutumia Mkoba Jumuishi wa MMMAM

Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wa MMMAM wamepanga kufanya mafunzo ya siku 14 kwa maafisa afya wa jamii, walezi wa watoto wadogo, wafanyakazi wa afya, walimu wa shule ya Awali, na walimu wa darasa la Kwanza, Pili na la Tatu, dawati la polisi la jinsia na watoto, timu nzima ya ulinzi wa mtoto na wasaidizi wa kisheria . Jumla ya washiriki 30 watafikiwa kwa Halmashauri kwa mwaka. Mafunzo yatatolewa na wakufunzi katika ngazi ya Halmashauri wakisimamiwa na wakufunzi wa ngazi ya mkoa kwenye halmashauri zote 184. Shughuli hii itamaliza mwaka 2022.

Shughuli 2.1.3.2: Kutoa mafunzo katika ngazi ya Halmashauri kuhusu unasihi wa afya ya akili na kisaikolojia na kutoa msaada kwa waliofanyiwa ukatili

Kupitia juhudi za MTAKUWWA, kuna wataalamu 423 katika Halmashauri 27 (Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Wauguzi/Madaktari na Walimu) waliofunzwa unasihi wa akili na kisaikolojia kusaidia waathirika wa ukatili. Pia kuna jumla ya wanachama 540 wa Kamati za Ulinzi wa Mama na Mtoto (WCPC) waliofunzwa katika Halmashauri 27 na waliofunzwa unasihi wa akili na kisaikolojia kusaidia waathirika wa ukatili. WEST na WAMJW kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, MICAS, Wadau wa Maendeleo, wadau wa Utekelezaji na AZAKI watatoa mafunzo kwa Wanasihi 2,512 wa ziada (wanasihi 16 kwa kila Halmashauri 157 zilizobaki). Mafunzo hayo kutoka ngazi ya baraza WCPC yatatolewa kwa WCPC ngazi ya Kata kuhusu unasihi ili kuongeza ufikiaji wa huduma za ushauri wa kitaalam kwa wanyanyasaji wa kila kata. Mafunzo hayo yanaendelea kutekelezwa katika MTAKUWWA na haihitaji bajeti.

Shughuli 2.1.3.3: Kutoa mafunzo katika ngazi ya kata kuhusu unasihi wa afya ya akili na kisaikolojia na kutoa msaada kwa waliofanyiwa ukatili nchi nzima

Hakuna wataalamu waliofunzwa juu ya unasihi wa akili na kisaikolojia katika ngazi ya Kata. Kwa hivyo jumla ya Kata 3956 zitapewa mafunzo. Wajumbe wa kamati za ulinzi wa mama na watoto watapewa mafunzo katika Kata hizo.

Shughuli 2.1.3.4: Kutoa mfunzo kwa watoa huduma wa afya kuhusu kijitabu cha ufuatiliaji na maendeleo ya mtoto kilichounganishwa na mkoba wa malezi kwa makuzi na maendeleo ya mtoto

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia kitengo cha Afya ya uzazi wa mama na mtoto itashirikiana na OR-TAMISEMI, Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania, Wadau wa Maendeleo na Wadau wanaotekeleza Mpango-MMMAM (AZAKI) kutoa mafunzo kwa Watoa Huduma za afya kuhusu matumizi ya Kitabu kipya cha ufuatiliaji wa ukuaji na maendeleo ya mtoto, na kitita cha mafunzo ya malezi na maendeleo ya mtoto, pamoja na kitabu cha lugha ya nukta nundu. Shughuli hii itafanyika kwa kuwatambua wawezeshaji 10 wa ngazi ya halmashauri watakao husika kutoa mafunzo/kufanya usimamizi shirikishi katika kila Halmashauri, kusambaza nakala 1,840 za kitabu cha afya na maendeleo ya mtoto kilichoandikwa kwa kutumia nukta nundu na kutoa mafunzo ya jinsi ya kukitumia kwa watoa huduma za afya kwenye vituo 12,319 vya kutolea huduma za afya katika Halmashauri. Mafunzo ya awali yatafanyika kwa mbinu mbalimbali ikiwemo mafunzo kazini yatakayochukua muda wa siku moja (1) katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya. Jumla ya watoa huduma za afya 24,638 watapewa mafunzo katika Mikoa 26 ambapo kila kituo cha huduma za afya kitatoa washiriki wawili (2). Kazi ya kufundisha itafanywa na wakufunzi 26 wa ngazi ya taifa, na wakufunzi 26 wa ngazi ya mkoa. Hivi sasa, mikoa ya Songwe, Iringa, Mbeya na Njombe tayari imepatiwa mafunzo ya matumizi ya kitabu kipya cha ufuatiliaji wa ukuaji na maendeleo ya mtoto.

Shughuli 2.1.3.5: Kuimarisha malezi yenye mwitikio, ujifunzaji wa awali na vipengele vya huduma za maji safi na mazingira kwa kutumia mkoba uliofanyiwa mapitio wa watoa huduma za afya katika ngazi ya jamii

Malezi yenye mwitikio, fursa za ujifunzanji awali, maji na usafi wa mazingira ni vipengele muhimu katika maendeleo ya mtoto. Ili kuhakikisha kwamba watoa huduma za afya katika ngazi ya Jamii wanatoa huduma kamilifu za malezi jumuishi, Kitita cha huduma za afya ya wanawake, Watoto wenye umri wa siku 0-28 na watoto wenye umri wa miezi 0-59 kitapitiwa na kuboreshwa, Mapitio ya kitita hicho yatafanywa kupitia warsha ya siku mbili ya wataalamu ili kuingiza masuala mbalimbali ya MMMAM. Warsha hizo zitajumuisha wataalamu 20.

Programu Jumuishi ya MMMAM itawatambua wawezeshaji/wasimamizi wakuu 10 kwa kila Halmashauri ambao watafanyiwa mafunzo kuhusu matumizi ya kitita kilichoboreshwa. Wawezeshaji hao watatoa mafunzo ya awali kwa watoa huduma za afya wawili kutoka kila kituo cha kutolea huduma ya afya kilichopo katika Halmashauri husika. Watoa huduma hao watawajibika kuwafundisha watoa huduma za Afya katika ngazi ya jamii waliopo kwenye vijiji/maeneo yao ya kazi kwa muda wa siku tatu. Hii itasaidia kuhamasisha huduma za malezi yenye mwitikio, ujifunzaji wa mapema, maji na usafi wa mazingira katika ngazi ya jamii.

Matokeo ya Papo kwa papo 2.1.4: Mkoba jumuishi wa mafunzo ya MMMAM kwa wanafunzi waliopo vyuoni umeandaliwa

Shughuli 2.1.4.1: Kuandaa programu ya mtandao wa Elimu masafa kuhusu MMMAM kwa walezi wa watoto wadogo na vyuo vya ualimu vya Elimu ya Awali

Ili mafunzo ya MMMAM kwa walezi wa watoto na walimu wa elimu ya Awali yaweze kutolewa kwenye taasisi nyingi, Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Elimu, Sayansi na teknolojia watashirikiana na Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania, Wadau wa Maendeleo, Wadau wanaotekeleza programu, walimu wa elimu ya Awali, vyuo vya ualimu na vyuo vya walezi wa watoto kuandaa programu ya mafunzo ya MMMAM kwa njia ya mtandao. Mchakato huo utahusisha manunuzi ya vifaa vya kompyuta zenye uwezo wa kuhifadhi data, kompyuta mpakato, mashine za uchapishaji nyaraka; na kuajiri mtaalamu mshauri atakayetoa huduma za kitaalamu na kusaidia uanzishaji wa programu ya mafunzo kwa njia ya mtandao. Wataalamu wengine watakaoajiriwa ni pamoja na mtaalamu wa ubunifu wa michoro, na wapiga picha. Pia mtandao utakaotumika kuwezesha mafunzo utasajiliwa katika Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Warsha mbalimbali zitafanyika ili kurekodi na kuhariri vipindi vya mihadhara ya mada mbalimbali za mafunzo. Jumla ya wakufunzi 15 watahitajika. Shughuli hii eimepangwa kukamilika ifikapo mwaka 2022.

Shughuli 2.1.4.2: Kutoa mafunzo ya awali kwa walimu wa elimu ya Awali na madarasa ya mwanzo ya shule za msingi (darasa la kwanza mpaka la tatu) kuhusu mtaala uliofanyiwa mapitio wa elimu ya Awali ambao umejumuisha vipengele vya MMMAM

Mtaala utakaofanyiwa mapitio na kujumuisha masuala ya MMMAM utatumiwa kufanya mafunzo ya awali kwa walimu 50,806. Kila shule itatoa walimu 3 watakaoshiriki mafunzo. Mafunzo yatafikia shule zote 16,401 za msingi katika halmashauri zote nchini. Shughuli hii itakamilika mwaka 2023.

Shughuli 2.1.4.3: Kutoa mafunzo ya awali kwa kamati za usajili wa vizazi katika mikoa 8

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto itashirikiana na wadau wakiwemo OR-TAMISEMI na Msajili wa Vizazi na Vifo, watatoa mafunzo ya awali kwa mikoa 8 yanayohusu mchakato wa usajili wa vizazi na kuwapatia watoto vyeti vya kuzaliwa kwa kuzingatia Kanuni za Usajili wa Vizazi na Vifo. Shirika la kuhudimia Watoto Duniani (UNICEF) imesaidia kifedha Mikoa 18 ((Lindi, Mtwara, Iringa, Mbeya, Shinyanga, Mara, Njombe, Simiyu, Geita, Songwe, Dodoma, Singida, Morogoro, Pwani, Ruvuma, Kilimanjaro, Tanga, Manyara, na Arusha); Mikoa 8 iliyobakia itapewa msaada kupitia utoaji wa mafunzo ya awali kwa timu ya watu watakaohusika na usajili wa vizazi kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Timu hizo zitakuwa na watu kumi (10) ambao ni Afisa Maendeleo ya jamii, Mratibu wa Wilaya wa Afya ya Uzazi na Mtoto, Afisa Ustawi wa jamii, Afisa Mipango, Mtaalamu wa Teknolojia ya Mawasiliano, Afisa manunuzi, Afisa Uhamiaji, Afisa Usalama, na Afisa wa Usajili wa Vizazi na Vifo kutoka ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Shughuli hii itafuatiwa na utoaji wa mafunzo kwa wasajili wasaidizi wa vizazi wanne (4) kutoka katika kila kituo cha kutolea huduma za afya. Mafunzo yatafanyika kwa siku nne na yatawezeshwa na maafisa wa Ofisi ya Msajili wa Vizazi na Vifo. Vifaa vinavyohitajika kufanikisha shughuli ya usajili wa vizazi ni pamoja na vifaa vya mawasiliano kwa njia ya mtandao na kompyuta ambavyo vitagawiwa kwa kila halmashauri; simu janja ambazo zitagawanywa kwa Wasajili Wasaidizi wa Vizazi na shajara (wino wa kufutia maandishi, kalamu na karatasi). Shughuli hii itakamilika mwaka 2022.

## Matokeo ya muda mfupi 2.2: Mifumo wa rufaa na mahusiano wa utoaji huduma ya malezi jumuishi umeimarishwa

### Matokeo ya papo kwa papo 2.2.1: Mifumo wa kutoa rufaa wa kesi za ukatili dhidi ya watoto imeimarishwa

Shughuli 2.2.1.1: Kufanya mapitio ya mifumo ya ulinzi wa mtoto (Dawati la jinsia) na kuandaa mwongozo wa kijamii kwa ajili ya kumbukumbu, kutoa taarifa na mfumo wa rufaa wa unyanyasaji wa watoto na utelekezaji ambao unawafikia watoto kuanzia miaka 0-8

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Ofisi ya OWM-SUBKVAU, OR-TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na teknolojia, Wadau wa Maendeleo, AZAKi, na Wizara ya Mambo ya Ndani wataendesha warsha nne (4) zitakazohusisha wataalamu mbalimbali ili kupitia miongozo ya ulinzi na usalama wa mama na mtoto. Lengo ni kuhakikisha kwamba huduma rafiki za watoto wenye umri wa miaka 0 – 8 zinapatikana. Miongozo itakayofanyiwa mapitio itaingiza masuala ya njia za kuhifadhi, kutoa taarifa na mifumo ya rufaa kwa matukio ya ukatili na utelekezaji wa watoto. Hatua hii itafuatiwa na kufanyika kwa warsha ya mafunzo ya awali kwa wataalamu wanaoishi katika jamii (viongozi wa serikali za vijiji/mitaa, AZAKi, walimu na watoa huduma za afya katika jamii) pamoja na Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa wa Maendeleo ya Jamii na Maafisa wa Dawati la Jinsia kuhusu mwongozo wa huo. Shughuli hii itakamilika mwaka 2022.

Shughuli 2.2.1.2: Kutoa mafunzo ya awali kwa wataalamu wanaoishi katika jamii kuhusu mwongozo wa kijamii kwa ajili ya kumbukumbu, kutoa taarifa na mfumo wa rufaa wa unyanyasaji wa watoto na utelekezaji ambao unawafikiwa watoto wadogo kuanzia miaka 0-8

Mwongozo wa jamii kwa ajili ya kuhifadhi kutoa taarifa na rufaa za matukio ya ukatili dhidi ya watoto wenye umri wa miaka 0-8 utatoa mwongozo wa jinsi ya kutoa huduma jumuishi za malezi kwa familia na jamii. Warsha ya mafunzo ya awali kuhusu matumizi ya mwongozo huu ni jambo umuhimu. Programu jumuishi ya MMMAM itawezesha utoaji wa mafunzo ya awali kwa watu 3,956. Kila Kata itatoa mshiriki mmoja, ambapo jumla kuna Kata 3,956 nchini. Warsha hiyo itafanyika kwa muda wa siku moja katika Halmashauri zote nchini.

Shughuli 2.2.1.3: Kufanya utambuzi wa wadau wa MMMAM katika ngazi mbalimbali (Mkoa, Halmashauri na Kata) kwa ajili ya kuwezesha ufanisi wa mfumo wa rufaa na mahusiano

Uratibu wa huduma za MMMAM ni muhimu ili kuboresha utoaji wa huduma za malezi jumuishi. Hivyo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na OR-TAMISEMI itafanya kazi kwa ukaribu na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wadau wa Maendeleo na AZAKi wataendesha zoezi la kuwatambua wadau wa MMMAM nchini. Mchakato huo utahusisha ukusanyaji wa taarifa nchini utakaofanyika kwa siku 14; na warsha ya kuandaa zana za kukusanyia taarifa, uchambuzi wa taarifa zilizokusanywa, tafsiri ya takwimu zilizokusanywa na maandalizi ya zana za kukusanyia taarifa, kuandaa taarifa na warsha ya wadau ili kuthibitisha taarifa hiyo. Mchakato utazingatia uwepo wa zana zinazotumika kutambua wadau ambazo zimeandaliwa na kutumika wakati wa kufanya uchambuzi wa hali halisi ya MMMAM. Pia orodha ya wadau wa MMMAM itachapishwa na kusambazwa nchini kote. Zoezi la kuwatambua wadau linatarajiwa kukamilika mwaka 2021.

Shughuli 2.2.1.4: Kuwatambua na kuwafikishia huduma za malezi jumuishi wanufaika wote wa TASAF wenye watoto wa umri wa miaka 0-8

Uboreshaji wa hali ya kiuchumi na kijamii ya familia ni jambo muhimu ili kuendeleza taratibu sahihi za malezi. Kaya masikini hupata amani pale zinapokuwa na shughuli mbadala za kujipatia mahitaji ya msingi ya maisha kama vile, misaada kupitia mipango ya hifadhi ya jamii. Kupitia TASAF, watoto walio katika kaya masikini watapatiwa huduma ya uhawilishaji wa fedha wenye masharti nafuu ili kuwawezesha kupata huduma mbalimbali ikiwemo huduma za malezi jumuishi. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itafanya kazi kwa karibu na wadau wengine kuwatambua watoto waliosajiliwa kwenye Mpango wa Hifadhi ya Jamii unaotekelezwa na TASAF ili kuhakikisha kuwa kuna usawa katika upatikanaji wa huduma za malezi shirikishi kwa watoto wote ifikapo mwaka 2022.

Matokeo ya Papo kwa papo 2.2.2: Njia salama / rafiki za utoaji wa taarifa za ukatili dhidi ya watoto zimeongezwa

Shughuli 2.2.2.1: Kutoa mafunzo ya awali kwa walimu wa elimu ya Awali/ walezi wa watoto wadogo/ watoa huduma za afya wa kijamii kuhusu njia rafiki za utaoji wa taarifa za ukatili dhidi ya watoto na kuwateua kuwa wanasihi

Shughuli hii inatambua juhudi za MTAKUWWA katika kuwatambua na kutoa mafunzo ya unasihi kwa walimu wa shule (Eneo la 7: Shule salama na stadi za maisha). Shughuli hii itawalenga watoto wadogo, hivyo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itashirikiiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – SUBKVAU, OR-TAMISEMI, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na wadau wengine wa MMMAM ili kuanzisha Madawati ya kupokea taarifa za ukatili dhidi ya watoto shuleni. Madawati hayo yatawezesha pia utoaji wa huduma ya msaada wa kisaikolojia na rufaa. Pia yatasaidia kuwatambua na kuwapa mafunzo ya awali walimu wa malezi na wanafunzi watakaoongoza juhudi za kukabiliana na ukatili kwa watoto.

Mpango uliopo unalenga kuwafikiia walimu 36.302 wa elimu ya Awali kwa kuwapa mafunzo ya awali ya unasihi wa watoto. Idadi hii inatokana na mpango wa kuwapa mafunzo ya awali walimu wawili kwa kila shule iliyopo nchini ambapo shule zinazomilikiwa na sekta ya umma ni 16,401 na shule zinazomilikiwa na sekta binafsi ni 1,751. Wawezeshaji 920 wa ngazi ya Halmashauri watapatiwa mafunzo. Katika vijiji 12,319 nchini, angalau kila mlezi wa watoto mmoja na Watoa za Afya katika ngazi ya Jamii watapatiwa mafunzo ili waweze kusaidia watoto kwenye jamii zao. Inatarajiwa kwamba vijiji vyote 12,619 vitafikiwa na huduma hii ifikapo mwaka 2025.

Shughuli 2.2.2.2 Kuwatambua na kuwapa rufaa watoto wasio na vyeti vya kuzaliwa kwenda kwenye vituo vya usajili wa vizazi vilivyo karibu

Vituo vya MMMAM katika jamii, vituo vya malezi kwa watoto wenye umri wa miaka 0 -2, Kona za MMMAM zilizopo kwenye vituo vya afya, na huduma za kuwatembelea watoto kwenye kaya zitatumika kuwatambua watoto ambao hawana vyeti wa kuzaliwa. Baada ya kuwatambua, wazazi/walezi wa watoto hao watapewa rufaa ili waende katika vituo vya kutolea huduma za afya au ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata kupata huduma ya usajili wa watoto wao kwenye daftari la vizazi. Mtoa huduma za afya, mlezi wa watoto katika vituo vya malezi ya watoto wenye umri wa miaka 0 – 2, na wasimamizi wa vituo vya malezi ya watoto katika jamii na madarasa ya elimu ya Awali katika shule watakuwa na jukumu la kuwapa rufaa watoto ili wakapate huduma ya kusajiliwa kwenye daftari la vizazi. Watoa huduma hao watapata mafunzo kwa kutumia Kitita Jumuishi cha taifa cha MMMAM, na kuelekezwa kuhusu umuhimu wa watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano kusajiliwa na kupata cheti cha kuzaliwa. Shughuli hii itatekelezwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa Programu

## Matokeo ya Muda Mfupi 2.3: Uwepo wa mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji uliokubalika

Matokeo ya papo kwa papo 2.3.1: Mfumo wa ukusanyaji taarifa za MMMAM na kuboresha masuala jumuishi ya MMMAM katika ngazi za Wilaya umeimarishwa

Shughuli 2.3.1.1 Kufanya uchambuzi wa Mifumo iliyopo ya Usimamizi wa tarifa zinazohusiana na MMMAM na kutambua viashiria vilivyokosekana

WAMJW, WEST,OR- TAMISEMI na OWM-SUBKVAU watafanya uchambuzi kwa kutumia mfumo wa takwimu uliopo (DHIS2,BEMIS-BEST, Mifumo ya shule inaunganishwa na BEMIS,CPMIS,ICMIS) ili kutambua viashiria vya malezi jumuishi na kuongeza vile vinavyo kosekana. Katika hali ya kukosa viashiria, Kwa mfano katika malezi yenye mwitikio na ujifunzaji wa awali, timu ya mapitio itarejea miradi inayolenga viashiria vya ulimwengu vilivyoshirikishwa. Mfano, katika malezi yenye mwitikio. Kutakuwa na safu ya vikao kazi angalau vitatu ili kupitia takimwu zilizopo na kuziimaarisha. Shughuli hii itaenda pamoja na

mkutano wa Maafisa wa ngazi za juu wa wizara za kisekta juu ya kuingiza viashiria vya malezi jumuishi vinavyokosekana katika mfumo wa taarifa uliopo, kazi hii imepangwa kukamilika mwaka 2022.

Shughuli 2.3.1.2 Kuingiza Viashiria vya MMMAM vilivyokosekana kwenye mifumo ya utoaji taarifa ya kisekta iliyopo na Tafiti za Kitaifa

Viashiria vilivyo tambuliwa vinatakiwa kujumuishwa kwenye mfumo wa taarifa wa kisekta ili kuweza kuzifuatilia. Hii itafanyika kwa kufanya mikutano mitatu ya mapitio ili kupitia viashiria husika ambao utahusisha washiriki 20 kwa siku tatu. Wataalamu wataandaa dashibodi ya MMMAM kwa siku 90. Baada ya kufanya hivyo, utafanyika mkutano wa siku 2 wenye washiriki 30 wa maafisa wa ngazi za juu wa Wizara za kisekta. Ili kuwezesha ukusanyaji wa taarifa, kutoa mafunzo kwa maafisa wawili wa Halmashauri juu ya ukusanyaji wa taarifa hii itafanyika kwa mwaka wa pili, mwaka wa Tatu, mwaka wa Nne na mwaka wa Tano kama ilivyooneshwa (Halmashauri 184 - washiriki 50 mwaka wa Pili, 45 mwaka wa Tatu, 45 mwaka wa Nne, 45 mwaka wa Tano).

Shughuli 2.3.1.3 Kutengeneza Kanzidata jumuishi ya MMMAM katika mfumo wa dashibodi kwa ajili ya kufuatilia viasharia vya malezi jumuishi kutoka katika mifumo ya utoaji taarifa ya kisekta iliyopo

Mpaka sasa kanzidata jumuishi ya MMMAM zipo kisekta zaidi na hazihusiani. Kanzidata ya MMMAM italenga viashitia vyote katika nchi ili kutoa jukwaa moja lenye taarifa jumuishi za MMMAM. Mfumo wa Kanzidata ya MMMAM utatumiwa na watoa huduma wote nchi nzima ikijumuisha, watoa huduma wa afya wa kijamii, Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa maendeleo ya jamii, Maafisa lishe, walezi wa watoto wadogo, walimu wa elimu ya Awali) kufundishwa malezi jumuishi. Ufuatiliaji wa ukuaji wa mkoba wa MMMAM na vifaa vya kupima hali ya lishe. Wizara/idara zinazohusika ( WAMJW, WEST, Wizzara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Katiba na Sheria, OR- TAMISEMI, OWM- SUBKVAU, Ega) watafanya kazi pamoja na NBS,TFNC, Wadau wa Maendeleo, Wadau wa Utekelezaji na AZAKi ilikuwezesha mchakato uliopangwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka wa kwanza. Mchakato huu utajumuisha kufanya vikao kazi ili kubaini na kukubaliana juu ya viashiria, Mfumo wa viashiria, dashibodi itakayo tumika kuweka taarifa za malezi jumuishi. Hii itafanyika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya waka wa kwanza wa program (2022).

Shughuli 2.3.1.4 Kutoa mafunzo ya awali kwa kupitia majukwaa kwa wajumbe wa MMMAM katika ngazi ya mkoa na Halmashauri kuhusu matumizi ya dashibodi ya kanzidata jumuishi kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji wa viashiria vya malezi jumuishi

Kwa ukusanyaji na ufuatiliaji mzuri wa taarifa, wahusika wa ukusanyaji wa taarifa wanatakiwa kupewa mafunzo juu ya mfumo wa ukasanyiji na uhifadhi wa taarifa. Hii itafanyika katika Serikali za mitaa zote ambapo mkutano wa siku moja kwa watu wa 5 kutoka katika sekta mbalimbali watapewa mafunzo kwa kila Mikoa 26 na Halmashauri 184. Kikao kazi kitaitishwa kwa wataalamu na wawakilishi wa maafisa wa wizara za kisekta kuandaa dashibodi kabla ya mwisho wa mwaka wa kwanza wa program (2022).

Shughuli 2.3.1.5 Kutoa mafunzo ya matumizi ya kanzidata jumuishi ya MMMAM kwa watoa huduma kwa ajili ya kufuatilia viashiria vya malezi jumuishi

Ubora wa taarifa unategemea sana uwezo wa wakusanyaji taarifa na uhifadhi wake. Programu itatoa mafunzo kwa watoa huduma katika Serikali za Mitaa yote ambayo itahusisha watu 608 watu 3 kutoka kwenye kila Halmashauri 184, mikoa 26 na 30 kutoka idara za serikali. Warsha ya siku mbili itafanyika kabla mwisho wa mwaka wa kwanza wa programu.

Shughuli 2.3.1.6 Kufanya ufuatiliaji wa pamoja wa mwaka wa MMMAM katika ngazi ya Halmashauri (Shule, vituo vya kulelea watoto na Vituo vya Afya)

Ufuatiliaji wa utekelezaji programu jumuishi ya kitaifa ya MMMAM ni muhimu kujua maendeleo. Mpango huu wa ufuatiliaji utakuwa wa mara kwa mara ambapo utahusu utekelezajiwa MMMAM katika ngazi zote. Hii itafanyika kupitia ufuatiliaji wa pamoja wa wadau (WEST, WAMJW, OWM-SUBKVAU, na Wadau) washiriki 20 kutoka ngazi ya Taifa (kwa MMikoa mitano iliochaguliwa kwa miaka miatano) utafanyika kwa siku Tano kwa kila Mkoa.

Matokeo ya papo kwa papo 2.3.2: Zana za uthibiti ubora zimeimarishwa kwa kuingiza vigezo vya uwezo maalumu wa mtoto

Shughuli 2.3.2.1 Kufanya mapitio ya zana za uthibiti ubora kwa elimu ya Awali ili kuingiza vipengele vya uwezo maalumu wa mtoto

WAMJW, WEST,OR-TAMISEMI na wadau wengine wamepanga kufanya mfululizo wa vikao vitano vya kuthibitisha na kukamilisha .mchakato huu utatumia zana uthibiti ubora zilizopo kwa elimu ya Awali, kujumuisha masuala ya jinsi ya kushughulikia uwezo maalumu kwa watoto. Uwezo maalum wa watoto unaweza maanisha watoto wenye shida katika ujifunzaji, wanaojifunza kwa haraka, wasichana/wavulana, na ulemavu. Shughuli hii itahusisha wadau; watu 15 kwa siku 3 na kikao kimoja cha kuthibitisha cha watu 40 kwa siku 2 na kikao kimoja cha kupitia na kukamilisha cha wato 20 kwa siku 2. Hii itakamilika katika mwaka wa kwanza wa program.

Shughuli 2.3.2.2 Kusambaza zana za uthibiti ubora za elimu ya Awali , vituo vya kijamii vya kulelea watoto chini ya miaka 5 ambazo zimejumuisha uwezo maalumu za mtoto

Zana za uthibiti ubora zilizo fanyiwa mapitio kwa(elimu ya awali,vituo vya MMMAM vya kijamii, na vituo vya kulelea watoto wachanga) zitasambazwa na mafunzo kufanyika katika ngazi ya Kitaifa na mpango wa kufikia Halmashauri na Mikoa yote nchini. Watu watakopewa mafunzo watakuwa Afisa elimu taaluma wilaya, Mthibiti ubora wa Shule, Afisa ustawi wa jamii, Afisa maendeleo ya jamii, Afisa mtendaji wa Kata na Walimu. Hii itajumuisha kufanya vikao vya mafunzo (kikao kimoja cha ngazi ya taifa kwa siku 3 kwa watu 10 watakao tengeneza timu ya taifa, mikutano mitano ya kanda kwa siku 3 kwa watu 166 ambao watakua Wakukufnzi wa Wakufunzi katika ngazi ya Mikoa na vikao 184 kwa siku 1 kwa watu 1,076 katika Serikali za mitaa, Walimu 32,802, Watendaji wa Kata 3,720 watakao pewa mafunzo kwa siku 1).

Matokeo ya papo kwa papo 2.3.3: Zana za uchunguzi kutambua watoto wenye ulemavu kwenye vituo vya kulelea watoto chini ya miaka 5 zimeandaliwa

Shughuli 2.3.3.1 Kupitia na kuboresha zana zilizopo za uchunguzi na utambuzi wa watoto chini ya umri wa miaka mitano

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina zana za uchunguzi lakini utambuzi wa watoto wenye ulemavu na wenye mahitaji maalumu haujajumuishwa katika zana iliyopo. Kwa kutambua kwamba utambuzi wa maendeleo uliochelewa au ulemavu ni muhimu kuhakikisha ufuatiliaji wa muda. Utambuzi wa watoto wenye uhitaji tofauti utafanyika kupitia madarasa ya elimu ya Awali. WEST, WAMJW na OWM- SUBKVAU, watafanya kazi kwa pamoja na wadau wa maendeleo na AZAKi kufanya warsha za mara kwa mara ili kupitia zana za uchunguzi zilizopo na kuimarisha ili kusaidia watoa huduma kuweza kutambua ulemavu na uhitaji maalumu kwa watoto kwa wakati. Warsha itahusisha watu 15 kwa muda wa siku 5 ambao utakamilishwa katika mwaka wa kwanza wa programu.

Shughuli 2.3.3.2 Kutoa mafunzo ya awali kwa maafisa wa Halmashauri ukijumuisha Afisa elimu wa Wilaya, Afisa taaluma wa Wilaya, Mthibiti ubora wa Shule, Maafisa Elimu wa Kata, Walimu wa Taaluma, Afisa Ustawi wa Jamii na Walimu wakuu juu ya zana za uchunguzi na utambuzi ya watoto wenye ulemavu na mahitaji maalumu iliyoboreshwa

Zana za uthibiti ubora zilizo thibitishwa zenye mjumuiko wa nyanja za ulemavu na uhitaji maalumu zitatolea mafunzo katika timu za Serikali za mitaa ikijumuisha Mkurugenzi wa Halmashauri, Afisa taaluma, Mthibiti ubora wa shule, Mtendaji wa Kata, Walimu wa taaluma, Afisa ustawi wa jamii, Afisa maendeleo ya jamii na walimu Wakuu. Mchakato utafanyika katika ngazi ya Halmashauri kwa kupitia ushirikiano wa Wizara zinazoongoza WEST, OR-TAMISEMI, WAMJW, OWM-SUBKVAU na AZAKi. Vikao vya mafunzo vitafanyika mabapo washiriki 1,840 watapewa mapfunzo ya zana za uchunguzi ili kutambua watoto wenye ulemavu na uhitaji maalum (watu 10 kwa kila Halmashauri). Mafunzo haya yatakuwa kwa siku moja katika ngazi ya Serikali za mitaa mwishoni mwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji.

Shughuli 2.3.3.3 Kufanya mapitio na kukamilisha rasimu ya orodha ya hatua za maelendeleo ya ukuaji wa mtoto ili kuongeza umri wa mpaka miaka 8

Kupitia juhudi za WAMJW (kitengo cha lishe) rasimu ya orodha ya viashiria vya maendeleo ya mtoto (miaka 0-3) imeandaliwa na ipo kwenye rasimu. Rasimu ya orodha ya viashiria vya maendeleo ya mtoto itasaidia wazazi, walezi na walezi wa watoto wadogo kuona mchakato wa maendeleo ya mtoto katika kipengele cha malezi jumuishi (kiakili, kijamii, kihisia na kimwili) kwa umri na kutoa msaada kwa kuzingatia umri. Orodha ya viashiria vya maendeleo ya mtoto inahitaji kufanyiwa mapitio ili kulenga watoto wa miaka 0-8 na kuidhinisha kwa kupitia angalau warsha 2 kukamilisha. Warsha hii itahususisha watu 20 kwa siku 5 kwa kila warsha.

## Matokeo ya muda mfupi 2.4: Takwimu za ubora na viwango zinapatikana ili kusaidia utekelezaji wa programu ya MMMAM

Matokea ya papo kwa papo 2.4.1: Utafiti kuhusu kiwango cha magonjwa na vifo kwa watoto wenye umri kati ya miaka 5-8 umefanyika

### Shughuli 2.4.1.1: Kuadaa andiko la utafiti

Andiko la utafiti litakalopitiwa na wataalamu litaandaliwa likijumuisha mchanganuo wa kufanya utafiti, mbinu za utafiti zitakazotumika, uchambuzi wa tafiti mbalimbali, mpango wa uchambuzi wa takwimu, mpango wa kusambaza taarifa za matokeo ya utafiti na zana zitakazotumika kukusanya takwimu na taarifa. Shughuli hii itaongozwa na OR-TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Vyuo Vikuu, Wadau wa Maendeleo, Wadau wanaotekeleza Mpango Jumuishi wa Taifa wa MMMAM, Shirika la Taifa la Takwimu, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu na OWM-SUBKVAU wataandaa warsha 3 za waandishi zitakazojumuisha watafiti na wataalamu wa afya. Shughuli hii itafuatiwa na kazi ya kukusanya takwimu za watoto wenye umri wa miaka 5 – 8 katika mikoa yote 26; uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa, kutafsiri matokeo ya uchambuzi na kuandaa taarifa ya matokeo ya utafiti. Kwa ujumla kutakuwa na warsha 4. Mchakato huo utafuatiwa na kufanyika kwa warsha ya siku moja ya kusambaza taarifa ya matokeo ya utafiti kwa wadau wa MMMAM.

### Shughuli 2.4.1.2: Kukusanya takwimu

Kazi ya ukusanyaji takwimu itafanyika kwa kushirikisha wadodosaji 52, ambapo kila mkoa Utatoa wadodosaji wawili. Shughuli hii itafanyika kwa muda wa siku 14 kwenye mikoa yote 26. Shughuli hii itakamilika katika robo ya tatu ya mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Taifa wa MMMAM (mwaka 2022).

### Shughuli 2.4.1.3: Kufanya warsha ya uchambuzi wa takwimu, tafsiri na uandishi wa taarifa

Takwimu zilizokusanywa zitafanyiwa uchambuzi na taarifa ya hali ya magonjwa na vifo vya watoto wenye umri wa miaka 5 – 8 itaandaliwa. Mchakato huu utahusisha waandishi 20 wa taarifa pamoja na wachambuzi wanne wa takwimu watakaoshiriki warsha ya uchambuzi na uandishi wa taarifa ya matokeo ya utafiti. Kila warsha itakayofanyika itachukua siku saba. Shughuli hii itakamilika katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji.

### Shughuli 2.4.1.4: Kufanya warsha ili kutoa matokeo ya utafiti

Utafiti unakuwa na umuhimu iwapo matokeo yake yatatumika kupitia na kuboresha utekelezaji wa Programu. Usambazaji wa taarifa za matokeo ya utafiti utaibua masuala muhimu yaliyoibuliwa kwenye utafiti na kuyafikisha kwa wadau wanaohusika, na hivyo kutumika kuboresha utekelezaji wa programu pale inapobidi. Ili kuweza kusambaza kikamilifu taarifa ya matokeo ya utafiti, wadau 100 wa MMMAM wataalikwa kushiriki warsha ya siku moja ya kuwasilisha taarifa ya matokeo ya utafiti ambapo nakala 500 za taarifa hiyo zitagawanywa.

Matokeo ya papo kwa papo 2.4.2: Tafiti kuhusu malezi yenye mwitikio kwa watoto wenye umri wa miaka 0-8 umefanyika

Shughuli 2.4.2.1: Kuandaa Andiko la utafiti

OR-TAMISEMI, OWM-SUBKVAU, WEST, na WAMJW (kitengo cha Afya ya Uzazi na Mtoto, Idara ya Ustawi wa Jamii) kwa kushirikiana na Vyuo Vikuu, Wadau wa Maendeleo, Wadau wanaotekeleza Program Jumuishi wa Taifa wa MMMAM, Shirika la Taifa la Takwimu, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu wataandaa andiko la utafiti lenye mchanganuo wa utafiti, mbinu za kufanya utafiti, uchambuzi wa taarifa za matokeo ya tafiti mbalimbali, mpango wa uchambuzi wa takwimu, mpango wa kusambaza taarifa za matokeo ya utafiti na zana za kukusanyia takwimu za utafiti. Jumla ya warsha 3 zitafanyika zikijumuisha watafiti na wataalamu wa malezi yenye mwitikio, afya na ustawi wa jamii. Shughuli hii itafuatiwa na kazi ya kukusanya takwimu za malezi yenye mwitikio za watoto wenye umri wa miaka 0 – 8 katika mikoa yote 26; uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa, kutafsiri matokeo ya uchambuzi na kuandaa taarifa ya matokeo ya utafiti. Kwa jumla kutakuwa na warsha 3 zitakazojumuisha watafiti 10 na kuchukua siku saba kwa kila warsha. Shughuli hii itakamilika katika mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Taifa wa MMMAM.

Shughuli 2.4.2.2 Kukusanya takwimu

Kazi ya ukusanyaji takwimu itafanyika kwa kushirikisha wadodosaji 52, ambapo kila Mkoa utatoa wadodosaji wawili. Shughuli hii itafanyika kwa muda wa siku 14 kwenye mikoa yote 26. Shughuli hii itakamilika katika robo ya tatu ya mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Programu Jumuishi wa Taifa wa MMMAM (mwaka 2022).

Shughuli 2.4.2.3 Kufanya warsha ya uchambuzi wa takwimu, Tafsiri na uandaaji wa taarifa

CTakwimu zilizokusanywa zitafanyiwa uchambuzi na taarifa ya hali ya magonjwa na malezi yenye mwitikio kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 8 itaandaliwa. Mchakato huu utahusisha waandishi 20 wa taarifa pamoja na wachambuzi wanne wa takwimu watakaoshiriki warsha ya uchambuzi na uandishi wa taarifa ya matokeo ya utafiti. Kila warsha itakayofanyika itachukua siku saba. Shughuli hii itakamilika katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji.

Shughuli 2.4.2.4: Kufanya warsha ili kutoa matokeo ya utafiti

Utafiti unakuwa na umuhimu iwapo matokeo yake yatatumika kupitia na kuboresha utekelezaji wa mipango. Usambazaji wa taarifa za matokeo ya utafiti utaibua masuala muhimu yaliyotambuliwa katika utafiti na kuyafikisha kwa wadau wanaohusika, na hivyo kutumika kuboresha utekelezaji wa programu pale inapobidi. Ili kuweza kusambaza kikamilifu taarifa ya matokeo ya utafiti, wadau 100 wa MMMAM wataalikwa kushiriki warsha ya siku moja ya kuwasilisha taarifa ya matokeo ya utafiti ambapo nakala 500 za taarifa hiyo zitagawanywa.

Matokeo ya papo kwa papo 2.4.3: Tafiti za viashiria vya malezi jumuishi zimefanyika

Shughuli 2.4.3.1: Kuandaa andiko la utafiti

OR-TAMISEMI, WEST, WAMJW kwa kushirikiana Ofisi ya Waziri Mkuu, Vyuo Vikuu, Wadau wa Maendeleo, Wadau wanaotekeleza Mpango Jumuishi wa Taifa wa MMMAM, Shirika la Taifa la Takwimu, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu wataandaa andiko la utafiti lenye mchanganuo wa utafiti, mbinu za kufanya utafiti, uchambuzi wa taarifa za matokeo ya tafiti mbalimbali, mpango wa uchambuzi wa takwimu, mpango wa kusambaza taarifa za matokeo ya utafiti na zana za kukusanyia takwimu za utafiti. Jumla ya warsha 3 zitafanyika zikijumuisha watafiti na wataalamu wa maeneo muhimu ya Malezi Jumuishi. Shughuli hii itafuatiwa na kazi ya kukusanya takwimu za maeneo yote muhimu ya malezi jumuishi kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 8 katika Mikoa yote 26; uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa, kutafsiri matokeo ya uchambuzi na kuandaa taarifa ya matokeo ya utafiti. Kwa jumla kutakuwa na warsha 3 zitakazojumuisha watafiti 10 na kuchukua siku saba kwa kila warsha. Shughuli hii itakamilika katika mwaka wa tatu wa utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Taifa wa MMMAM.

### Shughuli 2.4.3.2 Kukusanya takwimu

Kazi ya ukusanyaji takwimu itafanyika kwa kushirikisha wadodosaji 52, ambapo kila Mkoa utatoa wadodosaji wawili. Shughuli hii itafanyika kwa muda wa siku 14 kwenye mikoa yote 26. Shughuli hii itakamilika katika robo ya tatu ya mwaka wa tatu wa utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Taifa wa MMMAM (mwaka 2023).

### Shughuli 2.4.3.3 Kufanya warsha ya uchambuzi wa takwimu, tafsiri na uandishi wa taarifa.

Takwimu zilizokusanywa zitafanyiwa uchambuzi na taarifa ya hali ya viashiria vya Malezi Jumuishi kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 8 itaandaliwa. Mchakato huu utahusisha waandishi 20 wa taarifa pamoja na wachambuzi wanne wa takwimu watakaoshiriki warsha ya uchambuzi na uandishi wa taarifa ya matokeo ya utafiti. Kila warsha itakayofanyika itachukua siku saba. Shughuli hii itakamilika katika mwaka wa tatu wa utekelezaji.

### Shughuli 2.4.3.4: Kufanya warsha ili kutoa matokeo ya utafiti

Utafiti unakuwa na umuhimu iwapo matokeo yake yatatumiwa na wadau kupitia na kuboresha utekelezaji wa mpango. Usambazaji wa taarifa za matokeo ya utafiti utaibua masuala muhimu yaliyotambuliwa katika utafiti na kuyafikisha kwa wadau wanaohusika, na hivyo kutumika kuboresha utekelezaji wa programu pale inapobidi. Ili kuweza kusambaza kikamilifu taarifa ya matokeo ya utafiti, wadau 100 wa Malezi Jumuishi wataalikwa kushiriki warsha ya siku moja ya kuwasilisha taarifa ya matokeo ya utafiti ambapo nakala 500 za taarifa hiyo zitagawanywa. Shughuli hii itakamilika katika mwaka wa tatu wa utekelezaji.

## Matokeo ya papo kwa papo 2.4.4: Mapitio ya Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM yamefanyika

### Shughuli 2.4.4.1: Kufanya tathmini ya muhula wa kwanza wa utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM

Tathimini ya utekelezaji wa Program Jumuishi ya MMMAM itafanyika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya utekelezaji wake ili kupima maendeleo ya utekelezaji wa shughuli za mpango. Tathimini hiyo itafanyika katika mwaka wa tatu wa utekelezaji wa mpango, ambapo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ikishirikiana na wadau wengine wakiwemo vyuo vikuu, wadau wa maaendeleo, wadau wanaotekeleza mpango, na Shirika la Taifa la Takwimu wataajiri Mtaalamu Mshauri atakayefanya kazi kwa ushirikiano na timu ya wataalamu na wadodosaji ili kuandaa andiko la utafiti lenye mbinu za utafiti. Pia atakusanya takwimu kwenye maeneo yote nchini, atachambua takwimu zilizokusanywa na kuandaa taarifa ya matokeo ya utafiti. Pia mkutano wa wadau utafanyika ili kuwasilisha matokeo ya utafiti wa kutathmini ya utekelezaji wa mpango, kwa kutumia majukwaa mbalimbali ikiwemo mikutano ya wafadhili.

### Shughuli 2.4.4.1.1: Kuandaa andiko la tathmini

OR-TAMISEMI, WEST, WAMJW kwa kushirikiana Ofisi ya Waziri Mkuu, Vyuo Vikuu, Wadau wa Maendeleo, Wadau wanaotekeleza Programu Jumuishi wa Taifa wa MMMAM, Taasisi ya Taifa la Takwimu, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu wataandaa andiko la utafiti lenye mchanganuo wa utafiti, mbinu za kufanya utafiti, uchambuzi wa taarifa za matokeo ya tafiti mbalimbali, mpango wa uchambuzi wa takwimu, mpango wa kusambaza taarifa za matokeo ya utafiti na zana za kukusanyia takwimu za utafiti. Jumla ya warsha 3 zitafanyika zikijumuisha watafiti na wataalamu wa maeneo muhimu ya Malezi Jumuishi. Shughuli hii itafuatiwa na kazi ya kukusanya takwimu za maeneo yote muhimu ya malezi jumuishi kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 8 katika Mikoa yote 26; uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa, kutafsiri matokeo ya uchambuzi na kuandaa taarifa ya matokeo ya utafiti. Kwa jumla kutakuwa na warsha 3 zitakazojumuisha watafiti 10 na kuchukua siku saba kwa kila warsha. Shughuli hii itakamilika katika mwaka wa tatu wa utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Taifa wa MMMAM.

### Shughuli 2.4.4.1.2: Kukusanya takwimu

Kazi ya ukusanyaji takwimu itafanyika kwa kushirikisha wadodosaji 52, ambapo kila Mkoa utatoa wadodosaji wawili. Shughuli hii itafanyika kwa muda wa siku 14 kwenye mikoa yote 26. Shughuli hii itakamilika katika robo ya tatu ya mwaka wa tatu wa utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Taifa wa MMMAM (mwaka 2023).

### Shughuli 2.4.4.1.3: Kufanya warsha ya uchambuzi wa takwimu, tafsiri na uandishi wa taarifa

Takwimu zilizokusanywa zitafanyiwa uchambuzi na taarifa ya hali ya magonjwa na malezi yenye mwitikio kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 8 itaandaliwa. Mchakato huu utahusisha waandishi 20 wa taarifa pamoja na wachambuzi wanne wa takwimu watakaoshiriki warsha ya uchambuzi na uandishi wa taarifa ya matokeo ya utafiti. Kila warsha itakayofanyika itachukua siku saba. Shughuli hii itakamilika katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji.

### Shughuli 2.4.4.1.4: Kufanya warsha ili kutoa matokeo ya tathmini

Utafiti unakuwa na umuhimu iwapo matokeo yake yatatumiwa na wadau kupitia na kuboresha utekelezaji wa mpango. Usambazaji wa taarifa za matokeo ya utafiti utaibua masuala muhimu yaliyotambuliwa katika utafiti na kuyafikisha kwa wadau wanaohusika, na hivyo kutumika kuboresha utekelezaji wa programu pale inapobidi. Ili kuweza kusambaza kikamilifu taarifa ya matokeo ya utafiti, wadau 100 wa Malezi Jumuishi wataalikwa kushiriki warsha ya siku moja ya kuwasilisha taarifa ya matokeo ya utafiti ambapo nakala 500 za taarifa hiyo zitagawanywa. Shughuli hii itakamilika katika mwaka wa tatu wa utekelezaji.

### Shughuli 2.4.4.2: Kufanya tathmini ya mwisho wa Utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM

WAMJW ikishirikiana na wadau wengine wakiwemo vyuo vikuu, wadau wa maaendeleo, wadau wanaotekeleza mpango, na Shirika la Taifa la Takwimu wataajiri Mtaalamu Mshauri atakayefanya kazi kwa kufanya tathmini ya mwisho ya utekelezaji wa Program Jumuishi ya Taifa ya MMMAM ili kupima mafanikio ya utekelezaji wa Program Jumuishi ya Taifa ya MMMAM. Tathmini ya mwisho itapima viashiria vya matokeo ya muda mfupi, matokeo ya muda wa kati na matokeo yanayotarajiwa ya Program Jumuishi ya Taifa ya MMMAM. Tathmini ya mwisho itafanyika katika mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa mpango (2025/26).

### Shughuli 2.4.4.2.1: Kuandaa andiko la tathmini (zikiwemo andiko, mbinu, mapitio ya maandishi, mpango wa uchambuzi, usambazaji na zana za ukusanyaji takwimu).

OR-TAMISEMI, WEST, WAMJW kwa kushirikiana Ofisi ya Waziri Mkuu, Vyuo Vikuu, Wadau wa Maendeleo, Wadau wanaotekeleza Programu Jumuishi wa Taifa wa MMMAM, Shirika la Taifa la Takwimu, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu wataandaa andiko la utafiti lenye mchanganuo wa utafiti, mbinu za kufanya utafiti, uchambuzi wa taarifa za matokeo ya tafiti mbalimbali, mpango wa uchambuzi wa takwimu, mpango wa kusambaza taarifa za matokeo ya utafiti na zana za kukusanyia takwimu za utafiti. Jumla ya warsha 3 zitafanyika zikijumuisha watafiti na wataalamu wa maeneo muhimu ya Malezi Jumuishi. Shughuli hii itafuatiwa na kazi ya kukusanya takwimu za maeneo yote muhimu ya malezi jumuishi kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 8 katika Mikoa yote 26; uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa, kutafsiri matokeo ya uchambuzi na kuandaa taarifa ya matokeo ya utafiti. Kwa jumla kutakuwa na warsha 3 zitakazojumuisha watafiti 10 na kuchukua siku saba (7) kwa kila warsha. Shughuli hii itakamilika katika mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa Programu Jumuishi wa Taifa wa MMMAM (2026)

### Shughuli 2.4.4.2.2: Kukusanya takwimu

Kazi ya ukusanyaji takwimu itafanyika kwa kushirikisha wadodosaji 52, ambapo kila Mkoa utatoa wadodosaji wawili. Shughuli hii itafanyika kwa muda wa siku 14 kwenye Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Shughuli hii itakamilika katika robo ya tatu ya mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa Programu Jumuishi wa Taifa wa MMMAM (Mwaka 2026).

Shughuli 2.4.4.2.3: Kufanya warsha ya uchambuzi wa takwimu, tafsiri na uandishi wa taarifa

Takwimu zilizokusanywa zitafanyiwa uchambuzi na taarifa ya hali ya magonjwa na malezi yenye mwitikio kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 8 itaandaliwa. Mchakato huu utahusisha waandishi 20 wa taarifa pamoja na wachambuzi wanne wa takwimu watakaoshiriki warsha ya uchambuzi na uandishi wa taarifa ya matokeo ya utafiti. Kila warsha itakayofanyika itachukua siku saba. Shughuli hii itakamilika katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji.

Shughuli 2.4.4.2.4: Kufanya warsha ili kutoa matokeo ya tathmini

Utafiti unakuwa na umuhimu iwapo matokeo yake yatatumiwa na wadau kupitia na kuboresha utekelezaji wa mpango. Usambazaji wa taarifa za matokeo ya utafiti utaibua masuala muhimu yaliyotambuliwa katika utafiti na kuyafikisha kwa wadau wanaohusika, na hivyo kutumika kuboresha utekelezaji wa programu pale inapobidi. Ili kuweza kusambaza kikamilifu taarifa ya matokeo ya utafiti, wadau 100 wa Malezi Jumuishi wataalikwa kushiriki warsha ya siku moja ya kuwasilisha taarifa ya matokeo ya utafiti ambapo nakala 500 za taarifa hiyo zitagawanywa. Shughuli hii itakamilika katika mwaka wa mwisho wa utekelezaji (2026).

## *Matokeo ya Muda Mrefu 3: Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma bora zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa Watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao*

### Matokeo ya muda mfupi 3.1: Utoaji wa huduma bora za afya umeboreshwa

Matokeo ya papo kwa papo 3.1.1: Hali za afya na lishe kwa watoto wenye umri wa miaka 0-8 zimetambuliwa.

Shughuli 3.1.1.1: Kutoa huduma za mkoba mara kwa mara ili kuwatambua watoto wenye changamoto za ukuaji kwenye vituo vya kulelea watoto chini ya miaka 5, shule za Awali na madarasa ya mwanzo ya Shule za Msingi (darasa la kwanza mpaka la tatu)

Utambuzi wa watoto wenye changamoto za ukuaji katika shule za Awali umekuwa ni changamoto kwa miaka mingi. WAMJW wakishirikiana na OR-TAMISEMI, OWM-SUBKVAU, WEST pamoja na asasi za kiraia zimelenga kufanya ziara 4 za utambuzi kwa kutembelea Halmashauri zote 184 kila mwaka, kufikia vituo vyote vya kulelea watoto mchana na shule za Awali na kufanya utambuzi wa watoto wenye changamoto za kiafya yenye kuathiri ukuaji wa watoto. Mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka 2025 zoezi hili litakua limekamilika.

Matokeo ya Papo kwa papo 3.1.2: Utoaji wa huduma za afya kwa kina, ufuatiliaji na uchunguzi kwa watoto wadogo kwenye vituo vya afya umeongezeka.

Utoaji kikamilifu wa huduma za afya kwa watoto wenye umri chini ya miaka 5 na wale waliopo kwenye shule za Awali na vituo vya kulelea watoto mchana ni muhimu sana ili kuhakikisha watoto hawa wanakuwa vema na hivyo kuweza kujifunza wakiwa wanacheza. Programu itahakikisha watoto wote nchini wanafikiwa.

Shughuli 3.1.2.1: Kupitia na kuboresha huduma za afya kwa wanawake wajawazito, huduma za mama na mtoto baada ya kujifungua, huduma za afya kwa watu wenye maambukizi ya VVU na huduma jumuishi za matibabu ya watoto ili kuingiza vipengele vya malezi jumuishi katika kuwezesha utoaji wa huduma za kina; ufuatiliaji na uchunguzi wa hatua za ukuaji wa watoto

Ingawa kuna mikoba mingi kwenye sekta ya afya inayoshughulikia mahitaji ya kiafya kwa watoto, mikoba hii haitoshi kushughulikia vipengele vyote vya malezi jumuishi. Hivyo

kunahitajika kuingiza taarifa za ziada kwenye mikoba hiyo ili kuhakikisha malezi jumuishi yaliyo timilifu yanatolewa katika kila hatua ya ukuaji. Mapitio ya mikoba hiyo ni suala endelevu ambalo linahusisha wadau mahsusi ikiwa ni pamoja na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto (Idara ya watoto), Ofisi ya Raisi TAMISEMI pamoja na asasi za kiraia. Mapitio haya yatafanyika kwa kufanya makongamano 4 kila kongamano litafanyika kwa siku 3 likihusisha wataalamu 20 kwa kila kongamano.

Shughuli 3.1.2.2: Kuandaa Kijitabu cha afya na maendeleo ya mtoto kutumia maandishi ya nukta nundu (braille) ili kuongeza upatikanaji wa huduma kwa watu wenye uoni hafifu

Serikali itatengeneza kijitabu kidogo ambacho kinalezea kwa ukamilifu vipengele vyote vya malezi jumuishi. Hata hivyo akina mama wenye uoni hafifu wanaweza kupata shida katika kusimamia ukuaji wa watoto wao na kuwapatia huduma nyingine zinazochangia ukuaji. Ili kutatua changamoto hii, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Ofisi ya Raisi TAMISEMI pamoja na asasi za kiraia wamepanga kutengeneza kopi ya vijitabu hivi vya malezi ya watoto kwa maandishi ya nukta nundu (braille) kwa vituo 12,319 vya afya kwa msaada wa wataalamu wa maandishi ya nukta nundu.

Shughuli 3.1.2.3: Kuanzisha huduma mkoba za kliniki ya mama, baba na mtoto kufikia kwenye vituo vya kulelea watoto chini ya miaka 5, shule za Awali na madarasa ya mwanzo ya shule za msingi ( darasa la kwanza mpaka la tatu)

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Ofisi ya Waziri Mkuu Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Raisi-TAMISEMI watafanya kazi pamoja na wadau wengine katika kuhakikisha kuwa huduma za mama na mtoto pamoja na kliniki zinazotembea zinawafikia watoto wote katika vituo vya afya. Huduma hizi zitatolewa pia kwenye vituo vitatu vya kulelewa watoto mchana kulingana na aina ya vituo hivyo (vituo vitatu kwa kila aina ya vituo) katika kila kijiji hivyo kufanya vijiji vyote 12,319 pamoja na shule za elimu ya Awali 16,401 zinafikiwa ili kuwezesha kutoa huduma kwa watoto wadogo hadi kufikia mwaka 2025.

Shughuli 3.1.2.4: Manunuzi ya vifaa vya ufuatiliaji wa ukuaji na maendeleo ya mtoto (mizani ya kupimia uzito, Ubao wa kupimia urefu/kimo na vifaa vya michezo vinavyoendana na umri wa mtoto) katika vituo vya afya

Vifaa sahihi na vya kutosha kwa ajili ya kupima maendeleo ya mtoto vinahitajika kuwepo kwa ufanisi wa huduma. Kumekuwa na chanagamoto ya kuwepo na mizani za kutosha za kupimia uzito, mbao za kupimia urefu pamoja na vichezeo kwa ajili ya vipindi vya uchechemuzi kwa watoto. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Ofisi ya Raisi TAMISEMI itanunua mizani za kutosha za kupimia uzito, mbao za kupimia urefu pamoja na vichezeo mbalimbali na kuvisambaza vitu hivyo kwa vituo vyote vya afya 12,319 ili kusaidia huduma kwa watoto wanaotembelea vituo hivyo hadi kufikia mwaka 2025.

## Matokeo ya muda mfupi 3.2: Upatikanaji wa huduma toshelezi na sahihi za lishe umeongezeka

Matokeo ya papo kwa papo 3.2.1 Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe umepitiwa kuongeza vipengele vya malezi jumuishi

Shughuli 3.2.1.1 Kufanya mkutano wa kupitia mpango jumuishi wa Taifa wa Lishe wa pili ili kuhakikisha vipengele vya malezi jumuishi vimeingizwa

Kushiriki katika mapitio ya Mpango wa taifa wa Lishe–II ili kuingiza vipengele vya malezi jumuishi. Sektetarieti ya Programu ya taifa ya MMMAM inapaswa kufuatilia na kuhakikisha inashiriki katika mapitio ya mpango wa taifa wa lishe ili kuhakikisha mpango uliopitiwa umeingiza vipengele vya malezi jumuishi. Shughuli hii haijatengewa bajeti.

Matokeo ya papo kwa papo 3.2.2: Afua za lishe zinatolewa katika shule za Awali na madarasa ya mwanzo ya shule za msingi (darasa la kwanza hadi la tatu)

Shughuli 3.2.2.1: Kuchunguza na kutambua hali ya lishe na hatua za ukuaji kwa watoto wenye umri wa miaka 5 - 8 katika shule za awali na madarasa ya mwanzo ya shule za msingi (darasa la kwanza mpaka la tatu) kama sehemu ya programu za afya

Kwa kupitia program za afya shuleni, WAMJW kwa kushirikiana na WEST, OWM-SUBKVAU watafanya ziara kwa kila robo muhula wa mwaka kwa shule za elimu ya Awali 16,401 na kufanya uchunguzi wa kubainisha watoto wenye mahitaji ya lishe, watoto wenye ulemavu na changamoto nyingine za ukuaji na kuzitatua ufumbuzi ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri kwa wazazi na walezi wa watoto waliobainika kuwa na changamoto hizo pamoja na kuwapa rufaa kwenda kupata huduma zaidi. Shughuli hii itakuwa ni endelevu kwa kipindi chote cha program.

Matokeo ya papo kwa papo 3.2.3 Programu ya utoaji chakula shuleni kwa watoto wa shule za awali na na madarasa ya mwanzo ya shule za msingi (darasa la kwanza mpaka la tatu) imetekelezwa

Programu itatumia mwongozo wa lishe kwa shule za elimu ya Awali ambao tayari umeshatengenezwa ili kuelekeza makundi mbalimbali katika ngazi zote kuhakikisha mwongozo huo unatekelezwa.

Shughuli 3.2.3.1: Kutoa mafunzo ya awali ya siku 3 kwa wawezeshaji 20 wa kitaifa juu ya namna ya kutumia Mwongozo wa programu ya utoaji wa chakula Shuleni

Mafunzo ya siku 3 yatatolewa kwa wakufunzi 20 katika ngazi ya taifa kuhusu matumizi ya mwongozo wa mpango wa taifa wa lishe kwenye ngazi ya taifa.

Shughuli 3.2.3.2: Kutoa mafunzo ya awali ya siku 3 kwa wawezeshaji na wakufunzi kuhusu namna ya kutumia Mwongozo wa programu ya utoaji wa chakula shuleni katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri

Mkutano wa siku 3 wa mafunzo utafanyika kwa wakufunzi 6 kutoka kila Mkoa kwa Mikoa yote 26 na wakufunzi 5 kutoka Halmashauri zote 184 (Washiriki 1076) kuhusu matumizi ya mwongozo wa mpango wa lishe shuleni kwenye ngazi ya Mkoa na Halmashauri.

Shughuli 3.2.3.3: Kutoa mafunzo ya awali ya siku 3 kwa walimu na watendaji kata kuhusu namna ya kutumia Mwongozo wa programu ya utoaji wa chakula shuleni katika Halmashauri zote

Mkutano wa siku 3 wa mafunzo utafanyika kwa walimu 2 kwa kila shule ya awali katika shule zote 16,401 (32,802), watendaji kata 2 katika kila kata kwa kata zote 3,720 (7,440 Mtendaji kata, Afisa Elimu i Kata) katika halmashauri zote 184.

Shughuli 3.2.3.4: Kuanzisha shughuli za ufugaji kuku, wanyama wadogo na kilimo cha bustani katika ngazi ya shule ili kutoa chakula chenye virutubisho muhimu kwa watoto kupitia programu ya utoaji wa chakula shuleni na kubadilisha taratibu za ulishaji wa watoto katika ngazi ya kaya

Katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa lishe kwa watoto kupitia mpango wa lishe shuleni, Ofisi ya Raisi TAMISEMI, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na wadau wengine hawatafanya uhamasishaji peke yake kwa shule pamoja na wazazi na walezi kuanzisha bustani za mbogamboga shuleni pamoja na nyumbani, pia watahamasisha ufugaji wa kuku katika shule za madarasa ya elimu Awali 16,401 kupitia kamati za wazazi na walezi. Wazazi na walezi watahamasishwa kuchangia ufugaji wa kuku na kushiriki katika programu ya bustani za shule kwenye shule zilipo kwenye jamii yao.

Kufuatilia utekelezaji wa shughuli za ufugaji kuku, wanyama wadogo na kilimo cha bustani katika ngazi ya shule.

Matokeo ya papo kwa papo 3.2.4: Maadhimisho ya Siku ya afya na lishe vijijini yamefanyika yakijumuisha utoaji wa huduma mkoba za afya ya mama, baba na mtoto

Shughuli 3.2.4.1: Kufanya maadhimisho ya siku ya afya na lishe vijijini

## Matokeo ya Muda Mfupi 3.3: Huduma sahihi za malezi yenye mwitikio zimetolewa

Matokeo ya papo kwa papo 3.3.1: Kona jumuishi za MMMAM zenye vifaa vya kutosha vya michezo na vya kujifunzia zimeanzishwa

Shughuli 3.3.1.1: Kuanzisha kona jumuishi za MMMAM zenye vifaa vya kutosha vya michezo na kujifunzia vinavyoendana na umri wa mtoto kwenye vituo vyote vya afya (12,319) katika Halmashauri zote 184 nchini ili kutoa nafasi ya michezo na mawasiliano kati ya mlezi na mtoto; pia kusaidia kutambua uwezo na mahitaji ya mtoto na kufanya rufaa sahihi

Uanzishwaji wa kona jumuishi za MMMAM katika vituo vya kutolea huduma za afya utafanyika pamoja na mkakati wa kuvipatia vituo hivyo miongozo ya malezi na utengenezaji wa vifaa vya kuchezea na kujifunzia. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ofisi ya Waziri Mkuu SBAU, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo na wadau wengine wa MMMAM watatumia miongozo iliyopo kuanzisha vituo jumuishi vya MMMAM kwenye vituo 12,319 vinavyotoa huduma ya afya. Kila kituo cha kutolea huduma za afya kitaanzishiwa vituo viwili vya MMMAM (kituo kimoja kwenye kitengo cha huduma za afya ya uzazi, na kingine kwenye wodi ya watoto). Kona jumuishi za MMMAM zitakavyoanzishwa zitakuwa na kuta zilizopambwa kwa michoro rafiki kwa watoto. Pia zitakuwa na vifaa vya kuchezea watoto vilivyotengenezwa kwa malighafi inayopatikana katika jamii husika, vinavyozingatia umri mbalimbali wa watoto. Vituo hivyo vitatumika kama eneo la kuonesha na kuwafundisha wazazi na walezi michezo mbalimbali ya watoto, jinsi ya kuwasiliana na watoto, na taratibu mbalimbali za malezi yenye mwitikio. Vituo hivyo pia vitakuwa ni eneo salama la wazazi na walezi kuchangamana na watoto wao, pamoja na kutoa fursa ya kuweza kuwatambua watoto wenye mahitaji mahsusi wakiwemo watoto wenye changamoto ya ukuaji na ulemavu ili wapewe rufaa.

Matokeo ya Papo kwa papo 3.3.2: Huduma za mara kwa mara za unasihi wa malezi jumuishi kwa wazazi na walezi zimetolewa

Shughuli 3.3.2.1: Kutoa huduma za mara kwa mara za unasihi wa malezi jumuishi kwa wazazi na walezi

Watoa Huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya watafanya unasihi kwa wazazi/walezi wakati wanapohudhuria kwenye kliniki za Afya ya Uzazi, Vituo vya Huduma kwa Watu wenye maambukizi ya VVU na wodi za watoto. Watoa huduma za afya watatumia vipindi vya elimu ya afya vinavyotolewa kwenye kliniki za Afya ya Uzazi, Vituo vya Huduma kwa watu wenye maambukizi ya VVU na wodi za watoto kutoa unasihi. Mwongozo jumuishi wa MMMAM pamoja na vitendea kazi vingine vikiwemo chatipindu vitatumiwa na watoa huduma za afya kuwezesha mada mbalimbali za malezi jumuishi wakati wanapozungumza na kuwaelimisha wazazi na walezi.

Mada hizo ni pamoja na: malezi yenye mwitikio, fursa za kujifunza za awali, afya ya akili, msaada wa kijamii (hifadhi ya jamii), maji na usafi wa mazingira, jinsi ya kutengeneza vifaa vya kuchezea na kufundishia watoto vinavyozingatia umri mbalimbali wa watoto kwa kutumia malighafi zinazopatikana kwenye jamii. Ushiriki wa wanaume utahamasishwa ili kuongeza ufanisi wa malezi yenye mwitikio miongoni mwa wazazi na walezi wanaume. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, wadau wa maendeleo na wadau wengine wa MMMAM watasaidia vituo vya kutolea huduma za afya vipatavyo 12,319 kuendesha vipindi vya unasihi angalao viwili kwa mwezi. Walengwa wa unasihi ni wazazi/walezi wanaofika kwenye vituo hivyo kupata huduma.

## Matokeo ya Muda Mfupi 3.4: Fursa za ujifunzaji wa awali zimeongezeka

### Matokeo ya Papo kwa Papo 3.4.1: Fursa za ujifunzaji wa awali kwa watoto zimeongezeka

#### Shughuli 3.4.1.1: Kusaidia uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya malezi ya watoto wenye umri wa miaka 0 - 2 kwenye maeneo rasmi na yasio rasmi ya kazi ili kuimarisha unyonyeshaji, malezi yenye mwitikio na ujifunzaji wa awali

Hivi sasa imeonekana kwamba maeneo rasmi na yasiyo rasmi yanayotoa huduma ya kuwasaidia wazazi kulea watoto wenye umri wa miaka 0 -8 ambayo hayajasajiliwa. Maeneo hayo ni pamoja na ofisi, masoko na maeneo mengine ya biashara au maeneo ya shambani. Utaratibu mwingine unaotumika ni watoto kuachwa nyumbani ili walelewe na watoto wenzao wenye umri mkubwa wakati mama zao wanapokua kazini. Taratibu hizi zinawaweka watoto kwenye hatari ya kufanyiwa vitendo vya ukatili na ajali. Pia husababisha watoto kukosa fursa na mazingira bora ya kujifunza kwa ajili ya kuimarisha ukuaji na maendeleo yao.

Hata hivyo, takwimu zilizopo zinaonesha kuwa kuna vituo 923 vya kulelea watoto wenye umri wa miaka 0 – 8 vilivyosajiliwa nchini. Idadi hiyo ya vituo vilivyosajiliwa bado ni ndogo na haikidhi mahitaji yaliyopo. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itashirikiana na OR-TAMISEMi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na AZAKi kuhamasisha jamii kuanzisha vituo 200 vya malezi ya watoto wenye umri wa miaka 0 - 2. Vituo hivyo vitawekewa vifaa vinavyohitajika ikiwemo vifaa vya kulalia, vifaa vya kuchezea na samani zinazozingatia umri mbalimbali wa watoto, kwa kuzingatia maelekezo yaliyomo kwenye Mwongozo wa Viwango vya uanzishaji na Uendeshaji Vituo vya Malezi kwa Watoto Wenye Umri wa Miaka 0 – 2.

#### Shughuli 3.4.1.2: Kusaidia uanzishaji kwa vituo vya kulelea watoto vya MMMAM vinavyomilikiwa na jamii

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, OR-TAMISEMi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na AZAKi na wadau wengine wa MMMAM kutumia mbinu zinazotumiwa na wadau wengine kama vile UNESCO, BRAC na CiC kutanua wigo wa huduma ili zifikie maeneo mengine. Hatua hii itajumuisha uanzishaji wa vituo vya malezi ya matoto mchana vinvyomilikiwa na jamii vipatavyo 16,401. Vituo hivyo vitaanzishwa kwenye jamii husika na kwenye maeneo ya shule za msingi kwenye Halmashauri zote ifikapo mwaka 2025. Lengo la kuanzisha vituo hivyo ni kupeleka huduma ya elimu ya Awali karibu na maeneo wanayoishi watoto ambao wanakosa fursa hiyo kutokana na kushindwa kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Mchakato wa uansishawji wa vituo utatumia miongozo ya taifa ya uanzishaji, na uendeshaji wa vituo vya watoto wenye umri wa miaka 0 – 8, vituo vya kulelea watoto wadogo mchana, na vituo vya malezi jumuishi vinavyomilikiwa na jamii. Mchakato huo pia utajumuisha kusaidia jamii kuanzisha vikundi vya malezi vya wazazi vipatavyo 16,401 kwa kuzingatia mwongozo uliopo. Hii itasaidia kuhamasisha elimu ya malezi na utoaji wa huduma za MMMAM kwenye jamii.

Vikundi vya malezi vitajumuisha wazazi wa watoto wanaohudumiwa kwenye vituo vya malezi jumuishi vilivyoanzishwa. Halmashauri zitaviwezesha kifedha vikundi vya malezi

vipatavyo 16,401 kwenye jamii na shule kwa kutumia mpango wa kutoa mkopo wa 10% ili kusaidia uanzishaji wa Shughuli za uzalishaji mali ili kuongeza mapato ya kaya na huduma za msaada kwa watoto katika familia.

Shughuli 3.4.1.3: Kusaidia uanzishaji wa ujenzi wa madarasa ya Elimu ya Awali kwenye maeneo rasmi na yasiyo rasmi

Ili kupunguza msongamano kwenye madarasa ya shule ya awali, OR-TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na wadau wengine wataanzisha / kujenga madarasa ya elimu ya awali kwa kutumia mwongozo wa taifa na viwango vilivyopo ili kupunguza uwiano wa walimu na wanafunzi. Shughuli hii inatarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2025. Hivi sasa, kuna madarasa ya elimu ya awali kwenye karibia shule zote za msingi.

Hata hivyo kuna msongamano mkubwa wa wanafunzi kwenye madarasa hayo. Wazo la kuanzisha vituo shikizi vya elimu ya awali litatekelezwa ili kuwawezesha watoto wengi ambao hawajaandikishwa kupata huduma hiyo. Vituo shikizi viyaanzishwa kwenye maeneo yasiyofikika kwa urahisi.

Matokeo ya Papo kwa Papo 3.4.2: Msaada unaotolewa kwa familia na jamii wa kuwapa elimu ya malezi na kutoa huduma za malezi jumuishi umeongezeka

Shughuli 3.4.2.1: Kusaidia uanzishaji wa vikundi vya malezi katika jamii

Vikundi vya Malezi vya wazazi vitaanzishwa kwenye vijiji 16,401 ili kuhamasisha elimu ya Malezi na huduma za Malezi jumuishi kwa watoto katika jamii. Vikundi hivyo vitajumuisha wazazi wenye watoto kwenye vituo vya MMMAM vitakavyoanzishwa kwenye jamii. Mchakato wa kuanzisha vituo hivyo utazingatia maelekezo yaliymo kwenye mwongozo wa uanzishaji vikundi vya Malezi.

Shughuli 3.4.2.2: Kusaidia upatikanaji wa mitaji kwa vikundi vya malezi

Vikundi vya Malezi kwenye vijiji 16,401 vitapewa ruzuku ya kuanzishia huduma itakayotokana na mpango wa kuzipa halmashauri mkopo wa 10%. Ruzuku hiyo itasaidia uanzishaji wa shughuli za uzalishaji mali ili kuongeza mapato ya kaya na huduma za msaada kwa watoto katika familia.

## Matokeo ya muda mfupi 3.5: Upatikanaji wa huduma za ulinzi na usalama wa mtoto umeongezeka

Matokeo ya Papo kwa Papo 3.5.1: Vituo vya mkono kwa mkono vinavyotoa huduma za ulinzi na usalama kwa watoto wadogo vimeanzishwa.

Shughuli 3.5.1.1: Kuwezesha uanzishaji wa vituo 97 vya mkono kwa mkono katika hospitali za wilaya ambazo zitatoa huduma za ulinzi na usalama kwa mama na mtoto wakiwemo watoto wenye umri wa miaka 0-8

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; OR-TAMISEMI, OWM-SUBKVAU, Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na AZAKI na wadau wengine wa Malezi Jumuishi watawezesha mchakato wa kuanzisha vituo vya Mkono kwa mkono ili kuwezesha utoaji wa huduma sahihi za ulinzi na usalama wa watoto kwa wazazi na watoto wenye umri wa miaka 0 – 8. Hii itajumuisha kuwatambua wajumbe wa timu za watoa huduma watakaotoa msaada rafiki kwa mtoto.

Shughuli 3.5.1.2: Kutoa mafunzo ya awali kwa watoa huduma (wanasihi, manesi, madaktari, polisi na afisa ustawi jamii) kuhusu huduma rafiki kwa mtoto

Wizara zinazohusika zitatoa mafunzo kwa watoa huduma wapya wapatao 485 kutoka katika vituo 97 ambapo kila kituo kitatoa washiriki 5 wa mafunzo. Kila kituo cha Mkono-Kwa-Mkono katika Halmashauri 97 kitakuwa na watoa huduma 5 watakaotambuliwa ambao ni pamoja na Afisa wa Polisi, Muuguzi, Afisa Ustawi wa Jamii, Mnasihi, na Tabibu. Watoa huduma hao watapewa mafunzo kwa kutumia miongozo ya mafunzo iliyopo yenye maelekezo ya jinsi ya kuanzisha kituo cha Mkono-Kwa-Mkono kinachotoa huduma rafiki kwa mtoto ulioandaliwa na MTAKUWWA. Mafunzo yatafanyika mara mbili katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Programu

Shughuli 3.5.1.3: Kunzisha/ Kujenga vituo vipya 81 vya huduma ya mkono kwa mkono kwenye hospitali za Wilaya na kukarabati vituo 40 vya huduma ya mkono kwa mkono kwa kutumia majengo yaliyopo kwenye hospitali na kuweka samani na vifaa vikiwemo kona rafiki ya michezo yenye vifaa vya michezo

Timu ya watoa huduma waliopewa mafunzo itakuwa na wajibu wa kuanzisha/kukarabati Kituo-Cha-Mkono-Kwa-Mkono kwenye hospitali zilizo kwenye maeneo yao. Hii itahusisha kuvipatia vituo hivyo samani zinazozingatia umri mbalimbali wa watoto, mapambo na vifaa vya kuchezea. Hapa nchini kuna Vituo-vya-Mkono-Kwa-Mkono vipatavyo 16 vilivyoanzishwa na MTAKUWWA. Kwa hiyo Programu itaanzisha vituo vingine 81. Kati ya vituo hivyo 81 vitakavyoanzishwa, vituo 40 vinahitaji kukarabatiwa au kuwekewa vifaa kwenye majengo ya hospitali yaliyopo.

## *Matokeo ya Muda Mrefu Na. 4: Wazazi, walezi, familia na jamii wamejengewa uwezo wa kutekeleza taratibu sahihi za malezi jumuishi*

### Matokeo ya Muda Mfupi Na. 4.1: Uelewa kuhusu umuhimu wa huduma za malezi jumuishi katika jamii umeongezeka

Matokeo ya Papo kwa Papo Na. 4.1.1: Uhamasisha wa jamii kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wadogo katika miaka ya awali umefanyika)

Shughuli: 4.1.1.1: Kuandaa ujumbe wa MMMAM ili kuhamasisha na kuongeza uelewa wa umuhimu wa kuwekeza katika huduma za malezi jumuishi kupitia vyombo vya habari

Programu itatumia mbinu mbalimbali za kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wadogo. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, wazee na Watoto itafanya kazi na Idara ya Elimu ya Afya, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Asasi za Kiraia ili kuandaa jumla ya ujumbe 60 wa elimu kuhusu masuala ya MMMAM. Ujumbe utatangazwa kwenye redio mara moja kila mwezi kupitia vituo 34 vya radio za kijamii. Ujumbe utatangazwa pia mara mbili katika muda ambao watu wengi huwa nyumbani na unaopedwa na watu wengi kusikiliza redio. Utaratibu huu utaendelea kwa kipindi chote cha miaka mitano ya utekelezaji wa Programu. Programu hii itafanya kazi kwa ushirikiano na mpango wa Familia Bora, Taifa Imara – ili kuhakikisha kuwa ujumbe wa MMMAM hautofautiana.

Shughuli 4.1.1.2: Kujenga uelewa wa wadau muhimu katika jamii kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wadogo kuanzia miaka ya awali kwenye ngazi ya kata

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Mambo ya Ndani, Ofisi ya Waziri Mkuu – SUBKVAU, na AZAKi (ikijumuisha Taasisi za Dini na za kijamii) itawezesha uendeshaji wa mikutano 1,978 (ya siku moja) katika ngazi ya kata. Mikutano hiyo itajumuisha wadau 15 wanaohusika na suala la Malezi jumuishi katika jamii wakiwemo Taasisi za Kijamii, Taasisi za Dini na Maafisa Ugani wa sekta ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jeshi la Polisi, Kilimo, Elimu n.k. Hili litatekelezwa kwenye 50% ya kata zote nchini Tanzania ili kuongeza uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa kuwekeza katika huduma za Malezi jumuishi. Mikutano hiyo itafanyika kuanzia robo ya pili ya mwaka wa kwanza hadi robo ya pili ya mwaka wa pili wa utekelezaji wa Programu Mikutano hiyo itabeba ajenda inayolenga kuongeza uelewa wa umuhimu wa kutoa huduma timilifu za Malezi jumuishi kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 8, ikiwa ni pamoja na watoto wenye ulemavu na wenye mahitaji maalumu. Majadiliano yatahusu:

1. Kuanzisha na kusajili watoto kwenye vituo vya Malezi kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 2, vituo vya Malezi ya watoto mchana, vituo vya Malezi katika ngazi ya jamii, huduma ya elimu ya awali na madarasa ya I - III shule za Msingi kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 8;

2. Uajiri wa watoa huduma za Malezi ya watoto kwa ajili ya kutoa huduma kwenye vituo vya Malezi mchana pamoja na kwaandalia utaratibu wa kuwapa motisha;

3. Haki za watoto, aina mbalimbali za ukatili, njia rafiki za kuwafanya watoto watoe taarifa za ukatili na unyanyasaji waliofanyiwa pamoja na kuanzisha madawati ya huduma rafiki za ulinzi na usalama wa watoto; na

4. Kuanzisha vikundi vya malezi vya wazazi.

Shughuli 4.1.1.3: Kuandaa mikutano ya kuhamasisha viongozi wa kijamii, viongozi wa dini, sekta binafsi na viongozi mashuhuri kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwa watoto wadogo kuanzia miaka ya awali

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekinolojia, Wizara ya Mambo ya Ndani, Ofisi ya Waziri Mkuu – SUBKVAU, na AZAKi (ikijumuisha Taasisi za Dini na za kijamii) itawezesha kufanyika kwa mikutano inayojumuisha washiriki 20 wakiwemo viongozi wa kijamii, sekta binafsi na viongozi wenye ushawishi mkubwa kwenye jamii pamoja na viongozi wa dini,, washiriki wa Kamati za Ulinzi wa mama na mtoto; na watu wenye ulemavu kwenye vijiji na mitaa 8,292, ili kuongeza kiwango cha uelewa kuhusu umuhimu wa kutoa huduma timilifu ya Malezi Jumuishi. Mikutano hiyo itaendelea kufanyika katika kipindi chote cha mwaka wa pili hadi robo ya tatu ya utekelezaji wa programu.

Shughuli 4.1.1.4: Kufanya mikutano ya uhamasishaji kwa madiwani ili kuongeza kiwango cha uwekezaji kwenye huduma za malezi jumuishi

Upangaji wa bajeti ya serikali huanzia katika ngazi ya jamii ambapo vipaumbele vya kibajeti huibuliwa. Kwa kuzingatia faida itakayopatikana kupitia uelimishaji jamii utakaofanyika nchini kote, Program Jumuishi ya Taifa ya MMMAM itatoa fursa ya kuongeza uwekezaji kwa kutumia viongozi wanaotoa maamuzi wanaohusika na masuala ya bajeti na mipango. Watoa maamuzi wote watakapokuwa na uelewa mpana kuhusu umuhimu wa kuwekeza katika masuala ya Malezi jumuishi, wanaweza kusaidia kuongeza fedha zinazotengwa kwenye bajeti na kutoa kipaumbele katika masuala ya MMMAM kwenye bajeti. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Mambo ya Ndani, Ofisi ya Waziri Mkuu – SUBKVAU, na AZAKi itawezesha kufanyika kwa vikao 40 vya uhamasishaji na uelimishaji jamii (kikao kimoja kitafanyika kwa siku moja kwa kila Halmashauri). Vikao hivyo vitafanyika kwa Madiwani 1,840 kwenye Halmashauri 92, ambapo kikao kimoja kitajumuisha madiwani 20, Mikutano hiyo itafanyika kuanzia mwaka wa kwanza ambapo jumla ya mikutano 40 itafanyika na mwaka wa pili ambapo jumla ya mikutano 52 itafanyika.

Miongoni ma masuala yatakayojadiliwa kwenye mikutano hiyo ni pamoja na:

1. Lishe na afya bora, Malezi yenye mwitikio, ujifunzaji wa awali, ulinzi na usalama wa watoto. Pia itasisitiza umuhimu wa ushiriki wa wanaume katika Malezi ya watoto wakiwemo watoto wenye ulemavu na mahitaji maalumu wenye umri wa miaka 0 – 8; pamoja na masuala ya haki za watoto, aina mbalimbali za ukatili na unyanyasaji watoto, mifumo ya kushughulikia ulinzi na haki za watoto, na huduma rafiki za ulinzi na usalama wa watoto;

2. Usajili wa vizazi ikiwemo kuwapa watoto vyeti za kuzaliwa ikiwa ni mojawapo kati ya haki za msingi za mtoto;

3. Malezi chanya ya watoto ikijumuisha kuepuka taratibu zisizo sahihi za Malezi kwa mfano matumizi ya nguvu wakati wa kumlisha mtoto chakula;

4. Vituo vya huduma na ukarabati kwa watoto wenye mahitaji maalumu; na

5. Kuanzisha vikundi vya Malezi vya wazazi.

## Matokeo ya Muda wa Kati na. 4.2: Wazazi/walezi na jamiiwameshirikishwa katika kutoa/kuchangia huduma za malezi jumuishi

Matokeo ya Papo kwa Papo Na. 4.2.1: Mwongozo wa uanzishaji wa dawati la ulinzi wa mtoto shuleni umesambazwa

Shughuli 4.2.1.1: Kusambaza mwongozo wa uanzishaji wa dawati la ulinzi wa mtoto shuleni kupitia kuwajengea uwezo wa awali Maafisa elimu, Maafisa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Jamii kwenye Kata na Halmashauri zote

Mpango Jumuishi wa Taifa wa MMMAM unalenga kusambaza mwongozo wa dawati rafiki la ulinzi na usalama wa mtoto kwa watoa huduma wote ili waweze kuuelewa na kuutumia kama mwongozo wa kazi zao wakati wanapotoa huduma na kuzungumza na watoto katika ngazi zote. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itashirikiana na OR-TAMISEMI; Wizara ya Elimu; Sayansi na Teknoljia; TECDEN na AZAKi ili kuwezesha mikutano ya  siku moja ya kuelimisha jamii itakayohusisha washiriki 46 katika Halmashauri zote 184 hapa nchini. Washiriki wa mikutano hiyo ni pamoja na Maafisa  Elimu wa Kata wapatao 7,912, Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Elimu wa Wilaya, ambapo jumla ya washiriki wote watakaoelimishwa ni 8,464.

Mkakati huu utasaidia kuwezesha uanzishaji wa Madawati Rafiki ya Watoto kwenye vituo vya kulelea watoto wenye umri wa miaka 0 – 2, vituo vya Malezi ya watoto mchana katika jamii, vituo vya elimu ya awali kwenye jamii, na darasa (I - III katika za shule msingi. Ratiba ya kufanya mikutano hiyo itachukua kipindi cha miaka miwili, ambapo Halmashauri 92 zitafikiwa katika mwaka wa kwanza na zilizobaki 92 zitafikiwa katika mwaka wa pili.

Matokeo ya Papo kwa Papo Na. 4.2.2: Vituo vya kulelea watoto chini ya miaka 5 vimeanzishwa

Shughuli 4.2.1.1: Kushirikisha wazazi/ walezi na jamii, katika kusaidia kuendeleza huduma za malezi jumuishi kwenye vituo vya kulelea watoto chini ya miaka 5, elimu ya awali na madarasa ya mwanzo ya shule za msingi (darasa la kwanza hadi la tatu)

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itashirikiana na OR-TAMISEMI, AZAKI, Taasisi za Dini na Wadau wa Maendeleo kuwezesha mikutano katika ngazi ya jamii ambapo jamii 12,319 zitafikiwa. Lengo la mikutano hiyo ni kutoa elimu kwa jamii kuhusu kutoa huduma mbalimbali kwa watoto kwenye vituo vya Malezi ya watoto wenye umri wa miaka 0 – 2, vituo vya Malezi ya watoto mchana katika jamii, vituo vya elimu ya awali kwenye jamii, na madarasa ya elimu ya awali katika shule za msingi Huduma hizo ni pamoja na chakula bora, utengenezaji wa vifaa vya kuchezea na kujifunza vya watoto kwa kutumia malighafi inayopatikana katika jamii husika, vifaa vya kuchezea watoto kwenye maeneo ya nje ya nyumba, pamoja na kuwawezesha walimu/walezi wa watoto kwa kuwapa mbinu za msingi za kufundisha watoto wadogo.

Mara nyingi kuna changamoto ya utoaji wa chakula kwenye vituo vya Malezi ya watoto mchana hasa vilivyopo katika jamii hasa kwa familia masikini. Ili kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata angalau mlo mmoja, kama ziada ya milo anayokula nyumbani, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, Wizara ya Kilimo, AZAKi, Taasisi za Dini na Wadau wa Maendeleo watawezesha mikutano ya kuhamasisha jamii wakiwemo wazazi na walezi, kuhusu umuhimu wa kutoa chakula chenye ubora katika vituo vya kulelea watoto wenye umri wa miaka 0 – 2 na vituo vya Malezi ya watoto mchana na hivyo kuwapa watoto wote wanaohudhuria mafunzo kwenye vituo hivyo chakula  bora ifikapo mwaka 2025.

**Shughuli 4.2.2.2: Kuwezesha uanzishwaji na uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto chini ya miaka 5 (creches, Day care centres na Community based ECD centres) kwenye maeneo rasmi na yasiyo rasimi ili kuwezesha huduma za malezi jumuishi**

Ofisi ya Raisi – TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itashirikiana na AZAKI kutumia mwongozo uliotayarishwa wa Viwango vya Msingi vya Uendeshaji wa Vituo Vya Malezi ya Watoto Mchana na Vituo vya Malezi ya Watoto wenye Umri wa Miaka 0 – 2 ili kutoa mafunzo ya siku mbili. Mafunzo hayo yatafanyika kwenye kanda tisa na kuwafikia jumla ya walengwa 420 kutoka katika mikoa na wilaya zote. Washiriki wa mafunzo hayo ni Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ustawi wa jamii. Mafunzo katika kanda moja yatajumuisha washiriki 47.

ambapo mpango uliopo utawezesha kufikia Halmashauri zote 184 nchini Tanzania. Kanda hizo 9 na vituo ambavyo vitatumika kutoa mafunzo ni pamoja na: 1. Pwani, Dar es salaam na Morogoro; 2. Singida, Dodoma na Manyara; 3. Songea, Mbeya na Rukwa; 4. Tabora, Katavi na Kigoma; 5. Geita, Kagera na Mwanza; 6. Shinyanga, Simiyu na Mara; 7. Kilimanjaro, Arusha na Tanga; 8. Mtwara na Lindi; 9. Njombe, Ruvuma na Iringa. Mafunzo yanatarajiwa kukamilika katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Programu.

## *Kiambatisho 3 Mpango Uliowekewa bajeti Kamilifu*

## *Jumla ya bajeti ya Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM*

| Maelezo ya shughuli | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | JUMLA TSHS | Isiyokuwa na fedha | JUMLA USD | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Mazingira wezeshi yameboreshwa kuwezesha uratibu wenye ufanisi na utoaji huduma za malezi jumuishi | 21,557,340,000 | 25,911,545,000 | 23,222,816,100 | 29,056,720,110 | 28,099,607,481 | 127,848,028,691 | 127,848,028,691 | 55,106,909 | 13.97% |
| 2. Mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora imeimarishwa | 11,524,574,000 | 48,887,428,300 | 4,313,343,000 | 1,721,098,900 | 3,039,310,010 | 69,485,754,210 | 69,485,754,210 | 29,950,756 | 7.59% |
| 3. Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma bora na zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa Watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao | 111,409,297,000 | 143,770,728,200 | 143,935,162,800 | 142,423,987,750 | 151,255,512,155 | 692,794,687,905 | 692,794,687,905 | 298,618,400 | 75.72% |
| 4. Wazazi, walezi, familia na jamii wamejengewa uwezo wa kutekeleza taratibu sahihi za malezi jumuishi | 4,866,800,000 | 9,106,658,000 | 5,183,519,000 | 3,991,589,140 | 1,714,314,690 | 24,862,880,830 | 24,862,880,830 | 10,716,759 | 2.72% |
| ***Jumla*** | 149,358,011,000 | 227,676,359,500 | 176,654,840,900 | 177,193,395,900 | 184,108,744,336 | 914,991,351,636 | 914,991,351,636 | 394,392,824 | 100% |

## *Bajeti ya Matokeo ya Muda Mrefu*

| MATOKEO YANAYOTARAJIWA | ASILIMIA | JUMLA | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Matokeo ya Muda Mrefu 1: Mazingira wezeshi yameboreshwa kuwezesha uratibu wenye ufanisi na utoaji huduma za malezi jumuishi** | | | | | | | |
| Matokeo ya Muda Mfupi | | | | | | | |
| 1.1: Uhamasishaji wa masuala ya MMMAM katika ngazi zote umeimarishwa ili kuongeza uwajibikaji na upatikanaji wa huduma za malezi jumuishi | | 719,353,513 | 543,280,000 | 81,433,000 | 28,592,300 | 31,451,530 | 34,596,683 |
| 1.2: Uratibu wa sekta mbalimbali kwenye ngazi zote umeimarishwa | | 124,122,243,178 | 19,825,730,000 | 24,012,010,000 | 23,194,223,800 | 29,025,268,580 | 28,065,010,798 |
| 1.3:Sera, miongozo, mitaala na vitini vya kufundishia imeandaliwa/kufanyiwa mapitio ili kuingiza vipengele vyote vya malezi jumuishi | | 3,006,432,000 | 1,188,330,000 | 1,818,102,000 | - | - | - |
| ***JUMLA 1*** | 13.97% | 127,848,028,691 | 21,557,340,000 | 25,911,545,000 | 23,222,816,100 | 29,056,720,110 | 28,099,607,481 |
| **Matokeo ya Muda Mrefu 2: Mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora imeimarishwa** | | | | | | | |
| Matokeo ya Muda Mfupi | | | | | | | |
| 2.1: Uwepo wa watoa huduma wenye ujuzi na umahiri kwenye maeneo ya malezi jumuishi | | 29,086,421,300 | 2,883,444,000 | 23,870,570,500 | 2,038,522,000 | 293,884,800 | - |
| 2.2: Mfumo wa rufaa na muhusiano ya utoaji huduma ya malezi jumuishi umeimarishwa | | 22,675,640,800 | 186,660,000 | 22,488,980,800 | - | - | - |
| 2.3: Uwepo wa mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji uliokubalika | | 13,127,891,110 | 7,530,850,000 | 1,312,300,000 | 1,312,661,000 | 1,427,214,100 | 1,544,866,010 |
| 2.4: Takwimu za ubora na kiwango zinapatikana ili kusaidia utekelezaji wa programu ya MMMAM | | 4,595,801,000 | 923,620,000 | 1,215,577,000 | 962,160,000 | - | 1,494,444,000 |
| ***JUMLA 2*** | 7.59% | 69,485,754,210 | 11,524,574,000 | 48,887,428,300 | 4,313,343,000 | 1,721,098,900 | 3,039,310,010 |

| MATOKEO YANAYOTARAJIWA | ASILIMIA | JUMLA | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Matokeo ya Muda Mrefu 3: Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma bora na zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa Watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao | | | | | | | |
| Matokeo ya Muda Mfupi | | | | | | | |
| 3.1: Utoaji wa huduma bora za afya zimeboreshwa | | 32,942,277,628 | 859,280,000 | 14,182,685,000 | 15,498,539,100 | 1,143,701,680 | 1,258,071,848 |
| 3.2: Upatikanaji wa huduma toshelezi na sahihi za lishe umeongezeka | | 39,022,388,457 | 10,986,462,000 | 16,104,453,200 | 3,604,674,700 | 3,965,142,170 | 4,361,656,387 |
| 3.3: Huduma sahihi za malezi yenye mwitikio zimetolewa | | 13,456,043,700 | - | 4,065,270,000 | 4,471,797,000 | 4,918,976,700 | - |
| 3.4: Fursa za ujifunzaji wa awali zimeongezeka | | 605,205,889,120 | 99,131,200,000 | 109,044,320,000 | 119,948,752,000 | 131,943,627,200 | 145,137,989,920 |
| 3.5: Huduma za ulinzi na usalama wa mtoto zimetolewa | | 2,168,089,000 | 432,355,000 | 374,000,000 | 411,400,000 | 452,540,000 | 497,794,000 |
| ***JUMLA 3*** | 75.72% | 692,794,687,905 | 111,409,297,000 | 143,770,728,200 | 143,935,162,800 | 142,423,987,750 | 151,255,512,155 |
| Matokeo ya Muda Mrefu 4: Wazazi, walezi, familia na jamii wamejengewa uwezo wa kutekeleza taratibu sahihi za malezi jumuishi | | | | | | | |
| Matokeo ya Muda Mfupi | | | | | | | |
| 4.1: Uelewa kuhusu umuhimu wa huduma za malezi jumuishi katika jamii umeongezeka | | 16,900,042,320 | 4,866,800,000 | 6,776,528,000 | 2,620,376,000 | 1,255,399,200 | 1,380,939,120 |
| 4.2: Wazazi/walezi na jamii wameshirikishwa/wamehusishwa katika kutoa/kuchangia huduma za malezi jumuishi | | 7,962,838,510 | - | 2,330,130,000 | 2,563,143,000 | 2,736,189,940 | 333,375,570 |
| ***JUMLA 4*** | 2.72% | 24,862,880,830 | 4,866,800,000 | 9,106,658,000 | 5,183,519,000 | 3,991,589,140 | 1,714,314,690 |
| ***JUMLA KUU*** | | 914,991,351,636 | 149,358,011,000 | 227,676,359,500 | 176,654,840,900 | 177,193,395,900 | 184,108,744,336 |
| ***Asilimia*** | 100% | | 16% | 25% | 19% | 19% | 20% |

## *Grafu*

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mazingira wezeshi yameboreshwa kuwezesha uratibu wenye ufanisi na utoaji huduma za malezi jumuishi | 14.00% |
| 2. | Mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora imeimarishwa | 7.00% |
| 3. | Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma bora na zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa Watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao | 76.00% |
| 4. | Wazazi, walezi, familia na jamii wamejengewa uwezo wa kutekeleza taratibu sahihi za malezi jumuishi | 3.00% |



## Matokeo ya Muda Mrefu 1

| Shughuli # | Maelezo ya shughuli | Maelezo ya shughuli (shughuli ndogo ndogo, kiasi, idadi na muda) | Kiwango cha kipaumbele | Msaada wa kitaalamu unahitajika AU Mkoa | Maelezo ya mahitaji | Msimbo | # Idadi ya watu/ ukumbi | # Siku | Gharama TZS | # Idadi ya vipindi | Mwaka | | | | | JUMLA TZS | Fedha zilizopangwa | Kiasi cha fedha ambacho hakijapatikana | Mfadhali | Hali mbalimbali zinazoweza kusaidia shughuli kufanikiwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | | | | | |
| 1 | MATOKEO YA MUDA MREFU 1: Mazingira wezeshi yameboreshwa kuwezesha uratibu wenye ufanisi na utoaji huduma za malezi jumuishi | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 1.1 | MATOKEO YA MUDA MFUPI 1.1: Uhamasishaji wa masuala ya MMMAM katika ngazi zote umeimarishwa ili kuongeza uwajibikaji na upatikanaji wa huduma za malezi jumuishi | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 1.1.1 | Matokeo ya papo kwa papo 1.1.1: Mkakati wa uhamasishaji wa MMMAM umeandaliwa | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | Kuandaa Mkakati Jumuishi wa Kitaifa wa MMMAM unaotafsiri mfumo wa malezi jumuishi | Kuajiri mtaalamu elekezi (siku 30 @ TZS 400,000 kwa siku) | | | Ada ya Mtaalamu Elekezi | | 1 | 30 | 400,000 | 1 | 12,000,000 | | | | | 12,000,000 | | | | |
| | | Kufanya vikao 2 vya wadau vyenye washiriki 50 ili kuwashirikisha matokeo ya utafiti na kuyathibitisha | | | Posho ya kujikimu/ malazi (ndani ya nchi) | | 56 | 2 | 120,000 | 2 | 26,880,000 | | | | | 26,880,000 | | | | Kiwango cha posho TSHS 120,000 kwa mtu kwa siku |
| | | | | | Usafiri (basi, reli, teksi) | | 46 | 2 | 50,000 | 2 | 9,200,000 | | | | | 9,200,000 | | | | |
| | | | | | Ada ya uwezeshaji (Kuandika taarifa na matayarisho) | | 1 | 1 | 400,000 | 2 | 800,000 | | | | | 800,000 | | | | |
| | | | | | Chakula na viburudisho | | 56 | 1 | 20,000 | 2 | 2,240,000 | | | | | 2,240,000 | | | | |
| | | | | | Ukumbi | | 1 | 1 | 400,000 | 2 | 800,000 | | | | | 800,000 | | | | |
| | | | | | Printing and Photocopying Costs | | 1 | 1 | 10,000 | 2 | 20,000 | | | | | 20,000 | | | | |
| | | | | | Nishati (Mafuta) | | 5 | 2 | 230,000 | 2 | 4,600,000 | | | | | 4,600,000 | | | | |
| | | Kufanya vikao 2 vya wataalamu vyenye washiriki 15 ili kumpa mshauri elekezi maoni ya kitaalamu wakati wa kupitia sera | | | Posho ya kujikimu/ malazi (ndani ya nchi) | | 18 | 3 | 120,000 | 2 | 12,960,000 | | | | | 12,960,000 | | | | |
| | | | | | Usafiri (basi, reli, teksi) | | 14 | 1 | 50,000 | 2 | 1,400,000 | | | | | 1,400,000 | | | | |
| | | | | | Ada ya uwezeshaji (Kuandika taarifa na matayarisho) | | 1 | 3 | 300,000 | 2 | 1,800,000 | | | | | 1,800,000 | | | | |
| | | | | | Ukumbi | | 1 | 3 | 400,000 | 2 | 2,400,000 | | | | | 2,400,000 | | | | |
| | | | | | Chakula na viburudisho | | 18 | 3 | 20,000 | 2 | 2,160,000 | | | | | 2,160,000 | | | | |
| | | | | | Uchapishaji na kudurusu nyaraka | | 1 | 1 | 200,000 | 2 | 400,000 | | | | | 400,000 | | | | |
| | | | | | Nishati (Mafuta) | | 2 | 1 | 230,000 | 2 | 920,000 | | | | | 920,000 | | | | |

| Shughuli # | Maelezo ya shughuli | Maelezo ya shughuli (shughuli ndogo ndogo, kiasi, idadi na muda) | Kiwango cha kipaumbele | Msaada wa kitaalamu unahitajika AU Mkoa | Maelezo ya mahitaji | Msimbo | # Idadi ya watu/ ukumbi | # Siku | Gharama TZS | # Idadi ya vipindi | Mwaka | | | | | JUMLA TZS | Fedha zilizopangwa | Kiasi cha fedha ambacho hakijapatikana | Mfadhali | Hali mbalimbali zinazoweza kusaidia shughuli kufanikiwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | *2021* | *2022* | *2023* | *2024* | *2025* | | | | | |
| | ***Kufanya vikao vya siku moja vya menejimenti vyenye washiriki 30 ili kupokea maoni ya mwisho na kupitisha mkakati*** | | | | ***Chakula na viburudisho*** | | ***30*** | ***3*** | ***20,000*** | ***1*** | ***1,800,000*** | | | | | ***1,800,000*** | | | | |
| | | | | | Uchapishaji na kudurusu nyaraka | | 1 | 1 | 200,000 | 1 | 200,000 | | | | | 200,000 | | | | |
| | Kuidhinisha na kuzindua sera. Kufanya kikao cha siku 1 cha menejimenti chenye washiriki 30 cha kuzindua sera. | | | | Uchapishaji na kudurusu nyaraka | | 1 | 1 | 400,000 | 1 | 400,000 | | | | | 400,000 | | | | |
| | | | | | Chakula na viburudisho | | 1 | 1 | 200,000 | 1 | 200,000 | - | | - | | 200,000 | | | | |
| | | | | | | | 31 | 3 | 20,000 | 1 | 1,860,000 | | | - | | 1,860,000 | | | | |
| | Kufanya warsha ya siku 15 yenye washiriki 20 ya kutafsiri mkakati kwa lugha ya kiswahili. | | | | Posho ya kujikimu/ malazi (ndani ya nchi) | | 23 | 16 | 120,000 | 1 | 44,160,000 | | | | | 44,160,000 | | | | |
| | | | | | Usafiri (basi, reli, teksi) | | 19 | 2 | 50,000 | 1 | 1,900,000 | | | | | 1,900,000 | | | | |
| | | | | | Ada ya uwezeshaji (Kuandika taarifa na matayarisho) | | 1 | 15 | 300,000 | 1 | 4,500,000 | | | | | 4,500,000 | | | | |
| | | | | | Ukumbi | | 1 | 15 | 400,000 | 1 | 6,000,000 | | | | | 6,000,000 | | | | |
| | | | | | Uchapishaji na kudurusu nyaraka | | 1 | 1 | 200,000 | 1 | 200,000 | | | | | 200,000 | | | | |
| | | | | | Chakula na viburudisho | | 23 | 15 | 20,000 | 1 | 6,900,000 | | | | | 6,900,000 | | | | |
| | | | | | Nishati (Mafuta) | | 5 | 1 | 230,000 | 1 | 1,150,000 | | | | | 1,150,000 | | | | |
| | Kufanya vikao 6 vya kanda vyenye washiriki 60 vya siku 1 ili kusambaza mkakati ikijumuisha uchapishaji wa nakala . | | | | Posho ya kujikimu/ malazi (ndani ya nchi) | | 67 | 2 | 120,000 | 6 | 96,480,000 | | | | | 96,480,000 | | | | |
| | | | | | Usafiri (basi, reli, teksi) | | 45 | 2 | 50,000 | 6 | 27,000,000 | | | | | 27,000,000 | | | | |
| | | | | | Ada ya uwezeshaji (Kuandika taarifa na matayarisho) | | 1 | 1 | 400,000 | 6 | 2,400,000 | | | | | 2,400,000 | | | | |
| | | | | | Ukumbi | | 1 | 1 | 400,000 | 6 | 2,400,000 | | | | | 2,400,000 | | | | |
| | | | | | Uchapishaji na kudurusu nyaraka | | 1 | 1 | 200,000 | 6 | 1,200,000 | | | | | 1,200,000 | | | | |
| | | | | | Chakula na viburudisho | | 67 | 1 | 20,000 | 6 | 8,040,000 | | | | | 8,040,000 | | | | |
| | | | | | Nishati (Mafuta) | | 6 | 1 | 230,000 | 6 | 8,280,000 | | | | | 8,280,000 | | | | |
| | Jumla | | | | | | | | | | 293,650,000 | - | - | - | - | 293,650,000 | | | | |

| Shughuli # | Maelezo ya shughuli | Maelezo ya shughuli (shughuli ndogo ndogo, kiasi, idadi na muda) | Kiwango cha kipaumbele | Msaada wa kitaalamu unahitajika AU Mkoa | Maelezo ya mahitaji | Msimbo | # Idadi ya watu/ ukumbi | # Siku | Gharama TZS | # Idadi ya vipindi | Mwaka | | | | | JUMLA TZS | Fedha zilizopangwa | Kiasi cha fedha ambacho hakijapatikana | Mfadhali | Hali mbalimbali zinazoweza kusaidia shughuli kufanikiwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | *2021* | *2022* | *2023* | *2024* | *2025* | | | | | |
| ***1.1.2*** | Matokeo ya papo kwa papo 1.1.2: Uhamasishaji wa viongozi katika ngazi zote umefanyika | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| *1.1.2.1* | Kufanya mkutano na wadau wa maendeleo ili waweze kukubali kuchangia gharama za utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM | Kufanya kikao cha siku 1 cha uhamasishaji chenye washiriki 50 wakiwemo Wadau wa Maendeleo ili kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali za kusaidia utekelezaji. (Kitajumuisha Maafisa 5 wa Serikali) | | | Posho ya kujikimu/ malazi (ndani ya nchi) | | 10 | 2 | 120,000 | 1 | 2,400,000 | 2,640,000 | 2,904,000 | 3,194,400 | 3,513,840 | 14,652,240 | | | | kiwango cha mfumuko wa bei 10% kwa mwaka. |
| | | | | | Ada ya uwezeshaji (Kuandika taarifa na matayarisho) | | 1 | 1 | 400,000 | 1 | 400,000 | 440,000 | 484,000 | 532,400 | 585,640 | 2,442,040 | | | | |
| | | | | | Ukumbi | | 1 | 1 | 400,000 | 1 | 400,000 | 440,000 | 484,000 | 532,400 | 585,640 | 2,442,040 | | | | |
| | | | | | Uchapishaji na kudurusu nyaraka | | 1 | 1 | 200,000 | 1 | 200,000 | 220,000 | 242,000 | 266,200 | 292,820 | 1,221,020 | | | | |
| | | | | | Chakula na viburudisho | | 55 | 1 | 20,000 | 1 | 1,100,000 | 1,210,000 | 1,331,000 | 1,464,100 | 1,610,510 | 6,715,610 | | | | |
| | | | | | Nishati (Mafuta) | | 5 | 1 | 230,000 | 1 | 1,150,000 | 1,265,000 | 1,391,500 | 1,530,650 | 1,683,715 | 7,020,865 | | | | |
| | Jumla | | | | | | | | | | 5,650,000 | 6,215,000 | 6,836,500 | 7,520,150 | 8,272,165 | 34,493,815 | | | | |
| *1.1.2.2* | Kufanya mkutano wa uhamasishaji kwa wabunge kutoka kwenye kamati mbalimbali za bunge kuwajengea uelewa kuhusu Programu Jumuishi ya MMMAM. | Kufanya vikao vya siku 1 vya uhamasishaji vyenye washiriki Wabunge 40 kila mwaka. . | | | Posho ya kujikimu/ malazi (ndani ya nchi) | | 46 | 2 | 120,000 | 1 | 11,040,000 | 12,144,000 | 13,358,400 | 14,694,240 | 16,163,664 | 67,400,304 | | | | |
| | | | | | Usafiri (basi, reli, teksi) | | 37 | 2 | 50,000 | 1 | 3,700,000 | 4,070,000 | 4,477,000 | 4,924,700 | 5,417,170 | 22,588,870 | | | | |
| | | | | | Ada ya uwezeshaji (Kuandika taarifa na matayarisho) | | 2 | 1 | 400,000 | 1 | 800,000 | 880,000 | 968,000 | 1,064,800 | 1,171,280 | 4,884,080 | | | | |
| | | | | | Ukumbi | | 1 | 1 | 400,000 | 1 | 400,000 | 440,000 | 484,000 | 532,400 | 585,640 | 2,442,040 | | | | |
| | | | | | Uchapishaji na kudurusu nyaraka | | 1 | 1 | 200,000 | 1 | 200,000 | 220,000 | 242,000 | 266,200 | 292,820 | 1,221,020 | | | | |
| | | | | | Chakula na viburudisho | | 46 | 1 | 20,000 | 1 | 920,000 | 1,012,000 | 1,113,200 | 1,224,520 | 1,346,972 | 5,616,692 | | | | |
| | | | | | Nishati (Mafuta) | | 4 | 1 | 230,000 | 1 | 920,000 | 1,012,000 | 1,113,200 | 1,224,520 | 1,346,972 | 5,616,692 | | | | |
| | Jumla | | | | | | | | | | 17,980,000 | 19,778,000 | 21,755,800 | 23,931,380 | 26,324,518 | 109,769,698 | | | | |
| *1.1.2.3* | Kufanya mikutano ya uhamasishaji kwa maafisa kutoka ngazi za juu za wizara za kisekta ili waweze kuingiza viashiria na masuala ya MMMAM katika mifumo yao ya utoaji taarifa. | Vikao vya awali vya uhamasishaji vya wataalamu (washiriki 10 kwa siku 2) | | | Posho ya kujikimu/ malazi (ndani ya nchi) | | 12 | 2 | 120,000 | 1 | 2,880,000 | | | | | 2,880,000 | | | | |
| | | | | | Usafiri (basi, reli, teksi) | | 9 | 2 | 50,000 | 1 | 900,000 | | | | | 900,000 | | | | |
| | | | | | Ada ya uwezeshaji (Kuandika taarifa na matayarisho) | | 1 | 1 | 400,000 | 1 | 400,000 | | | | | 400,000 | | | | |
| | | | | | Ukumbi | | 1 | 2 | 400,000 | 1 | 800,000 | | | | | 800,000 | | | | |
| | | | | | Uchapishaji na kudurusu nyaraka | | 2 | 1 | 10,000 | 1 | 20,000 | | | | | 20,000 | | | | |
| | | | | | Chakula na viburudisho | | 12 | 1 | 20,000 | 1 | 240,000 | | | | | 240,000 | | | | |
| | | | | | Nishati (Mafuta) | | 1 | 1 | 230,000 | 1 | 230,000 | | | | | 230,000 | | | | |

